# Wanawake Walio Karibu na Mtume ﷺ

نساء حول الرسول (ﷺ)

Mwandishi:

**Muhammad 'Ali Qutb**

Mfasiri:

**Hamza Mtunu**

- Wanawake Walio Karibu na Mtume ﷺ
- Mwandishi: Muhammad 'Ali Qutb
- Mfasiri: Hamza Mtunu
- Kimepitiwa na: Yassir Salim na Abdusamad Salim
- Typesetting: Ally Said Abdallah na Khalfan Njama
- Chapa ya Kwanza 2019
- Nakala 3000
- Printed in: India


- © Ibn Hazm Media Centre

# Yaliyomo:

Zingatia....5
Neno Muhimu kwa Kila Msomaji....7
Kwanini tumeandaa kitabu hiki?....7
Kuhusu Maswahaba....7
Lengo la Elimu kwa Maswahaba....8
Mama Yake Mtume na Walezi Wake....9
Aminah Bint Wahab....11
Bi Halimah As-sa'diyah....17
Ummu Ayman, Barakah....23
Fatmah binti Asad ibn Hashim....27
**Wake za Mtume ﷺ....33**
Khadijah bint Khuwaylid....35
Sawdah bint Zam'a....45
Aishah bint Abi Bakr....49
Hafsah bint 'Umar....63
Zaynab bint Jahsh....75
Ummu Salamah binti Abi Umayyah....87
Ummu Habibah Ramlah binti Abi Sufyan....97
Juwayriyyah binti al-Haarith ibn Abi Diraar....107
Safiyyah binti Huyay ibn Akhtab....115
Maimunah binti al-Haarith....125
Zaynab binti Khuzaymah....129
Maria al-Qibtiyya....133

**Mabinti wa Mtume ﷺ.......................................................................137**
Zainab bint Muhammad.....................................................................139
Ruqayyah bint Muhammad................................................................145
Ummu Kulthum bint Muhammad......................................................149
Fatmah bint Muhammad....................................................................153
**Wanawake ambao Maisha yao Yanalandana na Maisha ya Mtume ﷺ.......163**
Fatmah Bint Al - Khattaab..................................................................165
Sumayyah Bint Khayyaat....................................................................175
Al-Khansaa, Tamadur binti Amr ibn Shareed........................................181
Ash - Shifaa binti 'Abdullah..................................................................187
Ar-Rumaysa binti Milhan (Ummu Sulaym) Al-Ansariyyah.....................189
Asmaa binti Abu Bakr As-Siddiiq..........................................................195
Asma binti Umays...............................................................................205
Asmaa binti Yaziid..............................................................................213
Atika Binti Zaid....................................................................................217
Hamna binti Jahsh...............................................................................221
Khawlah Bint Al-Azwari.......................................................................225
Nusaybah binti Ka'b - Ummu 'Umarah..................................................231
Safiyyah Binti Abdul Muttalib...............................................................241
Lubabah binti al-Harith, Ummu Fadl.....................................................247
Ummu Hani, Fakhita binti Abi Taalib.....................................................251
Ummu Hiram binti Milhan....................................................................255
Ummu Mihjan......................................................................................261
Zaynab, Ummu Rooman.......................................................................263

## Zingatia:

Kitabu hiki ni moja kati ya vitabu muhimu na vyenye kuvutia kwa Waislamu, hasa vijana. Ni kitabu ambacho kila kijana wa Kiislamu wakiwemo wale wanaosoma shule za sekondari na vyuoni wanapaswa kuvisoma na kujifunza. Ni kitabu kinachomuwezesha Muislamu mambo matatu:

(i) Kufahamu nafasi halisi ya mwanamke wa Kiislamu katika kuusimamisha Uislamu kinyume na inavyoelezwa na ilivyozoeleka.

(ii) Kuijua historia na kufahamu maswahaba walifanya nini mpaka wakapata heshima na kubashiriwa Pepo au kuondoka duniani hali ya kuwa Allah amewaridhia.

(iii) Kujifunza na kumtia hamasa msomaji katika kujiga manisha na matendo ya maswahaba na hivyo kumfanya awe Muislamu mzuri na kustahili ujira kwa Mola wake.

Ni muhimu kwa mzazi, mlezi au kijana mwenyewe kuhakikisha amesoma kitabu hiki, amezingatia na kumuhamasisha ndugu yake Muislamu kukisoma.

### Vitabu vingine muhimu ni:

1. Wanaume Walio Karibu na Mtume ﷺ.

# Neno Muhimu kwa Kila Msomaji

Sifa zote njema zinamstahiki Allah! Yeye ndiye Mkamilifu na hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa Haki isipokuwa yeye Allah! Amani na Salamu za heshima zimwendee Mtume wetu ﷺ, mbora wa viumbe na Mtume wa Mwisho – Muhammad ﷺ.

## Kwanini tumeandaa kitabu hiki?

Lengo la kuandaa kitabu hiki **si** kuongeza maarifa au taarifa walizonazo watu juu ya maswahaba wa Mtume ﷺ na wanawake wema waliotangulia. Hapana! Lengo la kuandaa kitabu hiki ni kuwasaidia wale wenye nia ya kutafuta radhi za Allah, waweze kufahamu wale waliotangulia (Maswahaba) walifanya nini mpaka wakasifiwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake ﷺ. Wakabashiriwa Pepo wakiwa hai. Na wengine wakarejea kwa Mola wao hali ya kuwa Allah Amewaridhia. Matumaini yetu ni kwamba, msomaji mwenye nia ya kufahamu mambo yatakayomuweka karibu zaidi na Allah na mwenye nia ya kuitafuta Pepo, basi mara asomapo kitabu hiki, atapata mambo mengi ya kujifunza, kuzingatia na kuamua kuyatekeleza katika maisha yake yote – Insha-Allah.

## Kuhusu Maswahaba

Katika kusoma kitabu hiki, msomaji atagundua sifa muhimu walizokuwa nazo maswahaba wa kike na wale wa kiume. Sifa ambazo zinatutofautisha sisi na wao. Msomaji atagundua kuwa: miongoni mwa sifa kuu walizokuwa nazo maswahaba ni kuwa na mapenzi ya kweli na ya dhati kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ﷺ na dini yao. Sio kwa kujipamba na kuvaa mavazi mazuri kama hijabu za thamani, majuba na kujipamba kwa ajili ya duniya; bali kwa namna walivyokuwa tayari kutoa mali zao, muda wao na uhai wao kwa ajili ya

kuupeleka mbele Uislamu na kutafuta radhi za Mola wao. Kwao, dunia ilikuwa haina thamani yeyote zaidi ya kuitumia kama fursa ya kutengeneza Akhera yao. Hakuna yeyote katika wao aliyetumia muda wake, rasilimali zake wala nafsi yake kuijenga na kuipamba dunia na kufurahia starehe za kidunia – Hakuna! Kwa ajili ya maisha ya dunia, kila swahaba alifanya yale yaliyokuwa ya lazima kumuwezesha kuishi. Wao Uislamu ilikuwa ndio ajenda kuu kwa masaa ishirini na nne, mengine yote yalikuwa ni ziada. Sisi tumefanya na tunafanya kinyume chake, sifa na starehe za dunia ndio agenda kuu, na kuitafuta Akhera ni ziada!

## Lengo la Elimu kwa Maswahaba

Maswahaba walisoma kwa lengo la kutaka kumjua Allah na kujua mipaka yake. Wajue wanapaswa kufanya nini kupata radhi zake na yepi yatawaongezea hadhi mbele ya Mola wao na wakahangaika kuyatekeleza kwa siri na kwa dhahiri, mchana na usiku. Hawakutafuta elimu kwa ajili ya kutafuta sifa na ukubwa, ushabiki, kuheshimiwa, uwezo wa kujenga hoja na kubishana wala kutengeneza makundi na mifarakano. Kwa wanazuoni wetu wa zama zetu, haya ya (kutafuta sifa na ukubwa, ushabiki, kuheshimiwa, uwezo wa kujenga hoja na kubishana na kutengeneza makundi na mifarakano) ndiyo ajenda. Pamoja na tofauti ya uelewa baina ya maswahaba, waliowaona maswahaba na wale waliowaona waliowaona maswaha; bado tofauti zao hazikuweza kuwafanya wawe maadui. Na hii ni kwa sababu walikuwa wakisoma kutafuta radhi za Mola wao Mlezi.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa Rehema zake na Huruma yake, Ajaaliye kila msomaji wa kitabu hiki aelewe, azingatie na afuate mwenendo wa Mtume na maswahaba ili kupata radhi za Allah! Amin

## Mama Yake Mtume na Walezi Wake

**Aminah Bint Wahab**

**Bi Halimah As-sa'diyah**

**Ummu Ayman, Barakah**

**Fatmah binti Asad ibn Hashim**

# Aminah Bint Wahab

Kwa hakika na yakini, Mfuko wa uzazi wa Bi Aminah Bint Wahab ulikuwa ni mfuko wa uzazi Mtukufu na wenye heshima kuliko mifuko yote ya uzazi.[1] Ilikuwa katika mfuko huu wa uzazi mimba Tukufu ya Mjumbe wa Allah ﷺ ilitunga.

Mbegu hii imepitia katika uzazi wa wanaume, kizazi baada ya kizazi. Mwenyezi Mungu kwa Utukufu na Hekima Yake Aliamrisha mbegu hii ipitie kwa Abdullah Ibn Abdul Muttalib. Kijana wa Kikureish aliyekuwa amewazidi wenzake Utukufu na uzuri. Katika macho yake kulikuwa na Nuru ya Mtume ﷺ inang'ara. Abdullah ndiye aliyefidiwa asichinjwe, baada ya Baba yake kuweka nadhiri ya kumtoa kafara kwa kutimiza ahadi yake. Kwa hili, Abdullah alikuwa mtu wa thamani kubwa ambae hajapata kutokea au kuwepo miongoni mwa Waarabu.

Tukio hili lilitokea ili Utukufu na matakwa ya Mwenyezi Mungu udhihirike, na mizizi ya matakwa haya ionekane katika Historia ya Mwanadamu. Na upatikane ushahidi wa Utukufu wa Maamuzi ya Mwenyezi Mungu na uchaguzi Wake. Hakuna mabadiliko katika Maneno Yake, na hakuna anayeweza kuzuia maamuzi Yake.

۞ إِنَّ ٱللَّهَ ٱصْطَفَىٰٓ ءَادَمَ وَنُوحًا وَءَالَ إِبْرَٰهِيمَ وَءَالَ عِمْرَٰنَ عَلَى ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٣٣﴾ ذُرِّيَّةًۢ
بَعْضُهَا مِنۢ بَعْضٍ ۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٣٤﴾

***"Hakika Mwenyezi Mungu Alimchagua Adam na Nuhu na kizazi cha Ibrahimu na kizazi cha Imran (Baada yake Musa, na Imran mwengine aliye baba yake Maryam) Juu ya walimwengu wote (wa zama zao)"* (3:33-34).**

[1] Tunasema hivi kwa sababu ulikuwa mfuko wa uzazi uliobeba mtu ambaye ni Mtume, kiongozi na Mjumbe wa mwisho wa Allah. Hii haimaanishi kwamba hatuamini kuwa Maryam Bint Imran (Mama wa Issa عليه السلام) alikuwa mbora wa wanawake wote.

Abdullah alitoka kwenda nje ya nyumba na baba yake – Abdul - Muttalib, baada ya kukombolewa kutoka katika kadhia ya kutaka kuchinjwa. Alitoka na hali akizidi kuongezeka Nuru. Mwanamke kutoka Bani Asad Ibn Abdu Uzza akakutana naye pembezoni mwa Ka'abah, baada ya kuuangalia uso uliokuwa unang'aa na Nuru ya Ki-Utume, akamwambia, "*We utapewa mfano wa Ngamia waliotolewa kafara kwa kukombolewa kwako kama utaingiliana na mimi sasa hivi."*

Abdullah akamjibu, 'bora nife kuliko kufanya kitendo haramu.' Na kwa majibu hayo mtu huyu Mtukufu aliuhifadhi na kuulinda Utukufu wa Dini.

Abdul-Muttalib mwishowe akamchagua Bi Aminah Bint Wahb, wa kabila la Zuhr, kuwa mke wa mtoto wake, Abdullah. Amina baada ya hapo akawa ni mmoja wa wanawake wa kikureishi katika ukoo wa wenye hadhi.

Mwangaliaji wa matukio kutoka Tibalah, Fatma Bint Murr Al-Kath'amiyah, pia alimuona Abdullah. Mwanamke huyu alikuwa mzuri sana miongoni mwa wanawake wazuri wa kiarabu wa zama hizo na alikuwa msafi na mwenye tabia nzuri. Aliiona Nuru ya Utume katika uso wa Abdullah. Na yeye akajitoa mwenyewe ili aolewe na Abdullah, lakini Abdullah alilikataa ombi lake.

Habari za Mtume atakayekuja kutokana na watoto wa Nabii Ismail عليه السلام zilikuwa zimezagaa kote Arabuni. Hii habari iliyozagaa inatokana na watu wa vitabu vilivyopita, waliokuwa wanahadithia yale yaliyokaririwa katika Taurat, na pia watu waliyahadithia yale yanayotoka kwa watabiri na wataalamu wa nyota kuhusu kuja kwa Mtume.

Kutokana na mazingira yaliyomzunguka Abdullah Ibn Abdul-Muttwalib kuhusu maisha yake ya ujana, malezi bora aliyopata na tabia zake nzuri, ilimpelekea kuwa ni mtu mwenye mvuto. Hali hii ya tabia zake nzuri alizokuwa akijulikana nazo, ziliwafanya baadhi ya wanawake na wasichana kutamani kupata ridhaa yake, kuwa naye kwa ajili ya kushikamana naye, ili awe mke wa mmoja wao. Lakini Mwenyezi Mungu Alivyotaka na maamuzi Yake ni Bi Amina awe mke wa Abdullah.

Mfuko wa uzazi wa Amina ulikuwa karibu utabeba mimba ya Mtume, na mfuko huu wa uzazi ukabeba amri iliyokusudiwa kwa ajili hiyo. Na mwisho

wa uhakika upo katika uwezo wa Allah, ambaye Anaamrisha Analolitaka kama Anavyopenda.

Wakati ujauzito wa Bi Aminah ulipokuwa upo na miezi michache; Abdullah akapata safari iliyomchukua kwenda Syria.[1] Wakati alipokuwa njiani anarudi maradhi yakampata na akakaa na Ami zake wa kabila la Najjar huko Yathrib, ambako walimuuguza na kumwangalia.

Hata hivyo, Abdullah akafariki kutokana na ugonjwa aliokuwa nao, na akamuacha mkewe aliyekuwa kijana – kuwa mjane. Bi Aminah akawa yupo katika msiba mkubwa uliosababishwa na kifo cha mpendwa mumewe, ambaye alikaa naye katika Ndoa miezi michache tu. Alilia kwa uchungu na kuwa na masikitiko makubwa.

Utengano huo ulikuwa mchungu sana, na uchungu ulizidi kwa kuwa na kiumbe alichobeba tumboni mwake (mimba ya Mtume ﷺ). Kiumbe ambacho tayari kilikuwa ni Yatima kabla hakijazaliwa na kabla ya kufungua macho na kuuona ulimwengu. Na hivyo ndivyo lilivyo daraja lake la kisaikolojia katika uchungu. Lakini alikuwa analo liwazo: moja ni yeye mwenyewe. Alikuwa ni mwanamke mwenye moyo wenye subira na uvumilivu wa hali ya juu. Pia alipata mtu wa karibu wa kumliwaza, naye ni Abdul-Muttalib. Abdul-Muttalib alimwangalia, kumtunza na kumpa huruma zake zote. Hakumuacha hata kwa sekunde; ila pale alipokuwa na kazi zake binafsi.

Liwazo lake lingine kubwa kabisa lilikuwa ni kwa mtoto wake (Mtume ﷺ) aliye tumboni. Hakuhisi aina yoyote ya taabu au usumbufu, wa kimwili au wa kisaikolojia. Namna alivyokuwa akihisi ni kinyume na haya. Alikuwa katika hali ya kuridhia na utulivu. Alikuwa akijihisi ni mtu mwingine tofauti na hali yake na hali ya wanawake wengine wakiwa wajawazito; kwa sababu alikuwa si mtu mwenye kuihitaji dunia na vitu vyake.

Kuna Mtu alimjia usingizini na akamwambia, 'una mimba ya kiongozi na Mtume wa Ummah huu kutoka kwa Allah.' Na huyo Mtu alimjia tena kabla ya

---

[1] Syria kutokana na Kijiografiya ya Waarabu na usemi wa utambuzi wao ilikuwa ni jimbo linaloambatanisha Palestina na Jordan, na kwa wakati huu wa sasa ni Syria na Lebanon. Na mji wa Gaza, katika mwambao wa Pwani ya Palestina, ilikuwa miji mikubwa kwa Makureish za biashara za kwa mara kwa mara.

kujifungua na akamwambia, ‘Sema baada ya kujifungua; “*Naomba hifadhi ya huyu mtoto kutoka kwa Yeye Mmoja (Allah) katika kila uovu na hasadi ya viumbe.”* Na baada ya kujifungua mpe jina la Muhammad.

Hivi ndivyo Bi Aminah alivyoendelea kuziona ndoto, zaidi ya ndoto moja, na zote zilikuwa zikimpa bishara njema, kumpa nguvu na faraja ili awe mwenye kusubiri na mstahamilivu, na kumliwaza katika ujauzito wake.

Siku ya kujifungua kwake ilikuwa siku adhimu, ilikuwa siku ya tarehe 12 katika mwezi wa *Rabee'ul – Awwal*, masaa ya Alfajiri. Muda huo ulikuwa na maana na umuhimu; ulikuwa na kipimo cha mstari wa upeo wa wakati, ulikuwa mpambazuko wa kuondoa giza katika jamii ya Binadamu, mkusanyiko wa giza uliosababisha Binadamu kupotea na kutoka katika njia iliyonyooka. Giza lilosababishwa na mikono ya Binadamu na udhalilishaji wake kwa Binadamu wenzake.

Ndiyo! Ulikuwa ni msimu wa masika (chipuko) baada ya baridi, dharuba na radi zinazotokana na baridi; na baada ya Giza lililotokana na mawingu. Ilikuwa ni wakati wa Masika kabla ya fukuto la kiangazi na kabla ya ukame na mabadiliko ya mazingira yanayokuja na Msimu wa Vuli.

Aminah akasema, “Nilipokuwa namzaa mtoto, nuru ilitoka pamoja naye. Nuru ambayo iliangaza kilicho baina ya Mashariki na Magharibi. Mwangaza wa Nuru hii uliangaza Mahekalu na Masoko ya Syria, mpaka nikawa naona shingo za Ngamia zilizopo katika mji wa Basra. Pia, nikaona bendera tatu zilizosimamishwa, moja Mashariki, moja Magharibi na ya tatu juu ya Ka'abah.”

Abdul-Muttalib, Babu yake Mtume, alikuja na kumchukuwa mtoto Muhammad mpaka kwenye Ka'abah, huku akizunguka naye na akisema, ‘Atukuzwe Allah Aliyenipa mimi huu Utukufu, wa kumpata mtoto huyu, mimi namuomba Allah Amlinde mtoto huyu.”

Baadhi ya hayo yaliyotajwa yameelezwa na Bi Aminah kwa Bi Halima, wa kabila la Bani Sa'd, ambaye alikuwa mlezi wa Mtume alipokuwa Mtoto mchanga.

Tutayazungumzia maisha yake, Inshaallah.

Hapa ndipo Bi Haleemah Bint Abi Dhu'ayb alipoingia katika maisha ya Muhammad kama mama yake wa pili.

Kabla hatujaendelea na mazungumzo ya maisha yake na mambo aliyoyafanya inatuhitaji tueleze maziwa ya mwanzo yaliyoingia katika Tumbo la Mtukufu Mtume.

Maziwa ya mwanzo yalitoka kwa Thuwaybah. Yeye alikuwa ni mtumwa, aliyeachwa huru na Ami yake Mtume, Abu Lahab (Abdul – Uzza Ibn Abdul – Muttalib). Abu Lahab alipata majonzi mazito alipofiwa na ndugu yake Abdullah, ambaye alikuwa akimpenda sana. Kwa hivyo, Thuwaybah alipomjia na bishara njema ya kuzaliwa Muhammad, alikuwa ni mwenye furaha kubwa na akamwacha huru Thuwaybah. Na hii ilikuwa ni tabia ya watukufu wa kiarabu na ndiyo utukufu wao na ufahari wao.

Inaonekana kuwa Thuwaybah alikaa na Bi Aminah, baada ya kujifungua, kwa muda wa siku chache. Bi Thuwaybah pia alikuwa amejifungua Mtoto, kwa hivyo mtoto Muhammad alinyonya ziwa lake mpaka alipokuja Bi Haleemah kumchukuwa kutoka kwake.

Nafasi ya Bi Haleemah katika malezi ya Mtume, katika utoto wake, yalikuwa na umuhimu wa kipekee katika makuzi ya Mtume. Nyakati mbili za kukaa kwake, katika makazi ya Bani Sa'd, yalikuwa na matukio mbalimbali muhimu katika maisha ya Mtume ﷺ.

# Bi Halimah As-sa'diyah

Kunyonyeshwa watoto na wanawake ambao sio mama zao wa kuwazaa na kuwaruhusu watoto hao kukuwa majangwani ilikuwa ndiyo tabia na mwenenedo wa watu watukufu, wa Daraja la juu, miongoni mwa Waarabu kabla ya Uislamu.

Bi Haleemah alikuja Makkah pamoja na wanawake wengine, kutoka katika kabila la banu Sa'd, kwa lengo la kutafuta watoto wa kunyonyesha. Kila aliyekuja alifanikiwa kupata mtoto, wa kumnyonyesha, isipokuwa Bi Haleemah.

Bi Haleemah anasema, "Kulikuwa hakuna mwanamke miongoni mwetu ambaye hakupewa fursa ya kumnyonyesha Mtume wa Mwenyezi Mungu, lakini punde tu, pale alipoambiwa kuwa ni Yatima, kila mtu alimkataa, na kusema, 'kitu gani mama yake atatupatia (kwa maana mama hana malipo mazuri), na sisi tunataraji malipo mazuri kutoka kwa Baba yake?" Kwa uwezo wa Allah, wenzangu baadhi yao waliweza kupata watoto wa kuwanyonyesha ila mimi, niliposhindwa kufanikiwa kupata mtoto wa kumnyonyesha, nikamwambia mume wangu, Al-Harith Ibn Abdul – Uzza, kwa uwezo wa Allah! sitaki kuwa miongoni mwa watakaorudi nyumbani na kuwa katika waliokosa mtoto wa kumnyonyesha. Nimeamua nimchukue yule mtoto Yatima."

Mume wangu akasema, "nenda kamchukuwe huenda Mwenyezi Mungu Akatubariki kupitiya kwake." Nikaenda nikamchukuwa yule mtoto. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nilimchukua tu kwa sababu sikuweza kupata mtoto mwengine.

Bi Haleemah akaendelea kuhadithia, "nilipomchukua na kuenda naye katika kipando changu (Ngamia) nilimnyonyesha kwa kadri Mwenyezi Mungu alivyo niwezesha na yeye akanywa mpaka akaridhika. Na ndugu yake pia akanywa mpaka akaridhika."[1] Mume wangu alienda kumkamua ngamia wetu,

[1] Anamaanisha mtoto wake aliyekuwa umri sawa na Muhammad ﷺ.

aliyekuwa mkongwe, na sote mimi na yeye tukanywa maziwa ya ngamia huyo mpaka tukashiba, na usiku ukapita vizuri hali ya kuwa tumeshiba na tumeridhika.

"Asubuhi, Mume wangu akaniuliza, "Haleemah kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu! naona umemkubali mtoto mwenye Baraka, Je hujaona Baraka zake tunazozipata toka tulipomchukuwa, na bado Mwenyezi Mungu Anazidi kutuzidishiya Baraka?"

"Tukaendelea na safari yetu ya kuelekea Kijijini kwetu. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, Punda wangu alitembea kwa haraka sana mpaka nikawapita wenzangu na wakashindwa kunifikia. Kwa mshangao wao katika hili wakaniuliza, 'Ewe binti wa Abu Dhu'ayb! ... je huyu ni yule yule Punda wako tuliyesafiri naye kabla?' Nikajibu, 'Ndiyo, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ndiyo huyu huyu!" Halafu wakasema, "Kwa uwezo wa Allah tunahisi kuna jambo lisilo la kawaida kuhusu huyu Punda wako!"

Tulipowasili katika Ardhi ya Banu Sa'd na kabla ya hapo sijapata kujuwa Ardhi iliyokuwa kame na kavu kuliko Ardhi hii yetu – ikawa sasa Kondoo wangu huwa wanapata lishe ya kutosha ya nyasi za kutosha na wanarudi hali ya kuwa wameridhika kwa kushiba na wanakuwa na wingi wa maziwa. Tunawakamua maziwa tunavyotaka na hakuna majirani katika majirani zetu wenye kupata maziwa hata tone kutoka kwa kondoo wao. Kondoo wao walikuwa wanapelekwa malishoni na wakirudi bado ni wenye njaa. Majirani zangu sasa ikawa wanawaambia wachungaji wao, angalieni na muwe mnachunga kondoo wanapochungwa kondoo wa Bi Haleemah. Na juu ya hivyo bado Kondoo wao wakawa wanarudi matumbo yao ni matupu na wenye njaa na wetu sisi wanarudi wameshiba, wameridhika na ni wenye kutoa maziwa. Mwenyezi Mungu akaendelea kutuonesha Baraka zake kwa uwazi ili tuzitambue na tuzifahamu.

Mtoto Muhammad alikuwa ni mwenye kukua kwa njia tofauti na watoto wengine; kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu alipofikia umri wa miaka miwili alikuwa na ngozi ya kunesa na kunepa. Na tukamrudisha kwa mama yake, hali ya kuwa hatuko radhi na pia kujutia kwa kuwa tutapoteza Baraka zake zilizotujia katika nyumba yetu kupitia yeye.

Mama yake alipomuona, tulimueleza, 'tunakuomba utuachie mwanao tukae naye kwa mwaka mmoja zaidi, tunaogopa maradhi ya milipuko ya hapa Makkah yasije kumuathiri." Tukaendelea kumuomba na kum-bembeleza mpaka akakubali turudi naye.

"Baada ya miezi miwili au mitatu baada ya kurudi naye, jambo la ajabu likatokea. Yeye na ndugu yake wa kulelewa walikuwa nyuma ya nyumba pamoja na Kondoo wetu, ambapo ndugu wa kulelewa alikuja mbio kwetu huku akisema kwa mshangao, "Ndugu yangu wa Kikureshi amejiwa na watu wawili waliovaa nguo nyeupe, wamemlaza chali na kumfungua (kumpasua) kifua."

"Baba yake wa kumlea na mimi tukaenda mbio, tukamkuta amesimama na rangi ya mwili wake imebadilika. Baba yake wa kumlea na mimi tukamkumbatia na kumuuliza, "mtoto wangu, nini kimekutokea?' Muhammad akajibu; 'watu wawili waliovaa nguo nyeupe walinijia mimi wakanilaza na kukifungua kifua changu na wakatoa kitu ndani ya kifua changu, na kukiondosha, halafu wakakirudisha kifua changu kama kwamba hawajanifungua." Sisi tukamchukua na kurudi naye nyumbani.

Baba yake wa kumlea akasema, "Haleemah, mimi naogopa ya kuwa mwanangu ameguswa na Jini kwa hivyo ni bora tumrudishe kwa familia yake kabla chochote kibaya hakijamtokea."

"Hivyo tukamrudisha kwa mama yake. Alipotuona, mama yake akashtuka na kutuuliza, 'kitu gani kimekurudisheni enyi wazazi walezi? Nyinyi mumemlea kwa uangalizi na ufanisi wa hali ya juu!" Nasi tukamjibu, "kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu hakuna jambo limetokea. Mwenyezi Mungu ametusaidia sisi kulipa madeni yetu, na sisi tunamuogopea lisije jambo baya likamtokea; ndio maana tumemrudisha."

"Mama yake hakutuamini. Akaendelea kusisitiza tumuambiye ukweli, na tulivyomwambia ukweli wa yaliyotokea, akasema, "Hivyo nyinyi mumeogopa kuwa anaweza kuguswa na Shetani?" Akasema, 'Hapana! kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu! Shetani hawezi kupata njia ya kumfikia. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kuna jambo kubwa kuhusu mtoto wangu huyu. Je, nikuambieni kitu kuhusu yeye?" Tukasema, "ndiyo tuambie." Na yeye akatuhadithia, 'nilipokuwa mja mzito na mimba yake, nilihisi kuwa sijabeba kitu ambacho chepesi kuliko yeye; na niliona katika ndoto nuru iliyokuwa ikitoka

kwangu iliyong'arisha mahekalu ya Syria. Na nilipojifungua kwangu kulikuwa tofauti na kwa watoto wengine. Alitoka katika njia ya uzazi kwa kujisaidia mwenyewe, kwa mikono yake mwenyewe na huku kichwa chake kikiangalia mbinguni. Basi msimuogopee chochote."

Hivi ndivyo Bibi Halimah رضي الله عنها alivyoachana na mtoto wake maalumu wa kumlea.

Baadaye katika maisha yake, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alizungumzia upekee wa kifani wa utoto wake, upekee wa ajabu, na namna alivyoelewa mambo, taswira na majina wakati alipokuwa akiishi na Bani Sa'd. Kuna idadi kubwa ya Maswahaba wake – رضي الله عنهم waliohadithia matukio haya ya utoto wake.

Mwisho wa vita vya Hunein, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokea Ngawira na mateka kutoka Hawazin, kama mali iliyotekwa vitani. Kundi la wajumbe kutoka Hawazin ambao walikwishasilimu, walimjia katika mahala panapoitwa Ji'ranah na wakamwambia, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!, sisi ni watu kutoka makabila mbalimbali, tumeguswa na balaa, tunakuomba utupe msamaha, na Mwenyezi Mungu Atakupa wewe kheri nyingi."

Dada yake wa kulelewa naye, Shayma, alikuwa ni mmoja wa mateka, akaja kwa Mtume ﷺ, kumuomba amwoneshee na kumuonea huruma, na akamkumbusha jinsi siku moja alivyomuuma na meno alipokuwa mgongoni kwake, alipo kuwa analelewa katika makazi ya Bani Sa'd. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliposikia hilo, akatandika kishali chake katika Ardhi, kwa ajili yake na akamwomba akae ubavuni mwake karibu naye.

Msemaji wa ujumbe, Zuhair Ibn Sard, akasimama na akasema; "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Shangazi zako na mama zako, ambao walikulea, ni miongoni mwa mateka ambao wamo ndani ya eneo lililozungushwa kwa ajili ya mateka. Na kama sisi tulimlea Abi Shammal au Nu'man Ibn Mundhir halafu jambo likatutokea sisi kutoka upande wako na likatutokea sisi kutoka kwao sisi kwa uhakika, matumaini na matarajio kutoka kweko ni matendo mema ya upole, huruma, utu na wema. Na wewe ni mbora wa wale walio-lelewa na mama walezi. Baada ya hapo wakasoma shairi na kumsifu Mtume ﷺ kuonesha upendeleo kwa watu wake waliomlea.

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema, "Sehemu ya Ngawira ambayo ni sehemu yangu na watoto wa Abdul Muttalib, yote ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na nyinyi."

Na Ma-Ansar wakasema, "chochote kinachotokana na sisi ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake."

Siku hiyo kwa hakika ilikuwa ni siku ya kupeana zawadi na kutendeana mema; na namna ilivyo siku hiyo ilikuwa ni siku yenye kuwakilisha utukufu, ubora na uzuri wa maadili katika ubora wake.

Mtume Muhammad ﷺ akarudi katika uvuguvugu wa kifua na moyo wa mama yake na huruma ya uangalizi wa babu yake "Abdul Muttalib"

Na alikuwa kishakuwa kijana mdogo ambaye uso wake Mtukufu ulijaa nuru yenye kuangaza, uonekano wake ulimletea fahari, ubora na utukufu. Moyo wake ulijazwa na alama za uongozi. Ulimi wake ulijaa maneno ya ukarimu, yaliyo matamu. Haya yote ni matokeo ya malezi ya Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka.

Bi Aminah رضي الله عنها alikuwa akimkumbatia mwanawe mpenzi. Na alikuwa anapata hisia za raha na utulivu alizokuwa anapata wakati mtoto alipokuwa bado yupo tumboni, na katika hali hii alikuwa ni mwenye kuhisi furaha, raha na amani ya hali ya juu.

Babu yake, Abdul Muttalib, kiongozi wa Makureish, hakuweza kustahamili kutokuwepo kwa Muhammad, na hakuchoka wala kuona taabu kumtafuta. Abdul Muttalib alikuwa ni mwenye kumtembelea mjukuu wake nyumbani kwa Bi Aminah, kila siku Asubuhi na jioni, na siku zingine zote. Na alikuwa akimuuliza "Vipi mtoto wangu Muhammad hajambo? Alikuwa akimbeba na kumkumbatia kwa mapenzi makubwa. Kwa kupitia Muhammad alikuwa akimuona mwanawe Abdullah, ambaye alifariki yu hali ametoka tu katika Ndoa, na kifo chake kilimletea na kumpa majonzi makubwa yasio na mfano. Abdul Muttalib aliona kwa mjukuu wake sifa na tabia za ajabu zilizomuongezea mapenzi zaidi kwake.

Muhammad ﷺ alipofikia umri wa miaka sita, mama yake akaomba ruhusa kutoka kwa babu yake Abdul-Muttalib, amchukuwe mwanawe kwenda naye Yathrib ili akazuru kaburi la mpenzi mumewe - Abdullah, na atumiye

baadhi ya masiku kuwaona na kukaa na mama zake wadogo wa kabila la Banu Najjar. Akampa ruhusa ya kumchukua na akamshauri ajiangalie kwa uzuri yeye mwenyewe na mtoto wake.

Bi Aminah akaondoka na mtoto; akifuatana na mfanyakazi wake Bi Barakah, ambaye alikuwa akimtumikia na kumwangalia mwanawe. Muhammad ﷺ alimpenda Bi Barakah na akimchukulia ni mmoja katika familia yake.

Bi Aminah alipofika katika kaburi la mumewe, alihisi uchungu na majonzi alipokuwa amesimama kando ya kaburi hilo, akijawa huzuni kubwa na kububujikwa na machozi, hali mtoto wake Muhammad yupo pembeni yake anaangalia. Naye katika mashafu yake tukufu, matone ya machozi yalionekana yanabubujika kama Lulu inayotiririka chini – kutokana na kuona huruma na huzuni ya mama yake; na kutokana na majonzi ya kifo cha baba yake ambaye hajawahi kumuona.

Ilitokea kuwa Homa iliyokuwa inaenea katika mji wa Yathrib ilimuambukiza Bi Aminah kabla hajaondoka Mjini Yathrib. Lakini hakuihisi mpaka alipokuwa njiani akirudi Makkah. Hali yake ilidhoofika sana, na alipofika katika kijiji kinachoitwa Ab'wa, akazidiwa na ugonjwa na akavuta pumzi yake ya mwisho (Akafariki).

Muhamamd ﷺ alilia kwa uchungu mkubwa na Malaika mbinguni pia walilia pamoja naye kwa kumhurumia.[1] Walilia kwa kumuonea huruma, kwa kuwa alipoteza wazazi wake wote wawili, katika hali ya utoto. ukiwa na upweke alioupata.

Tamati ya mama yake, Aminah bint Wahab, ikaishia hapo; na kijana mtoto Muhammad ﷺ akachukuliwa haraka kurudi Makkah na yule mwanamke, Barakah, aliyeachiliwa huru na wezee wake (Muhammad ﷺ).

[1] Hii ni kutokana na Riwaya nyingine.

# Ummu Ayman, Barakah

## Ewe mama yangu! Hakika Una nafasi yako Peponi!

Kama unataka kumtafuta mwanamke muhimu wa Kiislamu ili umzungumzie, basi bila shaka utakwenda kuitafiti historia ya Mtume Muhammad ﷺ, na hapo ndipo utakutana na Ummu Ayman رضي الله عنها, aliyefahamika pia kwa jina la Barakah. Mama ambaye Mtume ﷺ alikuwa akimtaja na akimwelezea kama "Mama baada ya mama yangu mzazi."

Barakah au Ummu Ayman رضي الله عنها alikuwa ni mama ambaye Mtume ﷺ alimthamini na kumuheshimu sana. Mama huyu alikuwa wa kwanza kumpokea Mtume ﷺ katika mikono yake pale Mtume ﷺ alipozaliwa, na ndiye mama ambaye Mtume ﷺ alimfahamu mpaka anafariki dunia. Huyu ni miongoni mwa akina mama wachache ambao Mtume ﷺ aliwahakikishia nafasi katika Pepo.

"Kuwa mama yake, Barakah. Nakuomba usimuache mwanangu," Haya yalikuwa ni maneno ya mama wa Mtume ﷺ, bi Amina akimwambia mama huyu (Barakah) wakati mama wa Mtume (bi Amina) akiwa anaaga dunia!

Ummu Ayman رضي الله عنها alizingatia usia aliopewa na bi Amina, na alitekeleza wajibu wake.

Mwanzo maisha ya mama huyu yalikuwa ni ya furaha. Akiwa kijana, mama huyu wa kihabeshi (mwafrika), aliuzwa kama Mtumwa pale Makkah. Kabla ya kuja Uislamu, biashara ya utumwa ilikuwa jambo la kawaida, na watumwa walikuwa wakiangaliwa sawa na wanyama. Lakini mama huyu, Barakah, alipata bahati akawa akitendewa wema na wale waliokuwa wakimmiliki. Ummu Ayman (Barakah رضي الله عنها) alikuwa amenunuliwa kama mtumwa na mtu mmoja mkarimu aliyefahamika kwa jina la Abdullah ibn Abdul Muttalib, ambaye ndiye baba wa Mtume ﷺ.

Barakah sio tu kwamba alikuwa na jukumu la kuangalia mambo yaliyoihusu nyumba ya Abdullah, bali alikuwa na jukumu la kumuhudumia bibi Amina, mama wa Mtume ﷺ baada ya kuwa ameolewa na bwana Abdullah (baba yake Mtume - ﷺ).

Ni mama huyu Ummu Ayman رضي الله عنها, aliyelala pembeni ya kitanda cha bi Amina na kumfariji, wiki mbili tu baada ya kuolewa, na mume wake kutakiwa kusafiri kwenda Syria, safari ambayo bwana Abdullah (baba wa Mtume) hakurejea tena nyumbani, bali alifariki akiwa huko. Ni mama huyu, Ummu Ayman (Barakah) aliyemuhudumia bi Amina (Mama wa Mtume - ﷺ) wakati wa ujauzito wake.

Alikuwa ni mama huyu, Ummu Ayman رضي الله عنها aliyempa habari bi Amina juu ya kifo cha mume wake kilichotokea huko Yathrib, (Hakujua kuwa mwanae pia angekuja kufariki na kuzikwa katika ardhi ile ile) ambayo leo ndio Madinah.

Mtume ﷺ alipokuwa akikabiliana na msiba juu ya msiba, Ummu Ayman alikuwa pamoja naye akimliwaza na kumtia moyo kama mama yake. Toka mama yake Mtume ﷺ alipofariki, wakati huo Mtume ﷺ akiwa na umri wa miaka sita (6), mpaka babu yake Abdul Muttalib alipofariki wakati Mtume ﷺ akiwa na umri wa miaka minane (8), Ummu Ayman رضي الله عنها alikuwa pamoja na Mtume ﷺ .

Ni baada ya Mtume ﷺ kumuoa Bi Khadijah رضي الله عنها ndio na yeye akaolewa baada ya kushauriwa na kusisitizwa kufanya hivyo na Bi Khadijah na Muhammad ﷺ. Ummu Ayman رضي الله عنها aliolewa na Ubayd ibn Zayd رضي الله عنه kutoka kabila la Khazraj la Yathrib (Madinah) na walijaaliwa kupata mtoto waliyemwita Ayman, na hapa ndio akapata jina hili Ummu Ayman رضي الله عنها.

Mtume ﷺ alipopewa Utume, Ummu Ayman رضي الله عنها alikuwa miongoni mwa Waislamu wa mwanzo kabisa kuukubali Uislamu, na kama ilivyokuwa kwa Waislamu wengine wa mwanzo, mama huyu alikabilina na mateso makali kutoka kwa Maquraishi kwa ujasiri mkubwa na subira. Ummu Ayman رضي الله عنها na Zayd ibn Harithah رضي الله عنه, ambaye alikuwa ni swahaba aliyeishi ndani ya familia ya Mtume ﷺ wakajitolea maisha yao na kuyaweka hatarini kwa kuchukua jukumu la kutafuta siri na mikakati ya makafiri dhidi ya Mtume ﷺ na Waislamu. Wakati wa vita vya Uhud, Ummu Ayman رضي الله عنها alikuwa

akiwapa maji wapiganaji wa Kiislamu wenye kiu na kuwahudumia wale waliojeruhiwa. Aliongozana na Mtume ﷺkatika baadhi ya misafara. Alijitahidi kuishi kwa kuzingatia misingi ya Uislamu. Mtume ﷺ alipokwenda kumjulia hali, Mtume ﷺ alikuwa akisema: “Vipi hali yako ewe mama yangu! Hujambo?” na yeye alikuwa akijibu,: “Sijambo ewe Mtume wa Allah, kwa kuwa Uislamu upo salama.”

Mume wa Ummu Ayman رضي الله عنها hakuishi muda mrefu toka wafunge ndoa, alifariki. Wakati Ummu Ayman akiwa na umri wa takriban miaka hamsini (50), Mtume ﷺ alisema wakati akizungumza na maswahaba zake kuwa: “Kama kuna mtu anataka kumuuoa mwanamke miongoni mwa wanawake wa Peponi, basi amuoe Ummu Ayman.” Mara moja Zayd ibn Harithah رضي الله عنه alisimama na kusema yeye yuko tayari kumuoa. Wawili hawa walifunga ndoa, na katika ndoa yao walijaaliwa kupata mtoto waliyemwita Usamah, mtoto ambaye alikuja kujulikana kwa jina, “Mtoto mpendwa wa mpendwa.” Hii ilimaanisha kuwa, Mtume ﷺ aliwapenda wote, Usamah na baba yake, Zayd. Miongoni mwa mambo yanayoonesha kujitolea kwa Ummu Ayman kwa ajili ya Uislamu na Mtume ﷺ, ni kuamua kwake kutembea kwa miguu akivuka jangwa lenye mchanga uliochemka kutoka Makkah kwenda Madinah kuungana na Mtume ﷺ. Pamoja na safari kuwa ngumu na nzito, alivumilia na alipewa habari njema alipofika Madinah. Alipofika Madinah, miguu ikiwa imevimba, akiwa amejaa vumbi miguuni na kwa hakika mwili mzima, Mtume ﷺ akamwambia: *“Ewe Ummu Ayman! Ewe mama yangu! Hakika unanafasi Peponi!”*

Ummu Ayman رضي الله عنها alirudi kuwa mjane baada ya mume wake Zayd kuuwawa shahidi katika vita vya Mutah vilivyotokea nchini Syria. Ummu Ayman aliishi na kushuhudia mwanae pia akiuwawa shahidi katika vita vya Hunayn. Ummu Ayman رضي الله عنها aliendelea kuishi mpaka akashuhudia “mwanae mwingine”, Mtume ﷺ (si mwanae wa kuzaa, bali kwa heshima aliyopewa) akifariki. Ummu Ayman رضي الله عنها alilia sana baada ya Mtume ﷺ kufariki. Alipoulizwa kwanini alikuwa akilia kiasi kile, Ummu Ayman رضي الله عنها alijibu kuwa “Naapa kwa jina la Allah kuwa, nilijua Mtume ﷺ siku moja atakufa; lakini nalia kwa sababu najua kuwa sasa hatutopokea tena Wahyi kutoka kwa Allah kwa ajili yetu.”

Ummu Ayman رضي الله عنها alifariki wakati wa Ukhalifa wa ‘Uthman Ibn Affan رضي الله عنه.

# Fatmah binti Asad ibn Hashim

## Aliyevikwa Nguo na Mtume ﷺ

Fatmah bint Asad رضي الله عنها, huyu ni mama wa Khalifa wa nne wa Waislamu, Ali Ibn Abu Talib رضي الله عنه, na mama mkwe wa mtoto wa Mtume ﷺ, Fatmah bint Muhammad. Mama huyu alizaliwa mwaka 570, takriban mwaka ambao Mtume ﷺ alizaliwa. Wajukuu wa mama huyu ni Hasan na Husain ambao pia ni wajukuu wa Mtume ﷺ; na watakuwa viongozi wa vijana wa Peponi. Mbali ya Ali رضي الله عنه, mama huyu alikuwa na watoto wengine wawili wa kiume, ambao ni Ja'far na Tayyir. Ja'far رضي الله عنه alikuwa kamanda maarufu wa majeshi ya Waislamu. Ja'far رضي الله عنه aliyaongoza majeshi ya Waislamu katika vita vya Mu'tah na aliuwawa shahidi katika vita hivi.

Wakati Mtume ﷺ alipokuwa mtu mzima na kuweka wazi kuwa yeye (Muhammad ﷺ) ni Mtume wa mwisho wa Allah, Mama huyu (Fatmah bint Asad) alimuunga mkono na kumkubali moja kwa moja na kusimama imara pamoja na Mtume Muhammad ﷺ. Udhalilishaji, vitisho na mateso havikuweza kubadili msimamo wake kwa namna yeyote ile. Mama huyu alikuwa akimpenda sana kupita kiasi mwanae Ja'far رضي الله عنه, hata hivyo, kutokana na Uislamu, mama huyu alikubali kutengana na mwanae huyu pamoja na mke wake, Asma bint Umays wakati Mtume ﷺ alipowataka wahame pamoja na kundi la Waislamu na kuelekea Uhabeshi ambayo kwa sasa ndiyo Ethiopia.

Fatmah bint Asad رضي الله عنها, kwa kuwa kwake miongoni mwa Waislamu wa mwanzo kuukubali Uislamu, kusilimu na kuchukua kiapo cha utii kwa Mtume ﷺ, alikabiliana na vikwazo vya kiuchumi na kijamii kutoka kwa Maquraishi wakati ule wa *Shi'ab* Abi Talib kwa miaka ile mitatu iliyokuwa migumu kwa Waislamu. Mama huyu pia alikuwa miongoni mwa kundi la Waislamu lililopata bahati ya kuhamia Madinah.

Abdul Muttalib, alikuwa mtu mwenye kubagua sana, baada ya kumchunguza mama huyu Fatmah bint Asad رضي الله عنها na kutambua kipaji na uwezo aliokuwa nao mama huyu, alipendekeza Fatmah bint Asad رضي الله عنها aolewe na mwanae Abu Talib. Wakati Mtume ﷺ alipoambiwa na Allah aanze kueneza ujumbe wa dini ya Kiislamu kwa ndugu na jamaa zake wa karibu, ni mama huyu aliyekuwa miongoni mwa watu wa mwanzo kabisa kuukubali wito wa Uislamu na kuchukua ahadi ya utii kwa Mtume ﷺ. Baada ya babu yake Mtume ﷺ, Abdul Muttalib kufariki, ulezi na uangalizi wa mtoto aliyekuwa yatima kwa wakati huo, Muhammad ﷺ ulihamia kwa Abu Talib. Mke wa Abu Talib, Fatmah bint Asad رضي الله عنها, alimlea Mtume Muhammad ﷺ kwa mapenzi makubwa sana kana kwamba alikuwa mwanae wa kumzaa. Mtume ﷺ alikuwa akikumbuka masiku ambayo mama huyu alikuwa akishinda bila kula, ili kichache kilichokuwepo aweze kula yeye (Mtume wa Allah) – hapo ilikuwa hakuna anayejua kuwa mtoto huyu yatima siku moja atakuja kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mtume ﷺ alimuheshimu sana mama huyu kiasi kwamba mama huyu, Fatmah bint Asad رضي الله عنها alipomtembelea Mtume ﷺ, Mtume ﷺ alikuwa akimpokea kwa heshima na mapenzi makubwa na akimwita ‘mama’. Baba yake mdogo pia alikuwa akimpenda sana. Muhammad ﷺ katika utoto wake, alikuwa na tabia njema sana na alikuwa mtoto aliyekuwa msafi muda wote kiasi kwamba Abu Talib alikuwa akimtumia kama mfano na kielelezo kwa watoto wengine.

Mara nyingi watoto wa kiume huwa wachafu kutokana na kucheza michezo mbalimbali na watoto wenzao wa kiume, michezo ambayo mara nyingi huwafanya wachafuke. Lakini hali ilikuwa tofauti kwa Muhammad ﷺ ambaye muda wote alikuwa akionekana msafi na nadhifu. Watu walikuwa wakifurahishwa na namna alivyokuwa kila walipomuona. Abu Talib alikuwa akipenda watoto wote wale chakula pamoja, kwa sababu alihisi kuwa, kwa wao kula pamoja huku Muhammad ﷺ akiwa miongoni mwao, chakula kitatosha na watoto hao hao wakila peke yao, basi hawatatosheka na watabaki kuwa wenye njaa. Mara nyingi Abu Talib alikuwa akimwambia mpwa wake (Muhammad ﷺ) kuwa alikuwa amebarikiwa, kwani daima kulikuwa na vitu vya kutosha anapokuwepo yeye Muhammad ﷺ.

Mama Fatmah bint Asad رضي الله عنها, hakuhisi tabu yeyote katika kumlea mtoto huyu – Mtume Muhammad ﷺ wakati wa utoto wake na hata katika

ujana wake. Katika utoto wake, Muhammad ﷺ aliongozana na baba yake mdogo katika msafara wa kibiashara nchini Syria. Wakiwa njiani, jambo lisilokuwa la kawaida na la kushangaza lilitokea, waliporejea Makkah, Abu Talib alimsimulia mke wake tukio hili.

Mtume ﷺ alianza kuwalingania na kuwaita katika Uislamu Maquraishi wa Makkah; Maquraishi ambao kwa wakati huo walikuwa wakiabudia masanamu waliyokuwa wameyaweka katika Ka'bah. Hawakuwahi kufikiri wala kudhania kuwa siku moja Mtume Muhammad ﷺ atakuja kuyakanusha, kuyakataa na kuyaona masanamu yao ambayo wao walikuwa wakiyaamini na wakiyaabudu kuwa yalikuwa hayana maana wala msaada wowote, na hapo hapo kuwa adui yao mkubwa kwa kuanza kutangaza imani mpya ambayo ilikuwa inaenda kinyume kabisa na dini na imani yao waliyorithi kutoka kwa wazee wao. Walikasirishwa sana na wakala kiapo kuwa watahakikisha wanamsambaratisha Mtume ﷺ na kuufutilia mbali Uislamu.

Ni katika muda huu, makafiri waliamua kutumia mbinu ovu kabisa za vitisho, mateso, ukatili na unyanyasaji wa kila aina kuwakatisha tamaa Waislamu waliokuwa wamesilimu na kuingia katika Uislamu, wakate tamaa, waritadi na kurudi katika ukafiri na kuabudu waliyokuwa wakiyaabudu hapo kabla. Ilikuwa ni kutokana na nguvu na ushawishi aliokuwa nao Abu Talib uliowafanya makafiri washindwe kumfanyia madhara Mtume Muhammad ﷺ. Abu Talib, alisimama imara pamoja na Mtume ﷺ kwa mapenzi makubwa na kumuhami muda wote. Hakuna adui yeyote aliyekuwa na uthubutu wa kumfanya chochote akiwa chini ya uangalizi na hifadhi ya Abu Talib. Mama huyu Fatmah bint Asad رضي الله عنها, alishirikiana vema na Abu Talib na alikuwa akitekeleza wajibu wake kama mama linapokuja swala la usalama wa Muhammad ﷺ. ni kwa sababu hii, haishangazi kuona Mtume ﷺ akimuheshimu sana mama huyu, Fatmah bint Asad رضي الله عنها. Kwa kuzingatia hali ya mashaka na hatari iliyokuwa ikiwakabili Waislamu wa Makkah wakati huo, Mtume Muhammad ﷺ aliona litakuwa ni jambo la busara kama baadhi ya Waislamu watahama na kuelekea Uhabeshi (Ethiopia), nchi ambayo mtawala wake alikuwa akifahamika vema kama mtu mkarimu na mvumilivu kwa imani za wengine.

Kiongozi wa msafara huu wa kuelekea Ethiopia (Uhabeshi) alikuwa ni Ja'far Ibn Abi Talib رضي الله عنه, ambaye alikuwa ni kaka wa Ali ibn Abi Talib (Khalifa

wa nne wa Waislamu), ambaye alikuwa pia mtoto kipenzi wa mama huyu, Fatmah bint Asad رضي الله عنها. Mama huyu alikuwa akimpenda sana mtoto huyu Ja'far; kwa sababu Ja'far رضي الله عنه alikuwa akifanana sana na Mtume Muhammad ﷺ, na alikuwa mtu mwenye busara na maarifa makubwa.

Ja'far رضي الله عنه alikuwa akionekana kana kwamba alikuwa amerithi ufasaha wa lugha na kujieleza kutoka katika familia yao. Alikuwa mtu aliyekuwa na uwezo mkubwa sana katika kufafanua mambo na kuweza kuwashawishi watu kwa hoja zake. Ni kutokana na maarifa na kipaji hiki alichokuwa nacho aliweza kujenga hoja na kumshawishi mfalme wa Uhabeshi wa wakati huo Najash, wakati makafiri wa Makkah walipotuma wajumbe wao kwenda kumshawishi mfalme Najash aliyekuwa amewapokea maswahaba, awakabidhi Waislamu kwa Makafiri.

Maquraishi wakaamua kuwazuia Waislamu katika eneo moja tena dogo na kuwadhibiti wasiende eneo jingine lolote kutafuta mahitaji yao kwa sababu nyingine yeyote. Walihakikisha kuwa, hakuna anayewasaidia au kushirikiana nao kiuchumi wala kijamii. Walikaa katika hali hii kwa muda wa takriban miaka mitatu. Hii yaweza kuwa miaka iliyokuwa migumu zaidi kwa Waislamu.

Kiuchumi, hali hii iliwaathiri sana kiasi ambacho hakikuwahi kutokea hapo kabla. Sauti za watoto zilikuwa zikisikika kila upande wakilia kutokana na njaa, huku watu wazima wakiwaangalia bila kuwa na namna yeyote ya kuweza kuwasaidia na kuishia kububujikwa na machozi. Ili kupambana na njaa kali iliyokuwa ikiwakabili, Waislamu walianza kula majani ya miti na nyasi. Mama huyu, Fatmah bint Asad رضي الله عنها alishuhudia na kuishi katika maisha haya magumu na ya kutisha huku akiwa na subira na uvumilivu wa hali ya juu kabisa, na hakuwahi kutetereka hata kidogo. Miaka kumi baada ya kushuka kwa *Wahyi* kwa mara ya kwanza kwa Mtume Muhammad ﷺ, ukimteua kuwa Mtume wa Allah ﷺ, Allah Aliyamaliza madhila haya ya njaa, kutengwa na mateso makali kwa Waislamu.

Ni katika miaka hii mitatu ya vikwazo vya kiuchumi na kijamii na kuzuiliwa kila aina ya ushirikiano, mama wa Waislamu, mke kipenzi wa Mtume ﷺ na msaidizi muhimu, Bi Khadijah رضي الله عنها, alifariki dunia.

Pigo la kuondokewa na mke huyu kwa Mtume ﷺ lilikuwa kubwa na lililoacha athari kubwa sana. Kabla hata Mtume ﷺ hajarudi katika hali yake ya

kawaida, akiwa bado na simanzi ya kuondokewa na mkewe Khadijah, Mtume ﷺ alikabiliwa na simanzi nyingine kubwa iliyotokana na kufiwa na msaidizi wake na mlezi wake, Abu Talib. Mwaka huu unafahamika kwa jina la 'Mwaka wa huzuni' katika historia ya Uislamu. Ni katika mazingira magumu ya kiwango hiki, mazingira yaliyoandamana na mateso, manyanyaso na kila aina ya madhila, Mwenyezi Mungu Akamuamuru Mtume wake ﷺ ahamie Madinah. Mama huyu, Fatmah bint Asad رضي الله عنها, alikuwa miongoni mwa Waislamu waliohama kuelekea Madinah.

Anas Ibn Malik رضي الله عنه anasema, Mtume ﷺ alipopata habari juu ya kifo cha mama Fatmah bint Asad, Mtume ﷺ alikwenda haraka sana nyumbani kwa mama huyu. Alipofika, Mtume ﷺ akakaa karibu na ilipokuwa maiti ya mama huyu na kumuombea dua. Akisema:

> *"Ewe mama yangu kipenzi! Namuomba Allah Akuweke katika hifadhi Yake. Mara nyingi ulikaa na kushinda na njaa ili mimi nile na kushiba. Ulinilisha na kunivisha vizuri kuliko hata ulivyojilisha na kujivisha mwenyewe. Bila shaka Allah Atakuridhia na kukulipa kheri kwa wema wako huu. Matendo yako yalilenga kutafuta radhi za Mola wako na mafanikio baada ya kufa kwako."*

Mtume ﷺ alitoa nguo yake itumike kama sehemu ya sanda, akisema kuwa, anamuomba Mwenyezi Mungu Amsamehe mama Fatmah bint Asad na amvishe mavazi ya Peponi.

Baada ya kaburi kuchimbwa, Mtume ﷺ alilikagua na kuhakikisha kuwa liko sawasawa, na kwa mikono yake mwenyewe, Mtume ﷺ alimlaza ndani ya kaburi mama Fatmah bint Asad رضي الله عنها. Hivyo mama huyu, Fatmah bint Asad رضي الله عنها alikuwa miongoni mwa watu wachache waliopata bahati ya makaburi yao kukaguliwa na Mtume ﷺ na kisha kwa mikono yake akamzika.

"Fatmah bint Asad رضي الله عنها ni mama mcha-Mungu na mwenye hadhi ya juu, mama ambaye alibashiriwa kuwa ataingia Peponi. Mtume ﷺ alimvalisha nguo yake na kumuombea dua Allah Amkirimu kwa kumvisha mavazi ya Peponi. Bila shaka, Allah Atamridhia na yeye ataridhia yale aliyoandaliwa na Mola wake mlezi.

## Wake za Mtume ﷺ

**Khadijah bint Khuwaylid**

**Sawdah bint Zam'a**

**Aishah bint Abi Bakr**

**Hafsah bint 'Umar**

**Zaynab bint Jahsh**

**Ummu Salamah binti Abi Umayyah**

**Ummu Habibah Ramlah binti Abi Sufyan**

**Juwayriyyah binti al-Haarith ibn Abi Diraar**

**Safiyyah binti Huyay ibn Akhtab**

**Maimunah binti al-Haarith**

**Zaynab binti Khuzaymah**

**Maria al-Qibtiyya**

# Khadijah bint Khuwaylid

Aliyetolewa Salamu na Allah na Malaika Jibril.

Imesimuliwa na Abu Hurairah رضي الله عنه kuwa, Malaika Jibril alikuja kwa Mtume ﷺ na kusema: "Ewe Mtume wa Allah! Huyu ni Khadijah رضي الله عنها, anakujia akiwa na chombo kilicho na kinywaji (au chakula). Atakapokufikia mtolee salamu kwa niaba ya Allah na kwa niaba yangu, na mpe habari njema kuwa hakika yeye ana kasri (jengo la kifahari) Peponi lililotengenezwa kwa lulu. Ndani ya kasri hilo hakutakuwa na taabu, kelele wala udhia." (Al-Bukhari)

'Abdullah ibn 'Abbas رضي الله عنه anasimulia kuwa, siku moja Mtume ﷺ alichora mistari minne chini (ardhini), kisha akawauliza maswahaba ikiwa wanafahamu mistari ile ilikuwa inawakilisha nini. Kwa nidhamu na heshima ya hali ya juu, wakajibu, bila shaka Mtume wa Allah ﷺ ndiye anayefahamu. Akawaambia kuwa, mistari ile ilikuwa inawakilisha wanawake wanne watukufu kuliko wote duniani. Wanawake hawa ni Khadijah bint Khuwaylid, Fatmah bint Muhammad, Maryam bint Imran – mama wa Nabii Issa na 'Asia bint Muzahim (Mkewe Firauni).

Khadijah رضي الله عنها alikuwa mtu wa kwanza kumkubali Mtume ﷺ na kuukubali Uislamu na kuikubali dini ya Kiislamu kama mfumo kamili wa maisha yake. Huyu ni mwanamke ambaye alipata bahati ya kipekee ya kutolewa salamu na Mwenyezi Mungu na Malaika Jibril.

Khadijah رضي الله عنها alizaliwa mwaka 556. Mama yake mzazi aliitwa Fatmah bint Zayd, na baba yake aliitwa Khuwaylid ibn Asad. Baba yake alikuwa mmoja kati ya viongozi mashuhuri katika kabila la Maquraishi, na alikuwa miongoni mwa wafanyabiashara wakubwa na waliofanikiwa. Baba yake aliuwawa katika vita mashuhuri, vita vya Fujjar. Hivyo Khadijah alilelewa na kukulia katika maisha ya starehe. Hapo kabla, Khadijah aliolewa na Abu Halah Malak ibn Nabash ibn Zarrarah ibn At-Tamimi, na kujaaliwa kuzaa naye watoto

wawili wa kiume, ambao waliwaita Halah na Hind. Khadijah alitamani sana kumuona mume wake akiendelea na kufanikiwa katika biashara, hivyo alimsaidia na kumpa fedha za kumuwezesha kuanzisha biashara kubwa. Kwa bahati mbaya, mume wake yule alifariki dunia. Baada ya muda kidogo, mjane aliyekuwa na umri mdogo – Khadijah, aliolewa na 'Atique ibin 'Aith ibn 'Abdullah Al-Makhzumi, na akafanikiwa kuzaa naye mtoto mmoja wa kike waliyemwita Hindah. Lakini Khadijah akatengana na mume wake kutokana na kushindwa kuelewana. Baada ya hapo, Khadijah aliamua kuelekeza nguvu zake na jitihada zake katika kuwalea watoto wake na kuendeleza biashara aliyorithi kutoka kwa marehemu baba yake. Umahiri wake katika biashara uliifanya biashara yake kuendelea kiasi cha kuenea miongoni mwa Maquraishi.

Mbinu na sera aliyokuwa akiitumia Khadijah na kuifanya biashara yake iendelee, ilikuwa ni kuajiri watu wenye kufanya kazi kwa bidii, waaminifu na waliokuwa na ujuzi wa mambo ya biashara kufanya mambo kwa niaba yake. Kwa sababu biashara zake zilitegemea zaidi uaminifu wa wafanyakazi waliokuwa wakitakiwa kusafiri masafa marefu kwa niaba yake. Alikuwa akisafirisha bidhaa zake nje ya nchi, kwa mfano alikuwa akisafirisha bidhaa kwenda Syria, na mawakala wake walikuwa wakinunua bidhaa kutoka masoko ya huko na kuja kuuza bidhaa zile nyumbani - Makkah.

Bi Khadijah alikuwa amesikia sifa za Muhammad ﷺ hususani kwa uaminifu wake, ukweli wake na tabia njema ambazo alikuwa amejipamba nazo Muhammad ﷺ. Hivyo Khadijah alimuomba Muhammad ﷺ akubali kuajiriwa na yeye (Khadijah) ili aongoze msafara wake wa kibiashara. Alikuwa na bahati, kwani Muhammad alikubali ombi lake na kukubali kuajiriwa na bibi Khadijah na kuanza kufanya kazi zake. Khadijah alimuagiza kuongoza msafara wa biashra zake na alimteuwa mjakazi wake Maysarah, mjakazi aliyemuamini sana aongozane na Mtume ﷺ na awe anamuhudumia.

Maysarah alifurahishwa na kuvutiwa sana na ukweli, uaminifu na tabia njema alizokuwa amejipamba nazo Muhammad ﷺ. Alivutiwa pia na namna alivyokuwa mchangamfu na alivyokuwa na mahusiano mema na watu na uwezo wake mkubwa katika kufanya biashara. Wakiwa njiani wanarudi wakitokea Syria, Muhammad ﷺ alilala chini ya mti ili kujipumzisha kwa muda. Mtawa mmoja wa kiyahudi aliyeitwa Nestora, alimuona na aliweza kutambua kitu kwa Muhammad ﷺ kutokana na elimu na maarifa ya dini aliyokuwa nayo

na hivyo akamuuliza Maysarah; huyu ni nani? Maysarah akamueleza kile alichokuwa akikifahamu kuhusu Muhammad ﷺ na heshima aliyokuwa nayo kutokana na busara, ukweli na uaminifu aliokuwa nao. Nestora akamwambia Maysarah kuwa, mtu huyu atainuliwa na kuwa Mtume ﷺ katika siku zijazo, kwa sababu hakuna mtu aliyewahi kupumzika chini ya mti huu isipokuwa Mitume.

Zipo simulizi pia zinazosema kuwa, Maysarah aliwaona Malaika wawili wakimfunika na kumpa kivuli Muhammad ﷺ kutokana na joto na jua kali.

Waliporejea nyumbani Makkah, Maysarah alimsimulia kila kitu Bi Khadijah na kumfahamisha kila kilichotokea wakiwa njiani wakati wa kwenda na wakati wa kurudi wakitokea Syria. Khadijah alihamasika sana na kuanza kufikiria namna gani anaweza kuwasilisha ombi lake la kutaka aolewe na Muhammad ﷺ. Lakini anawezaje kuwasilisha ombi lake la kutaka aolewe kwake? Khadijah alikuwa amekataa posa kadhaa kutoka kwa wanaume waliotoka katika familia zenye kuheshimika miongoni mwa Maquraishi. Kabila lake watalipokeaje jambo hili? Familia yake watasemaje kwa yeye kutoa wazo au kuomba kuolewa na Muhammad? Na zaidi ya yote je, ombi lake kwa kijana huyu ambaye alikuwa hata hajaoa litakubaliwa?

Wakati bado anatafakari na kujadiliana na nafsi yake juu ya jambo hili, usiku mmoja aliota jua lililokuwa linang'ara limeshuka kutoka mbinguni na kutua ndani ya uwanja wa nyumba yake, na jua hilo lilikuwa likiiangazia nyumba yake. Alipoamka, alienda kwa binamu yake ambaye alikuwa na utaalamu wa kutafsiri ndoto, binamu huyu alikuwa anaitwa Waraqah ibn Nawfal. Waraqah ibn Nawfal alikuwa mtu kipofu lakini aliyejaaliwa elimu ya kutafsiri ndoto pamoja na maarifa makubwa ya kuijua Taurati na Injili. Baada ya Khadijah kumsimulia ndoto ile, Waraqah ibn Nawfal alitabasamu, kisha alimwambia kuwa asihofu kwani ndoto ile ilikuwa ni ndoto nzuri na ni ndoto ya kheri. Alimfahamisha kwamba, jua aliloliona likishuka katika uwanja wa nyumba yake inaashiria kuwa Mtume ﷺ ambaye habari zake zimeandikwa katika Taurati na Injili ataiangazia nyumba yake na atapata nguvu wakati wa uhai wake.

Baada ya mazungumzo haya kati ya Khadijah na Waraqah, dhamira ya Khadijah kutaka kuwasilisha ombi lake la kutaka kuolewa na Muhammad ﷺ ikawa imepata msukumo mpya. Mmoja kati ya rafiki wa karibu sana wa Khadijah aliyeitwa Nafisah bint Manbah, alifahamu dhamira na hamu

aliyokuwa nayo Khadijah kutaka kuolewa na Muhammad ﷺ. Hivyo Nafisah akatoka na kwenda kwa Muhammad ﷺ na kumuomba idhini ili amuulize swali la binafsi na la siri. Muhammad ﷺ aliposema hana pingamizi na kwamba yuko tayari kuulizwa swali hilo, alimuuliza kwanini mpaka muda huo alikuwa bado hajaoa? Muhammad ﷺ akamjibu kuwa alikuwa hana uwezo wa kifedha kuweza kufanya hivyo. Kisha Nafisah akamuuliza kama atakuwa tayari kumuoa mwanamke mrembo kutoka katika familia tajiri na yenye kuheshimika, mwanamke ambaye alikuwa anatamani sana kuolewa na yeye. Muhammad ﷺ akamuuliza alikuwa anakusudia mwanamke yupi? Alipomfahamu mwanamke aliyekuwa anakusudia Nafisah katika mazungumzo yake, akasema yuko tayari ikiwa tu yeye mwenyewe (Khadijah رضي الله عنها) atakuwa tayari kuolewa naye. Habari za utayari wa Muhammad ﷺ kumuoa zilipomfikia Khadijah, Khadijah alifurahi sana. Wakati huo Mtume ﷺ alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano (25) na Khadijah alikuwa na umri wa miaka arobaini (40). Wajomba wawili wa Muhammad ﷺ, Hamzah na Abu Talib wakaenda kwa mjomba wa Khadijah, 'Umar ibn Asad na kupeleka posa rasmi na posa ile ilikubaliwa na maandalizi ya harusi yakaanza. Mama Halimah As-Sa'diyyah, mwanamke aliyemnyonyesha Muhammad ﷺ wakati wa utoto, alialikwa rasmi kuja kuhudhuria harusi na alisafiri kutoka kijijini kwake kuja Makkah kwa ajili hiyo. Wakati anaondoka kurudi kijijini baada ya harusi, Khadijah alimpa zawadi ya vyombo vya ndani, ngamia na mbuzi arobaini kama shukurani kwa kumlea na kumpa malezi mazuri Muhammad ﷺ wakati wa utoto wake.

Khadijah alipata baraka katika ndoa hii, na alijaaliwa kuzaa watoto sita. Watoto wawili wa kwanza walikuwa ni wa kiume, watoto hawa walikuwa ni Qasim na 'Abdullah; kisha walifuatia watoto wa kike ambao ni Zaynab, Ruqayyah, Ummu Kulthum na Fatmah. Ilikuwa ni nyumba na familia iliyojawa na furaha.Lakini Muhammad ﷺ alikuwa anahisi kuna kitu kinakosekana katika maisha yao na kwa hakika alikuwa anakosa raha na daima alikuwa hana furaha. Alikuwa akitumia muda wa masiku kadhaa katika pango la Hira na kutumia muda wake kufanya ibada na kutafakari kwa kina. Siku moja alimjia kiumbe ambaye alimshika kwa nguvu sana. Kisha kiumbe yule aliregeza namna alivyokuwa amemshika kwa nguvu na akamtaka asome; Muhammad ﷺ akajibu kuwa yeye hajui kusoma. Lakini kiumbe yule akarudia kama alivyokuwa amefanya mara ya kwanza na kurudia maneno yale tena na tena. Kisha alisoma Aya hizi ambazo ndizo zilikuwa Aya za mwanzo kushushwa katika Qur'an. Aya hizi ziko katika Surah Iqra au Al-'Alaq.

ٱقْرَأْ بِٱسْمِ رَبِّكَ ٱلَّذِى خَلَقَ ﴿١﴾ خَلَقَ ٱلْإِنسَٰنَ مِنْ عَلَقٍ ﴿٢﴾ ٱقْرَأْ وَرَبُّكَ ٱلْأَكْرَمُ ﴿٣﴾
ٱلَّذِى عَلَّمَ بِٱلْقَلَمِ ﴿٤﴾ عَلَّمَ ٱلْإِنسَٰنَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ﴿٥﴾

***"Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba. Amemuumba mwanadamu kwa pande la damu. Soma, na Mola wako ni Karimu sana. Ambaye Amemfundisha (Binadamu ilimu zote hizi) kwa wasita (msaada) wa kalamu. Amemfundisha mwanadamu (chungu ya) mambo aliyokuwa hayajui."* (96:1-5)**

Kisha kiumbe yule alitoweka. Tukio hili lilimshitua sana Muhammad ﷺ na akarudi nyumbani huku akitokwa na jasho na huku akitetemeka. Alimwita na kumuomba Khadijah amfunike shuka. Baada ya katulia na mwili wake kupoa, akamueleza mke wake kuwa alikuwa anahofia maisha yake, na akamsimulia tukio lote. Bi Khadijah رضي الله عنها alimuondoa hofu na kumwambia kuwa, "Bila shaka Mwenyezi Mungu atakuhifadhi na kukukinga na kila hatari ikiwa itatokea. Kwa sababu yeye Allah hatoweza kuruhusu madhara yakutokee wakati wewe ni mtu mwema na daima umekuwa ukiwapatanisha watu na umekuwa rafiki wa watu wote. Wewe ni mtu ambaye hujawahi kusema uongo, mtu mkarimu, mtu unaekubali kubeba na kutatua matatizo ya watu na ukiwasaidia waliokuwa na shida." Maneno haya ya kuliwaza na ya kutia moyo yaliyotolewa na Bi Khadijah yalimjengea Muhammad ﷺ ujasiri, nguvu na kujiamini. Kisha alimchukua na kuongozana naye kwa binamu yake Waraqah ibn Nawfal, ambaye mara moja alimtambua kiumbe aliyekutana na Muhammad ﷺ katika pango la Hira, kuwa kiumbe yule alikuwa ni Malaika Jibril, mjumbe wa Mwenyezi Mungu ambaye aliwahi pia kumtembelea Nabii Mussa. Waraqah ambae kwa wakati huo alikuwa mzee sana, alisema anatamani kama angeishi mpaka wakati ambao Muhammad ﷺ atafukuzwa na watu wake. Muhammad ﷺ alishangaa sana na kuuliza kama ni kweli inawezekana ikafika wakati ambao watu wake watamfukuza. Waraqah alimuhakikishia kuwa lilikuwa ni jambo la kawaida kabisa kwa wanadamu kutomkubali Mtume ﷺ aliyetokea miongoni mwao. Waraqah aliongeza kusema kuwa, anatamani angekuwa hai wakati huo na akawa na uwezo wa kumsaidia. Alimalizia kwa kumwambia Bi Khadijah kuwa, "Ikiwa mliyoniambia ni kweli, basi mume wako ni Mtume wa Allah ﷺ ambaye habari zake zimeandikwa katika vitabu vilivyotangulia – Taurati na Injili."

Watoto wote wanne wa kike walilelewa na kukua wakiwa na afya na tabia njema na wakapata malezi mazuri ya Kiislamu. Na wote walihamia Madinah pamoja na Mtume ﷺ japo Zainab alihamia Madinah baadaye kama tutakavyoona hapo baadaye.

Zaynab aliolewa na Abu ‘Aas ibn Rabi’ah na Ruqayyah aliolewa na ‘Uthman. Ruqayyah alipofariki, Mtume ﷺ alimuozesha ‘Uthman mwanae mwingine - Ummu Kulthum; Fatmah aliolewa na ‘Ali ibn Abi Talib. Watoto watatu wa kike walifariki wakati Mtume ﷺ akiwa bado yuko hai, na mwanae Fatmah alifariki dunia miezi sita baada ya Mtume ﷺ kufariki dunia.

Makafiri walipoona pamoja na mbinu na hila zao zote, bado Uislamu unawavutia wafuasi wengi sana, waliamua kuwatenga kijamii na kiuchumi watu wote wa ukoo wa Bani Hashim – Ukoo wa Mtume ﷺ. Hii ilitokea miaka saba toka Mtume ﷺ alipotangaza wazi kuwa yeye ni Mtume wa Allah. Jambo hili katika vitabu vya historia limetajwa kama *Shi’ab Abi Talib*.

Kuwasusia na kuwatenga huku kijamii na kiuchumi kulisababisha njaa, madhara na mateso makubwa. Watoto walikuwa wakishinda njaa huku watu wazima wakila majani. Pamoja na hayo yote, wafuasi thabiti wa Mtume ﷺ hawakurudi nyuma na kuikana dini yao ya kweli. bali hali hii iliwafanya wawe imara zaidi kiimani na kuwatakasa kuliko walivyokuwa hapo awali.

Bi Khadijah ambaye alikuwa amelelewa katika maisha ya starehe na utajiri wa baba yake, sasa alikuwa anayakabili maisha magumu na ya shida huku akiwa na subira na ujasiri wa hali ya juu, mambo ambayo ni muhimu sana kwa mtu anayekabiliwa na wakati mgumu. Tabia njema na matendo mema aliyokuwa nayo Khadijah yakamfurahisha sana Allah, kiasi cha kumfanya Allah amtumie salamu maalumu.

Bi Khadijah alikuwa mfano bora wa mke na mama. Mtume ﷺ aliishi katika nyumba ya Bi Khadijah, nyumba ambayo ilikuwa imejaa baraka kutokana na kuwepo Mtume ﷺ na nyumba yake kutembelewa mara kwa mara na Jibril (Amani iwe juu yake) alipokuwa akija kwa Mtume ﷺ akimletea *wahyi* – Qur’an kutoka kwa Mola wake. Nyumba yake ikawa kitovu cha Uislamu, sehemu ambayo maswahaba wote, wanawake kwa wanaume wakija mara kwa mara kupata faraja kutoka kwa Mtume Muhammad ﷺ na mke wake.

Baada ya Hijrah ambapo Mtume ﷺ alihamia Madinah, nyumba ya Khadijah ilikaliwa na kaka wa 'Ali. Baadaye nyumba hii ilikuja kununuliwa na Mu'awiyah ibn Abu Sufyan na kujenga msikiti. Hivyo, mahala palipokuwa nyumba ya Bi Khadijah pakawa ni sehemu ya watu wote kuswalia kwa zama zote. Palikuwa pakiswaliwa na Mtume ﷺ rakaa mbili asubuhi na jioni kabla hata Swala haijafaridhishwa na Allah. Baada ya kuukubali Uislamu na kujiimarisha katika kufanya ibada, alijikuta akipata amani na utulivu anapokuwa ndani ya Swala.

Afif Kindi anasimulia kuwa, 'Abbas ibn 'Abdul Muttalib alikuwa rafiki yake mkubwa na kwamba alikuwa akimtembelea mara kwa mara nchini Yemen kwa ajili ya biashara yao ya mafuta uzuri. Siku moja wakiwa wamesimama huku wakiwa wanazungumza katika mji wa Mina, walimuona kijana mmoja aliyekuwa na umbile zuri akija karibu yao. Aliosha mikono yake vizuri, kisha akaosha miguu yake, kisha akasimama kwa unyenyekevu akiwa ameweka mikono yake kifuani; Mara binti aliyeonekana kuwa anatoka katika familia yenye hadhi kubwa na kijana mwingine wakaungana naye. 'Afif akamuuliza 'Abbas, watu hawa walikuwa wanafanya nini, au ilikuwa ni aina mpya ya mazoezi? 'Abbas akajibu, kijana yule alikuwa ni ndugu yake, mtoto wa 'Abdullah, na mwanamke yule alikuwa ni mke wake. Alikuwa ni mwanamke mwenye hadhi kubwa na tajiri na mfano bora wa mke na mfano bora wa mama. Kijana aliyekuja kuungana nao alikuwa ni mtoto wa Abu Talib. Muhammad ﷺ alikuwa tayari ametangaza kuwa yeye ni Mtume wa Allah ﷺ na alikuwa ameanza kutangaza - Uislamu. Baadaye 'Afif aliukubali Uislamu, lakini siku zote alikuwa akisikitika sana kwanini hakuungana na Mtume Muhammad ﷺ katika Swala na dua siku ile, siku iliyokuwa ya kumbukumbu muhimu pale Mina, aliposikia kuhusu Uislamu kwa mara ya kwanza.

Bi Khadijah akafariki dunia, miaka mitatu tu kabla ya kutokea tukio muhimu katika historia ya Uislamu – tukio la Hijrah, ambapo Mtume ﷺ alihamia katika mji wa Madinah. Khadijah alifariki dunia akiwa na umri wa miaka sitini na tano (65), akiwa ameishi na Mtume Muhammad ﷺ na kuutumikia Uislamu kwa miaka takriban ishirini na tano (25). Mtume Muhammad ﷺ alipomuona Bi Khadijah akiwa katika dakika za mwisho za uhai wake, alimtia moyo na kumwambia hakika Allah amekuridhia na muda si mrefu utayaona yale ambayo Mwenyezi Mungu amekuandalia nawe utayafurahia

na kuyaridhia. Bi Khadija aliyafungua macho yake na kumuangalia mume wake kipenzi – Mtume wa Allah – Muhammad ﷺ, na roho yake ikauacha mwili.

Kaburi la Bi Khadijah liliandaliwa katika eneo lililoitwa Hujjun, jirani kabisa na mji wa Makkah. Mtume wa Allah - Muhammad ﷺakaingia ndani ya kaburi kukagua na kuhakikisha kuwa kila kitu kilikuwa sawa kama kilivyotakiwa kuwa. Kwa mikono yake mwenyewe akamzika mke wake – Bi Khadijah رضي الله عنها. Hivi ndivyo alivyofariki na kuzikwa mama wa Waislamu wote, mwanamke aliyejitolea kila kitu kwa ajili ya Uislamu. Mwanamke aliyeupokea na kuupa nguvu Uislamu katika siku zake za mwanzo kabisa na kumpa nguvu Mtume ﷺ. Huyu ndiye mtu wa kwanza kuukubali Uislamu baada ya Mtumeﷺ; Mwanamke wa kwanza Peponi na bibi wa wajukuu vipenzi wa Mtume ﷺ- Hasan na Hussein, vijana watakaokuwa mbele na kuwaongoza vijana kuingia Peponi.

Alipofariki Bi Khadijah, Mtume ﷺ aliingiwa na huzuni sana kwa kumpoteza mtu muhimu aliyemuunga mkono, akamtia nguvu na kujitolea kwa hali na mali kwa ajili ya Uislamu katika siku za mwanzo kabla Uislamu haujapata nguvu na ukipigwa vita na makafiri. Mwanamke aliyesimama imara wakati wa misukosuko na mateso.

Mmoja katika wasichana kutoka kabila la Maquraishi, Khawlah bint Hakim, alimtembelea Mtume ﷺ kumpa pole, na akamuona Mtume ﷺ akiwa katika hali ya huzuni sana kutokana na msiba wa mkewe. Alipompa pole, Mtume ﷺ aliitikia na kumwambia kuwa ni jambo la kawaida kuwa na huzuni kutokana na kuondokewa na mkewe kwa sababu hakika Bi Khadijah alikuwa mama bora kwa watoto wake ambao sasa amewaacha; alikuwa mwanamke mwaminifu na mtiifu ambaye alikuwa akishirikiana naye, na Mtume ﷺ akimwambia siri zake. Ilikuwa ni hali ya kibinadamu na ya lazima kutokea na kuhisi amepoteza kwa sababu alikuwa tayari kumuunga mkono na kumsaidia katika nyakati ngumu kabisa katika historia ya maisha yake. Kila wakati Mtumeﷺ alipotukanwa na makafiri, alikuwa akimtia moyo na akithibitisha kuwa na imani isiyoyumba.

Mmoja kati ya maswahaba anasimulia kuwa, kila wakati Mtume ﷺ alipoletewa zawadi, alikuwa akiagiza sehemu ya zawadi ile ipelekwe (igawiwe) kwa wanawake waliokuwa marafiki wa karibu wa Khadijah رضي الله عنها. Aishah

رضي الله عنها, ambaye alikuwa mmoja kati ya wake vipenzi wa Mtume Muhammad ﷺ anasema, kila mbuzi alipochinjwa, basi Mtume ﷺ alikuwa akiagiza sehemu ya nyama wapewe rafiki zake Bi Khadijah; Pale mama wa waumini Aishah alipohoji juu ya tabia hii, Mtume ﷺ alimjibu, "Nawajali sana marafiki zake, kwa sababu yeye Khadijah alikuwa na sehemu maalumu katika moyo wangu." Bi Aishah رضي الله عنها anasema, hakuwahi kujisikia wivu unaowapata wanawake kwa mke mwingine yeyote wa Mtume kama wivu aliousikia kwa Khadijah رضي الله عنها. Pia anasimulia kuwa, kila pale Mtume Muhammad ﷺ alipomtaja Bi Khadijah, alikuwa akimuelezea kwa kirefu na akimsifia kwa kila sifa nzuri na akimuombea msamaha kwa Mwenyezi Mungu.

Aishah رضي الله عنها anasimulia kuwa, kila pale Mtume ﷺ alipomzungumzia Bi Khadijah رضي الله عنها, alikuwa akimzungumzia kwa heshima ya hali ya juu. Siku moja wivu ukamjia mama wa waumini – Aishah na akazungumza maneno yasiyokuwa mazuri juu ya Bi Khadijah, na kumshangaa na kumuuliza Mtume ﷺ kwanini alikuwa kila wakati akimkumbuka na kumtaja kwa wema Bi Khadijah, wakati tayari Allah alikuwa amemjaalia na kumpa mke bora tena kijana. Jambo hili halikumfurahisha Mtume wa Allah ﷺ, kwa upole kama alivyokuwa, alimjibu, *"Sijawahi kupata mke bora kuliko yeye. Khadijah. Aliniamini wakati ambao watu wote, hata watu wa familia yangu na kabila langu walikuwa hawaniamini; yeye aliniamini kuwa kwa hakiki mimi ni Mtume ﷺ kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Alisilimu na kutoa mali zake zote na utajiri aliokuwa nao akinisaidia mimi kutangaza dini hii, na aliyafanya haya wakati ambao ilikuwa inaonekana kama dunia nzima ilikuwa iko dhidi yangu na ikinipiga vita; na kupitia kwake Allah alinijaalia kupata watoto."*

Kama Allah anavyosema katika Surah Al-Fajr katika Qur'an Tukufu, kuwa wataambiwa Waumini watukufu:

يَـٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفْسُ ٱلْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾ ٱرْجِعِىٓ إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةً مَّرْضِيَّةً ﴿٢٨﴾ فَٱدْخُلِى فِى عِبَـٰدِى ﴿٢٩﴾ وَٱدْخُلِى جَنَّتِى ﴿٣٠﴾

***"Ewe nafsi yenye kutua! Rudi kwa Mola wako, hali ya kuwa utaridhika (kwa utakayoyapata), na (Mwenyezi Mungu) aridhike na wewe. Basi ingia katika (kundi la) waja Wangu (wazuri). Uingie katika Pepo yangu."*** **(89:27-30)**

Nasi tunamwambia mama yetu, Bi Khadija! Rejea kwa Mola wako hali ya kuwa utaridhika (kwa utakayoyapata), na (Mwenyezi Mungu) aridhike na wewe.

# Sawdah bint Zam'a

## Natamani Allah Anifufue kama Mke wa Mtume ﷺ

Jina kamili la mama huyu ni Sawdah bint Zam'a ibn Qays ibn 'Abd Shams kutoka katika kabila la Banu Amir, ambao ni moja kati ya koo za Maquraish. Mama mzazi wa mama huyu aliitwa Ash-Shamus bint Qaus ibn Zayd ibn Amr kutoka ukoo wa Banu an-Najjar.

Kwa mara ya kwanza mama huyu aliolewa na as-Sakran ibn Amr, ambaye ni kaka wa Suhail ibn 'Amr al-'Amiriy. Wote wawili waliukubali Uislamu katika masiku ya mwanzo kabisa na kusilimu. Kutokana na misukosuko mikubwa iliyokuwa inawakabili Waislamu, Mtume ﷺ akawashauri baadhi ya Waislamu wahamie Uhabeshi (Ethiopia), mama huyu na mume wake walikuwa miongoni mwa Waislamu waliohama kunusuru imani zao. Na alikuwa miongoni mwa watu wanane tu kutoka katika ukoo wa Banu 'Amir waliohama na kuyaacha makazi yao na mali zao kwa ajili ya dini yao. Mara tu walipofika Uhabeshi, haikuchukua muda mrefu mume wake akafariki na mama huyu akabakia kuwa mjane.

Mtume ﷺ alikuwa akimuonea huruma sana mama huyu ambaye kimsingi alikuwa akihitaji kusaidiwa kutokana na umri wake kuwa mkubwa. Ni muhimu kukumbuka kuwa, mara baada ya mke wa Mtume ﷺ, Bi Khadijah kufariki, Mtume ﷺ alikuwa mwenye huzuni kubwa kiasi kwamba hakuna aliyethubutu kwenda kuzungumza naye juu ya suala la kuoa. Hii ni kwa sababu Bi Khadijah alikuwa na nafasi ya pekee katika moyo wa Mtume ﷺ. Ni Bi Khadijah aliyemuamini wakati wengine wakimkanusha; ni Bi Khadijah aliyetoa mali zake na utajiri wake wote kumsaidia Mtume ﷺ ili afanikiwe kueneza Uislamu; ni Bi Khadijah ambaye siku zote alikuwa akimtia moyo na kusimama imara wakati alipopata misukosuko; ni Bi Khadijah ambaye pamoja na kuwa alikuwa tajiri alikubali kuishi maisha dhalili na mateso makubwa baada ya kuwekewa vikwazo

na kufariki muda mfupi baada ya hapo; ni Bi Khadijah aliyemzalia watoto Mtume ﷺ ambao walifikia utu uzima na kuolewa. Basi nani angeweza kuchukua nafasi ya Bi Khadijah?

Baada ya muda mwingi wa huzuni aliokuwa nao Mtume ﷺ, Bi Khawlah alikwenda kuongea na Mtume ﷺ na kwa upole akamuuliza, "Kwanini usioe ewe Mtume wa Allah?" Mtume ﷺ akamuuliza Khawlah, "Nani anaweza kuchukua nafasi ya Khadijah?" Bila shaka kulikuwa hakuna mwanamke aliyekuwa na uwezo wa kuchukua na kuziba pengo aliloacha Bi Khadijah kwa namna yeyote ile. Hata hivyo, Khawlah alimjibu Mtume ﷺ kwa kumwambia kuwa, "Unaweza kumuoa yeyote umpendaye, mwanamke ambaye hajaolewa au aliyekwisha kuolewa na kuachwa." Mtume ﷺ akamuuliza, "kama mwanamke gani katika wanawake ambao hawajaolewa?" Khawlah akamjibu, "Mtoto wa rafiki yako kipenzi, Aishah bint Abu Bakr." Mtume ﷺ alikaa kimya kwa muda, kisha akamuuliza na ni, "Yupi mwanamke ambaye alikwisha olewa unayemkusudia?" Khawlah akamjibu "Sawdah bint Zam'ah رضي الله عنها." Kisha Mtume ﷺ akaamua kumuoa Sawdah na akamtuma Khawlah kwenda kuzungumza naye.

Khawlah alikwenda moja kwa moja kwa Sawdah bint Zam'ah na kumuuliza, "Je, ungependa Allah akupe baraka nyingi Sawdah?" Sawdah akamuuliza Khawlah, "Baraka zipi ewe Khawlah?" Khawlah akamwambia, "Mtume wa Allah amenituma kuleta posa kwako!" Huku akiwa mwenye furaha, Sawdah bint Zam'ah alikubali na kumwambia Khawlah, "Nenda kwa baba yangu ukamwambie juu ya jambo hilo." Khawlah akaenda kwa Zam'ah. Alipofika, alimsalimia Zam'ah ambaye kwa muda huo alikuwa mtu mzima sana kisha akamwambia, "Muhammad ibn Abdullah ibn Abdul Muttalib, amenituma nije kuleta posa kwa Sawdah." Mzee yule akapaza sauti, "Kheri kubwa. Yeye (Sawdah) anasemaje?" Khawlah akamjibu kuwa, "Yeye amekubali." Mzee Zam'ah akamwambia amwite mwanae Sawdah. Sawdah alipofika, Mzee Zam'ah akasema, "Sawdah, huyu mwanamke anadai kuwa Muhammad ibn Abdullah ibn Abdul Muttalib amemtuma kwangu kuleta posa ili akuoe. Hakika ni kheri kubwa. Je, unaniruhusu nikuozeshe kwake?" Sawdah bint Zam'ah akakubali huku akiamini kuwa hii ilikuwa ni heshima kubwa. Hivi ndivyo Sawdah bint Zam'ah alivyoolewa na Mtume Muhammad ﷺ na kuwa mmoja kati ya mama wa Waumini.

Leo wakati wanaume wengi wa Kiislamu wakiwa wanapoteza mvuto kwa wake zao na pengine wakiwaona kuwa wake zao wanapoteza mvuto, ni vema wakakumbuka kuwa, katika ndoa yenye furaha, moyo unahitaji zaidi ya uzuri wa mwili na kuvutia. Ndoa ya mama huyu inawakilisha na kutoa somo muhimu.

Mtume ﷺ alibakia na mama huyu akiilea familia ya Mtume ﷺ kwa muda wa miaka mitatu, ndipo akaja kumuoa mama wa Waumini, Aishah رضي الله عنها. Watu wa Makkah walipatwa na mshangao mkubwa. Inawezekanaje Mtume ﷺ amuoe mwanamke ambaye ni mtu mzima ambaye amepoteza kabisa uzuri na asiyevutia? Anawezaje kuchukua nafasi ya mama wa Kiquraish, mama wa Waumini, Bi Khadijah? Kama tulivyosema hapo kabla, kulikuwa hakuna mwanamke aliyekuwa na uwezo wa kuziba pengo aliloacha Bi Khadijah. Suala la Mtume ﷺ kumuoa mama huyu ilikua ni katika lengo la kutoa sadaka na kumsaidia na si sulala la matamanio au mapenzi.

Sawdah bint Zam'a aliishi akiihudumia familia ya Mtume ﷺ wakiwemo watoto wa marehemu Bi Khadijah kwa muda wa miaka mitatu. Katika muda wote huu, Mtume ﷺ aliweza kutekeleza wajibu wake kikamilifu katika kuutangaza Uislamu. Baada ya miaka mitatu, ndio wake wengine wa Mtume ﷺ wakaanza kuolewa na Mtume ﷺ katika nyakati tofauti wakiwemo Aishah, Hafsa, Zaynab, Ummu Salama na wengineo.

Baadaye mama wa Waumini, Sawdah bint Zam'a رضي الله عنها alikuja kufahamu kuwa Mtume ﷺ alimuoa kwa kumuonea huruma kutokana na kufiwa na mume wake na hivyo kubakia mjane tena katika umri mkubwa. Alikuja kulifahamu hili pale Mtume ﷺ alipotaka kumuacha na kumuepusha na majukumu mazito ya ndoa. Baada ya Sawdah bint Zam'a رضي الله عنها kufahamu nia ya Mtume ﷺ kutaka kumuacha, Sawdah bint Zam'a رضي الله عنها alijisikia kuchanganyikiwa na kuona anakwenda kuishi maisha ya tofauti sana. Hivyo aliamua kumkabili Mtume ﷺ na kumwambia, "Ewe Mtume wa Allah, naomba usiniache. Naapa kwa jina la Allah kuwa, kwa hakika mimi sihitaji mwanaume lakini natamani Allah anifufue kama mke wako siku ya Kiyama." Hivyo aliamua kwa hiari yake kama sehemu ya kupunguza majukumu na kumfurahisha Mtume ﷺ, akatoa sehemu ya siku ambazo Mtume ﷺ alipaswa kuwa nyumbani kwa Sawdah bint Zam'a رضي الله عنها, zitumike kwa mama Aishah. Mtume ﷺ akakubali na Allah akashusha Ayah ifuatayo katika Qur'an:

فَلَا جُنَاحَ عَلَيۡهِمَآ أَن يُصۡلِحَا بَيۡنَهُمَا صُلۡحٗاۚ وَٱلصُّلۡحُ خَيۡرٞ

***".....Basi si vibaya kwao wakitengeneza baina yao sulhu; maana sulhu ni kitu bora....".* (4:128)**

Bi Sawdah alibakia katika nyumba ya Mtume ﷺ kama mama wa Waumini na mke wa mbora wa viumbe wa Allah, Mtume Muhammad ﷺ. Tofauti na ilivyo kwa wanawake wengi wa zama zetu wenye umri mkubwa wanavyoingiwa na hofu kwa mume kuoa mwanamke mwingine hasa mwenye umri mdogo na hata kuanzisha uadui na ushindani, hali ilikuwa tofauti kwa mama Sawdah bint Zam'a pale alipoolewa mama Aishah na hakika hata walipoolewa wake wengine. Wanawake wote aliwapenda na kuwafanya rafiki zake na hata kumtania na kufurahi. Ushahidi wa haya ni maneno ya mama Aishah pale mama huyu Sawdah bint Zam'a alipofariki dunia. Inatosha kuwa somo muhimu kwa wanawake wa Kiislamu wenye haja ya kutafuta radhi za Mola wao katika ndoa zao na hasa pale mume wake anapooa mke wa pili au wa tatu au wanne.

Mama huyu, Sawdah bint Zam'a رضي الله عنها alifariki wakati wa Ukhalifa wa Umar ibn Khattab. Mama Aishah alikuwa akimkumbuka sana mama huyu na kusema: *"Hakuna mwanamke ambaye nilikuwa napenda kumtania isipokuwa Sawdah bint Zam'ah ambaye alisema alipokuwa mtu mzima, "Ewe Mtume wa Allah nazitoa siku zangu kwa Aisha. Lakini alikuwa na kiasi fulani cha ukali."* (Muslim)

# Aishah bint Abi Bakr

## Mke Aliyechaguliwa na Allah!

Bi Aishah رضي الله عنها, alizaliwa mwaka 614 na alipata bahati ya kuzaliwa na watu watukufu kwa pande zote mbili, baba na mama. Mama yake mzazi alikuwa ni Ummu Rooman na baba yake mzazi alikuwa ni Abu Bakr As-Siddiq.

Bibi huyu – mama wa Waumini – Aishah رضي الله عنها alikuwa akisema kuwa, alikuwa amejaaliwa na Allah sifa tisa ambazo zilikuwa zikimtofautisha yeye na wanawake wengine wote duniani isipokuwa Maryam bint 'Imran – Mama wa Nabii 'Issa عليه السلام.

Malaika Jibril aliileta picha yake na kumkabidhi Mtume Muhammad ﷺ, ikiwa imefunikwa ndani ya kitambaa cha hariri chenye rangi ya kijani na kumwambia kuwa hii ni picha ya msichana aliyechaguliwa na Allah, kuwa liwazo kwako hapa duniani na kesho Akhera.

Ni mwanamke bikira pekee aliyewahi kuolewa na kuwa mke wa Mtumeﷺ.

Wakati Mtume ﷺ anafariki dunia, alikuwa amelala juu ya mapaja yake – mapaja ya mama Aishah رضي الله عنها na alizikwa ndani ya nyumba yake.

Malaika Jibril alikuwa akishuka mara nyingi kwa Mtume ﷺ, Mtume ﷺ akiwa ndani ya nyumba yake, na alikuwa akija kwa mapenzi na heshima.

Mara nyingi *Wahyi* ulikuwa ukishushwa kwa Mtume Muhammad ﷺ wakiwa wamelala pamoja, wakiwa wamepumzika kwa amani, mapenzi na huruma.

Alikuwa binti wa rafiki wa kweli wa Mtume ﷺ, Abu Bakr As - Siddiqرضي الله عنه.

Ayah zilishushwa kutoka mbinguni zikithibitisha kuwa alikuwa hakufanya kosa kama ilivyokuwa ikienezwa na wanafiki na baadhi ya Waislamu.

Alizaliwa akiwa ni Muislamu na alilelewa katika mazingira masafi na kukulia mikononi mwa mbora wa viumbe, Mtume ﷺ Mola wa walimwengu wote – Allah Alimuahidi msamaha na ujira bora utokao kwake - Pepo.

Akiwa binti mdogo, alikuwa na kawaida ya kuchezea mwanasesere. Siku moja Mtume Muhammad ﷺ alimtembelea baba yake (Abu Bak رضي الله عنهr), na alimuona Aishah akicheza na farasi mwenye mbawa; wakati huo Aishah alikuwa na umri wa miaka mitano (5) tu, alipoulizwa anachezea nini, alijibu kuwa alikuwa anachezea farasi. Mtume ﷺ alitabasamu na kumwambia kuwa farasi huwa hana mbawa! Haraka Aishah رضي الله عنها alijibu kuwa Nabii Suleiman alikuwa na farasi mwenye mbawa, jambo linaloonesha wazi kuwa toka akiwa na umri mdogo alikuwa na busara na maarifa ya dini ikiwemo mambo ya historia. Akiwa na umri wa miaka minane (8), alibahatika kuandika historia yake, pale dola ya kwanza ya Kiislamu ilipokuwa ikisimama, alikuwa na uwezo wa kukumbuka hata matukio na mambo madogo madogo yaliyotokea. Mwaka uliofuata aliolewa na Mtume ﷺ na hivyo kuwa sehemu ya familia yake.

Vyumba vidogo vidogo vilijengwa jirani kabisa na msikiti wa Mtume ﷺ, na Aishah alipewa na kukaa katika moja ya nyumba hizo. Nyumba yake ilikuwa pembeni mwa ukuta wa mashariki wa msikiti na paa lake lilikuwa limetengenezwa kwa kutumia matawi ya miti na majani. Ilikuwa imefunikwa na aina ya shuka lililokuwa na uwezo wa kuzuia maji ya mvua kupenya na paa lilikuwa chini sana kiasi kwamba mtu akisimama alikuwa na uwezo wa kulishika paa la nyumba hiyo. Mlango wake ulikuwa daima haufungwi na muda wote pazia ilikuwa inaning'inia mlangoni. Jirani na chumba hicho cha mama Aishah رضي الله عنها katika sehemu iliyokuwa imeinuka kidogo, kulikuwa na chumba kidogo kingine kilichokuwa kimeunganishwa na chumba hiki. Ndani ya chumba hiki kulikuwa na zulia, godoro jembamba sana, mto wa kulalia uliojazwa magome ya miti, mtungi wa maji, sahani ndogo kwa ajili ya tende na bilauli ya kunywea maji. Hivi ndivyo vitu vilivyokuwa ndani ya chumba hiki, zaidi ya hayo chumba hiki kilikuwa na hazina kubwa sana ya imani.

Wakati Uarabuni yote ilipokuwa chini ya dola ya Kiislamu, nafaka na fedha nyingi vilianza kuingia kwa wingi katika hazina kuu ya dola ya Kiislamu. Hata hivyo, wakati Mtume Muhammad ﷺ anafariki dunia, ndani ya nyumba yake

kulikuwa hakuna chakula cha kutosha japo kwa siku moja. Aishah رضي الله عنها alidumu na utaratibu huu mpaka na yeye alipofariki dunia.

Haya ndiyo yalikuwa maisha ya Mtume ﷺ na wake zake. Ni kinyume kabisa na maisha yetu hivi leo ambapo mtu anapanga bajeti na kununua vyakula na mavazi vya kutosha mwezi mzima na hata miezi kadhaa mbele kana kwamba ana ahadi na Mola wake kuwa atakuwepo kwa miaka kadhaa mbele. Moyo wake haumsumbui wala akili haifikiri nini ametanguliza kwa ajili ya nafsi yake Akhera. Ukiuliza ni kwanini Waislamu tumekumbwa na hali hii, utaambiwa maisha ya sasa lazima uishi kwa bajeti! Kana kwamba sisi tumekuwa wa kwanza kuishi. Lakini ukweli ni kuwa imani yetu kwa Allah imeshuka na kuwa chini sana kiasi kwamba tunadhani tunatosheleza mahitaji yetu kutokana na nguvu, jitihada na mipango yetu na wala si kwa rehema zake Mwenyezi Mungu.[1]

Mama Aishah رضي الله عنها alikuwa mtu mkarimu sana, fedha zote alizokuwa akizipata alikuwa akizitoa kama sadaka haraka sana. Siku moja mama Aishah رضي الله عنها akiwa katika swaumu (akiwa amefunga), mtu mmoja alikuja nyumbani kwake na kumuomba chakula. Mama Aishah رضي الله عنها alimuagiza mjakazi wake ampe kipande cha mkate walichokuwa nacho. Mjakazi wake akamwambia mama Aishah رضي الله عنها kuwa, kulikuwa hakuna kitu kingine ambacho angeweza kukitumia kama chakula wakati wa kufuturu. Mama Aishah رضي الله عنها akamjibu yule mjakazi wake, "Msaidie mama mwenye njaa, na mambo ya jioni muachie Allah. Huyu ndiye mama wa Kiislamu – Mama wa Waumini na kigezo chema kwa akina mama wa Kiislamu wa leo na zama zote. Kwa rehema zake Allah, jioni ilipofika, mtu mmoja alimletea sahani iliyokuwa na nyama iliyopikwa! Je, huu si mfano bora katika kumtegemea Allah ukweli wa kumtegemea?

Mama Aishah رضي الله عنها aliuza nyumba aliyokuwa akiimiliki na kutoa fedha alizozipata kutokana na mauzo ya nyumba ile sadaka. Ni mfano bora kiasi gani kumjua mama huyu na kujifunza kutoka kwake. Hakika tunaye mama mwema tunaeweza kujifunza ukarimu kutoka kwake! Japo nafsi zilizojaa uasi na kuipenda dunia zinashangaa na kuyakataa haya!

---

[1] Imethibiti katika hadithi sahihi zilizopo katika Bukhari na Muslim kuwa Bwana Mtume ﷺ alikuwa anaweka na kuhifadhi chakula cha kutosha familia yake cha mwaka mzima. (Mhariri)

Mama Aishah رضي الله عنها alimpenda sana mtoto wa dada yake, 'Abdullah ibn Zubayr. Alimpenda sana dada yake na daima alikuwa akijitahidi kumsaidia mahitaji yake. Siku moja 'Abdullah ibn Zubayr alimwambia mama Aishah kuwa alipaswa kuongeza ukarimu wake.Mama wa Waumini رضي الله عنها alijisikia vibaya na kuvunjika moyo baada ya kusikia maneno yale na aliapa kuwa hatozungumza naye tena. Baadaye alipokaa na kutulia na moyo wake kupoa, alijilaumu sana kwa kuwa na mawazo ya namna ile. Aliwaachia huru watumwa kadhaa kama fidia ya kuvunja ahadi aliyoichukua.

Mama Aishah رضي الله عنها alikuwa na moyo laini (moyo wenye huruma na mwingi wa imani), siku moja alikuja mtu aliyekuwa anaomba msaada mlangoni kwake huku muombaji yule akiwa amebeba watoto wawili. Wakati huo, Aishah رضي الله عنها alikua na kokwa tatu tu za tende. Alimpa tende zile mama yule aliyekuja kuomba, na yeye alimpa kila mtoto tende moja na yeye mwenyewe akaanza kula tende ya tatu. Mmoja kati ya watoto wale akala tende yake haraka haraka na kuanza kumuangalia usoni mama yake aliyekuwa akila tende yake. Mama yule alishindwa kuvumilia kumuona mwanae akiendelea kumuangalia huku akiwa na njaa. Mama yule aliitoa tende aliyokuwa akila mdomoni mwake, akaigawa sehemu mbili na kumpa kila mtoto nusu yake. Mama Aishah رضي الله عنها alipoliona tukio hili, alishindwa kudhibiti machozi yake.

Ni mara ngapi tunawafukuza au kutowajali watu wenye njaa na shida wanapokuja kutuomba wakiwa na njaa na waliodhoofika? Mara ngapi tumewapita bila kujali watu waliokuwa na njaa au wenye shida ilhali tukiwa na uwezo wa kuwasaidia? Mara ngapi tumekula tukashiba huku ndugu zetu katika imani wakiwa na njaa na walioharibikiwa? Je, haitoshi kujifunza na kupata mazingatio kutoka kwa mama wa Waislamu – Mama Aishah رضي الله عنها?

Katika mwezi wa Sha`ban, mama Aishah رضي الله عنها aliongozana na Mtume Muhammad ﷺ aliyekuwa akiongoza jeshi la Waislamu kuelekea Qadid, ambapo Waislamu walipigana vita vidogo dhidi ya kabila la Banu Mustaliq. Ndani ya msafara huu kulikuwa pia na wanafiki kadhaa, ambao nao walikuwa sehemu ya jeshi lililoshiriki vita hivi. Mama Aishah رضي الله عنها alikuwa ameazima mkufu kutoka kwa mdogo wake Asma' رضي الله عنها. Wakiwa njiani wanarejea, jeshi la Waislamu liliweka kambi njiani kupumzika, na mama Aishah رضي الله عنها akaenda mbali jangwani kwa ajili ya kujisaidia. Akiwa njiani anarejea, aligundua kuwa mkufu ule ulikuwa umedondoka njiani, na aliupata baada ya kuutafuta

kwa muda mrefu kidogo. Alipofika mahala alipokuwa ameuacha msafara, alikuta msafara ule umekwisha ondoka. Utaratibu uliozoeleka ilikuwa mwanamke alijitenga na kundi la wanaume, alikuwa akikaa ndani ya kifaa kilichojengwa mfano wa hema. Kisha muendesha ngamia alikuwa akiweka kifaa kile juu ya ngamia. Kwa kuwa mama Aishah رضي الله عنها alikuwa na umbile dogo na mwepesi, haikuwa rahisi kugundua kuwa hakuwemo ndani ya kifaa kile wakati kinanyanyuliwa na kuwekwa juu ya ngamia. Mama Aishah رضي الله عنها alilala chini na kusubiri watakapogundua kuwa hayumo, warejee.

Safwan Ibn Mu'attil رضي الله عنه alikuwa amepewa jukumu la kubaki nyuma akikagua na kuhakikisha kuwa mahala ambapo Waislamu walikuwa wamepumzika hawakuacha au kusahau kitu chochote, ilipofika asubuhi aliwasili na kumkuta mtu amelala akiwa amejifunika *Jilbab*. Aishah رضي الله عنها alipomsikia Safwan ibn Mu'attil, aliamka na kupanda ngamia. Na Safwan ibn Mu'attil alianza kutembea akimuongoza ngamia yule kwa kutumia hatamu.

Wakati wa mchana, wakati Waislamu wakiwa ndio kwanza wamefika katika kituo kingine cha kupumzika, walimuona Aishah akiwasili akiwa na Safwan. Ghafla zikaenea habari na minong'ono katika mji wa Madinah kuwa Aishah رضي الله عنها alikuwa na tabia mbaya na kwamba uaminifu wake ulikuwa ni wa kutiliwa mashaka. Uzushi na minong'ono hii ilikuwa ikienezwa na Abdullah ibn Ubayy ibn Salul. Maswahaba wakubwa na waaminifu, Hasan ibn Thabit, Hamnah bint Jahsh na Mastah ibn Athathah رضي الله عنهم nao walijiunga katika kusambaza uzushi huu ulioasisiwa na mkuu wa wanafiki. Mtume ﷺ alifadhaika sana aliposikia taarifa na uzushi ule, lakini muda wote huo Aishah رضي الله عنها hakuwa na taarifa yeyote juu ya uzushi ule.

Siku moja usiku, mama Aishah alitoka na mama wa Mastah ibn Athathah. Mama Aishah akawa anaongea na kubadilishana naye mazungumzo. Mama Aishah akawa anasema kwamba ni maswahaba wa Mtume ﷺ waliopigana vita vya Badr ndio waliokuwa wanastahili heshima. Mama yule akagundua kuwa Aishah alikuwa hajui nini kilikuwa kinazungumzwa mitaani kuhusu yeye – juu ya tuhuma za uongo zilizokuwa zikisambazwa na wanafiki.Mama yule akamwambia mama Aishah kile kilichokuwa kikizungumzwa juu yake bila yeye kuwa na habari. Aliporudi nyumbani, alimuomba ruhusa mumewe – Mtume Muhammad ﷺ na kwenda kuwatembelea wazazi wake.

Alipokuwa kwa wazazi wake, muda wote alikuwa akilia sana kwa uchungu, wazazi wake walijaribu kum-bembeleza huku wakimuhakikishia kuwa kila kitu kitamalizika kwa uwezo wa Allah. Lakini alizidi kulia kwa uchungu kwa sababu hakuwahi kufikiria hata siku moja kama watu tena waliodai kuwa ni Waislamu wangeweza kuzusha uongo mbaya na mkubwa kiasi kile tena kwake yeye – mke wa Mtume wa Allah. Baada ya kulia mfululizo usiku na mchana kutwa kwa siku mbili, mama Aishah akawa mgonjwa. Asubuhi ya siku ya tatu, Mtume ﷺ akaja kumjulia hali; Kwa ujasiri mkubwa Mtume ﷺ akamwambia kwamba, ikiwa ni kweli alifanya makosa (akafanya machafu) basi anapaswa kumuomba msamaha Allah. Aishah alimwambia mume wake kwamba, ikiwa atakataa kuwa hakufanya jambo hilo hakuna mtu atakayemuamini; lakini kwa hakika yeye hakufanya kosa hilo na Allah Anatosha kuwa shahidi. Jibu sahihi kwa tuhuma hizi ilikuwa ni kunukuu maneno ya baba wa Yusuf, pale aliposema:

فَصَبْرٌ جَمِيلٌ ۖ وَٱللَّهُ ٱلْمُسْتَعَانُ عَلَىٰ مَا تَصِفُونَ ﴿١٨﴾

***"........Basi (yangu mimi ni) subira njema, na Mwenyezi Mungu ndiye aombwaye msaada kwa haya mnayoyasema."*** **(12:18)**

Ni katika wakati huu, Ayah zilishushwa zikimtakasa mama Aishah kuwa kwa hakika hakuwa amefanya kosa lolote. Baada ya *Wahyi* kumalizika, Mtume ﷺ alikwenda tena kwa mama Aishah رضي الله عنها huku akiwa anatabasamu na kuanza kusoma Ayah zile zilizoshushwa:

إِنَّ ٱلَّذِينَ جَآءُو بِٱلْإِفْكِ عُصْبَةٌ مِّنكُمْ ۚ لَا تَحْسَبُوهُ شَرًّا لَّكُم ۖ بَلْ هُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۚ لِكُلِّ ٱمْرِئٍ
مِّنْهُم مَّا ٱكْتَسَبَ مِنَ ٱلْإِثْمِ ۚ وَٱلَّذِى تَوَلَّىٰ كِبْرَهُۥ مِنْهُمْ لَهُۥ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١١﴾ لَّوْلَآ إِذْ
سَمِعْتُمُوهُ ظَنَّ ٱلْمُؤْمِنُونَ وَٱلْمُؤْمِنَٰتُ بِأَنفُسِهِمْ خَيْرًا وَقَالُوا۟ هَٰذَآ إِفْكٌ مُّبِينٌ ﴿١٢﴾ لَّوْلَا
جَآءُو عَلَيْهِ بِأَرْبَعَةِ شُهَدَآءَ ۚ فَإِذْ لَمْ يَأْتُوا۟ بِٱلشُّهَدَآءِ فَأُو۟لَٰٓئِكَ عِندَ ٱللَّهِ هُمُ ٱلْكَٰذِبُونَ ﴿١٣﴾
وَلَوْلَا فَضْلُ ٱللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُۥ فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْءَاخِرَةِ لَمَسَّكُمْ فِى مَآ أَفَضْتُمْ فِيهِ عَذَابٌ عَظِيمٌ
﴿١٤﴾ إِذْ تَلَقَّوْنَهُۥ بِأَلْسِنَتِكُمْ وَتَقُولُونَ بِأَفْوَاهِكُم مَّا لَيْسَ لَكُم بِهِۦ عِلْمٌ وَتَحْسَبُونَهُۥ هَيِّنًا
وَهُوَ عِندَ ٱللَّهِ عَظِيمٌ ﴿١٥﴾ وَلَوْلَآ إِذْ سَمِعْتُمُوهُ قُلْتُم مَّا يَكُونُ لَنَآ أَن نَّتَكَلَّمَ بِهَٰذَا

سُبْحَٰنَكَ هَٰذَا بُهْتَٰنٌ عَظِيمٌ ﴿١٦﴾ يَعِظُكُمُ ٱللَّهُ أَن تَعُودُوا۟ لِمِثْلِهِۦٓ أَبَدًا إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ
﴿١٧﴾ وَيُبَيِّنُ ٱللَّهُ لَكُمُ ٱلْءَايَٰتِ ۚ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٨﴾ إِنَّ ٱلَّذِينَ يُحِبُّونَ أَن تَشِيعَ
ٱلْفَٰحِشَةُ فِى ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْءَاخِرَةِ ۚ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا
تَعْلَمُونَ ﴿١٩﴾ وَلَوْلَا فَضْلُ ٱللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُۥ وَأَنَّ ٱللَّهَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٠﴾ ۞ يَٰٓأَيُّهَا
ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَتَّبِعُوا۟ خُطُوَٰتِ ٱلشَّيْطَٰنِ ۚ وَمَن يَتَّبِعْ خُطُوَٰتِ ٱلشَّيْطَٰنِ فَإِنَّهُۥ يَأْمُرُ
بِٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ ۚ وَلَوْلَا فَضْلُ ٱللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُۥ مَا زَكَىٰ مِنكُم مِّنْ أَحَدٍ أَبَدًا وَلَٰكِنَّ
ٱللَّهَ يُزَكِّى مَن يَشَآءُ ۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢١﴾

***“Hakika wale walioleta uwongo huo (kwa kumsingizia Bibi Aisha – mkewe Mtume – kuwa amezini) ni kundi miongoni mwenu, (ni jamaa zenu). Msifikiri ni shari kwenu, bali hiyo ni heri kwenu. Kila mtu katika wao atapata aliyoyachuma katika madhambi hayo. Na yule aliyejitwika sehemu yake kubwa miongoni mwao, atapata adhabu kubwa (zaidi). Mbona mliposikia (habari) hii, wanaume Waislamu na Wanawake Waislamu hawakuwadhania wenzao mema, na kusema “huu ni uzushi dhahiri?”. Mbona hawakuleta mashahidi wanne? Na walipokosa kuleta mashahidi, basi hao mbele ya Mwenyezi Mungu ni waongo. Na kama isingelikuwa juu yenu fadhila ya Mwenyezi Mungu na rehema Yake katika dunia na akhera, bila shaka ingelikupateni adhabu kubwa kwa sababu ya yale mliyoyashughulikia. Mlipoupokea (uongo huo mkawa mnautangaza) kwa ndimi zenu na mkasema kwa vinywa vyenu msiyoyajua, na mlifikiri ni jambo dogo, kumbe mbele ya Mwenyezi Mungu ni kubwa. Na mbona, mliposikia, hamkusema: “Haitujuzii kuzungumza haya: Utakatifu ni wako (Mola wetu!). Huu ni uwongo mkubwa.” Mwenyezi Mungu Anakunasihini msirudi kabisa kufanya mfano wa haya, ikiwa nyinyi ni Waislamu kweli. Na Mwenyezi Mungu Anakubainishieni Aya zake; na Mwenyezi Mungu ndiye Ajuaye, Mwenye hikima. Kwa yakini wale wanaopenda uenee uovu kwa wale walioamini; watapata adhabu***

***iumizayo katika dunia na akhera; na Mwenyezi Mungu ndiye Anayejua (ya maslaha yenu), na nyinyi hamjui. "Na (yangetokea machafuko makubwa) isingelikuwa fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema Yake na kuwa Mwenyezi Mungu ni Mpole, Mwenye huruma. Enyi mlioamini! Msifuate nyayo za Shetani; na atakayefuata nyayo za Shetani (atapotea) kwani yeye huamrisha mambo ya aibu na maovu; na lau kuwa si fadhila za Mwenyezi Mungu na rehema yake juu yenu asingalitakasika miongoni mwenu hata mmoja, lakini Mwenyezi Mungu humtakasa Amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia (na) Mwenye Kujua."* (24:11-21)**

Wazazi wake walifurahi sana na wakapata nguvu; Walifurahi sio tu kwa sababu mtoto wao alikuwa hakufanya kosa lile la uzinifu, bali pia kwa sababu mtoto wao amepata heshima ya kuwa sababu ya kushuka Ayah za Qur'an; na kwamba ni Qur'an iliyokuja kumsafisha na kuthibitisha kuwa kwa hakika hakuwa amefanya kosa. Walimtaka mtoto wao kuinuka na kumshukuru mume wake. Aishah رضي الله عنها akajibu, "Bila shaka napaswa kuwa mwingi wa shukurani kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu yeye ameshusha Ayah za Qur'an kwa ajili yangu – kwa ajili ya kuniondoa na kuniweka huru kutokana na tuhuma zilizoenezwa na wanafiki."

Baada ya tukio hili, mapenzi ya Mtume ﷺ kwa mama Aishah رضي الله عنها yakaongezeka mara dufu. Siku moja 'Amr ibn 'Aas رضي الله عنه alimuuliza Mtume Muhammad ﷺ, 'nani alikuwa anampenda sana katika dunia hii?' Mtume ﷺ akajibu kuwa, 'anampenda zaidi Aishah رضي الله عنها kuliko mtu mwingine yeyote.' Kisha 'Amr ibn 'Aas رضي الله عنه akamuuliza Mtume wa Allah ﷺ, 'nani alikuwa anampenda zaidi miongoni mwa wanaume wote?' Mtume ﷺ akasema 'anampenda zaidi baba wa Aishah (Abu Bakr رضي الله عنه) kuliko wote.' Katika tukio moja, 'Umar ibn Al-Khattab alimkataza binti yake Hafsah asishindane na Aishah رضي الله عنها kwa sababu Mtume Muhammad ﷺ alikuwa akimpenda na kumthamini sana.

Mtume ﷺ alikuwa akipenda sana kumsikiliza mama Aishah رضي الله عنها wakati akizungumza na mara zote alikuwa akitabasamu wakati mama Aishah alipokuwa akizungumza. Pengine hili linaweza kuwa somo na funzo muhimu

kwa wanaume namna ya kuishi na kuongea na wake zao bila kujali ni mke mkubwa, mdogo au mwanaume huyo ana wake wangapi.

Katika sherehe moja ya 'Eid, kulikuwa na Waafrika waliokuwa wakionesha ujuzi na maarifa yao katika kutumia mikuki; Aishah رضي الله عنها alitamani na yeye ashuhudie maonesho yale. Mtume ﷺ akasimama mbele yake ili na yeye aangalie maonesho yale na kufurahi bila yeye mwenyewe (Aishah) kuonekana. Na Mtume ﷺ hakuondoka pale mpaka mama Aishah رضي الله عنها alipokuwa ameangalia na kutosheka.

Pamoja na kuangalia burudani hizi, bado mambo haya hayakumfanya Mtume Muhammad ﷺ asahau wajibu na majukumu yake kwa Allah. Aliposikia adhana, haraka sana alijiandaa na kuelekea msikitini. Mapenzi yake kwa Allah yalikuwa juu na yalishinda kila kitu.

Walipoweka kambi mahala fulani jangwani, na mkufu wa mama Aishahرضي الله عنها ukaanguka na kupotea kwa mara nyingine. Baadhi ya maswahaba walitumwa kwenda kuutafuta. Ilipoadhiniwa Swala ya alfajiri, kulikuwa hakuna maji kwa ajili ya kutawadha. Maswahaba wakawa na hofu watafanyaje ili kushika udhu kwaajili ya Swala.Wakaanza kumlaumu mama Aishah kuwa ndiye aliyesababisha, kwa sababu walichelewa kutoka pale wakiwasubiri wenzao waliokwenda kutafuta mkufu wake. Baba yake (Abu Bakr) alimlaumu sana mwanae kwa kusababisha hali ile, hali iliyokuwa inatishia Waislamu kushindwa kutekeleza ibada ya Swala. Ni katika wakati huu, Ayah ifuatayo ilishushwa kwa Mtume ﷺ

وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰٓ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَآءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ ٱلْغَآئِطِ أَوْ لَٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُوا۟
مَآءً فَتَيَمَّمُوا۟ صَعِيدًا طَيِّبًا فَٱمْسَحُوا۟ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ عَفُوًّا غَفُورًا ﴿٤٣﴾

***" ...Na kama mkiwa wagonjwa (mmekatazwa kutumia maji) au mmo safarini au mmoja wenu ametoka msalani (chooni) au mmewagusa wanawake – na msipate maji – basi ukusudieni (tayamamuni) udongo safi, mpake nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kurehemu na Kusamehe (na) Mwenye Kughufiria."*** **(4:43)**

Watu walimshukuru sana mama Aishah kwa yeye kuwa sababu ya Allah Mwingi wa Rehema kuwahurumia na kuwapa njia ya kufanya kutokana na yeye. Ni katika wakati huu, Abu Bakr As-Siddiq رضي الله عنه alikuja kubaini na kufahamu ni kwa kiasi gani Allah alikuwa amemridhia Aishah رضي الله عنها.

Mwaka wa tisa baada ya Hijrah, Uislamu ulikuwa umeenea bara Arabu lote, na Madinah ikawa kitovu cha dola Kiislamu. Baadhi ya wake wa Mtume ﷺ wakaomba waongezewe posho ya matumizi. Jambo hili halikumfurahisha Mtume wa Allah ﷺ, akaamua kuwa mwezi mmoja atajitenga na wake zake na kukaa peke yake.

Baada ya siku ishirini na tisa (29) alikuja nyumbani kwa mama Aishah, na kumtaka achague baada ya kushauriana na wazazi wake; achague kati ya kuendelea kuishi na Mtume ﷺ na hali yake ngumu ya kimaisha au amuache na aende kuishi maisha yenye wasaa (maisha mazuri). Aishah رضي الله عنها hakuwa na shaka yeyote wala hakupata tabu katika kuchagua kwake. Mara moja alijibu kuwa, yeye na wazazi wake wako tayari kujitoa muhanga kwa ajili ya Mtume ﷺ ikiwa hali itawataka wafanye hivyo, na kwamba kulikua hakuna haja ya yeye kwenda kushauriana na wazazi wake juu ya jambo hili.Alisisitiza kwamba yeye anachagua kuishi na kuwa na Mtume ﷺ kuliko dunia yote na anasa zote zilizomo. Tabasamu la furaha liliupamba uso wa Mtume ﷺ.

Kisha Allah Akashusha Ayah ifuatayo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ قُل لِّأَزْوَٰجِكَ إِن كُنتُنَّ تُرِدْنَ ٱلْحَيَوٰةَ ٱلدُّنْيَا وَزِينَتَهَا فَتَعَالَيْنَ أُمَتِّعْكُنَّ وَأُسَرِّحْكُنَّ سَرَاحًا جَمِيلًا ﴿٢٨﴾ وَإِن كُنتُنَّ تُرِدْنَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَٱلدَّارَ ٱلْءَاخِرَةَ فَإِنَّ ٱللَّهَ أَعَدَّ لِلْمُحْسِنَٰتِ مِنكُنَّ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٢٩﴾

***"Ewe Mtume! Waambie wake zako: "Ikiwa mnapenda maisha ya (hii) dunia na uzuri wake (mimi sinayo, na mimi siwezi kukulazimisheni kukaa na mimi katika hali ya ufakiri; basi mkipenda nikuacheni), njooni, nitakupeni kitoka nyumba, (baadhi ya matumizi) na kukuacheni muwachano mzuri".Na kama mnamtaka Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na nyumba ya akhera, basi Mwenyezi Mungu Amewaandalia wafanyao mema hayo, miongoni mwenu, malipo makubwa".*** **(33:28-29)**

Wake wote wa Mtume ﷺ wakachukua msimamo sawa na aliouchukua mama Aishah رضي الله عنها.

Katika matukio mawili, mama Aishah رضي الله عنها alimuona malaika Jibril:

Katika tukio la kwanza, mama Aishah alimuona Mtume ﷺ akiongea na mtu mmoja aliyekuwa amepanda farasi; alipomuuliza Mtume ﷺ kuhusu mtu yule alikuwa ni nani, Mtume ﷺ alishangaa kusikia kuwa mama Aishah رضي الله عنها alikuwa amemuona na akamjibu kuwa alikuwa ni Malaika Jibril aliyekuja katika umbile la mwanadamu na kwamba Malaika Jibril alikuwa anamsalimia. Mama Aishah رضي الله عنها akafurahi sana na kumuomba Allah Amlipe kheri mgeni yule (Malaika Jibril) na mwenyeji wake (Mtume Muhammad ﷺ).

Anas anasimulia kuwa: Wakati fulani Mtume wa Allah ﷺ alikuwa akiswali ndani ya nyumba ya mama Aishah رضي الله عنها, mama Aishah akamuona mtu mmoja amesimama nje ya mlango. Baada ya Mtume ﷺ kumaliza kuswali, alimfahamisha juu ya mtu yule aliyesimama pale nje kuwa alikuwa ni Malaika Jibril. Mtume Muhammad ﷺ akamkaribisha aingie ndani lakini Malaika Jibril akajibu kuwa, huwa (Malaika) hawaingii katika nyumba ambayo kuna mbwa au kuna picha. Mtume ﷺ alipoangaza ndani ya nyumba, aliona mtoto wa mbwa kwenye kona ndani ya nyumba; walipomfukuza yule mtoto wa mbwa na kuondoka Malaika Jibril akaingia ndani. Aishah رضي الله عنها alifikia kuwa na hadhi kubwa kiasi hiki kutokana na elimu na ucha-Mungu wa hali ya juu. Mama huyu alifahamika pia kwa elimu kubwa aliyokuwa nayo. Kila mtu alikuwa akimuuliza katika mambo mbalimbali yanayohusu dini; Takriban hadithi 2,210 za Mtume ﷺ zimepokelewa kupitia kwake. Yeye ni miongoni mwa maswahaba saba waliopokea hadithi nyingi za Mtume ﷺ.

Wakati wa wema waliotangulia *(Khulafa-u-Rashidin)*, hukumu zake *(Fatwa)* zilikuwa zinakubalika. Mtu mmoja alimuuliza Masruq kama mama Aishah رضي الله عنها alikuwa ana ujuzi katika masuala ya Shariah hususan katika masuala ya mirathi. Masruq aliapa kuwa aliwaona na kuwashuhudia maswahaba wakimuuliza maswali magumu yanayohusu mirathi. 'Urwah ibn Zubayr رضي الله عنه, mtoto wa mdogo wake Aishah رضي الله عنها – Asma alikuwa akimtembelea mara kwa mara na kujadiliana nae juu ya maswala mbalimbali yanayohusu dini. Maswahaba wengine walikuwa wakimuonea wivu 'Urwah kwa sababu yeye alikuwa huru na alikuwa anaweza kumuona na kuongea naye muda wowote.

Wakati fulani Mtume ﷺ na mama Aishah walikuwa hawajisikii vizuri (walikuwa wanaumwa). Mtume ﷺ akasema kumwambia mkewe, ikiwa mama Aishah رضي الله عنها atafariki kabla yake, basi atamuosha, atamvika sanda, atamzika na atamuombea dua. Kwa lugha laini mama Aishah akajibu kwa utani kuwa inaonekana Mtume atafurahia kifo chake; kisha mama Aisha رضي الله عنها akasema kama yeye (mama Aishah رضي الله عنها) atafariki mapema kabla yake, itamlazimu Mtume ﷺ aoe na kuleta mke mwingine ndani ya nyumba yake. Mtume ﷺ kusikia maneno yale, akatabasamu.

Kaka yake Aishah رضي الله عنها, 'Abdur-Rahman alikuja nyumbani kwa Mtume ﷺ akiwa ameshika mti wa mswaki mkononi mwake; Mtume ﷺ aliuangalia kama mtu aliyekuwa akiutamani au kuuhitaji. Mama Aishah رضي الله عنها alitambua mara moja na akamuuliza kama Mtume ﷺ alikuwa akihitaji. Mtume wa Allah ﷺ aliashiria kwa kichwa kuwa alikuwa anahitaji, mama Aishah akaulainisha kwa meno yake kisha akampatia mswaki ule Mtume ﷺ. Mtume ﷺ alisafisha meno yake; na akawa akichovya mkono wake mara kwa mara katika chombo kilichokuwa na maji na kuufuta uso wake tena na tena na huku akirudia kusema maneno haya:

"Hapana Mola apasae Kuabudiwa kwa Haki isipokuwa Allah; Hakika, Maumivu ya kutokwa na roho yanauma sana!" Kisha aliangalia juu na kusema, "Naelekea kwa kipenzi changu."

Wakati fulani mama Aishah aliota ndoto kuwa miezi mitatu inayong'ara ilikuwa imeshuka ndani ya nyumba yake. Mtume ﷺ alipofariki, alizikwa ndani ya nyumba ya mama Aishah; baba yake – Abu Bakr رضي الله عنه akamwambia kuwa, sehemu ya ndoto yake ilikuwa imekamilika siku ile – kwamba mwezi mmoja (Mtume wa Allah) ulikuwa tayari unaiangazia nyumba yake. Baadaye, baba yake Aishah (Abu Bakr) na Umar ibn Al-Khattab رضي الله عنهما walifariki na wakazikwa ndani ya nyumba ya mama Aishah رضي الله عنها jirani kabisa na lilipo kaburi la Mtume ﷺ na kutimiza ndoto yake iliyohusu miezi mitatu kushuka ndani ya nyumba yake.

Imam Dhahabi ananukuu hadithi ya Mtume ﷺ akisema kuwa, roho za mitume hutoka (mitume hufariki) mahala wanapopapenda zaidi; Hii inamaanisha kuwa, bila shaka Mtume alifariki dunia akiwa sehemu aliyoipenda zaidi – nyumbani kwa mama Aishah رضي الله عنها.

Mama Aishah رضي الله عنها alifariki dunia na kuelekea katika makazi matukufu aliyoandaliwa na Mola wake – Peponi, tarehe 17 mwezi wa Ramadhani mwaka wa 58 Hijiriya, akiwa na umri wa miaka 66.Alizikwa katika eneo maarufu la Jannatul Baqi', na swahaba wa Mtume ﷺ - Abu Hurairah رضي الله عنه ndiye aliyeongoza Swala ya jeneza.

# Hafsah bint ‘Umar

## Mke wa Mtume Peponi

Siku moja Malaika Jibril alimwambia Mtume wa Allah ﷺ kuhusu Hafsah رضي الله عنها: *“Mara nyingi mwanamke huyu huwa amefunga na hufanya sana ibada, na atakuwa mke wako Peponi.”* (Mustadrak Al-Hakim 4/15)

Hafsah رضي الله عنها alikuwa ni binti wa swahaba maarufu na Khalifa wa pili baada ya Khalifa Abu Bakr - ‘Umar ibn Khattab رضي الله عنهما ambaye pia anafahamika kama Umar Al-Faruq رضي الله عنه. Mjomba wa mama huyu alikuwa Zayd ibn Khattab رضي الله عنه na bila shaka, ni dada wa ‘Abdullah ibn ‘Umar.

Hafsah رضي الله عنها alikuwa mwanamke mcha-Mungu sana, mwanamke ambaye alikuwa akitumia muda wake mwingi sana katika Swala na mara nyingi alikuwa katika Swaumu. Alikua mjuzi na mtaalamu wa kuandika; lakini pia alikuwa fasaha katika kuzungumza na mfuasi sahihi na mwaminifu wa Uislamu.

Hafsah bint Khattab رضي الله عنها alikuwa mwenye sifa nyingi nzuri na za kicha-Mungu kiasi kwamba mama Aishah alifikia kusema kuwa, miongoni mwa wake wa Mtume ﷺ, basi angeweza kujilinganisha naye. Maisha yake yalikuwa ya kawaida na ya kupigiwa mfano, kwa sababu yeye alilelewa na swahaba anayefahamika kwa ucha-Mungu na msimamo usioyumba hasa linapokuja swala la Uislamu na kumuamini Allah na Mtume wake ﷺ. ‘Umar ibn Khattab رضي الله عنه, huyu ndiye baba mzazi wa mama huyu. Bila shaka unaweza kuvuta hisia na kupata picha mtoto aliyelelewa na swahaba huyu atakuwa mtoto mwenye malezi gani.

Hafsah رضي الله عنها alizaliwa katika familia ya shujaa na bingwa wa mieleka –’Umar ibn Khattab رضي الله عنه ambaye alifahamika sana kwa taaluma na ujuzi aliokuwa nao katika sanaa ya mapigano ya kutumia mikono. Katika miaka ya kukua kwake, mama Hafsah رضي الله عنها alijikuta akipata bahati ya kukua na

kulelewa katika mazingira ya Kiislamu, wakati ambao wazazi wake wote, shangazi zake na wajomba zake wakiwa tayari wamesilimu na kuingia katika Uislamu. Alipofikia umri wa kutosha, aliolewa na Khunais ibn Hudhaifa As-Sahmi. Bwana huyu alikuwa amevutiwa na ulinganiaji na mafundisho aliyokuwa akiyafanya Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه na kuamua kuingia katika Uislamu.

Kutokana na mateso makali, ukatili na unyanyasaji uliopindukia, Khunais ibn Hudhaifa alilazimika kuhamia Madinah yeye pamoja na mke wake. Alipofika Madinah, alipokelewa na Rafa'h ibn 'Abdul Munthir na kuishi katika nyumba yake kama mwenyeji wake pale Madinah.

Wote wawili, mke na mume – Khunais ibn Hudhaifa na Hafsah رضي الله عنها wakayapenda na kuyafurahia maisha mapya pale Madinah. Mama Hafsah رضي الله عنها alijiwekea utaratibu wa kuhifadhi Qur'an kila ilipokuwa ikishushwa. Kisha alikuwa akijitahidi kuelewa maana na ujumbe uliokuwa umebebwa na Ayah zile na kuzifanyia kazi. Wakati huo, mume wake alikuwa akijiandaa kwa ajili ya Jihad huku akiwa na furaha na hamu kubwa kupata fursa ya kushiriki katika ibada kubwa ya kuupigania Uislamu huku akijiimarisha zaidi katika mbinu za sanaa ya mapigano kwa kutumia mikono. Muda wote alikuwa anafuatilia nyendo za maadui na alikuwa anasubiri kwa hamu kukabiliana nao.

Habari ziliwafikia Waislamu kuwa, baada ya Maquraishi wa Makkah kufanya maandalizi ya kutosha kwa ajili ya vita walivyokusudia kuwasambaratisha Waislamu na kuufuta Uislamu, walikuwa wameanza safari kuja Madinah chini ya uongozi wa Abu Jahl. Waislamu chini ya uongozi wa Mtume ﷺ, wakiwa hawana silaha walifika katika viwanja vya Badr na wakaweka kambi yao huku wakidhibiti vyanzo vya maji. Kitu pekee walichokuwa nacho Waislamu ilikuwa ni imani thabiti kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ﷺ.

Khunais ibn Hudhaifa mume wa Hafsah رضي الله عنها, 'Umar ibn Khattab (Faruq), mjomba wa Hafsah na binamu yake wote walikuwa sehemu ya wapiganaji katika jeshi la Waislamu. Mume wa Hafsah رضي الله عنها alikuwa na hamu sana ya kuhakikisha anapambana kwa nguvu sana katika vita ile na kuhakikisha anapeleka ushindi kwa Waislamu na kupeleka msiba mkubwa kwa jeshi la makafiri wa Makkah. Hatimaye majeshi ya pande mbili yalikutana na vita vikaanza. Khunais ibn Hudhaifa akapambana kishujaa huku akipenya

katikati ya maadui na kushambulia kwa nguvu sana. Akajeruhiwa vibaya sana, hata hivyo viongozi wengi wa makafiri wakauwawa na Waislamu wakapata ushindi mkubwa. Hii ilikuwa ni miongoni mwa vita kubwa kabisa katika historia ya Uislamu, vita vya Badr; vita ambavyo watu wachache wasiokuwa na silaha waliwashinda maelfu ya wapiganaji waliokuwa na silaha tena waliojiandaa vema kwa ajili ya vita dhidi ya Waislamu.

Hafsah bint Khattab رضي الله عنها aliposikia matendo ya kishujaa aliyoyafanya mume wake, alifurahi sana, na kumpongeza kwa kazi aliyoifanya katika uwanja wa vita. Lakini alifahamu fika kuwa, katika hali aliyokuwa nayo mume wake, alihitaji kupata matunzo na uangalizi maalumu kadri ilivyowezekana. Alisoma Aya kutoka Surat Al-Anfal, Ayah ambayo ilishushwa kutokana na vita vya Badr:

وَمَا جَعَلَهُ ٱللَّهُ إِلَّا بُشۡرَىٰ وَلِتَطۡمَئِنَّ بِهِۦ قُلُوبُكُمۡۚ وَمَا ٱلنَّصۡرُ إِلَّا مِنۡ عِندِ ٱللَّهِۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ۝١٠

***"Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila iwe bishara (habari ya furaha) na ili nyoyo zenu zitue kwayo. Na hakuna msaada (wa kufaa) ila utokao kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima)."*** **(8:10)**

Maneno haya kutoka katika Qur'an, maneno ya Allah Mtukufu yanayowaahidi Waislamu ushindi yalimtia moyo na kumzidishia furaha.Alilielekea jukumu la kumuuguza mume wake ili arejee kuwa na afya njema. Lakini haikusaidia, kwani Allah tayari alikuwa amepanga kumuinua daraja na kumuweka katika mahala patukufu – Peponi, sawa na wale waliotangulia kabla yake katika njia ya Allah Mtukufu. Siku chache baadaye, maumivu ya majeraha yaliongezeka na hatimaye mume wa Hafsah رضي الله عنها akafariki dunia na kurejea kwa Mola wake.

Mtume ﷺ alipopata habari ya kifo chake, aliandaa maziko yake katika eneo la Jannatul Baqi, jirani kabisa na lilipokuwa kaburi la mjomba wake Hafsah رضي الله عنها. Mtume ﷺ mwenyewe ndiye aliyeongoza Swala ya jeneza. Kama ilivyo kwa binadamu yeyote, Hafsah رضي الله عنها alijihisi uchungu wa kuondokewa na mumewe. Hata hivyo, kama muumini wa kweli alimkabidhi yote Allah akiamini kuwa Yeye ndiye Aliyemuumba mume wake na alikuwa amerejea Kwake. Baada ya hapo, Hafsah رضي الله عنها alizidisha ibada na kumkumbuka zaidi Mwenyezi Mungu. Wakati huo, Hafsah رضي الله عنها alikuwa na umri wa miaka ishirini na moja (21) tu.

Ama kwa upande wa baba yake Hafsah رضي الله عنها – Umar ibn Khattab, jambo hili lilimuumiza na kumuhuzunisha sana kumuona mwanae Hafsah رضي الله عنها yuko katika huzuni ya kufiwa na mume wake tena katika umri ule wa miaka ishirini na moja tu. Ukimya na ujasiri wake katika hali hii, kuzidisha kwake ibada za Swala na kusoma sana Qur'an vilimzidishia nuru katika moyo wake. Hata hivyo bado alikuwa anasumbuliwa na upweke, jambo ambalo sasa lilikuwa limekuwa sehemu ya maisha yake. Baada ya kutafakari kwa kina huku akimuonea huruma binti yake, 'Umar ibn Khattab رضي الله عنه aliamua kumuendea rafiki yake 'Uthman ibn Affan رضي الله عنه, ambaye kwa wakati huo na yeye alikuwa amefiwa na mke wake Ruqayyah – mtoto wa Mtume Muhammad ﷺ. Umar ibn Khattab رضي الله عنه aliamini kuwa, kwa kuwa wote wawili Hafsah na Uthman wana shida zinazofanana. Hafsah kafiwa na mumewe na Uthman kafiwa na mkewe. Itasaidia kuondoa unyonge wao ikiwa watafunga ndoa na kuishi pamoja. Baada ya kufikiria wazo hili, Umar ibn Khattab aliondoka moja kwa moja kwenda kwa 'Uthman رضي الله عنه. Baada ya kusalimiana naye na kumpa pole kufuatia kifo cha mke wake, alianzisha mazungumzo juu ya kile alichokusudia. 'Uthman alitazama chini kwa muda kisha akamwambia rafiki

yake kipenzi Umar ibn Khattab kuwa, alihitaji muda zaidi kulitafakari kwa kina jambo hili alilomuwasilishia – wazo la kumuoa Hafsah bint Khattab رضي الله عنه.

'Umar ibn Khattab رضي الله عنه alikutana kwa mara nyingine na rafiki yake Uthman Ibn Affan رضي الله عنه baada ya masiku kadhaa na kumkumbusha juu ya pendekezo lake. 'Uthman رضي الله عنه akamjibu kuwa kwa sasa alikuwa bado hajawa na mpango wa kuoa. Baada ya kutoka hapo, Umar ibn Khattab رضي الله عنه aliondoka moja kwa moja na kwenda kwa Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه na kumuomba amuoe bint yake Hafsah. Abu Bakr رضي الله عنه naye aliinamisha kichwa chini na hakumjibu chochote.

'Umar ibn Khattab رضي الله عنه alikuwa akijisikia vibaya kwa sababu alikuwa akihisi kuwa, watu aliokuwa akiwaendea na kuwaomba wamuoe mwanae Hafsah رضي الله عنها walikuwa aidha wanamkwepa au walikuwa hawataki kumuoa bint yake Hafsah. Alikuwa na matarajio makubwa sana ya kukubaliwa mapendekezo yake na alikuwa akijiandaa kuwa na furaha juu ya jambo hili, lakini mambo hayakwenda vile alivyotarajia. Halikuwa jambo alilolitarajia kutokea hasa ukizingatia nafasi yake, nafasi ya wale aliowaendea na hadhi ya binti yake. Watu aliowaendea aliamini itakuwa heshima kwake kuungana nao na kuwa na mafungamano ya kidugu kutokana na mwanae. Akiwa na huzuni ya kupata majibu ambayo hakuyatarajia. Akiwa mwenye huzuni na mnyonge, Umar ibn Khattab alienda kwa Mtume ﷺ na kumuelezea hali aliyokuwa nayo na yale yaliyokuwa yamejiri. Mtume ﷺ alitabasamu na kumwambia hapaswi kuwa na huzuni au kuwa mnyonge, na kwamba kama Allah Akipenda, Atampatia Hafsah mume bora kuliko 'Uthman na 'Uthman atampatia mke bora kuliko Hafsah.

'Umar ibn Khattab alifurahi na kufarijika kusikia maneno haya ya Mtume ﷺ, lakini bado alikuwa akijiuliza ni mwanaume gani huyo atakae kuwa bora kuliko Abu Bakr na Uthman ibn Affan? Siku chache baadaye Mtume ﷺ akamuozesha mwanae Umm Kulthum bint Muhammad (mtoto wa Mtume wa Allah) kwa 'Uthman ibn Affan. 'Umar ibn Khattab رضي الله عنه akathibitisha kuwa sehemu ya kwanza ya maneno ya Mtume wa Allah ﷺ yametimia – kwamba Allah Atampa Uthman mke bora kuliko Hafsah. Kwa sababu ni kweli kuwa mtoto wa Mtume alikuwa bora kuliko mtoto wa Umar ibn Khattab. Swali likabakia juu ya nani atakuwa mume wa Hafsah ambaye Mtume wa Allah ﷺ alisema atakuwa bora kuliko Abu Bakr na 'Uthman?.

Baada ya hapo Mtume ﷺ akapeleka posa kwa ajili ya kumuoa Hafsah. ‘Umar ibn Khattab رضي الله عنه hakuamini kile alichokisikia, kwa sababu hii ilikuwa ni zaidi ya heshima kubwa kwake na kwa mwanae pia. Hii ilimaanisha kuwa mwanae sasa anaingia katika orodha ya wanawake wenye heshima ya pekee, heshima ya kuwa mke wa Mtume ﷺ na mama wa Waumini wote. Wakati huo tayari Mtume ﷺ alikuwa amekwisha waoa Aishah na Sawdah رضي الله عنهما. Hivi ndivyo mama Hafsah, mtoto wa swahaba maarufu na Khalifa wa pili Umar ibn Khattab رضي الله عنه alivyokuja kuolewa na Mtume wa Allahﷺ mwaka wa tatu baada ya Hijrah, kabla ya vita vya Uhud. Wakati huo mama Hafsah alikuwa na umri wa miaka ishirini na mbili (22) tu.

Imam Bukhari katika kitabu chake cha hadithi As-Sahih Al-Bukhari, kuna hadithi ifuatayo ikilizungumzia tukio hili:

Imesimuliwa na ‘Abdullah ibn ‘Umar: Umar ibn Al-Khattab رضي الله عنه anasema, “Mwanangu Hafsah bint ‘Umar alipofiwa na mume wake Khunais ibn Hudhaifa As-Sahrni ambaye alikuwa mmoja kati ya maswahaba wa Mtume wa Allah ﷺ ambaye alipigana katika vita vya Badr na baadaye akafariki akiwa Madinah, nilimwendea ‘Uthman ibn ‘Affan na kutoa mapendekezo kuwa amuoe Hafsah nikimwambia kuwa, “Kama uko tayari, nitakuozesha mwanangu Hafsa bint ‘Umar,” baada ya kumwambia hivyo, alijibu, “nahitaji muda zaidi wa kutafakari jambo hili”. Nilisubiri kwa siku kadhaa na nilipomuuliza kwa mara nyingine aliniambia kuwa, “Sijawa na nia ya kuoa kwa sasa.” Baada ya hapo nilimuendea Abu Bakr na kumwambia, “Kama utapenda, niko tayari kukuozesha mwanangu Hafsah bint ‘Umar.” Alikaa kimya na hakusema chochote na nilimchukia sana kuliko nilivyomchukia Uthman. Baada ya siku kadhaa kupita, Mtume wa Allah ﷺ akataka kumuoa na nikamuozesha. Baadaye Abu Bakr alikutana na mimi na kuniambia, “Ulichukia pale ulipotaka kuniozesha Hafsah na sikukupa jibu lolote?” Nikamjibu “Ndiyo”. Abu Bakr akaniambia, “Hakuna kilichonizuia kukubali ombi lako isipokuwa nilikuwa na habari kuwa Mtume wa Allah ﷺ alikuwa anakusudia kumuoa Hafsah na sikutaka kufichua siri ya Mtume wa Allah ﷺ. Lakini kama angebadili dhamira yake (Mtume) basi bila shaka ningekubali kumuoa Hafsah.”

Mwanachuoni mkubwa na maarufu, Sa’id ibn Al-Musayyab رضي الله عنه anasema; ubashiri wa Mtume ﷺ ulithibiti kuwa ni kweli kwa sababu, Mtume wa Allah alikuwa ni mume bora kwa Hafsah kuliko Uthman ibn Affan, na Ummu

Kulthum alikuwa ni mke bora kwa 'Uthman kuliko Hafsah. Baada ya ndoa, Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه alikutana na rafiki yake 'Umar ibn Khataab na akamwambia ukweli kwamba, Mtume ﷺ alikuwa amemdokeza juu ya dhamira yake ya kutaka kumuoa Hafsah. Hii ndiyo sababu aliamua kukaa kimya na hakujibu kitu pale Umar ibn Khattab رضي الله عنه alipomwendea na kutaka amuoe Hafsah. Kwa sababu hakuona kama ni jambo la busara kufichua dhamira ya Mtume ﷺ. Kama mambo yangekwenda kinyume chake (kama Mtume ﷺ asingemuoa Hafsah) kwake yeye (Abu Bakr) ingekuwa ni jambo la furaha na heshima kukubali kumuoa Hafsah na hivyo kuunga udugu. 'Umar ibn Khattab رضي الله عنه alifurahi sana na katika kuonesha furaha yake, Umar ibn Khattab akasoma Aya hii Tukufu:

هَٰذَا مِن فَضْلِ رَبِّي لِيَبْلُوَنِيٓ ءَأَشْكُرُ أَمْ أَكْفُرُ ۖ وَمَن شَكَرَ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِۦ ۖ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ رَبِّي غَنِيٌّ كَرِيمٌ ۝٤٠

***"....Haya ni kwa fadhila za Mola wangu, ili anijaribu nitashukuru au nitakuwa mwizi wa fadhila; Na anayeshukuru, anashukuru kwa manufaa ya nafsi yake; na anayekufuru, kwa hakika Mola wangu ni mkwasi, (hana haja naye) na Karimu. "* (27:40)**

Wakati Umar ibn Khattab akimuaga mwanae, Umar ibn Khattab رضي الله عنه alimwambia na kumuusia mwanae Hafsah kwamba, asijaribu hata siku moja kushindana na Aishah رضي الله عنها. Mke ambaye alikuwa ni kipenzi zaidi kwa Mtume wa Allah na ambaye yeye alikuwa bora kuliko Hafsah رضي الله عنها kwa namna nyingi. Alimwambia kuwa, anapaswa kumuheshimu sana Aishah رضي الله عنها na kuishi kwa furaha kama mmoja kati ya wanafamilia ndani ya familia bora kuliko familia zote- familia ya Mtume ﷺ.

Baada ya kuwa mama wa Waumini na kuishi ndani ya nyumba ya Mtume ﷺ, Hafsah akaongeza bidii na kujifunza hata yale mambo madogo madogo ambayo ilikuwa vigumu kujifunza alipokuwa nje ya familia ya Mtume wa Allah ﷺ. Alikuwa na uwezo wa kuhifadhi mazungumzo yake na Mtume Muhammad ﷺ kwa usahihi jambo lililomfanya kuongeza nafasi yake ya kujifunza na kuuelewa Uislamu. Alikuwa sasa amepata nafsi ya kujadiliana na kujifunza jambo lolote lililokuwa likimtatiza katika mambo yanayohusu hukumu mbalimbali.

Jabir ibn 'Abdullah Ansari رضي الله عنه anasimulia kuwa amepokea kutoka kwa Ummu Mubashir kwamba; Ummu Mubashir anasema, yeye na Hafsah رضي الله عنها na Mtume ﷺ walikuwa wamekaa wakiongea. Mtume ﷺ akasema, watu wote waliochukua ahadi ya utii siku ile ya Hudaybiyah chini ya mti watakwenda Peponi, na hakuna atakayekwenda motoni. Akauliza linawezekana vipi hilo. Mtume ﷺ akajisikia vibaya kwa swali lile, lakini Hafsah رضي الله عنها hakuishia hapo au kukata tamaa, bali alinukuu kipande cha Aya kutoka Surat Maryam.

وَإِن مِّنكُمْ إِلَّا وَارِدُهَا ۚ كَانَ عَلَىٰ رَبِّكَ حَتْمًا مَّقْضِيًّا ﴿٧١﴾

***"Wala hakua yoyote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia (hiyo Jahanamu). ..."* (19:71)**

Katika kumjibu swali hili, Mtume ﷺ alinukuu Aya inayofuata katika Sura hiyo hiyo, Surat Maryam

ثُمَّ نُنَجِّي الَّذِينَ اتَّقَوا وَّنَذَرُ الظَّالِمِينَ فِيهَا جِثِيًّا ﴿٧٢﴾

***"Kisha Tutawaokoa wale wamchao (Mungu); na Tutawaacha madhalimu humo wamepiga magoti."* (19:72)**

Habari hii ya namna Hafsah alivyokuwa akibishana na Mtume ﷺ zikaenea katika mji wa Madinah. Siku hiyo Mtume ﷺ alijisikia vibaya; na pale Umar ibn Khattab رضي الله عنه ('Umar Faruuq) alipopata habari zile alimfokea vikali mwanae - Hafsah. Hafsah رضي الله عنها akajitetea kuwa, hata Aishah رضي الله عنها pia alikuwa akizungumza na kujadiliana naye kwa namna ile ile. Baba yake (Umar ibn Khattab) akamuonya kwa mara nyingine kuwa asishindane na Aishah رضي الله عنها na awe na nidhamu vinginevyo atajisababishia matatizo.

Miongoni mwa wake zake Mtume ﷺ, mama Aishah رضي الله عنها, Ummu Habiibah, Sawdah na Hafsah رضي الله عنهما wote wanatoka katika kabila la Qurayshi. Wake zake wengine wanatoka katika makabila mengine. Kila baada ya Swala ya 'Asr, Mtume ﷺ alikuwa akiwatembelea kila mmoja kwa muda mfupi ili kujua kama walikuwa wana mahitaji yeyote. Kuwatembelea huku kulikuwa ni kwa kila siku ikiwa Mtume ﷺ alikuwa yupo, na kila mmoja alikuwa akimsubiri kwa hamu kuja kwake nyumbani mwake. Mara chache iliwahi kutokea kuwa alitumia muda mwingi zaidi nyumbani mwa mkewe Zaynab

رضي الله عنها, Jambo hili halikumfurahisha mama Aishah, na aliamua kuzungumza na Hafsah na Sawdah رضي الله عنهما juu ya jambo hili. Walijadiliana na wakafahamu kuwa mmoja kati ya ndugu wa Zaynab alikuwa amemletea aina fulani ya asali na alikuwa akimpa Mtume ﷺ kila siku. Chakula hiki kilikuwa ni chakula alichokuwa anakipenda zaidi Mtume ﷺ na hivyo ilimfanya awe anachelewa kwa muda kidogo katika nyumba ya Zaynab رضي الله عنها, akifurahia. Aishah رضي الله عنها alikuwa anampenda sana Mtume ﷺ, kiasi kwamba alikuwa hawezi kuvumilia kumuona Mtume ﷺ, akichelewa kuja nyumbani kwake. Lakini kutokana na alivyokuwa akimuheshimu, alikuwa hawezi kumpinga waziwazi.

Hivyo alijadiliana na Hafsah na Sawdah رضي الله عنهما, na wakakubaliana kuwa pale Mtume ﷺ atakapokwenda nyumbani kwa yeyote kati yao, kila mmoja atasema kuwa kulikuwa na harufu mbaya ilikuwa inatoka mdomoni kwa Mtume ﷺ. Wakiamini kuwa, ikiwa atasikia jambo lile kutoka kwa wake zake wote watatu, ataamini bila shaka kuwa ni kutokana na asali aliyokula, na ataamua kuacha kula asali moja kwa moja. Kama jambo hili lingekuwa limetokea katika maisha ya mtu wa kawaida bila shaka lingekuwa halina madhara yeyote. Lakini jambo hili lilikuwa limepangwa na mama hawa litokee kwa Mtume wa Allah – Mtume wa mwisho – Muhammad ﷺ. Mtume ﷺ ambaye kila neno lake na kila tendo lake vinachukuliwa kama Shariah na muongozo kwa Waislamu kwa zama zote. Kwa maana hiyo jambo hili lilikuwa na uzito tofauti na athari tofauti. Mama hawa walipofanya jambo hili – kila mmoja akidai anasikia harufu mbaya ikitoka mdomoni kwa Mtume ﷺ, Mtume ﷺ akasema basi hatokula tena asali. Allah Akashusha Ayah ifuatayo inayopatikana katika Surat At-Tahrim.

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِىُّ لِمَ تُحَرِّمُ مَآ أَحَلَّ ٱللَّهُ لَكَ ۖ تَبْتَغِى مَرْضَاتَ أَزْوَٰجِكَ ۚ وَٱللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ۝١

***"Ewe Mtume! Mbona (kwa nini) unaharamisha alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu! Unatafuta radhi za wake zako (ndiyo maana ukafanya hivi)? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu."*** **(66:1)**

Ni katika wakati huu ambapo Mtume ﷺ alimwambia siri mke wake Hafsah na kumtahadharisha kuwa asimwambia mtu mwingine yeyote. Lakini mama Hafsah akamwambia siri ile rafiki yake na mke mwenzake, mama Aishah

رضي الله عنها. Allah Akamfunulia Mtume ﷺ yale yaliyokuwa yakitokea baina ya wake zake. Mwenyezi Mungu Akabainisha katika Aya ifuatayo inayopatikana pia katika Surat At-Tahrim:

وَإِذْ أَسَرَّ ٱلنَّبِىُّ إِلَىٰ بَعْضِ أَزْوَٰجِهِۦ حَدِيثًا فَلَمَّا نَبَّأَتْ بِهِۦ وَأَظْهَرَهُ ٱللَّهُ عَلَيْهِ عَرَّفَ بَعْضَهُۥ

وَأَعْرَضَ عَنۢ بَعْضٍ ۖ فَلَمَّا نَبَّأَهَا بِهِۦ قَالَتْ مَنْ أَنۢبَأَكَ هَٰذَا ۖ قَالَ نَبَّأَنِىَ ٱلْعَلِيمُ ٱلْخَبِيرُ ﴿٣﴾

***"Na Nabii alipo mwambia mmoja wa wake zake jambo la siri. Basi alipo litangaza yule mke, na Mwenyezi Mungu akamdhihirishia Mtume, alimjuvya sehemu na akaacha sehemu nyengine. Alipo mwambia hayo, huyo mke akasema: Nani aliye kwambia haya? Mtume akasema: Kaniambia Mjuzi Mwenye khabari zote! ."*** **(66:3)**

Mwaka ambao bara Arabu lilikuwa chini ya dola ya Kiislamu, utajiri ulikuwa mwingi na mali nyingi zilikuwa zikiletwa katika hazina ya Waislamu (Baitul-mal) kutoka sehemu mbalimbali za bara Arabu; Baadhi ya wake wa Mtume ﷺ waliokuwa wakitamani kuishi maisha ya starehe, wakatoa mapendekezo ya kuongezewa posho kwa ajili ya matumizi yao. Pale 'Umar ibn Khattab aliposikia jambo hili alikasirika sana, na akamwambia mwanae Hafsah رضي الله عنها kwamba anatakiwa amwambie baba yake (Umar ibn Khattab) kama atahitaji kitu chochote na asithubutu kupeleka madai yake kwa Mtume ﷺ. Aliwashauri pia mama wa Waumini wote (wakeze Mtume wote) wasimsumbue Mtume ﷺ kwa kupeleka madai yeyote. Ummu Salamah hakukaa kimya juu ya jambo hili, aliona kama Umar alikuwa anawaingilia na aliamua kumwambia wazi wazi kuwa anapaswa (Umar ibn Khattab) kuacha kuingilia mambo yanayowahusu wao, wakeze Mtume ﷺ.

Ilikuwa ni katika wakati huu ambapo Mtume ﷺ alikuwa ameanguka kutoka juu ya farasi na kuumia. Kutokana na haya yaliyokuwa yakitokea, aliamua kujitenga na kuamua kwenda katika chumba kilichokuwa sehemu iliyoinuka, chumba kilichokuwa jirani kabisa na nyumba ya Aishah. Mji wote wa Madinah ulijaa minong'ono na wanafiki walikuwa wakisambaza habari kuwa Mtume ﷺ alikuwa amewaacha wake zake. Lakini kimsingi na kwa uhakika kabisa hakuna kitu kama hicho kilichowahi kutokea. Maswahaba wote wakawa wamehuzunishwa na jambo hili, lakini hakuna yeyote kati yao aliyekuwa na ujasiri wa kuweza kumkabili Mtume ﷺ na kuongea naye ana kwa ana.

Baadaye Umar ibn Khattab ('Umar Faruq) رضي الله عنه akisukumwa na ujasiri wake alikwenda kumkabili Mtume ﷺ na kumuuliza ikiwa minong'ono iliyokuwa imeenea ni ya kweli. Mtume ﷺ alipokana kuwa si kweli, Umar ibn Khattab رضي الله عنه alifurahi sana. Kisha alimuomba ruhusa ili atangaze habari hii njema kwa Waislamu wote. Aliporuhusiwa, alikwenda akiwa na furaha na kuwafahamisha Waislamu na jamii kwa ujumla kuwa kila kitu kilikuwa kiko vizuri ndani ya nyumba ya Mtume ﷺ. Mji mzima ukapata habari kuwa Mtume wa Allah hakuwa amewaacha wake zake. Baada ya siku ishirini na tisa, Mtume ﷺ alirejea na kuingia ndani ya nyumba ya mama Aishah. Huku akitabasamu, mama Aishah akamuuliza Mtume ﷺ kwanini amerejea kabla ya mwezi kumalizika? Mtume ﷺ akamjibu mara nyingi mwezi muandamo huwa na siku ishirini na tisa. Mama Hafsah akamuahidi baba yake – Umar ibn Khataab رضي الله عنه kuwa, hata siku moja hatoomba tena kuongezewa fedha za matumizi na alisimama juu ya ahadi yake mpaka mwisho wa uhai wake.

Mama Hafsah رضي الله عنها bint Umar ibn Khattab alifariki dunia mwaka 41 Hijiriyah akiwa na umri wa miaka hamsini na tisa (59). Wakati mauti yanamkuta, mama Hafsah alikuwa yuko ndani ya Swaumu. Swala ya jeneza iliongozwa na aliyekuwa Gavana wa mji wa Madinah - Marwan ibn Al-Hakam. Abu Hurairah na Abu Sa'id Khudri رضي الله عنهما, maswahaba wa Mtume ﷺ walikuwa miongoni mwa maswahaba walioubeba mwili wa marehemu – mama wa Waumini Hafsah bint Umar ibn Khattab رضي الله عنه kwenda kuuzika katika eneo la Jannatul Baqi'. Kaka zake wawili, 'Abdullah ibn 'Umar na 'Asim ibn 'Umar رضي الله عنهما waliulaza mwili wa dada yao ndani ya kaburi. Miongoni mwa watu waliohudhuria maziko hayo ni Salem bin 'Abdullah, 'Abdur-Rahman ibn 'Abdullah na Hamzah ibn 'Abdullah ambao wote ni watoto wa swahaba mwaminifu na mcha-Mungu 'Abdullah ibn 'Umar ibn Khattab رضي الله عنه.

Hivi ndivyo mwandishi na msomaji wa Qur'an, mama aliyetoa uhai wake na muda wake wote wa ujana katika kufanya ibada, kufunga Swaumu na kutafakari juu ya yale aliyoyaumba Mwenyezi Mungu alivyoaga dunia na kurejea kwa Mola wake.

Ayah hii tukufu kutoka katika kitabu cha Allah, inayopatikana katika Surat Al-Qamar inatosha na kufaa kumuaga mama yetu – mama wa Waumini wote katika zama zote – Hafsah bint Umar ibn Khattab رضي الله عنه.

إِنَّ ٱلْمُتَّقِينَ فِى جَنَّـٰتٍ وَنَهَرٍ ﴿٥٤﴾ فِى مَقْعَدِ صِدْقٍ عِندَ مَلِيكٍ مُّقْتَدِرٍۭ ﴿٥٥﴾

***"Bila shaka wamchao Mwenyezi Mungu watakuwa katika mabustani na mito. Katika makao mazuri katika (Pepo) ya (Mwenyezi Mungu) – Mfalme Mwenye uweza (wa kila kitu)."*** **(54:54-55)**

# Zaynab bint Jahsh

## Aliyefungishwa Ndoa na Allah!

Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها alikuwa mtoto wa Umaimah bint 'Abdul Muttalib ibn Hashim, ambaye alikuwa shangazi yake Mtume ﷺ. Kaka yake alikuwa mtu maarufu - 'Abdullah ibn Jahsh. Na kaka yake mwingine alikuwa mtaalamu wa mashairi katika wataalamu wa Kiislamu akiitwa Abu Ahmad ibn Jahsh. Dada yake alikuwa miongoni mwa maswahabi maarufu wa Mtume ﷺ akiitwa Hamnah bint Jahsh. Wajomba zake walikuwa Hamzah ibn 'Abdul Muttalib رضي الله عنه – shujaa wa vita na kiongozi wa mashahidi na 'Abbas ibn 'Abdul Muttalib رضي الله عنه – aliyefahamika vema kutokana na ukarimu wake. Shangazi yake mwingine alikuwa ni Safiyyah bint 'Abdul Muttalib ibn Hashim.

Mama huyu Zaynab رضي الله عنها, alizaliwa takriban miaka thelathini (30) kabla ya Hijrah (Kabla ya Waislamu kuhamia Madinah) na aliingia katika Uislamu kutokana na kuvutiwa na mafundisho ya Uislamu kutoka kwa kaka yake 'Abdullah ibn Jahsh رضي الله عنه. Alikuwa binti mrembo, mwenye busara na aliyelelewa vizuri.

Hofu ya kuenea kwa Uislamu miongoni mwa Maquraishi ilikuwa kubwa na hivyo kupelekea vitisho na mateso kwa Waislamu wa mwanzo walioikubali dini hii. Baadhi yao walikuwa wakilazwa chali juu ya mawe yaliyochemka huku wengine wakiburuzwa juu ya mchanga wa jangwani uliochemka huku wakiwa wamevuliwa nguo. Wengine walikuwa wakifunikwa ndani ya mazulia na kuwashiwa moto ili wapate tabu na dhiki kwa moshi na kukosa hewa. Kila siku Waislamu wa mwanzo walikuwa wakishuhudia na kukabili aina tofauti tofauti za mateso yaliyobuniwa na makafiri ili kuwavunja moyo na kuwakatisha tamaa.

Ardhi na mji wa Makkah ukawa unaonekana mdogo kwa Waumini japo walikuwa wachache kwa idadi yao. Mtume ﷺ alikuwa akiwausia na kuwahimiza Waislamu kuwa na subira na kuwa na ujasiri wa kuyakabili na kuyavumilia

mateso.Lakini baadaye akawapa ruhusa ya kuhamia Uhabeshi (Ethiopia) na baadaye kuhamia Madinah. Wakiongozwa na 'Abdullah ibn Jahsh رضي الله عنه, familia yote ya Jahsh waliondoka na kuhama. Msafara wao ulimjumuisha ndugu yao aliyekuwa mshairi na kipofu, Ahmad ibn Jahsh رضي الله عنه, ambaye alikuwa anavutia sana kwa uwezo mkubwa wa kumudu lugha aliokuwa nao. Alitunga shairi lililoelezea kwa kina mateso waliyokuwa wakiyapata Waislamu wa mwanzo mikononi mwa Maquraishi, sababu za kuhama kwao na matendo ya kishujaa waliyokuwa wakiyafanya Waislamu. Mpaka leo, shairi hili linachukuliwa kama kielelezo cha ubora wa fasihi katika lugha ya Kiarabu.

Muda ulikwenda Waislamu wakiwa wamekaa kwa amani pale Madinah, na mahusiano baina ya Muhajiruun na Ansar yakaimarika na wakawa wanaishi kama ndugu wakiwa na mapenzi ya hali ya juu baina yao. Walikuwa wakionekana kana kwamba walitoka katika familia moja na kulelewa na mzazi mmoja kwa mapenzi ya namna moja. Hakukuwa na mbora katika jamii ile awe mtumwa au muungwana bali ukubwa au utukufu wake ulitegemea kiwango chake cha ucha-Mungu na tabia njema alizojipamba nazo.

Katika Ummah huu wa kupigiwa mfano wa Mtume ﷺ, Mtume wa Allahﷺ akamwambia binamu yake - Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها, kuwa alikuwa ameamua kumuozesha kwa Zayd ibn Harithah, mtumwa aliyeachwa huru na mtoto wa Mtume ﷺ wa kupanga. Zaynab رضي الله عنها hakufurahishwa na jambo hili.Akamwambia Mtume ﷺ kuwa yeye (Zaynab) alikuwa anatoka katika ukoo na familia yenye hadhi kubwa na kwamba hakufurahi wala hakuwa tayari kuolewa na mtumwa aliyeachwa huru. Alihofu kuwa kulikua na uwezekano mkubwa wakashindwa kuishi vizuri kutokana na tofauti za hadhi ya familia zao. Mtume ﷺ akamjibu kuwa, alikuwa amemchagua Zayd amuoe yeye na hivyo inampasa kukubali. Kabla ya Zaynab رضي الله عنها hajajibu kitu, Aya ifuatayo ilishushwa kwa Mtume ﷺ. Aya hii inapatikana katika Surat Al-Ahzab,

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥٓ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ ٱلْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ

وَمَن يَعْصِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

***"Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri,***

***wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, amepotea upotofu (upotevu) ulio wazi (kabisa).”* (33:36)**

Hivyo Zaynab na Zayd رضي الله عنهما wakafunga ndoa. Lakini baada ya muda kukawa hakuna masikilizano kwa kuwa walitoka katika familia zenye hadhi tofauti.

Zaynab رضي الله عنها alikuwa mtu wa kuchagua na toka mwanzo kabisa mwa ndoa yao kulikuwa na kuvutana na kubishana. Zayd akahisi kuwa hadhi, heshima na kile ambacho mwanaume anatarajia kukipata kutoka kwa mke wake alikuwa hakipati kutoka kwa mke wake. Akiwa amekatishwa tama kuendelea na ndoa yake, Zayd alikwenda kwa Mtume ﷺ na kumwambia kuwa, alikuwa amekata tamaa kabisa kwa sababu alikuwa anaona kuwa yeye (Zayd) na Zaynab walikuwa hawendi sawa. Ushauri alioupata kutoka kwa mlezi na mwalimu wake – Mtume ﷺ umebakia kuwa sehemu ya Qur’an:

أَمۡسِكۡ عَلَيۡكَ زَوۡجَكَ وَٱتَّقِ ٱللَّهَ

***....Shikamana na mkeo na umche Mwenyezi Mungu......”* (33:37)**

Pamoja na jitihada zote hizo, bado ndoa hii haikudumu muda mrefu, na Zaynab aliachika kutoka kwa Zayd رضي الله عنها.

Waarabu walikuwa wanaamini kuwa ilikuwa ni makosa kumuoa mke aliyeachwa na mtoto wa kupanga. Allah Aliamua kuifuta kawaida hii iliyozoeleka miongoni mwa Waarabu. Hivyo Allah Mtukufu Akamtuma Malaika Jibril kuja na ujumbe maalum kwa Mtume ﷺ na kumfahamisha kuwa, siku moja Zaynab atakuwa mke wake. Mtume ﷺ alipata tabu kwa sababu aliingiwa na mawazo vipi na namna gani watu watalipokea jambo hili ambalo kwa hakika lilikuwa likienda kinyuma na utamaduni na mazoea ya Waarabu. Lakini wakati yeye anafikiria yote haya, jambo hili lilikuwa nje ya uwezo wake kwa sababu lilikuwa ni jambo lililoamuliwa na Mola wa Walimwengu wote. Jukumu lake yeye ilikuwa kulipokea na kusubiri kile kilichokadiriwa na Allah kitimie tu. Lakini kama vile haitoshi.

Allah Akashusha Ayah ifuatayo katika Qur’an:

وَإِذْ تَقُولُ لِلَّذِىٓ أَنْعَمَ ٱللَّهُ عَلَيْهِ وَأَنْعَمْتَ عَلَيْهِ أَمْسِكْ عَلَيْكَ زَوْجَكَ وَٱتَّقِ ٱللَّهَ وَتُخْفِى فِى
نَفْسِكَ مَا ٱللَّهُ مُبْدِيهِ وَتَخْشَى ٱلنَّاسَ وَٱللَّهُ أَحَقُّ أَن تَخْشَىٰهُ ۖ فَلَمَّا قَضَىٰ زَيْدٌ مِّنْهَا وَطَرًا
زَوَّجْنَٰكَهَا لِكَىْ لَا يَكُونَ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ حَرَجٌ فِىٓ أَزْوَٰجِ أَدْعِيَآئِهِمْ إِذَا قَضَوْا۟ مِنْهُنَّ وَطَرًا ۚ
وَكَانَ أَمْرُ ٱللَّهِ مَفْعُولًا ﴿٣٧﴾

***"Na (Wakumbushe) ulipomwambia yule ambaye Mwenyezi Mungu amemneemesha (kwa kumuafikia Uislamu) na wewe ukamneemesha (kwa kumpa uungwana. Naye ni Bwana Zaid ibn Haritha ulipomwambia): "Shikamana na mkeo na umche Mwenyezi Mungu (usimuache)" na ukaficha katika nafsi yako aliyotaka Mwenyezi Mungu kuyatoa (Nayo ni kuwa Mwenyezi Mungu Amekuamrisha umuoe wewe huyo mkewe atakapomuacha ili iondoke ile itikadi iliyokuwa ikiitikadiwa ya kuwa mtoto wa kulea ni kama mtoto wa kumzaa), na ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye haki zaidi ya kumchelea. Basi alipokwisha Zaid haja yake na mwanamke huyo, Tulikuoza wewe ili isiwe taabu kwa Waislamu kuwaoa wale watoto wao wa kupanga wanapokuwa hawana haja nao. Na amri ya Mwenyezi Mungu ni yenye kutekelezwa".*** **(33:37)**

Baada ya Zaynab bint Jahsh kumaliza muda wake wa eda, Mtume ﷺ akatuma posa ili amuoe kupitia kwa Zayd ibn Harithah رضي الله عنه. Zayd ibn Harithah alipokwenda kwa Zaynab, alimkuta akikanda ngano. Akiwa amempa mgongo, Zayd رضي الله عنه alimpa ujumbe aliotumwa na Mtume ﷺ kuwa Mtume ﷺ alikuwa amemchagua kujiunga na kundi la mama wa Waumini. Zaynab akamjibu kuwa, hawezi kutoa jibu kwa wakati huo, na kwamba alitaka kupata ushauri kutoka kwa Mola wake. Zaynab رضي الله عنه alianza kuswali na kumuomba muongozo Allah. Alikuwa bado yuko katikati ya Swala, Mtume ﷺ akapokea ujumbe kupitia kwa Jibril kuwa ndoa tayari ilikuwa imeshafungwa mbinguni na Allah Mwenyewe! Baada ya kupokea ujumbe na maelekezo haya, Mtume ﷺ akaondoka kwenda kwa Zaynab رضي الله عنه bila kuchukua tahadhari wala kuchunga mipaka yoyote inayopaswa kuchukuliwa kwa watu wa jinsia tofauti wasiokuwa mume na mke na wanaoweza kuoana. Hakumfahamisha kwamba

anakwenda wala hakumuomba ruhusa ya kwenda kwake. Kuna nukta chache za kuzingatia katika ndoa hii.

Amri ya Allah kupitia Qur'an ndiyo iliyotoa ruhusa kwa Zaynab kuolewa na Mtume ﷺ na hivyo kusimama kama mzazi au shahidi kuthibitisha kuwa ndoa ilifungwa. Ndoa hii iliondoa mila na utamaduni potofu kuwa mtoto wa kumlea ni mtoto wako hasa, jambo ambalo hapo kabla lilikuwa linazuia baba mlezi kumuoa mke wa mtoto huyo ikiwa ataachwa au kufiwa na mumewe.

Zaynab alikuwa akijisifu mbele ya wake wengine wa Mtume ﷺ kuwa, ndoa yake na Mtume ﷺ haikufungwa na familia yake bali ilifungwa na Allah Mwenyewe Mbinguni.

Pale wanafiki walipomlaumu Mtume ﷺ kwa ndoa hii, Mwenyezi Mungu Aliwajibu Akisema:

مَّا كَانَ عَلَى ٱلنَّبِيِّ مِنۡ حَرَجٖ فِيمَا فَرَضَ ٱللَّهُ لَهُۥۖ سُنَّةَ ٱللَّهِ فِي ٱلَّذِينَ خَلَوۡاْ مِن قَبۡلُۚ وَكَانَ أَمۡرُ
ٱللَّهِ قَدَرٗا مَّقۡدُورًا ٣٨ ٱلَّذِينَ يُبَلِّغُونَ رِسَٰلَٰتِ ٱللَّهِ وَيَخۡشَوۡنَهُۥ وَلَا يَخۡشَوۡنَ أَحَدًا إِلَّا ٱللَّهَۗ
وَكَفَىٰ بِٱللَّهِ حَسِيبٗا ٣٩

***"Hapana lawama kwa Mtume katika (kufanya) yale ambayo Mwenyezi Mungu Amembainishia (hukumu yake): ndiyo kawaida ya Mwenyezi Mungu kwa wote waliopita zamani; na amri ya Mwenyezi Mungu ni mpango uliopangwa vizuri. Wale (Mitume waliopita kabla yako) waliokuwa wakifikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kumuogopa wala hawamuogopi yoyote isipokuwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ndiye Atoshaye kuhisabu."*** **(33:38-39**)

Ili kutoa ufafanuzi wa wazi zaidi na kumaliza minong'ono na hoja za makafiri na wale waliokuwa bado nyoyo zao zina shaka, Allah Akashusha Aya ifuatayo ambayo pia inapatikana katika Surat Al-Ahzab:

مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَآ أَحَدٖ مِّن رِّجَالِكُمۡ وَلَٰكِن رَّسُولَ ٱللَّهِ وَخَاتَمَ ٱلنَّبِيِّـۧنَۗ وَكَانَ ٱللَّهُ بِكُلِّ شَيۡءٍ
عَلِيمٗا ٤٠

***"Muhammad si baba wa yoyote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Mungu na Mwisho wa Mitume, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu."* (33:40)**

Baada ya hapo, Mwenyezi Mungu Akashusha Aya zifuatazo kwa ajili ya kuweka sawa na kufafanua hadhi aliyonayo mtoto wa kupanga (mtoto wa kumlea):

وَمَا جَعَلَ أَدْعِيَآءَكُمْ أَبْنَآءَكُمْ ۚ ذَٰلِكُمْ قَوْلُكُم بِأَفْوَٰهِكُمْ ۖ وَٱللَّهُ يَقُولُ ٱلْحَقَّ وَهُوَ يَهْدِى
ٱلسَّبِيلَ ﴿٤﴾ ٱدْعُوهُمْ لِءَابَآئِهِمْ هُوَ أَقْسَطُ عِندَ ٱللَّهِ ۚ

***"..,.wala Hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa wana wenu hasa; hayo ni maneno yenu ya vinywa vyenu; na Mwenyezi Mungu Ndiye anayesema kweli, Naye huongoa njia (ya uwongofu). Waiteni kwa (ubini wa) baba zao, maana huo ndio uadilifu mbele ya Mwenyezi Mungu..."* (33:4-5)**

Ni wakati wa ndoa hii, Mwenyezi Mungu Akashusha Aya kuweka utaratibu wa Waislamu kuingia nyumbani kwa Mtume ﷺ na kuweka zuio kwamba, hakuna ruhusa kwa Muislamu yeyote atakayeruhusiwa kumuoa mke wa Mtume ﷺ baada ya Mtume ﷺ kufariki. Amri hizi mbili zilikuja ndani ya Aya moja katika Surah ileile, Mwenyezi Mungu Anasema:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَدْخُلُوا۟ بُيُوتَ ٱلنَّبِىِّ إِلَّآ أَن يُؤْذَنَ لَكُمْ إِلَىٰ طَعَامٍ غَيْرَ
نَـٰظِرِينَ إِنَىٰهُ وَلَـٰكِنْ إِذَا دُعِيتُمْ فَٱدْخُلُوا۟ فَإِذَا طَعِمْتُمْ فَٱنتَشِرُوا۟ وَلَا مُسْتَـْٔنِسِينَ لِحَدِيثٍ ۚ إِنَّ
ذَٰلِكُمْ كَانَ يُؤْذِى ٱلنَّبِىَّ فَيَسْتَحْىِۦ مِنكُمْ ۖ وَٱللَّهُ لَا يَسْتَحْىِۦ مِنَ ٱلْحَقِّ ۚ وَإِذَا
سَأَلْتُمُوهُنَّ مَتَـٰعًا فَسْـَٔلُوهُنَّ مِن وَرَآءِ حِجَابٍ ۚ ذَٰلِكُمْ أَطْهَرُ لِقُلُوبِكُمْ وَقُلُوبِهِنَّ ۚ وَمَا
كَانَ لَكُمْ أَن تُؤْذُوا۟ رَسُولَ ٱللَّهِ وَلَآ أَن تَنكِحُوٓا۟ أَزْوَٰجَهُۥ مِنۢ بَعْدِهِۦٓ أَبَدًا ۚ إِنَّ ذَٰلِكُمْ
كَانَ عِندَ ٱللَّهِ عَظِيمًا ﴿٥٣﴾

***"Enyi Mlioamini! Msiingie nyumba za Mtume ila (mpaka) mpewe ruhusa kwenda kula, pasipo (kwenda kukaa) kungojea kiive. Lakini***

***mtakapoitwa ingieni, na mnapokwisha kula tawanyikeni. Wala msiweke mazungumzo, maana jambo hili linamuudhi Mtume, naye anakuoneeni haya; lakini Mwenyezi Mungu Haoni haya kusema haki. Nanyi mnapowauliza (wakeze) waulizeni nyuma ya pazia. Kufanya haya kutasafisha nyoyo zenu na nyoyo zao. Wala haikupasieni (haitakikani) kumuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu. Wala kuwaoa wake zake baada yake; kabisa. Hakika jambo hilo ni (dhambi) kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu."* (33:53)**

Mama Aishah رضي الله عنها anasema, kwa kuzingatia hadhi na daraja, Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها alikuwa yuko sawa na yeye. Mama Aishah رضي الله عنها anasema pia kuwa hakuwahi kumuona mtu mwingine yeyote aliyekuwa akifanya bidii sana kujikurubisha karibu na Mwenyezi mungu kwa kufanya ibada zaidi ya mama huyu – Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها. Alikuwa mwingi wa kutoa sadaka na ukarimu wake kwa ndugu zake ulikuwa ni wa hali ya juu na wa kupigiwa mfano.

Wakati mama Aishah رضي الله عنها alipotuhumiwa na wanafiki kuwa amefanya machafu na tuhuma zile kuenea mji mzima wa Madinah, tuhuma zile zilimsumbua na kumuathiri hata Mtume ﷺ mwenyewe. Mtume ﷺ akamuuliza mama Zaynab رضي الله عنها alikuwa na maoni gani kuhusu jambo hili lililomuhusu mama Aishah رضي الله عنها (mke mwenziye). Tabia njema ya mama huyu inajidhihirisha katika majibu yake kwa Mtume ﷺ juu ya jambo hili pale alipoulizwa. Bila kuchelewa wala kutafuna maneno mama Zaynab رضي الله عنها alijibu yeye (Zaynab) asingependa kujihusisha, wala asingependa kumtia doa au kasoro macho yake, masikio yake wala ulimi wake kwa tuhuma mbaya kiasi kile. Huku akiapa kwa Jina la Allah, Zaynab رضي الله عنها alisema, hakika yeye anamfahamu mama Aishah رضي الله عنها kama mwanamke mcha-Mungu na mwenye tabia njema. Anamfahamu kuwa ni mwanamke mwenye sifa zisizokuwa na mfano hasa kwa uadilifu, ucha-Mungu na uaminifu. Kisha akamalizia kwa kusema hakuwahi kuona wala kudhania jambo lolote baya kwa mama Aishah رضي الله عنها (mke mwenziye) isipokuwa wema.

Mama Aishah رضي الله عنها anasema, bila shaka Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها angeweza kutumia fursa ile kutoa maoni ya kumchafua na kumkandamiza hasa ukizingatia kuwa walikuwa ni wake wenza na hivyo kuwa washindani. Mama Aishah anasema, kwa hakika hakuwahi kumsahau mama Zaynab bint Jahsh

رضي الله عنها (mke mwenziye) kwa namna alivyosimama imara pamoja naye katika wakati ambao karibu dunia yote (watu wote) walikuwa dhidi yake.

Katika tukio moja, Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها alimwita mama Safiyyah (mke wa Mtume) Myahudi na jambo hili likamkera na kumuudhi sana Mtume ﷺ. Kimsingi Mtume ﷺ alikasirika kiasi cha kuacha kuzungumza na Zaynab. Mama Zaynab aligundua kuwa alikuwa amefanya kosa kubwa sana na hivyo kumkera Mtume ﷺ. Kisha alimuomba mama Aishah awe msuluhishi baina ya Mtume ﷺ na mama Zaynab, na kumuomba amfahamishe mume wao kuwa kwa hakika yeye Zaynab ametambua kosa lake na anajutia na kutubia kwa kosa alilolifanya. Kwa sababu mama Aishah رضي الله عنها alikuwa mtu pekee anayeweza kuongea naye wazi wazi. Mtume ﷺ alipokwenda kumtembelea mama Aishah رضي الله عنها, mama huyu alitafuta fursa nzuri na kuanzisha mazungumzo juu ya jambo hili, na kumuombea radhi Zaynab mke mwenziye. Mtume ﷺ akamsamehe mama Zaynab رضي الله عنها na hatimaye maisha ya familia baina yao yakarejea kuwa mazuri.

Je, hatuoni mfano mzuri juu ya mama hawa? Wake wa Mtume ﷺ. Bila shaka wanatosha kuwa darasa kwa akina mama wa Kiislamu leo hii na mahusiano baina yao ikiwemo kupendana, kuhurumiana na kuthaminiana pamoja na kuwa wake wenza. Wao kwao, ndoa ilikuwa ni ibada kwa maana halisi ya ibada katika kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Ndio maana uke wenza haikuwa vita, au chanzo cha chuki, wivu na ugomvi. Mambo ambayo huondoa kabisa dhana ya ndoa kama ibada na kutafuta radhi za Allah.

Mama Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها alipofariki dunia, mama Aishah رضي الله عنها alikumbuka wakati ambao Mtume ﷺ aliposema kwamba miongoni mwa wake zake, ataanza kukutana na mke ambaye mikono yake ni mirefu. Mama Zaynab رضي الله عنها alikuwa ni mfupi na kwa maana hiyo mikono yake ilikuwa ni mifupi pia. Wake wa Mtume ﷺ waliyaelewa maneno yale kama yalivyo na hivyo wakaanza kupima urefu wa mikono yao. Ni baada ya kufariki Zaynab ndiyo walipokuja kufahamu maana ya maneno yale ya Mtume ﷺ. Ukweli ni kwamba, Mtume ﷺ aliposema kuwa mwenye mikono mirefu alimaanisha mtu mkarimu na aliyependa kutoa sadaka na kuwakirimu watu zaidi kuliko wengine; mtu ambaye muda wote alikuwa akifikiria namna ya kuwanufaisha watu wengine. Kulikua na ubashiri ndani ya kauli hii ya Mtume ﷺ, ubashiri ambao ulikuja kuwa wazi baada ya kufariki Zaynab bint Jahsh.

Ubashiri ule ulikuwa na maana kuwa Mtume ﷺ atakutana na Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها Peponi kabla ya kukutana na wake zake wengine. Na alifariki kabla ya wake zake wengine wote wa Mtume ﷺ.

Mama Aishah anasema, Zaynab رضي الله عنها alikuwa akifanya kazi kwa mikono yake mwenyewe, na kile alichokuwa akikipata kutokana na kazi ya mikono yake alikuwa akikitoa sadaka. Anaongeza kusema kuwa mama Zaynab رضي الله عنها alikuwa anamuogopa Mwenyezi Mungu, mwanamke mkweli aliyejitahidi kujiepusha na anasa, starehe na mapambo ya dunia na kwamba matendo yake yote yalikuwa yakilenga kumfurahisha Mwenyezi Mungu. Wakati mwingine alikuwa akishikwa na hasira na haraka alirejea na kutubia na kuomba msamaha kwa Mola wake. Alikuwa mtu mwenye moyo safi, moyo ambao haukubeba chuki, choyo wala jambo lolote baya ambalo lingeweza kuchafua moyo wake na matendo yake.

Mtume ﷺ alikuwa na ratiba iliyopangwa vizuri sana kwa wake zake. Baada ya Swala ya 'Asr alikuwa na kawaida ya kupita kila nyumba ya mke wake kujua habari za familia na kuuliza ikiwa kuna shida yeyote na kama ilikuwepo alikuwa akiitatua na kisha akienda nyumba nyingine. Alikuwa makini sana na alijitahidi kuwa muadilifu na kuhakikisha kuwa alikuwa anatenda haki kwa wake zake wote ikiwemo muda alioutumia kwa kila mke na mahitaji yao. Pale mama Zaynab رضي الله عنها alipoletewa na ndugu zake aina fulani maalumu ya asali, ilitokea kuwa Mtume ﷺ aliipenda sana asali ile. Kila mama Zaynab رضي الله عنها alipompa asali ile Mtume ﷺ, Mtume alikuwa akitumia muda mwingi kiasi ndani ya nyumba yake (Zaynab), akila asali ile na kuifurahia. Wakeze wengine walikosa subira na uvumilivu kuendelea kusubiri zamu yao. Hivyo mama Aishah, Sawda, na Hafsah wakapanga mpango wao wa siri. Wakakubaliana kuwa kila mmoja atakuwa akimwambia Mtume ﷺ kuwa, kulikuwa na harufu fulani iliyokuwa ikitoka ndani ya kinywa cha Mtume ﷺ. Waliamini kuwa, kama wote watatu watatoa madai yanayofanana, bila shaka Mtume ﷺ atafahamu na kuamini kuwa bila shaka kitu pekee kinachoweza kuwa kimemfanya atokwe na harufu mbaya mdomoni itakuwa ni asali aliyokula. Na kwa kuwa Mtume ﷺ alikuwa yuko makini na alithamini sana suala la usafi wa kinywa cha mtu, bila shaka ataacha kula asali. Mama zetu, mama wa Waumini wakatekeleza mpango wao. Hawakuwa na nia yeyote mbaya ila walichotaka wao ilikuwa Mtume ﷺ aje katika nyumba zao mapema.

Ikumbukwe kuwa hadhi ya mama zetu – wake za Mtume ﷺ, walikuwa na hadhi tofauti na wake wengine kama tunavyobainishiwa ndani ya Qur'an katika Aya ifuatayo:

يَٰنِسَآءَ ٱلنَّبِيِّ لَسۡتُنَّ كَأَحَدٖ مِّنَ ٱلنِّسَآءِ

***"Enyi wakeze Mtume, nyinyi si kama yoyote tu katika wanawake wengine..."* (33:32)**

Na kile walichokitarajia kutokea, – mpango wao ukafanikiwa. Mtume ﷺ akaahidi kuwa kuanzia wakati huo hatokula tena asali. Kama tulivyosema huko nyuma, kama jambo hili lingekuwa limemtokea mtu wa kawaida lisingekuwa na madhara yeyote kijamii. Lakini hapa Mtume ﷺ alikuwa anaapa na kujiepusha na jambo ambalo halikuharamishwa na Allah, jambo ambalo lingewafanya wafuasi wake wote – Waislamu kujiepusha na jambo hili ambalo Allah hakulikataza. Ni kwa sababu hii, Mwenyezi Mungu Akapinga uamuzi huu kwa kushusha Aya ifuatayo inayopatikana ndani ya Qur'an:"

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ لِمَ تُحَرِّمُ مَآ أَحَلَّ ٱللَّهُ لَكَۖ تَبۡتَغِي مَرۡضَاتَ أَزۡوَٰجِكَۚ وَٱللَّهُ غَفُورٞ رَّحِيمٞ ۝١

***"Ewe Mtume! Mbona (kwa nini) unaharamisha alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu! Unatafuta radhi za wake zako (ndiyo maana ukafanya hivi)? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu."* (66:1)**

Matokeao ya kushushwa kwa Ayah hii, Mtume ﷺ ilimlazimu kuvunja uamuzi na kiapo chake juu ya kuiepuka asali, na ikamlazimu kufuata utaratibu aliouweka Allah kwa mtu anaevunja kiapo au ahadi aliyochukua au kuiweka. Mama yetu - Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها alitenga mahala maalum ndani ya nyumba yake kwa ajili ya kufanyia ibada na kutumia muda mwingi katika kuswali, kumtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi, kusoma Qur'an, kutafakari kwa kina juu ya uwezo na huruma ya Allah na mengine mfano wa hayo. Mtume ﷺ alikuwa akiswali mahala hapa baadhi ya nyakati (sio swala za faradhi). Hivyo mama huyu alikuwa anaamini kuwa alipaswa kumuomba Mwenyezi Mungu msaada au muongozo kwa kuswali na kupitia dua kabla ya kuamua au kufanya jambo lolote. Maamuzi yake yote makubwa katika maisha yake alikuwa akiyafanya kupitia njia hii – kuswali na kuomba dua ili Allah Ampe muongozo

nini afanye au asifanye. Kimsingi hii ndio sababu hata pale Mtume ﷺ alipopeleka posa kutaka kumuoa, alimuelekea Allah kwa kuswali na dua ili Mwenyezi Mungu ampe muongozo juu ya jambo lile.

Mama huyu mcha-Mungu – Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها alifariki wakati wa Ukhalifa wa 'Umar ibn Khattab (Umar Al-Faruq) akiwa na umri wa miaka hamsini na tatu (53). Alipogundua kuwa sasa muda si mrefu atafariki dunia na kwenda kukutana na Mola wake, aliwaambia watu waliokuwa wamemzunguuka kuwa alikuwa amejiandalia sanda yake yeye mwenyewe. Ikiwa Khalifa 'Umar ibn Khattab atatuma sanda nyingine, moja itumike kumzikia na nyingine itolewe sadaka. Hivi ndivyo alivyokuwa mama huyu – mwingi wa kutoa sadaka lakini zaidi mtu aliyejiepusha na kupenda makuu au anasa za dunia hii. Pazia liliwekwa baina ya mwili wake na watu wengine japo mwili wake ulikuwa tayari umefunikwa na kuzunguushwa ndani ya sanda. Khalifa 'Umar ibn Khattab ndiye aliyeongoza swala ya jeneza (swala ya maiti) ya mama huyu, Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها; Ndugu zake - Usamah ibn Zayd, Muhammad ibn 'Abdullah ibn Jahsh, 'Abdullah ibn Abi Ahmad ibn Jahsh na Muhammad ibn Talhah ibn 'Abdullah ndio walioingia ndani ya kaburi na kuupokea kisha kuustiri (kuuzika) mwili wa Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها katika kaburi lake sehemu waliyozikwa watu wengine watukufu - Jannatul - Baqi'.

Alikuwa mama mkarimu na mwenye moyo wa huruma kiasi kwamba, kufariki kwake haikuwa msiba wa familia yake tu, bali masikini na mafakiri wa mji wote walibubujikwa na machozi kwa kuondokewa na mtu aliyezijua shida zao na aliyewafuta machozi na kuwaondolea njaa na huzuni pale walipokuwa na shida. Wakati anafariki, aliacha nyumba ambayo ilinunuliwa na Walid ibn 'Abdul Malik kwa gharama ya Dirham elfu hamsini na akaifanya sehemu ya eneo la msikiti wa Mtume ﷺ pale Madinah.

يَٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفۡسُ ٱلۡمُطۡمَئِنَّةُ ٢٧ ٱرۡجِعِيٓ إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةٗ مَّرۡضِيَّةٗ ٢٨ فَٱدۡخُلِي فِي عِبَٰدِي ٢٩ وَٱدۡخُلِي جَنَّتِي ٣٠

***"Ewe nafsi yenye kutua! Rudi kwa Mola wako, hali ya kuwa utaridhika (kwa utakayoyapata), na (Mwenyezi Mungu) aridhike na wewe. Basi ingia katika (kundi la) waja Wangu (wazuri). Uingie katika Pepo yangu."*** **(89:27-30)**

# Ummu Salamah binti Abi Umayyah

## Aliyepewa Mume Bora baada ya Kufiwa na Mume Bora

Mtume ﷺ anasema: *"Mwenyezi Mungu ameniamuru kuoa wanawake wa Peponi tu".*

Ummu Salamah رضي الله عنها alishiriki katika kuchukua ahadi siku ile ya Hudaybiyah; hivyo anastahili kuwa Mwanamke wa Peponi.

Jina halisi la mama huyu ni Hind bint Abi Umayyah ambaye alikuja kuwa maarufu kwa jina la Ummu Salamah. Mama huyu alizaliwa katika familia mashuhuri na alijaaliwa kuwa mwenye akili nyingi na mwingi wa busara. Kabla ya kuolewa na Mtume ﷺ, mama huyu aliolewa na 'Abdullah ibn 'Abdul Asad Makhzumi ambaye ndiye anafahamika pia kama Abu Salamah. Bwana huyu alikuwa mtoto wa shangazi yake Mtume ﷺ aliyeitwa Barrah bint Abdul Muttalib. Bwana huyu pia ni miongoni mwa watu wa mwanzo kuukubali na kuingia katika Uislamu. Alikuwa akifahamika vema kutokana na uaminifu wake, ukarimu, uvumilivu na mwingi wa subira. Inafahamika kuwa alikuwa miongoni mwa watu wa mwanzo na pengine wa kumi na moja kuingia katika Uislamu. Alikuwa pia ndugu wa Mtume ﷺ kutokana na kunyonya pamoja.

Ummu Salamah رضي الله عنها pia alikuwa miongoni mwa watu wa mwanzo kuingia katika Uislamu. Mama wa Ummu Salamah alikuwa anaitwa 'Atikah bint 'Amer ibn Rabi'ah Ibn Malik ibn Khazimah. Na baba yake alikuwa anaitwa Abu Umayyah ibn 'Abdullah Ibn 'Amr ibn Makhzum, mtu ambaye alikuwa na utajiri mkubwa na mtu maarufu miongoni mwa jamii yake kutokana na kujitolea kwake na ukarimu wake. Ummu Salamah رضي الله عنها alionekana wazi kuwa alikuwa amerithi tabia hii ya ukarimu kutoka kwa baba yake. Alikuwa mtu mkarimu sana kwa jirani zake. Alipoolewa na kijana mtanashati, kijana kutoka

familia tajiri na mwenye hadhi sawa na yeye kutoka familia ya Makhzum, aliishi maisha ya furaha sana katika ndoa yake na watu wote katika familia zao walikuwa wenye furaha.

Lakini mambo yalibadilika ghafla baada ya wanandoa hao kuingia katika Uislamu. Familia yote ikawa dhidi yao; watu wao wa karibu na waliokuwa na ushawishi mkubwa katika familia yao wakaanza kuwapiga vita. Watu kama Walid ibn Mughirah Makhzumi, wakaanza kuwaletea shida na usumbufu wa hali ya juu. Mambo yalivyokuwa mazito na magumu sana, Mtume ﷺ aliwashauri baadhi ya maswahaba wake kuhamia Uhabeshi (Ethiopia), mahala ambapo mfalme aliyekuwa anatawala huko, pamoja na kuwa alikuwa mkristo wakati ule, bado alikuwa mwenye busara na mvumilivu kwa dini mpya. Watu kumi na sita (16) wakiwemo wanaume kumi na mbili (12) na wanawake wanne (4) wakaondoka kuelekea Uhabeshi. Ummu Salamah رضي الله عنها na Abu Salamah walikuwa ni miongoni mwa watu hao kumi na sita (16) waliohamia Uhabeshi.

Ummu Salamah رضي الله عنها anasimulia kuwa maisha ya Uhabeshi yalikuwa ni maisha mazuri na ya amani, hakukuwa na unyanyasaji wowote uliotokana na wao kuwa Waislamu. Akiwa huko, alijaaliwa kupata mtoto wa kike ambaye walimwita Zaynab رضي الله عنها. Baadaye wakapata bahati ya kupata mtoto wa kiume ambaye walimwita Salamah, mtoto ambaye alikuja kupelekea wote wakafahamika kwa majina ya Ummu Salamah رضي الله عنها na Abu Salamah.

Mtoto wao wa tatu alikuwa pia mtoto wa kiume, ambaye walimwita ‘Umar. Na baadaye walipata mtoto mwingine wa kike ambaye walimwita Durrah. Hivyo maisha yalikuwa mazuri na ya furaha na siku na miaka ikapita wakiishi huko. Mtawala wa Uhabeshi, Najashi alikuwa mtu mkarimu sana kwa wageni na wahamiaji. Viongozi wa makafiri walipopata habari kuwa Waislamu wanaishi kwa furaha huko Uhabeshi, walihofia kuwa Waislamu sasa watakuwa wanajijenga na hivyo kuwa tishio kwa utawala wao. Hivyo waliamua kuchukua hatua madhubuti kuufuta Uislamu.

Baada ya kujadiliana kwa kina waliandaa mpango maalum wa kutimiza kile walichokuwa wakikitamani. Makafiri wakawatuma wanasiasa hodari na mabingwa wa ushawishi miongoni mwa Waarabu kwa wakati ule, Amr ibn ‘Aas na ‘Abdullah ibn Abi Rabi’ah wakiwa na zawadi nyingi kwa ajili ya mfalme Najashi, kwa lengo la kumshawishi mfalme awatoe na kuwakabidhi wahamiaji

wa Kiislamu kwa makafiri wa Makkah. Mfalme Najashi alikuwa mtu aliyekuwa na akili na mawazo huru, mtu mkweli na mtu mwenye mtazamo wa mbali. Hivyo alimwita kiongozi wa wahamiaji wa Kiislamu ili kujitetea na kuwasilisha utetezi wake dhidi ya madai yaliyowasilishwa na wawakilishi wa makafiri wa Makkah. Baada ya kusikiliza maelezo ya kiongozi wa Waislamu, mfalme Najashi aliwaambia wawakilishi wawili waliotumwa na makafiri wa Makkah kuwa, bila shaka wahamiaji wale (Waislamu) ni watu wema na hivyo walikuwa wako huru kuishi Uhabeshi kwa muda wowote watakaotaka wao kuishi. Na zaidi ya hapo, aliahidi kuwa ataendelea kuwapa ulinzi kadri itakavyohitajika. Aliwataka wajumbe wa makafiri kutoka Makkah wachukue zawadi walizokuja nazo na waondoke. Aliwahakikishia kuwa hata kama mtu atakuja na zawadi sawa na mlima wa dhahabu ili awatoe wahamiaji wale wa Kiislamu katu hatofanya hivyo. Ummu Salamah رضي الله عنها aliandika kumbukumbu hii muhimu ya Waislamu wa mwanzo kufanya kitendo cha kuhama, kutoka Makkah kwenda Uhabeshi na kuuzungumzia ukarimu aliokuwa nao mfalme Najashi katika namna ambayo mpaka leo imekuwa sehemu muhimu katika historia ya Uislamu.

Ummu Salamah رضي الله عنها anasimulia kuwa, maisha yao nchini Uhabeshi yalikuwa maisha ya amani na kwa hakika, Mfalme Najashi alikuwa mtu mkarimu sana. Lakini pamoja na hayo bado walikuwa na hamu sana ya kurejea nyumbani Makkah. Walikuwa wakisubiri kwa hamu hali ya amani irejee Makkah ili waweze kurejea katika nchi yao waliyoipenda. Siku moja habari ziliwajia kwamba 'Umar ibn Khattab رضي الله عنه alikuwa amesilimu na kwamba hali ya Makkah ilikuwa imebadilika kabisa. Ilielezwa kuwa, kutokana na ushawishi, ujasiri, ushujaa na ukakamavu aliokuwa nao 'Umar رضي الله عنه, mateso dhidi ya Waislamu yalikuwa yamekoma. Waislamu wote walijawa na furaha kwa habari njema zilizowafikia.

Ummu Salamah رضي الله عنها anasema kuwa, waliamua kurejea nyumbani – Makkah, na 'Uthman ibn 'Affan رضي الله عنه pia aliamua kurejea nyumbani akiwa pamoja na familia yake. Walipofika Makkah, walikuja kufahamu kuwa habari zile zilikuwa ni uvumi tu na hazikuwa habari za kweli na hali ilikuwa ni mbaya zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Waislamu walikuwa wamegeuzwa na kufanywa shabaha ya kila aina ya uhalifu na mateso. Lakini wakati huo walikuwa tayari wamechelewa kwa sababu tayari walikuwa wamekwishafika Makkah.

Kutokana na mateso na manyanyaso waliyokuwa wakiyapata Waislamu, Waislamu waliamua kuhamia Uhabeshi kwa mara ya pili. Ni katika wakati huu, Mtume ﷺ aliwashauri baadhi ya maswahaba kuhamia Madinah. Ujumbe wa watu kutoka Madinah ulikuwa umewasili kutoka kwa Waislamu waliochukua ahadi ya utii kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ﷺ siku ile ya kuchukua kiapo na ahadi ya utii pale 'Aqabah. Waislamu wa huko walikuwa wakiwaalika Waislamu kwenda na kuanzisha makazi yao Madinah na Mtume ﷺ alikuwa amekubali. Watu wa Ansar kama walivyokuja kufahamika hapo baadae, walikuwa wameahidi kuishi nao na kuwaangalia ndugu zao Waislamu watakaohamia huko.

Abu Salamah رضي الله عنه na familia yake wakafanya maandalizi ya safari ya kwenda Madinah kwa kutumia ngamia. Lakini wanafamilia wa Ummu Salamah رضي الله عنها wakaja juu, wakisema Abu Salamah رضي الله عنه yuko huru kwenda popote apendapo lakini lazima amuache mtoto wao – mke wake. Walisema kama utani kuwa, alikuwa hampi maisha ya amani na utulivu mke wake, kila mara yuko njiani mara Uhabeshi mara Madinah.

Familia ya Abu Salamah رضي الله عنه ilipopata habari juu ya msimamo wa familia ya Ummu Salamah رضي الله عنها, waliingilia kati wakipinga mtazamo na uamuzi wa familia ya Ummu Salamah na kuamua kuwachukua watoto wa Abu Salamah رضي الله عنه. Familia ikagawanyika, Abu Salamah akaondoka kwenda Madinah; mke wake (Ummu Salamah) akabaki na familia yake na watoto wakachukuliwa na wazazi wa Abu Salamah رضي الله عنه. Kutokana na kutenganishwa na mume wake na watoto, Ummu Salamah muda wote alikuwa akilia kwa uchungu. Kila siku alikuwa akienda eneo ambalo yeye na familia yake (Abu Salamah na watoto) walitenganishwa na kukaa pale akiwalilia vipenzi vyake. Siku moja, mmoja kati ya watu wa familia yake alipita mahala pale na kumkuta Ummu Salamah رضي الله عنها akiwa amekaa mahala pale akilia kwa uchungu na kumuuliza, nini kilikuwa kimetokea ambacho kilimfanya awe akilia? Ummu Salamah رضي الله عنها alimueleza kile ambacho kilimfanya awe ndani ya huzuni muda wote. Mtu yule alikwenda kuzungumza na kuwashauri watu wa familia zote mbili, akiwalaumu kwa ukatili waliokuwa wameufanya dhidi ya mwanamke aliyekuwa hana namna yeyote ya kuweza kujisaidia au kujitetea. Kwa hisia na namna alivyolielezea jambo lile, wanafamilia wakaona walikuwa wamefanya makosa na wakajutia uamuzi waliouchukua. Upande wa wazazi

wa Abu Salamah رضي الله عنه wakaamua kumrejeshea watoto wake, na wazazi wake wakamruhusu kuondoka kuelekea Madinah.

Lakini sasa atawezaje kusafiri kwenda Madinah peke yake na watoto? Hakuna mtu aliyekuwa tayari kumsindikiza. Baadaye alijipa matumaini na ujasiri kwa kuwa sasa alikuwa yuko na watoto wake, aliamua kuanza safari kuelekea Madinah. Alipofika katika eneo lililoitwa Tan'im, alikutana na 'Uthman ibn Talhah 'Abdari, ambaye mpaka wakati huo alikuwa bado hajaingia katika Uislamu. 'Uthman ibn Talhah akamuuliza alikua anaenda wapi peke yake. Ummu Salamah رضي الله عنها akajibu kuwa alikua anakwenda kuungana na mume wake. Alishangaa sana kuona hakuna mtu yeyote katika familia yake aliyekuwa tayari kuongozana naye na kumsindikiza. Ummu Salamh رضي الله عنها akasema, hakuna yeyote aliyekuwa tayari kufanya hivyo na hivyo alikuwa akimtegemea Allah Peke Yake katika safari yake, hakika Yeye (Allah) ndiye Mlinzi na ndiye Mwenye Kumtoshereza. 'Uthman ibn Talhah 'Abdari akashika hatamu ya ngamia na kumwambia kuwa atamsaidia kufika kule anakotaka kwenda - Madinah.

Ummu Salamah رضي الله عنها anasema, ilikuwa sio jambo la kawaida kukutana na mtu muungwana, mtu mwenye moyo wa huruma kiasi kile asiye na dhamira yeyote mbaya. Kila walipofika mahala pa kupumzika, alikuwa akimfunga ngamia kwenye mti na kwenda mbali sana kulala chini na kupumzika. Alikuwa akifanya hivi ili kumpa faragha Ummu Salamah رضي الله عنها ili aweze kupumzika akiwa huru yeye na watoto wake. ulipofika muda wa kuondoka, alikuwa akimleta ngamia na kumfanya akae chini ili Ummu Salamah رضي الله عنها na wanae waweze kupanda. Alipopanda juu ya ngamia yeye na watoto wake, alikuwa akishika hatamu za ngamia na kuanza kutembea. Baada ya siku kadhaa walifika Quba ambayo haikuwa mbali sana na ulipo mji wa Madinah. Watu wa Banu 'Amr ibn 'Auf walikuwa wameweka makazi yao pale; 'Uthman ibn Talhah 'Abdari akasema, kwa kuwa Abu Salamah naye alikuwa ameweka makazi yake pale, basi anaweza kumuacha Ummu Salamah رضي الله عنها mahala hapo na kurejea Makkah. Ummu Salamah anasimulia katika kitabu chake kuwa, tabia njema na moyo wake wa huruma ulimuathiri sana Ummu Salamah رضي الله عنها. Furaha aliyokuwa nayo alipoiona familia yake imerudi kuwa pamoja ilikuwa kubwa sana kiasi kwamba ni vigumu kuieleza mtu akapata picha vipi hali ilikuwa. Itoshe kusema kuwa, hatimaye familia

iliyogawanyika makundi matatu ikarejea kuwa pamoja na watoto wakaendelea kupata malezi bora ambayo hayapatikani isipokuwa kwa familia iliyo pamoja.

Abu Salamah رضي الله عنها alipata bahati ya kushiriki katika vita vitakatifu na maarufu, vita vya Badr na baadaye akapata nafasi na fursa muhimu ya kushiriki vita vya Uhud kwa ajili ya kuuhami na kuutetea Uislamu – dini ya Allah Mtukufu. Lakini katika vita vya Uhud, Abu Salamah رضي الله عنها alijeruhiwa vibaya kwa mkuki. Alipata matibabu kwa muda wa mwezi mzima lakini hakupata nafuu. Jeraha lilikuwa linaonekana limepona, lakini kumbe lilikuwa linaonekana vile kwa juu tu na lilikuwa likiendelea kusambaa ndani kwa ndani. Baada ya miezi miwili toka vita vile vya Uhud, Mtume ﷺ alipata taarifa kuwa kabila la Banu Asad walikuwa wanapanga mipango ya kuwashambulia Waislamu. Aliwaagiza maswahaba zake wajiandae kwa vita, na akamteua Abu Salamah رضي الله عنه kuwa kamanda wa majeshi ya Waislamu. Waislamu walishinda vita na majeshi ya Banu Asad yalisambaratishwa. Waislamu wakapata ngawira nyingi kutokana na vita hivi. Mtume ﷺ alikuja kumjulia hali Abu Salamah na kumkuta akiwa amelala huku hali yake ikiwa mbaya sana. Mtume ﷺ aligundua kuwa Abu Salamah alikuwa anakaribia kufariki dunia, aliweka mkono juu yake na kumpa pole. Mtume ﷺ akamuombea dua, na Abu Salamah alimuomba Allah msamaha na kumuomba aipe familia yake mlezi mfano wake. Pia, alimuomba Allah ampe Ummu Salamah mume bora ambaye hatomfanya awe mwenye huzuni wala mwenye kumpa taabu.

Baada ya kuomba dua hii, mume wa Ummu Salamah رضي الله عنها alifariki dunia na Mtume ﷺ akamfunika macho yake. Ummu Salamah akawa anafikiria dua aliyoombewa na mume wake muda mfupi kabla ya kufariki, na kujiuliza nani anaweza kuwa mume bora kwake kuliko alivyokuwa Abu Salamah. Ummu Salamah رضي الله عنها akamuomba Mtume ﷺ amfundishe nini akiombe kwa ajili yake mwenyewe, Mtume akamfundisha kuomba msamaha kwa ajili yake na kwa ajili ya marehemu mume wake - Abu Salamah na amuombe Mwenyezi Mungu amjaalie na kumruzuku mwisho mwema.

Ummu Salamah رضي الله عنها anasema, alimuomba Allah na Allah akamjibu dua yake. Alipomaliza muda wake wa kukaa eda, Abu Bakr As-Siddiq alipeleka posa ili amuoe lakini Ummu Salamah akakataa. Kisha 'Umar ibn Khattab akapeleka posa, lakini akakataa pia kuolewa naye. Kisha Mtume ﷺ akapeleka posa ili amuoe. Ummu Salamah akasema alikuwa na mambo matatu ambayo

kama Mtume ﷺ atakuwa tayari kuyavumilia basi yeye atakuwa tayari kuolewa naye. Kwanza alisema yeye ni mwingi wa hasira na jazba, hivyo alihofia kuwa huenda akamkosea adabu Mtume ﷺ na hivyo kupoteza thawabu za matendo yake yote aliyoyafanya hapo kabla; Pili yeye Ummu Salamah alikuwa mwanamke mwenye umri mkubwa; Na tatu, yeye Ummu Salamah alikuwa na watoto wengi. Mtume ﷺ akamjibu kuwa: atamuombea kwa Allah na kama Allah atapenda hasira na jazba alizokuwa nazo zitaondoka. Ama kuhusu yeye kuwa mwanamke mwenye umri mkubwa, yeye (Mtume) pia alikuwa ana umri mkubwa; Na kuhusu watoto, kwa hakika hiyo ndiyo ilikuwa sababu hasa ya yeye kupeleka posa kwake ili apate fursa ya kuwalea na kusaidiana majukumu ya ulezi. Ummu Salamah anasema, majibu haya yalimpa faraja sana na hivyo akakubali kuolewa na kuwa mmoja kati ya wake wa Mtume wa Allah ﷺ. Hivi ndivyo Allah Alivyojibu dua ya Abu Salamah; na Ummu Salamah na kuolewa na Mtume ﷺ katika mwezi Shawwal, mwaka wa nne (4) baada ya Hijrah.

Mama Aishah anasimilia kuwa, ilikuwa ni kawaida ya Mtume ﷺ kuwatembelea wake zake wote baada ya Swala ya 'Asr. Alipofika katika kila nyumba ya mke wake, alikuwa akiwajulia hali na kuwauliza kama walikuwa wana mahitaji yeyote ambayo walihitaji kutimiziwa. Alikuwa akianzia nyumbani kwa Ummu Salamah kwa sababu yeye alikuwa ni mtu mzima zaidi kuliko wake zake wote kwa wakati huo, na alikuwa akimalizia mzunguuko wake kwa mama Aishah.

Kutokana elimu na busara aliyokuwa nayo Ummu Salamah, vitu hivi vilimfanya awe na hadhi kubwa. Baada ya makubaliano ya Hudaybiyah, Mtume ﷺ aliwaamuru maswahaba zake kuchinja wanyama waliokuja nao kwa ajili ya ibada ya Hijjah, na wanyoe nywele katika vichwa vyao. Lakini maswahaba wote walionekana wazito kutii amri hii na kufanya jambo hili. Ummu Salamah alipoona hali hii, alipendekeza kwa Mtume ﷺ kuwa asiongee na yeyote kumtaka afanye jambo hili, na badala yake atoke yeye (Mtume) nje ya hema lake, achinje mnyama wake na kunyoa nywele zake. Kisha ataona athari ya yeye kufanya kile alichoagiza maswahaba wafanye. Kile alichokitarajia ndiyo kilichotokea – Maswahaba wote wakafanya kile ambacho Mtume ﷺ alifanya.

Ummu Salamah رضي الله عنها alikuwa mwanamke mwerevu na mwingi wa busara. Alikuwa mwanamke aliyeelimika na alikuwa mwanamke aliyejitolea hasa kwa watu masikini na watu wenye mahitaji.

Aya kadhaa za Qur'an zilishushwa kwa Mtume ﷺ, Mtume ﷺ akiwa ndani ya nyumba ya mama huyu. Mfano mzuri ni Aya ifuatayo iliyopo ndani ya Surat Al-Ahzab:

إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجْسَ أَهْلَ ٱلْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾

***"...Mwenyezi Mungu Anataka kukuondoleeni uchafu, enyi watu wa nyumba (ya Mtume), na (anataka) kukutakaseni kabisa kabisa.* (33:33)**

Pia Aya zifuatazo zilizopo ndani ya Surat At-Tawbah zilishushwa kwa Mtume ﷺ, Mtume ﷺ akiwa ndani ya nyumba ya Ummu Salamah رضي الله عنها.

وَءَاخَرُونَ ٱعْتَرَفُوا۟ بِذُنُوبِهِمْ خَلَطُوا۟ عَمَلًا صَٰلِحًا وَءَاخَرَ سَيِّئًا عَسَى ٱللَّهُ أَن يَتُوبَ عَلَيْهِمْ ۚ

إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٠٢﴾

***"Na (wako) wengine wamekiri dhambi zao (wametubia kwa Mwenyezi Mungu, wakapokelewa). Wamechanganya vitendo vizuri na vingine vibaya. Asaa Mwenyezi Mungu akapokea toba zao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe (na) Mwingi wa Kurehemu."* (9:102)** Na:

وَعَلَى ٱلثَّلَٰثَةِ ٱلَّذِينَ خُلِّفُوا۟ حَتَّىٰٓ إِذَا ضَاقَتْ عَلَيْهِمُ ٱلْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ وَضَاقَتْ عَلَيْهِمْ

أَنفُسُهُمْ وَظَنُّوٓا۟ أَن لَّا مَلْجَأَ مِنَ ٱللَّهِ إِلَّآ إِلَيْهِ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوبُوٓا۟ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلتَّوَّابُ

ٱلرَّحِيمُ ﴿١١٨﴾

***"Na (pia akawaelekea kwa rehema yake) wale watatu waliongojeshwa (kukubaliwa toba yao kwa yale makosa yao makubwa waliyoyafanya); hata ardhi ikawa dhiki kwao, pamoja na wasaa wake; na nafsi zao zikadhikika juu yao, na wakayakinisha ya kwamba hakuna kwa kumkimbia Mwenyezi Mungu ila (kuelekea) Kwake, kisha (Mwenyezi Mungu) akawaelekea kwa rehema Yake ili wapate kukubaliwa toba yao. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye apokeaye toba na Mwenye rehema."* (9:118)**

Aya hii inazungumzia kutubia kwa dhati kwa maswahaba watatu Ka'b ibn Malik, Hilal ibn Umayyah na Mararah ibn Ar-Rabi'. Maswahaba hawa watatu, bila kuwa na sababu yeyote ile ya msingi, walikwepa kutoka na jeshi la Waislamu wakati lilipotoka kwenda katika vita vya Tabuk. Hivyo wakatengwa na Mtume ﷺ na maswahaba wengine. Maswahaba hawa walibakia katika hali hii huku wakiomba msamaha kwa Mwenyezi mungu kwa muda mrefu, mpaka pale Allah alipoamua kuwasamehe. Mtume ﷺ alikuwa amelala nyumbani kwa Ummu Salamah رضي الله عنها wakati Ayah hii ya mwisho ikishushwa kwake. Aliamka katika sehemu ya mwisho ya usiku na kumfahamisha mke wake Ummu Salamah kuwa dua ya kuomba msamaha kwa maswahaba hawa watatu ilikuwa imekubaliwa. Ummu Salamah akamuuliza Mtume ﷺ kama habari njema hizi zilipaswa kuwafikia maswahaba wale muda huo wa usiku. Mtume ﷺ akasema kulikuwa hakuna haja ya kuwasumbua katika usiku mwingi kiasi kile. Baada ya Swala ya Al- Fajr aliwaita na kuwapongeza. Walifurahi sana na hali ilikuwa hivyo kwa maswahaba wote.

Ummu Salamah رضي الله عنها alikuwa na bahati ya kushiriki vita vingi vilivyo na umuhimu mkubwa katika historia ya Uislamu. Ummu Salamah alikuwa na Mtume ﷺ wakati wa vita dhidi ya Bani Mustalaq, Ta'if, Khaybar, Hunayn na walikuwa pamoja wakati wa kuikomboa Makkah. Alikuwepo wakati wa kuingia makubaliano ya kihistoria – makubaliano yaliyopelekea kupatikana kwa mkataba wa Hudaybiyah na kiapo cha utii cha Ridhwan.

Salmaan Al-Farsi anasimulia kuwa, mtu mmoja alimwambia kuwa Malaika Jibril alikuwa ameshuka kutoka mbinguni na alikuwa akizungumza na Mtume wa Allah ﷺ. Salmaan alipokwenda pale alikuta mtu aliyekuwa akizungumza na Mtume ﷺ alikuwa ni Dahiah Al-Kalbi, na wakati huo Ummu Salamah pia alikuwa pamoja nao. Baada ya mazungumzo kumalizika, Mtume ﷺ akawauliza kama walikuwa wanamfahamu mtu aliyekuwa akizungumza nae. Ummu Salamah akajibu kuwa, alikuwa mmoja kati ya wafuasi wake waaminifu, Dahiah Al-Kalbi; Huku akitabasamu, Mtume ﷺ akamwambia kuwa hakika yule alikuwa Malaika Jibril aliyekuja akiwa katika sura ya kibinadamu

Ummu Salamah alikuwa mtu aliyekuwa na elimu kubwa katika masuala ya dini. Alikuwa amehifadhi Hadithi za Mtume ﷺ zipatazo Mia tatu themanini na Saba (387) kichwani kwake. Alikuwa anafahamu kwa kiwango cha juu kabisa mpaka mambo madogo madogo yanayohusu hukumu juu ya udugu wa

kunyonya na mambo ya talaka. 'Abdullah ibn 'Abbas alikuwa akimtaka ushauri juu ya mambo mengi yaliyohusu Shari'ah (hukumu za Kiislamu). Aliyekuwa akiongoza orodha ya maswahaba ambao walikuwa na uwezo mkubwa sana katika mambo ya Shariah alikuwa ni Ummu Salamah.

Ilikuwa ni vigumu sana kumpata mtu ambaye alikuwa mtaalamu na aliyemudu lugha mfano wa Ummu Salamah. Alipokuwa akizungumza, maneno yake yalikuwa yakichaguliwa na yalikuwa yakijieleza kwa utaalamu wa hali ya juu katika kuwasilisha wazo au ujumbe alioukusudia. Maandishi yake yalikuwa fasaha na yaliyowasilisha ujumbe kwa namna bora kabisa. Maswahaba na wafuasi wengi wamenukuu simulizi nyingi kutoa kwake.

Ummu Salama رضي الله عنها alijaaliwa kuishi umri mrefu na kufariki dunia akiwa na umri wa miaka themanini na nne (84), na alifariki mwaka wa 62 Hijiriyah. Ummu Salamah رضي الله عنها aliishi mpaka akauona utawala wa Makhalifa waongofu *(Khulafa' Ar-Rashidin*). Mke wa kwanza kufariki dunia baada ya kufariki Mtume ﷺ alikuwa ni mama wa Waislamu - Zaynab bint Jahash, na mke wa mwisho wa Mtume ﷺ kufariki baada ya kufariki Mtume wa Allah alikuwa ni Ummu Salamah. Wakati anafariki mama yetu huyu – Ummu Salamah رضي الله عنها, ilikuwa ni zama za utawala wa Yazid ibn Mu'awiyah na alizikwa katika eneo ambalo walizikwa wake wengine wa Mtume ﷺ katika eneo la Jannatul Baqi'.

يَٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفۡسُ ٱلۡمُطۡمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾ ٱرۡجِعِيٓ إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةٗ مَّرۡضِيَّةٗ ﴿٢٨﴾ فَٱدۡخُلِي فِي عِبَٰدِي ﴿٢٩﴾ وَٱدۡخُلِي جَنَّتِي ﴿٣٠﴾

***"Ewe nafsi yenye kutua! Rudi kwa Mola wako, hali ya kuwa utaridhika (kwa utakayoyapata), na (Mwenyezi Mungu) aridhike na wewe. Basi ingia katika (kundi la) waja Wangu (wazuri). Uingie katika Pepo yangu."* (89:27-30)**

# Ummu Habibah Ramlah binti Abi Sufyan

## Kupitia kwa Mfalme Niliolewa na Mtume!

Waraqah ibn Nawfal, 'Uthman ibn Huwayrith ibn Asad, Zayd ibn 'Amr ibn Nafil na 'Ubaydullah ibn Jahash walikuwa ni marafiki wanne ambao walikuwa wakikerwa sana kwa kitendo cha masanamu kuabudiwa katika Makkah na kwa hakika katika bara Arabu. Mara kadhaa walikuwa wakikutana na kujadili juu ya jambo hili. Usiku mmoja walipokuwa wakijadili juu ya jambo hili, walikubaliana kufanya utafiti kujua dini ya Nabii Ibrahim – dini ya haki na ya kweli ambayo watu walitakiwa kuifuata. Baada ya makubaliano haya, kila mmoja alishika njia kuelekea upande wake kuitafuta dini hiyo ya Nabii Ibrahim – Mtume wa Allah ﷺ.

Waraqah ibn Nawfal yeye akaamua moja kwa moja kuachana na kuabudu masanamu, akaacha kula nyama iliyochinjwa kwa ajili ya kuyatolea sadaka masanamu au wanyama waliochinjwa kwa jina la masanamu na akahifadhi Taurati na Injili kwa moyo kama vile vijana wetu wanavyohifadhi Qur'an hivi leo.

Binamu yake - Bi Khadijah رضي الله عنها ambaye baadaye alikuja kuwa mke wa Mtume, alimpeleka Muhammad ﷺ kwake (Waraqah ibn Nawfal) baada ya kupokea *Wahyi* wa kwanza katika pango la Hira. Waraqah akamfahamisha Bi Khadijah kuwa, aliyemtokea Muhammad ﷺ alikuwa Malaika yule yule ambaye alikuwa akileta ujumbe *(Wahyi)* kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa Mitume wengine waliotangulia. Alisisitiza kuwa, lazima Muhammad ﷺ atakuwa ni Mtume wa mwisho aliyeteuliwa na Allah, ambaye kuja kwake kulikuwa kumeelezwa wazi katika vitabu vilivyotangulia vya Taurati na Injili. Na kwamba muda si mrefu Muhammad ﷺ atainuliwa katika daraja na hadhi ya juu kabisa; na kwamba mataifa yote watakuwa dhidi yake na atalazimishwa kuihama ardhi

aliyozaliwa. Hata hivyo, Waraqah ibn Nawfal alifariki dunia kabla Mtume Muhammad ﷺ hajaanza kutangaza wazi kuwa yeye ni Mtume wa Allah ﷺ.

'Uthman ibn Huwayrith ibn Asad, yeye alisafiri na kuelekea Syria, na kufanya kazi kama mmishionari wa dini ya kikrito – akiutangaza ukristo. Akawa rafiki mkubwa wa mfalme na mtawala wa Warumi – Kaisari, na aliinuliwa na kupandishwa cheo mpaka akafikia hadhi (cheo) ya kuwa Baba Mtakatifu.

Zayd ibn 'Amr ibn Nafil yeye pia aliacha kuabudia masanamu. Aliacha kula wanyama waliokufa bila kuchinjwa na kuacha kunywa damu za wanyama. Alichukia kabisa jambo la kula nyama zilizotokana na wanyama waliochinjwa kwa ajili ya masanamu na mara zote alikuwa akizungumzia dini ya Nabii Ibrahim ﷺ. Bwana huyu pia alifariki kabla Mtume ﷺ hajaanza kutangaza bayana kuwa yeye ni Mtume wa Allah.

'Ubaydullah ibn Jahash akawa katika mashaka juu ya ipi haki na ipi batili. Bwana huyu alimuoa bint aliyekuwa mrembo wa sura na maumbile, mwanamke aliyekuwa na busara na msomi kutoka familia ya kiongozi wa kabila la Maquraishi - Abu Sufyan Sakhr ibn Harb.

Ilikuwa katika wakati huu, mji wa Makkah na vitongoji vyake na kwa hakika bara Arabu lilitikiswa na habari kuwa Muhammad ﷺ alikuwa akipinga masanamu yote. Na kwamba alikuwa akiwalingania watu kumuabudu Allah na alikuwa akitangaza wazi kuwa yeye (Muhammad) alikuwa ni Mtume wa Allah ﷺ. Bint mwenye busara wa Abu Sufyan – Ramlah bint Abu Sufyan, akaukubali Uislamu na mume wake pia akaukubali na hivyo wote wawili wakasilimu. Kaka zake wawili 'Abdullah ibn Jahsh na Abu Ahmad ibn Jahsh walikuwa tayari wameshasilimu. Dada zake, Zaynab hint Jahsh na Hamnah bint Jahsh pia walisilimu. Zaynab bint Jahsh alikuja baadaye kuolewa na Mtume ﷺ na hivyo kuwa miongoni mwa mama wa Waumini. Familia yote iliukubali Uislamu. Lakini kwa bahati mbaya, akiwa Uhabeshi 'Ubaydullah aliukana Uislamu baada ya kuwa ameukubali hapo mwanzo.

Abu Sufyan Sakhr ibn Harb رضي الله عنه alikuwa ni kiongozi miongoni mwa viongozi wa Maquraishi, mtu ambaye aliongoza jeshi la makafiri katika vita kadhaa dhidi ya Waislamu. Mbali ya mtoto wake wa kike Ramlah, bwana huyu alikuwa na watoto wawili wa kiume, Yazid na Mu'awiyah. Ramlah bint Abu Sufyan رضي الله عنها aliukubali Uislamu na kusilimu wakati ambao Uislamu ulikuwa

ukikabiliwa na upinzani mkubwa sana na Waislamu walikuwa wakikabiliwa na udhalilishaji na mateso makali kutoka kwa makafiri. Abu Sufyan alikuwa mtu mwenye ushawishi mkubwa na mwenye kuheshimika miongoni mwa Maquraishi, lakini alikuwa hana msaada wowote kwa bint yake Ramlah. Alikuwa hana msaada wowote kumtetea lakini alikuwa hana uwezo wa kumzuia kuukubali Uislamu na kusilimu na kutangaza wazi kuwa alikuwa ameingia katika Uislamu.

Wakati huo, baada ya kuitafakari kwa kina hali ilivyokuwa, Mtume ﷺ aliona kuwa Waislamu walikuwa wakipata mateso makubwa kutoka kwa Maquraishi. Na sasa njia iliyokuwepo kuwaepusha Waislamu na mateso zaidi ilikuwa ni kuwataka Waislamu wahame. Hivyo aliwaamuru Waislamu wahamie Uhabeshi, sehemu ambayo mtawala wake alikuwa akifahamika kwa upole na ukarimu wake kwa wageni na wahamiaji hususani wale waliokimbia mateso kutoka kwa viongozi katili katika nchi zao.

Ramlah bint Abu Sufyan رضي الله عنها na mume wake walikuwa katika kundi la pili lililohamia Uhabeshi. Wakiwa huko uhamishoni, Ramlah رضي الله عنها alijaaliwa na Allah kuzaa mtoto wa kike, mtoto ambaye walimwita Habibah na kuanzia hapo Ramlah رضي الله عنها akajulikana pia kama Ummu Habibah رضي الله عنها. Masiku yalikwenda haraka huku yeye Ramla au Ummu Habibah رضي الله عنها akijishughulisha na kumlea mwanae na muda aliokuwa na nafasi akiutumia kufanya ibada mbali mbali na kumkumbuka na kumtaja Mwenyezi Mungu.

Usiku mmoja, mama huyu aliota uso wa mume wake ukiwa umeharibika vibaya. Aliamka kutoka usingizini akiwa amehamaki na kufadhaika. Hata hivyo ndoto ile haikuwa ndoto iliyofaa kumsimulia mume wake. Siku chache baadaye mume wake alimwambia mkewe (Ramlah) kwamba, mwanzoni alikuwa mkristo akasilimu na kuingia katika Uislamu. Lakini toka alivyokuja Uhabeshi, amefikiria na kutafakari kwa makini sana na kugundua kuwa Ukristo ndio mfumo na imani sahihi inayompelekea mtu katika mafanikio ya maisha. Hivyo aliamua kuritadi na kurejea katika Ukristo. Alimshauri mkewe kufanya kama alivyofanya yeye (kuritadi) na kuwa Mkristo.

Mara moja ikambainikia Ramlah رضي الله عنها kuwa bila shaka hii ndiyo ilikuwa maana ya ndoto ile aliyoiota. Ndoto ambayo aliiona sura ya mume wake ikisinyaa na kuwa ndogo na kisha kuonekana imeharibiwa vibaya. Ndoto

hii ilimaanisha kuwa alikuwa amepoteza hadhi yake kama Muislamu. Kisha bi Ramlah akamsimulia mume wake ndoto ile, akitaraji kuwa pengine ingeweza kumfanya amuogope Mwenyezi Mungu ndani ya moyo wake. Lakini alikuwa tayari amekwishapotea njia ukweli wa kupotea; sio sura yake tu, bali hata moyo wake ulikuwa tayari umeshaharibiwa vibaya. Alianza kunywa pombe na akabobea katika ulevi kiasi kwamba muda mwingi alikuwa amelewa. Ummu Habibah sasa alikuwa amevunjika moyo na kujihisi mnyonge, huku akiwa na wasiwasi juu ya hatima ya mwanae na hatima yake mwenyewe. Ummu Habibah رضي الله عنها – Ramlah, alimuomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu abakie imara ndani ya imani yake.

Baada ya muda, 'Ubaydullah akafariki kutokana na kunywa pombe kupita kiasi. Ummu Habibah akawa amepata ahueni, lakini angeweza kufanya nini ili kuendelea na maisha na kukidhi mahitaji yake? mambo mawili tu yalikuwa yanamshughulisha – kumlea mwanae na ibada. Baadhi ya nyakati alikuwa akikutana na kujadiliana na wanawake wengine waliokuwa Uhabeshi juu ya yale yaliyokuwa yakiendelea kwa wakati huo. Ruqayyah رضي الله عنها, mtoto wa Mtume ﷺ, Asma' bint 'Umays na Laylah bint Abi Hashmah walikuwa wanawake wema na walikuwa ndio watu wake wa karibu aliokuwa akikaa na kuzungumza nao pale alipopata nafasi ya kufanya hivyo. Lakini haikupita muda mrefu wanawake hawa walirejea nyumbani - Makkah. Lakini bado kulikuwa na wanawake wengine wema ambao walikuwa rafiki zake na walimfanya abakie kuwa mtulivu.

Miaka ilipita na ramani ya utawala wa Kiislamu ikabadilika na vita vikaendelea kupiganwa baina ya Waislamu na makafiri. Mkataba wa Hudaybiyah ukasainiwa. Usiku mmoja akiwa amelala aliota mtu mmoja akimwita, "Mama wa Waumini". Alipoamka sio tu kwamba alijisikia na kujihisi mwenye furaha, bali alijisikia fahari kubwa. Wakati huo Mtume ﷺ alikuwa amehamia Madinah na dola ya Kiislamu ilikuwa imesimama na Madinah ikiwa ndio makao makuu yake. Mtu mmoja alipokuwa akizungumza na Mtume ﷺ juu ya hali ya mambo yalivyokuwa Uhabeshi, akatamka kuwa Ummu Habibah, bint kutoka familia tajiri na maarufu alikuwa akiishi kwa dhiki kule Uhabeshi, baada ya mume wake kuritadi na baadaye kufariki. Na kwamba amekuwa akiishi katika hali ngumu kwa muda sasa. Mtume ﷺ alivyosikia habari hii, alimtuma 'Amr ibn Umayyah kwenda kwa Mfalme Najashi akiwa na ujumbe

kwamba ikiwa Ummu Habibah atakuwa tayari (ataridhia) basi Mtume ﷺ yuko tayari kumuoa na kumtaka Mfalme Najashi kusimamia ndoa hiyo ikiwa Ummu Habibah atakubali.

Mfalme Najashi alipopata ujumbe ule, alimtuma mjakazi wake - Abraha kwenda kwa Ummu Habibah. Ummu Habiba alifurahi sana aliposikia pendekezo na posa ile kutoka kwa Mtume ﷺ. Kutokana na furaha aliyokuwa nayo, alimzawadia mjakazi yule aliyetumwa ujumbe (Abraha) mapambo yote ya fedha aliyokuwa ameyavaa – bangili, hereni pete na mikufu. Abraha akamwambia Ummu Habiba kuwa, atatakiwa pia amteue mtu atakaemuwakilisha katika hafla ya harusi kama mzazi wake. Ummu Habiba akamtaja ndugu yake kutoka katika kabila la Maqurashi, Khalid ibn Sa'id ibn 'Aas.

Jioni ile ile Mfalme Najashi akatuma ujumbe kwenda kwa Ja'far ibn Abi Talib akimtaka aende yeye na ndugu zake (Waislamu) wote nyumbani kwa Mfalme. Baada ya Waislamu wote kuwa wamekusanyika katika ukumbi wa Mfalme, Mfalme alitangaza habari ya ndoa ya Ummu Habibah. Baada ya kumshukuru na kumtukuza Allah alisema, amepokea ujumbe na ombi kutoka kwa Mtume ﷺ akimtaka yeye (Mfalme Najashi) asimamie ndoa baina ya Mtume ﷺ na Ummu Habibah ikiwa atakubali kuolewa na Mtume ﷺ, na kwamba Mfalme alikuwa anampa Dinar Mia Nne (400) Ummu Habibah kama mahari yake kwa niaba ya Mtume wa Allah.

Kisha muwakilishi wa Ummu Habibah رضي الله عنها, Khalid ibn Sa'id ibn 'Aas, akasoma ujumbe kwa sauti, ujumbe huo ulisomeka:

"Sifa zote njema ni zake Allah, Yeye (Allah) ndiye Mwenye kushukuriwa, ndiye Mwenye kuombwa msaada na ndiye Mwenye kuombwa msamaha; Nashuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na ninashuhudia kuwa Muhammad ﷺ ni Mtume wake. Naapa kwa yule aliyemtuma (Mtume Muhammad) akiwa na dini ya haki na muongozo ili dini hiyo iwe juu ya dini zote za upotovu japo washirikiana na makafiri watachukia. Nimekubali ombi la Mtume ﷺ na kumuozesha Ummu Habibah bint Abu Sufyan. Namuomba Allah atie Baraka juu ya ndoa hii na aifanye iwe ndoa yenye matunda kwa Baraka za Mtume Muhammad ﷺ."

Kisha Najashi alikabidhi Dinar Mia nne (400) kwa Khalid ibn Sa'id. Hakuna mke mwingine yeyote wa Mtume ﷺ aliyeolewa kwa mahari kubwa kiasi hiki

ila Ummu Habibah. Wageni wote waliposimama wakitaka kuondoka baada ya kumalizika tukio hili, Mfalme Najashi aliwataka wasubiri chakula kilichoandaliwa kwa ajili ya kusherehekea harusi.

Ummu Habibah alikuwa mama mcha-Mungu na mwingi wa shukurani na hivyo Mwenyezi Mungu akampa heshima na kumuinua kufikia daraja la kuwa miongoni mwa mama wa Waumini – Mmoja kati ya wakeze Mtume ﷺ. Ummu Habibah alimtumia Abraha Dinar hamsini (50) na kumwambia kuwa, kwa rehema zake Allah sasa alikuwa na fedha, na kumuomba radhi kwa kushindwa kumzawadia katika wakati uliokuwa muafaka zaidi, kwa sababu kwa wakati ule alipomletea taarifa za posa kutoka kwa Mtume ﷺ alikuwa hana chochote cha kuweza kumpa zaidi ya mapambo machache aliyompa. Alimuomba Abraha kutumia fedha zile kujinunulia nguo na mapambo. Abraha naye akampa mkoba mdogo ambao ndani yake ulikuwa na marashi yaliyokuwa na thamani kubwa ambayo Mfalme Najashi aliwaagiza wake zake wamtumie Ummu Habibah. Na akamkabidhi pia mapambo yale yale ambayo aliyapokea kutoka kwake (kutoka kwa Ummu Habibah), huku akiomba radhi kuwa hakuwa na uwezo wa kumpa vitu vilivyo na thamani. Abraha alimtumia pia ujumbe Mtume ﷺ kuwa yeye alikuwa amesilimu, lakini kusilimu kwake alikuwa amekufanya kuwa siri. Alimuagiza Ummu Habibah رضي الله عنها kuwa, mara tu atakapokutana na Mtume ﷺ – kipenzi cha Waislamu wote, amfikishie salamu hizo bila kusahau na kwamba hilo ndilo analoweza kufanya mwanamke masikini kama yeye.

Ummu Habibah رضي الله عنها alipofika Madinah alimsimulia Mtume ﷺ yale yote yaliyotokea Uhabeshi na ukarimu wa Mfalme Najashi na jinsi ndoa ilivyoandaliwa na kufanyika. Alimwambia pia kuhusu mtumwa wa kike - Abraha na salamu nyingi tena za heshima ya hali ya juu alizomtuma amfikishie Mtume ﷺ. Mtume ﷺ alifurahishwa sana na salamu zile; katika kumrejeshea salamu, alimuombea kwa Mwenyezi Mungu amjaaliye ukamilifu na uongofu. Abu Sufyan alipopata habari juu ya ndoa ya mwanae alifurahi sana na kuidhihirisha furaha yake japo kuwa mpaka wakati huo alikuwa bado hajaingia katika Uislamu. Alisema Mtume ﷺ alikuwa ni mtu aliyejaaliwa na mwenye kuheshimika.

Wakati Maquraishi walipovunja mkataba wa Hudaybiyah, Abu Sufyan alifunga safari kwenda Madinah kujaribu kufunga mkataba mpya. Alipofika

Madinah, alimtembelea bint yake – Ummu Habibah رضي الله عنها; alipotaka kukaa chini tu, Ummu Habibah alisimama haraka na kukunja zulia jepesi lililokuwa limetandikwa alilotaka kukalia baba yake. Abu Sufyan alishangaa na kumuuliza mwanae kama yeye (baba yake) alikuwa hana hadhi ya kukalia zulia lile au zulia lile lilikuwa halina hadhi ya kukaliwa na yeye. Ummu Habibah akamjibu kuwa, zulia lile lilikuwa likitumiwa na mtu msafi na mtu muhimu – Mtume ﷺ, na mtu aliyekua akiabudia masanamu alikuwa hana hadhi ya kukaa juu ya zulia lile kwa sababu hakuwa msafi, na kuongeza kuwa hii ndio sababu iliyomfanya aliondoe yeye asilikalie. Abu Sufyan alikasirika sana na kumwambia mwanae kuwa alikuwa amesahau na kukosa adabu toka alipoondoka katika mikono yake (ulezi wake). Ummu Habibah رضي الله عنها akamjibu baba yake kuwa, Uislamu umemfundisha adabu na nidhamu; Na zaidi ya hayo, Uislamu umemfundisha kuwa usafi una maana nyingine. Kwa kuwa hakuwa akijua maana ya msingi ya maneno haya, alikuwa anaona anatukanwa. Ummu Habibah رضي الله عنها akasema, "Namshukuru Allah kwa kuniongoza katika njia na kuukubali Uislamu. Nilishangazwa kuona kuwa, pamoja na baba yangu kuwa mtu muelewa mkubwa na kiongozi wa moja katika makabila ya Maquraishi, alikuwa bado hajaukubali Uislamu. Alikuwa bado anadanganywa na starehe za dunia. Lakini kwa kuzingatia vipimo vya kawaida vya kuitambua dini ya haki na maisha sahihi kwa hakika alikuwa yuko nyuma sana tena mbali na ukweli. Hivi inawezekana vipi mtu mwenye akili aabudu jiwe ambalo halisikii wala halioni? Jiwe ambalo haliwezi kujibu maombi yake wala kuyakataa!?" Abu Sufyan hakufurahishwa na yale aliyoambiwa na bint yake. Abu Sufyan akamuuliza mwanae, itawezekana vipi yeye katika umri ule akanushe dini na miungu waliyokuwa wakiiamini wazee wake na kufuatwa na kizazi hadi kizazi?

Ummu Habibah رضي الله عنها alikuwa na hamu sana ya kumuona baba yake na kaka yake wanaingia katika Uislamu ili hatimaye Mwenyezi Mungu Awalipe Pepo. Alikuwa hataki watoke katika dunia hii wakiwa makafiri kama ilivyokuwa kwa Abu Jahl, Walid ibn Al-Mughirah, 'Aas ibn Wa'il, 'Utbah ibn Rabi'ah na Shaybah ibn Rabi'ah. Wakati Waislamu walipoikomboa Makkah, Abu Sufyan na Mu'awiyah waliposilimu na kuchukua ahadi ya utii kwa Mtume ﷺ, furaha yake ilikuwa kubwa isiyokuwa na mfano. Aya ifuatayo ya Qur'an ilishushwa:

عَسَى ٱللَّهُ أَن يَجْعَلَ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ ٱلَّذِينَ عَادَيْتُم مِّنْهُم مَّوَدَّةً ۚ وَٱللَّهُ قَدِيرٌ ۚ وَٱللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٧﴾

***"Asaa Mwenyezi Mungu Atatia mapenzi baina yenu na hao maadui zenu, na Mwenyezi Mungu ni Muweza. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe (na) Mwingi wa Kurehemu; (atawawafikia kusilimu."*** **(60:7)**

Ibn 'Abbas anasema, Aya hii ilishushwa wakati wa ndoa baina ya Mtume ﷺ na Ummu Habibah رضي الله عنها. Ndoa hii iliwavutia watu maarufu na waliokuwa na hadhi na mamlaka katika makabila ya Maquraishi kama vile Abu Sufyan, Mu'awiyah na Yazid ibn Abu Sufyan. Wakashawishika na Allah Akaingiza mapenzi katika nyoyo zao juu ya dini ya Allah, wakasilimu na kujiunga na wafuasi wengine wa Mtume ﷺ.

Abu Al-Qasim ibn Asakar akimnukuu Hassan anasema: Siku moja Mu'awiyah alimtembelea Mtume ﷺ na alikaa na Ummu Habibah رضي الله عنها akiwa pembeni yake. Alipotaka kuondoka, Mtume ﷺ alimwita na kumuomba wakae. Kisha Mtume ﷺ, akamwambia kuwa, kwa hakika yeye (Mtume) anatamani wote watatu wangekaa pamoja na kunywa kinywaji cha Peponi.

Maneno haya yalikuwa na maana kuwa, Mwenyezi Mungu Akipenda wote watatu wawe pamoja Peponi. Katika namna ile ile, habari njema na ubashiri juu ya Ummu Habibah رضي الله عنها kuwa mtu wa Peponi unapatikana katika kauli maarufu ya Mtume ﷺ kwamba, hakika yeye ameamrishwa kuoa wanawake wanaostahili kuwa wanawake wa Peponi, hivyo mama huyu - Ummu Habibah ni mtu wa Peponi.

Hii ina maana kuwa wake wote wa Mtume ﷺ – ambao ni mama wa Waumini wamebashiriwa habari njema kuwa Wote watakwenda Peponi.

Jina halisi la Mfalme Najashi, kiongozi na mtawala wa Uhabeshi alikuwa anaitwa Ashamah, jina lililokuwa na maana ya "Zawadi". Jina hili liliendana na tabia yake, kwa sababu alikuwa mtoaji mkubwa wa sadaka na alipenda sana kutoa na kuwasaidia watu wenye shida. Jina lake kwa hakika lilikuwa limepata mtu mwenye kushabihiana nalo hasa. Alikuwa ni mtawala mwenye huruma sana. Alisilimu na kuingia katika Uislamu baada ya kuona mfumo na mwenendo wa maisha wa Kiislamu kutoka kwa Waislamu waliohamia Uhabeshi wakitokea Makkah.

Malaika Jibril alimpa habari Mtume ﷺ juu ya kifo cha Mfalme huyu kilipotokea kutokana na sababu za kawaida. Mtume ﷺ akamuombea msamaha

kwa Mwenyezi Mungu kwa dhambi na makosa aliyokuwa ameyafanya. Maswahaba wa Mtume ﷺ na wahamiaji wote waliokwenda Uhabeshi wakitokea Makkah – wanaume kwa wanawake, waliopata uhuru wa kutosha kumuabudu Mola wao bila mateso wala udhalilishaji katika ufalme wake, walihuzunika sana walipopata taarifa juu ya kifo cha Mfalme Najashi. Wote walikumbuka wema wake, ukarimu wake, ushirikiano aliowapa na hifadhi aliyowapa wakati wa hali ngumu iliyokuwa ikiwakabili. Walimuombea msamaha kwa Allah ili amsamehe dhambi zake na amlipe Pepo.

Kutokana na elimu na uwezo wake mkubwa wa kuzielewa na kuzihifadhi hadithi, Ummu Habibah رضي الله عنها alipewa hadhi na kushika namba tatu miongoni mwa wake za Mtume ﷺ. Mtu aliyeshika namba moja katika orodha hii ni mama Aishah na wa pili ni Ummu Salamah رضي الله عنها. Kuna jumla ya hadithi za Mtume ﷺ zipatazo sitini na tano zilizopokelewa na Ummu Habibah رضي الله عنها. Baadhi ya hadithi hizo zimenukuliwa na wanaume kama Mu'awiyah, 'Abdullah ibn 'Utbah ibn Abu Sufyan, 'Urwah ibn Zubayr, Salem ibn Shawal Ibn Maki na Abu Al-Jarrah ibn Qurashi. Miongoni mwa wanawake walionukuu hadithi kutoka kwake ni Zaynab bint Umm Salamah Makhzumiyyah na Safiyyah bint Shaybah 'Abdariah.

Katika Sahih Al-Bukhari imetajwa kwamba, siku tatu baada ya kupokea taarifa ya msiba wa baba yake Ummu Habibah رضي الله عنها alitumia manukato. Kisha alisema, hakukuwa na hitajio la yeye kutumia manukato siku ile, lakini Mtume ﷺ amesema: *"Ni haramu kwa Mwanamke wa Kiislamu anayemuamini Allah na siku ya Mwisho kulia (kutokana na msiba) kwa zaidi ya siku tatu, isipokuwa kwa mume wake. Kisha ataendelea kukaa eda kwa miezi minne na siku kumi."*

Kuna hadithi nyingine iliyopokelewa na Ummu Habibah imenukuliwa na Abul Jarrah Qurashi katika Musnad kuhusu (umuhimu wa) kupiga mswaki. Ummu Habibah رضي الله عنها anasema, Mtume ﷺalisema: *"Kama sio kuchelea uzito kwa Ummah wangu, basi ningefaridhisha (ningefanya kuwa lazima) kwa Ummah wangu kupiga mswaki kabla ya kila Swala kama ambvyo hutawadha kabla ya kila Swala."*

Hadithi nyingine aliyosimulia imenukuliwa katika Musnad Abu Ya'la, Musnad Abu Ahmad na vitabu vingine vya kuaminika vya hadithi kama vile

Abu Dawud, An-Nasa'i, At-Tirmidhi na ibn Majah. Hadithi hii inahusiana na Swala ya Adhuhuri. Mtume ﷺ anasema: *"Yeyote mwenye kudumu kuswali rakaa nne za Sunna, mbili kabla na mbili baada ya Swala ya Dhuhur, Mwenyezi Mungu Atauharamisha moto wa Jannamu juu yake."*

Mtu mmoja alipompelekea habari kuwa 'Uthman ibn 'Affan ameuwawa nyumbani kwake baada ya kuwa amezingirwa, mama huyu alihuzunika sana na alimuomba Allah, mikono ya muuaji ikatike ili ajulikane na iwe aibu kwake kwa jamii. Na Mwenyezi Mungu akajibu dua yake. Mtu mmoja akaingia ndani ya nyumba ya muuaji wa Khalifa Uthman ibn Affan رضي الله عنه na kumshambulia bwana yule – muuaji kwa upanga; na muuaji yule alipojaribu kujihami kwa mkono wake wa kulia, mkono ule ulikatwa. Kisha bwana yule alitaka kumponyoka mshambuliaji na kukimbilia mitaani huku akiwa ameshikilia shuka yake kwa meno. Lakini hakuweza kufanya hivyo, shuka ilianguka na akabaki uchi mbele ya watu wote mtaani.

Wakati wa utawala wa kaka yake - Mu'awiyah, mama huyu alitembelea mji mkuu wa Syria, Damascus. Ilikuwa wakati wa utawala huu, mama huyu alifariki dunia akiwa katika mji wa Madinah katika mwaka 44 Hijiriyah. Kabla ya kifo chake, Ummu Habibah رضي الله عنها alituma ujumbe kwa mama Aishah رضي الله عنها na Ummu Salamah رضي الله عنها akiwaomba radhi ikiwa kuna kosa lolote alilowafanyia walipotofautiana au kutokukubaliana. Wote Aishah na Ummu Salamah رضي الله عنهما waliguswa sana na ujumbe huu na mwenendo huu na hatua hii aliyoichukua. Bila shaka, anastahili kuambiwa:

يَـٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفْسُ ٱلْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾ ٱرْجِعِىٓ إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةً مَّرْضِيَّةً ﴿٢٨﴾ فَٱدْخُلِى فِى عِبَـٰدِى ﴿٢٩﴾ وَٱدْخُلِى جَنَّتِى ﴿٣٠﴾

***"Ewe nafsi yenye kutua! Rudi kwa Mola wako, hali ya kuwa utaridhika (kwa utakayoyapata), na (Mwenyezi Mungu) aridhike na wewe. Basi ingia katika (kundi la) waja Wangu (wazuri). Uingie katika Pepo yangu."*** **(89:27-30)**

# Juwayriyyah bintil - Haarith ibn Abi Diraar

## Aliyeomba Kilicho Bora na Kupewa Kilicho Bora na kizuri Zaidi

Jina kamili la mama huyu ni Barrah bint Al-Haarith ibn Abi Diraar رضي الله عنها, jina ambalo ndilo alilopewa na wazazi wake. Mtume ﷺ alimbadilisha jina na kumwita "Juwayriyah". Suala la Mtume ﷺ kubadilisha majina ya maswahaba wake halikuwa jambo geni, kwani alikwisha fanya hivi kwa maswahaba wengine pia, iwe kwa wanawake au kwa wanaume. Mara nyingi Mtume ﷺ alikuwa akifanya hivi ikiwa jina alilokuwa akitumia swahaba kabla ya kuingia katika Uislamu halikuwa na maana nzuri na wakati mwingine alikuwa akifanya hivi kumfanya swahaba aache kila alichokuwa nacho katika ukafiri.

Ama kuhusu kwanini Mtume ﷺ alibadili jina la mama huyu kutoka jina lake la awali la 'Barrah', kuna maoni tofauti juu ya hili, wengine wakisema Mtume ﷺ aliamua kufanya hivyo kwa maana ya kuachana na jina alilolitumia wakati wa ukafiri, huku wengine wakiamini alifanya hivyo kwa sababu ya ubora wa maana ya jina jipya alilopewa na Mtume ﷺ.

Mtume ﷺ hakupenda mtu kujisifu yeye mwenyewe, na jina 'Barrah' linatokana na neno 'birr', ambalo lina maana ya 'aliye bora au mcha-Mungu'. Inawezekana vipi mtu ajiite wazi 'mcha-Mungu' kwa kutumia jina hilo? Bila shaka ni jambo lisilokubalika. Mtume ﷺ asingependa kumsikia mtu akisema "Nimetoka nyumbani kwa 'Barrah'" (Ikiwa na maana nimetoka nyumbani kwa mcha-Mungu au kwa aliye bora)." Na Allah ndiye Mjuzi juu ya yote.

Jina "Juwayriyah" linatokana na neno "Jaariyah". Neno hili ni neno la kiarabu ambalo hutumika mara nyingi kwa mtoto wa kike au mwanamke mwenye hadhi baada ya kuwa huru. Hivyo linaweza kutumika kumsifu au kuonesha mapenzi na heshima.

Juwayriyah ni nani hasa? Juwayriyah alikuwa ni binti wa chifu wa kabila la Banu Mustaliq, aliyeitwa Al-Haarith ibn Abi Diraar. Na mama huyu aliolewa na mmoja katika viongozi maarufu na mashuhuri wa kabila lao akiitwa Mani ibn Safwaan.

Banu Mustaliq ni moja kati ya makabila ambayo yalipigana vita dhidi ya Waislamu huku wakiwa na dhamira ya kuizima Nuru ya Allah kwa vinywa vyao na mikono yao. Banu Mustaliq walibakia katika kiza na ujinga wa ukafiri na wakakusanya silaha na kufanya maandalizi ili kuwavamia Waislamu na kuushambulia mji wa Madinah.

Mtume ﷺ, kiongozi shupavu na Mtume wa Allah ﷺ, alikuwa ameteua maafisa usalama miongoni mwa maswahaba wake makini na mahiri kufuatilia nyendo za maadui ili kufahamu njama zao na maandalizi waliyonayo kutaka kuwashambulia Waislamu. Mtume ﷺ aliweza kufahamu dhamira, mipango na maandalizi waliyokuwa nayo Banu Mustaliq kutaka kuwavamia Waislamu kupitia mmoja kati ya maafisa usalama wake. Kama kiongozi na Kamanda mwenye ujuzi na mzoefu, Mtume ﷺ aliamua kufanya mashambulizi ya kushitukiza dhidi yao. Mtume ﷺ alisogea na kuweka kambi karibu na kisima kiitwacho Al-Muraysee. Kisha aliwashambulia vikali na kuzima kabisa matumaini yao na ndoto zao za kutaka kuwashambulia Waislamu.

Hapa ndipo ilipoanza safari na historia muhimu ya mama huyu, Juwayriyah. Sasa tumpe nafasi mama wa Waumini, Aishah bint Abu Bakr رضي الله عنها ili atueleze nini kilitokea katika masiku hayo:

“Mtume ﷺ aliwachukua wanawake kutoka kabila la Banu Mustaliq kama mateka. Alichukua moja ya tano ya wanawake wote na waliosalia, aliwagawa miongoni mwa maswahaba zake, huku akiwapa mbili ya tatu ya wanawake wale, askari waliokuwa wakitumia farasi na moja ya tatu akiwapa askari wa miguu.

Juwayriyah akawa miongoni mwa wanawake waliogawiwa kwa Thaabit ibn Qays al-Ansaari. Kabla ya kuchukuliwa mateka, mama huyu alikuwa ameolewa na binamu yake akijulikana kwa jina la Mani ibn-Safwan ibn Maalik ibn Judaymah, ambaye anafahamika pia kwa jina la Dhu Ash-Shafra. Mama huyu alikuwa mtu mwenye busara, na aliingia katika makubaliano na Thaabit ibn Qays ili ajikomboe kwa kulipa fidia ya Waqiyah tisa.”

Mama Aishah رضي الله عنها anamuelezea mama huyu, Juwayriyah akisema "Alikuwa mwanamke mwenye kuvutia. Hakuna mwanamume yeyote aliyemuona isipokuwa mwanamume huyo alivutiwa na mama huyu. Wakati Mtume ﷺ akiwa amekaa, mara Juwayriyah aliingia na kuanza kuzungumza na Mtume ﷺ kuhusu makubaliano yake na Thaabit kuhusu kujikomboa. Naapa kwa jina la Allah, mara tu nilipomuona Juwayriyah, sikufurahi kumuona anaingia na kwenda mbele ya Mtume ﷺ, kwa sababu nilifahamu bila shaka kuwa, Mtume ﷺ ataona yale niliyoyaona kwa Juwayriyah. Kisha Juwayriyah akaanza kuongea na Mtume ﷺ na kusema, 'Ewe Mtume wa Allah! Mimi naitwa Juwayriyah, mtoto wa Al-Haarith – ambaye ni kiongozi wa watu wake. Bila shaka unafahamu vema nini kimenitokea (juu ya kuchukuliwa kwangu mateka). Mimi nimekuwa katika sehemu ya mgao wa Thaabit ibn Qays na nimekubaliana naye nijikomboe kwa kumlipa Waqiyah tisa. Nakuomba unisaidie ili nijikomboe na kujiweka huru.' Mtume ﷺ akamjibu: *"Je, unahitaji kilichokuwa bora kuliko hicho?".*

Juwayriyah akamuuliza, 'Ni kipi hicho kilicho bora zaidi ya niombacho?' Mtume ﷺ akamjibu: *"nitalipa fidia hiyo kwa niaba yako, kisha nitakuoa."*

Mama Juwayriyah akajibu, 'Ndiyo Ewe Mtume wa Allah.' Kisha Mtume ﷺ akasema: *"Tayari nimeshafanya hivyo (nimeshakulipia na kukuoa)."*

Tukio hili linatufanya kuvutiwa na kujadili kidogo juu ya baadhi ya ndoa za Mtume ﷺ. Kuna mazingatio makubwa kwa wanaume kwa kila ndoa ya Mtume ﷺ. Kuoa kwake kulitokana na mapenzi (kupenda) kama ilivyo kwa binadamu wengine walivyoumbwa na Allah na kuwekewa mapenzi katika maumbile yao. Hata hivyo kupenda haikuwa sababu kubwa na ya pekee katika kuoa kwake.

Kuna ushahidi mwingi na wa kutosha toka katika ndoa yake ya mwanzo kabisa na Bi Khadijah wakati yeye Mtume ﷺ akiwa kijana mwenye nguvu wakati Bi Khadijah alikuwa mwenye umri wa miaka arobaini (40) na pengine akikaribia kukoma hedhi. Kisha alimuoa bi Sawdah رضي الله عنها, mwanamke aliyekuwa mnene na mwenye uzito mkubwa. Hata hivyo, mama huyu, Sawdah رضي الله عنها alikuwa miongoni mwa Waislamu wa mwanzo na miongoni mwa Wanawake wa Kiislamu waliohama kwa ajili ya Allah na Mtume ﷺ kutoka Makkah kwenda Madinah na mwanamke aliyekuwa akimuabudu Allah ukweli

wa kumuabudu. Kisha Mtume ﷺ akamuoa Aishah, na amri ya kumuoa mama huyu ilitoka kwa Allah. Hata hivyo hakuanza maisha ya ndoa na binti huyu mpaka baada ya takriban miaka miwili. Na hata wakati huo, ilikuwa ni baada ya baba wa mama huyu, Abu Bakr رضي الله عنه kumkumbusha na kumsisitiza juu ya jambo hili. Ni muhimu sana kukumbuka kuwa kulikuwa na mahusiano ya karibu sana baina ya Mtume ﷺ na familia ya Abu Bakr رضي الله عنه. Hivyo ndoa hii ilikuwa na umuhimu katika kuimarisha na kutia nguvu udugu na uhusiano ambao tayari ulikuwepo. Na hili linakuwa na nguvu zaidi katika jamii ambayo mahusiano ya koo yanapewa nafasi kubwa na hivyo kwa kufanya hivi ilisaidia pia katika harakati za kueneza Uislamu.

Mtume ﷺ pia akaunga udugu na ukoo wa Ummayyah baada ya kumuozesha mabinti zake wawili, Ruqayyah na Ummu Kulthum, ‘Uthmaan Ibn Affan رضي الله عنه, mmoja kati ya watu waliokuwa na ushawishi mkubwa katika ukoo wa Ummayyah kwa hadhi yake, utajiri aliokuwa nao na ushawishi.

Unaweza pia kuzingatia ndoa ya Mtume ﷺ na mama wa waumini, Ummu Habibah رضي الله عنها. Mama aliyekuwa akihangaika na kutaabika kutokana na upweke uliotokana na ujane na kuhama kwake. Mama huyu alikuwa mtoto wa Abu Sufiyaan رضي الله عنه, mmoja kati ya watu mashuhuri miongoni mwa Maquraysh katika siasa na vita, na akiwa pia Chifu wa kabila la Banu Umayyah. Tumekwisha nukuu maneno aliyoyatamka Abu Sufiyaan alipopata habari kuwa Mtume ﷺ amepeleka posa ili amuoe binti yao. Hii inadhihirisha busara aliyokuwa nayo Mtume ﷺ. Kuimarisha udugu na mahusiano mema ni miongoni mwa mambo muhimu katika kueneza Uislamu. Sasa turejee katika kufuatilia historia ya Juwayriyah na namna alivyokuja kuwa miongoni mwa wanawake waliokuwa karibu na Mtume ﷺ.

Tumeona namna gani Juwayriyah alivyoanza mazungumzo yake na Mtume ﷺ, alianza kwa kumwita: “Ewe Mtume wa Allah!” sentensi hii ilimaanisha na kuweka wazi imani yake juu ya Uislamu na Mtume ﷺ.

Kisha mama huyu akasema, “Mimi naitwa Juwayriyah, mtoto wa Al-Haarith – ambaye ni kiongozi wa watu wake. Bila shaka unafahamu vema nini kimenitokea (juu ya kuchukuliwa kwangu mateka). Mimi nimekuwa katika sehemu ya mgao wa Thaabit ibn Qays na nimekubaliana naye nijikomboe kwa kumlipa Waqiyah tisa. Nakuomba unisaidie ili nijikomboe na kujiweka huru.”

Juwayriyah alikuja kwa Mtume ﷺ na kuomba kilicho bora na kupewa kilicho bora na kizuri zaidi.

Bila shaka hatua hii aliyoichukua Mtume ﷺ iliacha athari kubwa sana katika moyo wa mama huyu na kwa hakika katika nyoyo za watu wa familia na ukoo wake. Mama Aishah رضي الله عنها anasema, "Taarifa juu ya Mtume ﷺ kumuoa mama huyu zilipowafikia maswahaba, maswahaba walianza kusema, 'Inawezekanaje shemeji zake Mtume ﷺ washikiliwe mateka?!'. Maswahaba wakawaachia huru mateka wote waliokuwa nao kutoka kwa Banu Mustaliq (kwa sababu walikuwa kama shemeji zake Mtume), na wale walioachiwa walikuwa kiasi cha kaya mia moja! Hii haikuwa kwa sababu nyingine yeyote ila kutokana na ndoa ya Mtume ﷺ na Juwayriyah." Ni katika hatua hii, mama Aishah رضي الله عنها anasema: "Simfahamu mwanamke mwingine yeyote ambaye aliwahi kuleta neema kwa watu wake zaidi ya neema aliyoileta Juwayriyah kwa watu wake. Na hii ilikuwa ni mara tu baada ya kutoka katika vita vya Muraysee' dhidi ya watu wa Banu Mustaliq."

Mama huyu, Juwayriyah رضي الله عنها anazo sifa nyingi zinazothibitisha utiifu wake na imani yake thabiti juu ya Allah na Mtume ﷺ. Itoshe kuwa yeye alikuwa katika familia na nyumba ya Mtume ﷺ, nyumba ambazo Ayah za Mwenyezi Mungu zilikuwa zikishushwa kwa Mtume wa Allah ﷺ.

Ibn Abbas anasimulia kuwa, hapo kabla Juwayriyah alikuwa anaitwa 'Barrah', na Mtume ﷺ akamwita 'Juwayriyah'. Kisha anasema: "Mtume ﷺ aliswali Swala ya Alfajiri, kisha akaondoka nyumbani kwa Juwayriyah. Mtume ﷺ aliendelea kuwa nje ya nyumba yake na kurejea baada ya adhuhuri na kumkuta bado mama huyu akiwa pale pale alipomuacha. Juwayriyah akamwambia Mtume ﷺ kuwa, "Nimekaa sehemu hii (nikifanya dhikiri) toka uliponiacha."

Mtume ﷺ kusikia vile, akamwambia Juwayriyah kuwa: *"Mimi nimetamka maneno manne mara tatu toka nilipokuacha, na kama ibada (dhikri) zako zote ulizozifanya toka asubuhi zitapimwa katika mizani na kulinganishwa uzito na maneno yangu haya (manne), basi maneno yangu yatakuwa mazito kuliko dhikri zako zote ulizozifanya toka asubuhi, Maneno haya ni: "Ametakasika Allaah na Sifa njema zote ni Zake, kwa hisabu ya viumbe Vyake, na radhi Yake, na uzito wa arshi Yake, na wino wa maneno Yake."*

Pamoja na ucha-Mungu wake na kujituma katika kufanya ibada, alikuwa na uwezo mkubwa sana wa kuhifadhi na kutunza kumbukumbu. Mama huyu alihifadhi hadithi nyingi za Mtume ﷺ.

Miongoni mwa hadithi zilizopokelewa na mama huyu ni ile iliyosimuliwa na Abu Ayyuub Al-Ataqi, aliyepokea kutoka kwa Juwayriyah ambaye anasimulia kuwa: "Mtume ﷺ alikwenda nyumbani kwake (Juwayriyah) siku ya Ijumaa na kumkuta akiwa amefunga Swaumu (ya Sunnah). Mtume ﷺ akamuuliza Juwayriyah: *"Je, ulifunga jana (Alhamisi)?"*

Juwayriyyah رضي الله عنها akajibu, "Hapana." Mtume ﷺ akamuuliza: *"Je, unatarajia kufunga kesho (siku inayofuata)?"*

Juwayriyyah رضي الله عنها akajibu, "Hapana." Mtume ﷺ akamwambia: *"Basi vunja swaumu yako."*

Zipo hadithi nyingine nyingi ambazo zilipokelewa na mama huyu na zinatumika katika kutoa hukumu juu ya maswala mbalimbali ya Kiislamu.

Hata katika suala la kujamiiana (kufanya tendo la ndoa) kisha kumwaga mbegu za uzazi nje, jambo ambalo limekuwa na mjadala mkubwa juu ya uhalali au uharamu wake na wanazuoni wengi kutofautiana juu ya jambo hili (wengine wakilikubali na wengine wakilipinga); jambo hili lilifafanuliwa na Mtume ﷺ baada ya vita dhidi ya Banu Mustaliq, vita ambavyo matokeo yake yalimuinua mama huyu, Juwayriyah رضي الله عنها.

Bukhaari na Muslim wameandika hadithi iliyopokelewa na Abu Sa'eed al-Khudri ambaye anasema, "Tulitoka na Mtume ﷺ kwenda katika vita dhidi ya Banu Mustaliq na tulipata mateka miongoni mwa waarabu. Kukaa bila wake likawa jambo gumu kwetu, na tukatamani kufanya tendo la ndoa na kumwaga mbegu nje. Tulipotaka kufanya tendo la ndoa na kumwaga mbegu nje, tukasemezana sisi kwa sisi, 'Tunawezaje kumwaga mbegu nje bila kumuuliza Mtume ﷺ wakati tuko naye (ili kujua hukumu yake)?' Tulimuuliza Mtume ﷺ juu ya hili, naye akatujibu kuwa: *"Ni bora msifanye hivyo, kwa sababu ikiwa kuna nafsi ambayo Allah Ametaka iwepo (iishi), basi itakuwepo."*

Kauli ya Mtume ﷺ kuwa: *"Ikiwa kuna nafsi ambayo Allah Ametaka iwepo (iishi), basi itakuwepo."*

Ina maana kuwa: Mkimwaga mbegu za uzazi nje au msimwage nje, yote ni sawa. Kwani baadhi ya mbegu za uzazi zinaweza kuingia kwa mwanamke kabla kutoa na kumwaga nje na mimba uliyokuwa ukijaribu kuikwepa bado inaweza kutokea. Na kwa kuwa tukio hili lilitokea wakati wa vita dhidi ya Banu Mustaliq, basi ni hukumu iliyo sahihi.

Baba wa Juwayriyah رضي الله عنها, Al-Haith ibn Abi Diraar alikuwa akifahamu nyendo za mwanae, toka kuwa chini ya miliki ya Thaabit ibn Qays kama mateka, mpaka kuwa mke wa Mtume Muhammad ﷺ. Al-Haarith ibn Abi Diraar aliamua kwenda Madinah kumkomboa mwanae akiwa na ngamia mia moja (100), akiwa na matumaini kuwa, Mtume ﷺ atakubali kupokea ngamia hawa mia moja kama fidia.

Alipofika jirani na mji wa Madinah, aliwaangalia ngamia wake na namna walivyokuwa wakimvutia. Aliamua kuchagua ngamia wawili waliokuwa wakimvutia zaidi na kuwaweka pembeni wasiwe miongoni mwa ngamia atakaowatoa kwa Mtume ﷺ ili kumkomboa binti yake. Aliwachagua ngamia wale waliokuwa wazuri zaidi na kuwafunga vizuri na kumkabidhi mtu abaki akiwalinda.

Kisha aliondoka na ngamia waliosalia na kwenda nao mbele ya Mtume ﷺ. Wakati huo Mtume ﷺ alikuwa amekaa ndani ya msikiti. Alimsalimia na kumuomba apokee ngamia wale kama kikomboleo na kumkabidhi binti yake, Juwayriyah. Mtume ﷺ alimkaribisha na kumuuliza huku akitabasamu, “Vipi kuhusu ngamia wale wawili uliowabagua na kuwaweka pembeni, ukawafunga kamba na kuwaacha mahala fulani?” Ghafla baba wa Juwayriyah, Al-Harith ibn Abi Diraar akakosa la kusema na alionekana wazi kupigwa na butwaa. Ulimi wake ulishindwa kudanganya. Al-Haarith ibn Abi Diraar akasema: “Nakiri kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa Haki isipokuwa Allah, na wewe Muhammad ni Mtume wa Allah! Naapa kwa Jina la Allah kuwa, hakuna yeyote aliyefahamu jambo hili isipokuwa Allah Peke Yake.” Baada ya Al-Haarith ibn Abi Diraar kuingia katika Uislamu, watu wote kutoka kabila la Banu Mustalaq wakasilimu na kuukubali Uislamu baada ya Al-Haarith ibn Abi Diraar kuwasimulia kile kilichotokea na kuwalingania na kuwataka waukubali Uislamu. Bila shaka hii ni neema ya wazi Aliyoishusha Allah kwa Juwayriyah na watu wa kabila lake kupitia kwa Mtume ﷺ.

Juwayriyah رضي الله عنها aliishi miaka hamsini (50) toka baada ya kufanyika Hijrah. Imeelezwa na wana historia kuwa, mama huyu Juwayriyah رضي الله عنها alikuwa na umri wa miaka sitini na tano (65) alipofariki dunia. Aliyekuwa Gavana wa mji wa Madinah wakati huo, Marwaan ibn al-Hakam, ndiye aliyeongoza Swala ya jeneza na alizikwa katika viwanja vya Jannatul - Baqi.'

Mwenyezi Mungu Amuwie radhi mama yetu!

Na yeye awe radhi na aliyoandaliwa na Mola wake!

Mwenyezi Mungu Ampe makazi mema Peponi. Amin!

# Safiyyah binti Huyay ibn Akhtab

## Hakika Amesema Kweli

Jina kamili la mama huyu ni: Safia Bint Huyay bin Akhtab bin Sa'yah bin Amr bin Ubayd ibn Ka'b bin Al-Khazraj bin Habib bin Nadir bin al-Kham bin Yakhurn bin Imran. Mama yake alikuwa anaitwa Barrah bint Samaual Darin Bani Quraidhah. Mama huyu Safia رضي الله عنها takriban alizaliwa miaka miwili tu baada ya Mtume ﷺ kupewa Utume au miaka kumi na moja kabla ya Hijirah.

Toka akiwa mdogo, Safiyyah رضي الله عنها alikuwa anapenda sana kusoma na kujifunza historia. Ni kupitia katika kusoma kwake, alikuja kufahamu kutabiriwa kwa Mtume wa mwisho atakayetokea katika bara Arabu. Kwa sababu jambo hili lilikuwa limebashiriwa na kuandikwa katika vitabu vilivyotangulia. Hata hivyo alishangazwa na namna watu walivyokuwa wakikanusha Utume wa Muhammad ﷺ baada ya kutokea akiambatana na dalili zilizokuwa wazi. Zaidi ya yote hayo, Safiyyah alistaajabishwa na mambo makubwa mawili: kwanza alistaajabishwa na chuki iliyopitiliza ya baba yake juu ya Mtume ﷺ na Waislamu bila kujali dalili za hoja zilizokuwa wazi katika vitabu vilivyotangulia. Jambo la pili lililomstaajabisha ni tabia ya uongo na unafiki aliyokuwa nayo baba yake kwa watu wake. Mfano mzuri ni pale alipowaahidi wayahudi wenzie kuwa atawaunga mkono na kuwasaidia ikiwa watavunja makubaliano yao na Mtume ﷺ, makubaliano ya Hudaybiyya. Hata hivyo, baada ya wenzake kuvunja mkataba, aliwatupa mkono na hakujali yale waliyokuwa wamekubaliana.

Safiyyah bint Huyay رضي الله عنها aliolewa mara mbili kabla ya kuolewa na Mtume ﷺ. Mara ya kwanza aliolewa na Salam bin Musykam, ambaye alikuwa ni mmoja katika viongozi wa Banu Quraydhah. Lakini ndoa yao haikudumu kwa muda mrefu. Mara ya pili aliolewa na Kinanah ibn Rabi' ibn Abil Hafiq, ambaye pia alikuwa ni kiongozi wa Banu Quraydhah kabla ya Mtume ﷺ hawajaikomboa Khaibar.

Namna gani mama huyu, Safiyyah bint Huyay رضي الله عنها alikuja kuwa mmoja kati ya wake wa Mtume ﷺ na hivyo kuwa mama wa Waumini, ni jambo linalotoa somo muhimu katika ulimwengu wa Da'wah katika Uislamu. Basi msomaji, fuatilia kisa hiki kizuri na ufaidi na kujifunza pamoja nasi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Baba wa mama huyu, Huyay ibn Akhtab alikuwa mmoja kati ya viongozi wa mayahudi na alikuwa adui mkubwa wa Uislamu na Waislamu katika zama zake. Bwana huyu alikuwa mtu wa fitina na mtu hatari sana kwa Waislamu kwa sababu yeye alikuwa ni kiongozi wa moja kati ya makabila matatu makubwa ya wayahudi yaliyokuwa yakiishi katika mji wa Madinah. Yeye alikuwa ni kiongozi wa kabila la Banu Nadhir; makabila mengine ya wayahudi waliokuwa wakiishi Madinah wakati huo ni Banu Qaynuqaa' na Banu Quraydhah. Ni muhimu sana kuweka sawa toka mwanzo kuwa, tunaposema 'kabila', kuna tofauti sana kati ya makabila ya kwetu na makabila haya ya Wayahudi. Makabila ya Wayahudi yalikuwa mfano wa taifa kwa namna walivyojipanga kiutawala, kisiasa, kijeshi, kimkakati na silaha!

Mtume ﷺ alipohamia Madinah, alianza kuijenga jamii mpya ya Ummah wa Kiislamu. Katika kutekeleza jambo hili, ilimlazimu kuingia makubaliano na kufanya mikataba kadhaa na baadhi ya koo za kiyahudi; lakini haikuchukua muda mrefu wayahudi walivunja makubaliano waliyowekeana. Banu Qaynuqaa' walikuwa wa kwanza kuvunja makubaliano wakifuatiwa na mayahudi kutoka kabila la Banu Nadhir.

Siku moja Mtume ﷺ aliongozana na kundi dogo la maswahaba kwenda kwa Mayahudi wa Banu Nadhir akiwa na lengo la kutaka kulipa fidia ya watu wawili ambao waliuwawa kwa bahati mbaya kama Sharia ya Kiislamu inavyoelekeza. Na Mtume ﷺ alifanya hivi kwa sababu kulikuwa na makubaliano kati yao na yeye Mtume. Walimkaribisha kwa heshima kubwa na hata kufikia kusimama kuonesha nidhamu na utii kwake. Lakini kwa siri, kiongozi wao Huyay ibn Akhtab akawashauri kuwa huu ulikuwa muda muafaka na fursa nzuri ya kumuuwa Mtume wa Allah ﷺ na kumaliza harakati za kusimamisha Uislamu. Aliingiwa na mawazo haya ya kishetani baada ya kuona Mtume ﷺ ameongozana na idadi ndogo ya maswahaba. Wengi katika mayahudi wale wakakubaliana na mawazo na mapendekezo yake. Hii ndio kawaida ya makafiri wote katika zama zote, si watu wa kuwaamini moja kwa moja mnapokubaliana

au wanaposema jambo. Wasemacho kwa midomo yao si kilicho ndani ya vifua vyao.

Hii ndio mila na kanuni ya makafiri wote duniani mpaka leo, japo baadhi ya Waislamu huwaamini na kujifanya wanajenga urafiki nao. Lakini huyu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu; Malaika Jibril akaja kwa Mtume ﷺ na kumfahamisha mipango waliyokuwa wanaandaa mayahudi dhidi yake. Mtume ﷺ akasimama haraka na kuondoka. Kama adhabu, Mtume ﷺ aliwaamuru wayahudi wa Banu Nadhir wahame katika mji wa Madinah tena akawapa muda maalumu na kuwataka wawe wameondoka ifikapo muda huo. Lakini mayahudi hawa wakakataa na badala yake wakajifungia ndani ya ngome zao. Kiongozi mkuu wa wanafiki 'Abdullah ibn Ubayy ibn Saluul, akawaunga mkono na kuwaahidi kuwa atawasaidia kupambana dhidi ya Mtume ﷺ.

Muda waliopewa kuhakikisha wamehama ulipomalizika, jeshi la maswahaba likawazingira, na kiongozi wa wanafiki ibn Saluul hakuwaunga mkono kama alivyowaahidi. Kwa sababu ya mpango wao wa kutaka kumuua Mtume ﷺ, Mtume ﷺ akawalazimisha waondoke katika mji wa Madinah. Mwenyezi Mungu Anasema katika Qur'aan:

هُوَ ٱلَّذِىٓ أَخْرَجَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ مِنْ أَهْلِ ٱلْكِتَٰبِ مِن دِيَٰرِهِمْ لِأَوَّلِ ٱلْحَشْرِ ۚ مَا ظَنَنتُمْ أَن
يَخْرُجُوا۟ ۖ وَظَنُّوٓا۟ أَنَّهُم مَّانِعَتُهُمْ حُصُونُهُم مِّنَ ٱللَّهِ فَأَتَىٰهُمُ ٱللَّهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوا۟ ۖ
وَقَذَفَ فِى قُلُوبِهِمُ ٱلرُّعْبَ ۚ يُخْرِبُونَ بُيُوتَهُم بِأَيْدِيهِمْ وَأَيْدِى ٱلْمُؤْمِنِينَ فَٱعْتَبِرُوا۟ يَٰٓأُو۟لِى
ٱلْأَبْصَٰرِ ﴿٢﴾ وَلَوْلَآ أَن كَتَبَ ٱللَّهُ عَلَيْهِمُ ٱلْجَلَآءَ لَعَذَّبَهُمْ فِى ٱلدُّنْيَا ۖ وَلَهُمْ فِى ٱلْءَاخِرَةِ عَذَابُ
ٱلنَّارِ ﴿٣﴾

***"Yeye ndiye Aliyewatoa waliokufuru miongoni mwa watu wa kitabu (Mayahudi wa Bani Nadhir) katika nyumba zao (huko Madinah); wakati wa uhamisho (wao) wa kwanza. Hamkudhani kuwa watatoka, (kwa nguvu walizokuwa nazo Madinah), nao walidhani ya kuwa ngome zao zitawalinda na (kufikwa na amri ya) Mwenyezi Mungu; lakini Mwenyezi Mungu Aliwajia kwa mahali wasipopatazamia, na Akatia woga katika nyoyo zao; (wasiweze kupigana na Waislamu waliokuja kupigana nao).***

***Wakawa wanazivunja nyumba zao kwa mikono yao na kwa mikono ya Waislamu; basi enyi wenye macho (maoni)! Zingatieni. Na lau kama Mwenyezi Mungu Asingaliwaandikia uhamisho Angaliwaadhibu hapa duniani (adhabu kubwa zaidi kuliko hii); na katika Akhera watapata adhabu ya Moto."*** **(59:1-3)**

Hivyo waliondoka katika mji wakiwa wanyonge na waliodhalilika kwa njama zao za kutaka kumuua Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Ni baada ya hatua hii, kiongozi wao Huyay ibn Akhtab alianza kuzunguuka huku na kule kueneza propaganda na kuhamasisha makafiri kuunganisha nguvu ili kukabiliana na Waislamu. Alikuwa akipandikiza chuki na kuwasha morali ndani ya nyoyo za makafiri ili wamchukie Mtume ﷺ, maswahaba na dini yenyewe ya Kiislamu. Katika kuhakikisha anapata uungwaji mkono wa kutosha na hivyo kuwa na nguvu aliyoamini inaweza kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu, bwana huyu alikuwa akizunguuka katika miji ya Khaybar, Makkah na Madinah. Ni jitihada hizi za Huyay zilizopelekea kutokea kwa vita vya Al-Ahzab ambavyo pia vinafahamika kama vita vya Handaq. Vita hivi vilifuatiwa na vita vya Waislamu dhidi ya mayahudi wa Banu Quraydhah, ambao kwa wakati huo walikuwa bado wanaishi Madinah. Na hii ni kwa sababu wao waliungana na makafiri katika vita vya Al-Ahzab bila kujali kuwa walikuwa na makubaliano baina yao na Mtume ﷺ, makubaliano ambayo hayakuwaruhusu kushirikiana na maadui wa Waislamu.

Ni muhimu kukumbuka kuwa, Huyay ibn Akhtab alikuwa kiongozi wa kabila la Banu Nadhir, hata hivyo ilitokea kwamba, wakati Waislamu wakiwa na vita na mayahudi wa kabila la Banu Quraydhah, bwana huyu naye alikuwa kwao. Bwana huyu, Huyay ibn Akhtab akajikuta amechukuliwa mateka pamoja na mateka wengine kutoka kabila la Banu Quraydhah. Mayahudi kwa hiari yao, wakaomba swahaba wa Mtume, Sa'd ibn Mu'adh رضي الله عنهatoe hukumu juu yao. Walimchagua Sa'd ibn Mu'adh رضي الله عنه kwa sababu waliwahi kuwa na ushirikiano nae na alikuwa jamaa yao hapo kabla. Hivyo waliamini kuwa Sa'd ibn Mu'adh رضي الله عنه atatoa hukumu yenye nafuu kwao. Hata hivyo mambo yalikuwa kinyume na walivyotarajia, kwani Sa'd ibn Mu'adh رضي الله عنه aliamuru wote wauwawe. Ni baada ya Sa'd ibn Mu'adhرضي الله عنه kutoa hukumu hii, Mtume ﷺ akamwambia Sa'd ibn Mu'adh: *"Hakika umewahukumu kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu kutoka mbingu ya saba".*

Baadaye Khaybar ikakombolewa na Waislamu. Baada ya mapambano makali na magumu, hatimaye Waislamu wakapata ushindi na kuikomboa Khaybar. Ni katika vita hivi, Safiyyah bint Huyay alichukuliwa mateka na Waislamu, na katika kugawana mateka, mama huyu akawa sehemu ya mgao wa Dihyah ibn Khaleefah al-Kalbi. Mama huyu, Safiyyah bint Huyay alikuwa mwanamke mwenye heshima, mzuri na zaidi ya yote alikuwa mtoto wa kiongozi wa kabila la Banu Nadhir na kwa wakati huo, alikuwa ni mke wa kiongozi (chifu) wa Khaybar aliyeitwa Kinanah ibn Abi al-Huqayq.

Anas رضي الله عنه anasema, "Kabla Mtume ﷺ hajamuoa Safiyyah bint Huyay, alimuuliza, 'Unafahamu nini kuhusu mimi?' Safiyyah akajibu, 'Ewe Mtume wa Allah, nilikuwa nikitarajia (kuja kwako) toka zama za ujahili (ukafiri), na nilikuwa nikitamani kuwa siku moja Mwenyezi Mungu Akipenda niingie katika Uislamu." Haya ndiyo yalikuwa majibu ya Safiyyah bint Huyay. Tukio la Safiyyah kupigwa na mume wake wakati wa ukafiri kwa kumsimulia kuwa ameota jua likishuka kifuani kwake kama tutakavyoona huko mbele ni moja katika ishara kuwa Mama Safiyyah alikuwa na imani na kwa hakika alitabiriwa kuja kuwa mmoja katika wake za Mtume ﷺ.

Mtume ﷺ alimpa Safiyyah bint Huyay ruhusa ya kuchagua; achague kati ya kuingia katika Uislamu na kuolewa na Mtume ﷺ au abakie katika dini yake na kuachwa huru na asiendelee kuwa mateka. Safiyyah akachagua kusilimu na kuolewa na Mtume ﷺ kwa hiari yake mwenyewe. Hivi ndivyo mama huyu alivyopata bahati ya kuingia katika orodha ya mama wa Waumini.

Akiwa mke wa Mtume ﷺ, mama huyu alikuwa na mchango mkubwa katika maisha ya Mtume ﷺ na hivyo kutoa mchango wake mkubwa katika kuwalingania watu kuukubali Uislamu. Baadhi ya mambo ambayo Waislamu wanaweza kujifunza kutoka katika historia ya mama huyu ni haya:

Mtume ﷺ alipoyaangalia macho ya Safiyyah رضي الله عنها, aliona rangi isiyokuwa ya kawaida jichoni (kama jicho lililovia damu). Mtume ﷺ akamuuliza, hali ile ilitokana na nini? Mama Safiyyah akajibu: "Nilipokuwa mke wa Kinanah ibn Abi al-Huqayq, siku moja niliota jua likishuka kifuani kwangu. Nilimsimulia ndoto ile mume wangu; baada ya kumsimulia alihamaki na kunipiga kofi kwa nguvu usoni huku akisema, 'Unataka kuwa mke wa Mfalme wa Waarabu?'" Hili linatukumbusha tukio muhimu sana lililosimuliwa katika Qur'an, tukio linalohusu ndoto ya Nabii Yusufu:

إِذْ قَالَ يُوسُفُ لِأَبِيهِ يَٰٓأَبَتِ إِنِّى رَأَيْتُ أَحَدَ عَشَرَ كَوْكَبًا وَٱلشَّمْسَ وَٱلْقَمَرَ رَأَيْتُهُمْ لِى سَٰجِدِينَ ﴿٤﴾

***"Kumbuka Yusufu alipomwambia baba yake: "Ewe baba yangu! Hakika mimi nimeona (katika ndoto) nyota kumi na moja na jua na mwezi. Nimeviona (vyote hivi) vikinisujudia".***

Hii ni dalili kuwa, mayahudi walikuwa na kawaida ya kuzungumza na kujadiliana katika kukutana kwao kuhusu kuja kwa Mtume Muhammad ﷺ, na hivyo wengi katika wao walikuwa wanafahamu kuja kwake na walikuwa wanajua ukweli juu ya dini ya Uislamu aliyokuja nayo. Simulizi juu ya kusilimu kwa kiongozi wa mayahudi (Rabbi), Abdullah ibn Salaam ni ushahidi tosha juu ya hili pia. Kushuka kwa jua juu ya kifua cha mama huyu, Safiyyah رضي الله عنها ni dalili ya imani yake kwa Mtume ﷺ. Inaonesha wazi kuwa mama huyu alikuwa akimuamini Allah na Mtume wake ﷺ. Hakulazimishwa kuolewa na Mtume ﷺ kama inavyoweza kufikiriwa au kudhaniwa na watu wasiokuwa na elimu au wajinga. Bila shaka maisha aliyoishi mama huyu wakati Mtume ﷺ akiwa hai na hata baada ya kufariki Mtume ﷺ yanatosha kuthibitisha mapenzi yake kwa Allah na Mtume wake ﷺ.

Mtume ﷺ hakuondoka Khaybar mpaka mama Safiyyah alipomaliza siku zake. Alimpandisha katika kipando chake na wakaondoka. Walipofika katika eneo fulani, Mtume ﷺ alimtaka mke wake wapumzike kwa muda hapo. Hata hivyo mama huyo hakuridhia na hili halikumfurahisha Mtume ﷺ kwa sababu toka mwanzo hakulazimishwa. Walipofika katika eneo liitwalo Saliba', Ummu Sulaym (mmoja kati ya wake wa Mtume) alimtana nywele na kumpulizia manukato. Ummu Sinan al-Aslamiyah anasema: "Safiyyah alikuwa mwanamke mpole sana; Baada ya Mtume ﷺ kupumzika na mke wake, asubuhi nilimuuliza Safiyyah, Mtume ﷺ amekwambia nini?' Naye akajibu kuwa, 'Aliniuliza kitu gani kilinifanya nikatae kupumzika kwa mara ya kwanza? Nami nikamjibu kuwa, 'mayahudi walikuwa karibu na sehemu ile hivyo nilichelea (nilihofia) wasikudhuru.'" Jibu hili liliongeza mapenzi ya Mtume ﷺ kwa mama huyu.

Huyu ndiye mama Safiyyah, mama ambaye baba yake aliuwawa miongoni mwa mateka baada ya vita dhidi ya mayahudi wa Banu Quraydhah. Mama ambaye mume wake Kinaanah ibn Abi al- Huqayq aliuwawa na

Waislamu katika harakati za kuikomboa Khaybar na ambaye aliwashuhudia watu wake wakiuwawa. Pamoja na hayo yote, bado mama huyu alikuwa anachelea (anaogopa) Mtume ﷺ asidhuriwe na hivyo kuchukua hatua kuhakikisha Mtume ﷺ anakua salama. Hakuna chochote kilichomfanya awe katika hali hii zaidi ya Imani. Baada ya kufika Madinah na kuingia katika familia ya Mtume ﷺ kama mama wa Waumini. Baadhi ya wake wa Mtume ﷺ waliingiwa na wivu, jambo ambalo huwatokea wanawake wengi.

Ibn Sa'd anasimulia kutoka kwa 'Ata ibn Yasar kwamba: "Mara Safiyyah alipowasili Madinah akitokea Khaybar, alifikia katika nyumba iliyokuwa ikimilikiwa na Haarithah ibn an-Nu'man. Wanawake wa ki-Ansaar wakapata taarifa na wakaja kumuona na kumjulia hali mke wa Mtume ﷺ. Mama Aishah pia alikuja akiwa amefunika uso (amevaa *niqab*). Baada ya kuwa ameondoka, Mtume ﷺ alimuuliza mama Aishah, 'umeona nini?' mama Aishah akajibu, 'Nimemuona mwanamke wa kiyahudi!!' Mtume ﷺ akamwambia Aishah, 'Usiseme hivyo. Kwa hakika yeye amesilimu na anautekeleza Uislamu kikamilifu.'" Sio mama Aishah peke yake aliyejisikia vibaya, wanawake wengine wa Mtume ﷺ walijisikia wivu kutokana na mama huyu. Ibn Sa'd anasimulia kutoka kwa mama Aishah kuwa:

"Mtume ﷺ alikuwa safarini, na ngamia wa mama Safiyyah akawa mgonjwa. Zaynab bint Jahsh alikuwa na ngamia wa ziada, hivyo Mtume ﷺ akamuombea mama Safiyyah ngamia kwa mama Zainab bint Jahsh akisema, 'Ngamia wa Safiyyah ni mgonjwa, unaweza kumuazima ngamia wako tafadhali?' Zaynab akajibu, 'Nimpe ngamia wangu yule mwanamke myahudi?'"

Kimsingi yalikuwepo mengine yaliyokuwa yakisemwa na wake za Mtume ﷺ kuhusu mama huyu.

Msaidizi wake Kinaanah anasimulia kuwa, Safiyyah alimsimulia kuwa: "Mtume ﷺ aliingia nyumbani kwake baada ya kuwa yeye (Safiyyah) zimemfikia habari kuwa Aishah na Hafsah huwa wanasema wao ni wa karibu zaidi na Mtume ﷺ kuliko yeye (Safiyyah) na kwamba wao walikuwa ni wake zake lakini pia walikuwa ndugu zake." Alipomwambia maneno haya Mtume ﷺ, Mtume ﷺ akamwambia (Safiyyah), 'Ungewaambia kuwa, 'Vipi mnaweza kuwa bora kuliko mimi wakati mume wangu ni Muhammad, baba yangu ni Harun na mjomba wangu ni (Nabii) Mussa?"

Moja katika sifa kubwa alizokuwa nazo mama huyu ni busara na hekima ya hali ya juu. Siku moja mjakazi wake alitunga maneno na kwenda kumshitaki kwa 'Umar ibn Khattab akidai kuwa, Safiyyah anaipenda Jumamosi na huwaonea huruma sana wayahudi. 'Umar alipomwita na kumuuliza juu ya jambo hili, mama huyu alijibu kuwa:

"Ama kuhusu Jumamosi, mimi siithamini tena kwa sababu Allah amenipa m-badala na kunichagulia siku ya Ijumaa; Na kuhusu wayahudi, bado kati yao ninao ndugu zangu miongoni mwao, hivyo napaswa kuwatendea wema." Mama Safiyyah رضي الله عنها alifahamu vema kuwa mjakazi wake ndiye aliyepeleka maneno yale. Alipomuuliza:

"Kwanini umefanya hivyo?"

Mjakazi wake akajibu, "Ni shetani (alinihadaa)".

Kisha Safiyyah رضي الله عنها akamwambia, "Nenda uko huru."

Bila shaka Safiyyah رضي الله عنها alimuacha huru mjakazi wake kwa sababu alisema kweli kuwa ni shetani ndiye aliyemuhadaa. Safiyyah رضي الله عنها alikuwa mama muelewa na mwenye busara kiasi hiki.

"Hakika yeye ni mkweli" haya ni maneno ya Mtume ﷺ juu ya mama yetu, Safiyyah bint Huyay رضي الله عنها. Huu ni ushahidi kutoka katika kinywa cha mtu ambaye sio tu kwamba hasemi uongo, bali hasemi kwa kutamani kwake kusema.

Ibn Sa'd anasimulia kwa mapokezi sahihi kutoka kwa Zayd ibn Aslam رضي الله عنه ambaye anasema kuwa: "Wake za Mtume ﷺ walikusanyika na kumzunguuka wakati Mtume ﷺ akiwa mgonjwa, ugonjwa ambao ulikuwa ndio sababu ya kifo chake. Safiyyah رضي الله عنها akasema: "Ewe Mtume wa Allah! Natamani ningekuwa nakabiliana na maradhi yanayokukabili mimi (natamani ningekuwa naumwa mimi kwa niaba yako)!"

Kusikia vile, wake za Mtume ﷺ wakaanza kunong'onezana. Mtume ﷺ akawaamuru akisema: *"Nendeni mkasafishe vinywa vyenu".*

Wakamuuliza Mtume ﷺ, "Kwanini tukafanye hivyo? (kwanini tukasafishe vinywa vyetu?!)" Mtume ﷺ akawaambia: *"Kwa sababu mmenong'onezana ili kumdhihaki. Naapa kwa jina la Allah! Hakika amesema kweli."*

Hata baada ya kufariki Mtume ﷺ, Safiyyah رضي الله عنها aliishi kama mama wa Waumini akiwa mwenye heshima na mcha-Mungu. Na alibakia hivyo katika umri wake wote. Mama huyu, Safiyyah bint Huyay رضي الله عنها alifariki katika mwaka wa 52 baada ya Hijirah. Na ilikuwa wakati wa uongozi wa Mu'aawiyah ibn Abi Sufiyan, na alifariki akiwa amehifadhi hadithi nyingi za Mtume ﷺ.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu amuwie radhi mama yetu, mama wa waumini – Safiyyah bint Huyay. Amin!

# Maimunah bintil - Haarith

## Mcha-Mungu; na dada wa Wacha-Mungu

Jina kamili la mama huyu ni Maimunah bint Al-Harith ibn Hazan ibn Bujair, ibn al-Hazm, ibn Rubwaiba ibn Abdullah, ibn Hilal, ibn Amer, ibn Sa'sa'a Al-Hilaliyya.

Mama yake mzazi alikuwa anaitwa Hind bint Awf ibn Zuhair ibn Al-Harith ibn Hamata ibn Humair. Dada wa mama huyu ni Lubaba mkubwa (Ummu Al-fadhl), na Lubaba mdogo. Mama huyu pia alikuwa na udugu na Asmaa bint Umays na Salma bint Umays Dada wa Maimunah, Ummu Al-Fadhl, alikuwa mke wa Al-Abbas رضي الله عنه (mjomba wa Mtume ﷺ. Ndugu yake, Asmaa bint Umays aliolewa na Jafaar ibn Abu Talib - binamu wa Mtume ﷺ ambaye ni moja katika mashahidi maarufu. Ndugu yake mwingine, Salma bint Umays alikuwa mke wa Simba wa Allah, Hamzah ibn Abdul Mutallib - Mjomba wa Mtume ﷺ na kiongozi wa waliouwawa mashahidi. Maimunah alikuwa anatoka katika familia tukufu miongoni mwa familia za Kiquraishi.

Maimunah ambaye baadaye alifahamika pia kwa jina la Barra, alitamani kuolewa na Mtume ﷺ. Alitoka na kwenda kwa dada yake, Ummu al Fadhl ili kuzungumza naye juu ya jambo hili, na yeye (Ummu al Fadhl) akazungumza jambo hili na mume wake, Al-Abbas. Baada ya kuambiwa habari ile, mara moja Al-Abbas akaenda kwa Mtume ﷺ, na kumfahamisha ombi la Maimunah, na ombi lake kwa Mtume ﷺ likakubaliwa.

Wakati taarifa zile zinamfikia Maimunah, kuwa Mtume ﷺ amekubali ombi lake, Maimunah alikuwa juu ya ngamia. Mara moja alishuka chini na kusema, "Ngamia na kila kilichobebwa na ngamia ni kwa ajili ya Mtume wa Allah ﷺ."

Mtume ﷺ na bi Maimunah walifunga ndoa katika mwezi wa Shawwal, katika mwaka wa saba (7) baada ya Hijirah; muda mfupi baada ya Waislamu

wa Madinah kuruhusiwa kufanya Umrah katika msikiti Mtukufu wa Makkah chini ya makubaliano ya mkataba wa Hudaybiyya. Mwenyezi Mungu akashusha Ayah hii kuzungumzia ndoa hii:

وَٱمۡرَأَةٗ مُّؤۡمِنَةً إِن وَهَبَتۡ نَفۡسَهَا لِلنَّبِيِّ إِنۡ أَرَادَ ٱلنَّبِيُّ أَن يَسۡتَنكِحَهَا خَالِصَةٗ لَّكَ مِن دُونِ ٱلۡمُؤۡمِنِينَۗ

***".....mwanamke Muislamu akijitoa mwenyewe bure kwa Mtume, kama mwenyewe Mtume akitaka kumuoa. Ni halali kwako tu (kumuoa mwanamke bure bila ya mahari) si kwa Waislamu wengine...."* (33 : 50)**

Baada ya Mtume ﷺ kukaa siku tatu Makkah kama walivyokubaliana katika mkataba wa Hudaybiya, Makafiri wa Makkah wakamtaka aondoke. Mtume ﷺ akawaomba wamruhusu afunge ndoa akiwa pamoja na ndugu zake Maquraishi na kwamba angewaalika katika sherehe ya ndoa yake, lakini wakakataa kata kata. Kimsingi makafiri wa Kiquraish walikuwa wanakataa Mtume kuendelea kukaa nao kwa sababu walijua athari inayoweza kutokea na kuathiri nyoyo za watu, hivyo walimtaka aondoke haraka iwezekanavyo. Ndoa ilifungwa sehemu iliyojulikana kwa jina la Sarf, kiasi cha maili kumi kutoka Makkah, katika mwezi wa Shawwal ndani ya mwaka wa saba baada ya Hijrah.

Mtume ﷺ akampa jina la Maimunah, likiwa na maana ya "Aliyebarikiwa", kwa sababu walifunga ndoa baada ya tukio lenye baraka, tukio la kufanya Umrah Makkah wakitokea Madinah, baada ya kukaa huko bila kufika Makkah kwa muda wa miaka saba. Maimunah aliishi na Mtume ﷺ kwa muda wa miaka mitatu tu, baada ya hapo Mtume ﷺ alifariki dunia. Alikuwa mama aliyelelewa vema na mwenye tabia njema. Alikuwa akielewana na kila mtu na hakuna taarifa yeyote inayoonesha kwamba aliwahi kuwa na mgogoro na mke yeyote wa Mtume ﷺ – kwa maana ya mke mwenzake. Mama Aisha, mama wa waumini رضي الله عنها anasema kuhusu mama huyu (mke mwezie), "Yeye (Maimunah) alikuwa mwanamke mwenye kumuhofu zaidi Mwenyezi Mungu kuliko sisi sote wake wa Mtume na alikuwa akifanya kila linalowezekana kudumisha mahusiano mema na udugu. Ni kutokana na sifa zake njema, Mtume ﷺ anathibitisha kwa kusema, "Maimunah na dada zake, Ummu al-fadhl, Salma na Asmaa ni wanawake wacha-Mungu."

Mtume ﷺ alianza kuhisi maradhi yaliyopelekea kifo chake akiwa ndani ya chumba cha mama huyu, Maimunah رضي الله عنها. Kisha akaomba ridhaa ya wake zake ili ahamie katika chumba cha mama Aishah رضي الله عنها. Mama huyu alikuwa mwenye elimu kubwa na alikuwa akiwafundisha watu elimu ya dini na Sunnah. Mfano, mpwa wake, ibn Abbas رضي الله عنه (ambaye alikuwa mmoja kati ya watu wenye elimu kubwa sana ya dini) alikwenda nyumbani kwa Maimunah رضي الله عنها kumtembelea akiwa hakutana nywele, Maimunah رضي الله عنها akamuuliza kwanini alikuwa hakutana nywele? Ibn Abbas رضي الله عنه akajibu kuwa mke wake alikuwa katika siku zake. Maimunah رضي الله عنها akamwambia kuwa: Mtume ﷺ alikuwa akiingia katika nyumba ya mke wake aliyekuwa katika siku zake, akilala juu yake au akikaa juu ya mapaja yake na akisoma Qur'an. Hii ikiwa na maana kuwa, mke kuwa katika siku zake si sababu ya kisheria kumfanya awe vile.

Wakati fulani alifahamu kuwa, mpwa wake alikuwa halali kitanda kimoja na mke wake ikiwa mke wake yuko katika siku zake za hedhi; Maimunah akamwambia kuwa, hivi sivyo alivyokuwa akifanya Mtume ﷺ wakati mmoja kati ya wake zake alipokuwa katika siku zake.

Imesimuliwa kuwa, siku moja mmoja katika ndugu zake alimtembelea, na aliweza kutambua kuwa ndugu yake yule alikuwa amelewa. Mama Maimunah رضي الله عنها akamtaka ndugu yake yule akubali kosa kuwa amelewa, na akubali kuchapwa viboko themanini (80), vinginevyo asiende tena kumtembelea Maimunah. Mama huyu wa Waumini amepokea na kusimulia hadithi nyingi za Mtume ﷺ.

Sheikh Ath-Dhahabi anasema, mama huyu amepokea hadithi saba (7) ambazo zimenukuliwa katika vitabu vyote vya Hadith vya Sahihi Bukhari na Muslim. Na kwamba hadithi moja imeripotiwa katika kitabu cha Bukhari pekee, Hadithi tano zimeripotiwa katika kitabu cha Hadithi cha Muslim pekee na hivyo kufanya jumla ya hadithi zilizopokelewa na mama huyu kuwa kumi na tatu (13).

Mama wa Waumini, Maimunah bint Al-Harith رضي الله عنها, alifariki mwaka wa 51 baada ya Hijrah. Ibn Ataa anasema, "Maimunah alipofariki, nilikwenda mimi, nikiongozana na ibn Abbas رضي الله عنه ambaye alipofika alisema, "Msimtikise na muoneeni huruma, yeye ni mama yangu."

Maimunah رضي الله عنها alipofariki, Mama wa Waumini, Aishah bint Abu Bakr رضي الله عنها alisema: “Ewe Maimunah umefariki. Naapa kwa Jina la Allah, hakika (Maimunah) alikuwa mcha-Mungu na mtu aliyedumisha udugu na mahusiano mema. Mwenyezi Mungu Amuonee huruma”. Mama Maimunah رضي الله عنها alizikwa katika eneo la Saraf (eneo ambalo yeye na Mtume ﷺ walifunga ndoa), na hivi ndivyo alikuwa ameusia mama Maimunah رضي الله عنها.

# Zaynab binti Khuzaymah

## Mfano bora wa Subira

Mama huyu, Zaynab bint Khuzaymah رضي الله عنها alikuwa ni ndugu wa Ummu al-Fadhl na mama wa Waumini, Maimunah. Zaynab, Ummu al-Fadhl na Maimunah walikuwa wanachangia mama lakini walikuwa hawatokani na baba mmoja.

Zaynab bint Khuzaymah رضي الله عنها alikuwa miongoni mwa wanawake waliokuwa na bahati, kwani alikuwa miongoni mwa wale waliosilimu na kuingia katika Uislamu wakati wa mwanzo kabisa wa Uislamu. Baada ya hapo, mama huyu aliolewa na 'Abdullah ibn Jahsh رضي الله عنه, na walihama pamoja kuelekea Uhabeshi (Ethiopia) baada ya kushauriwa kufanya hivyo na Mtume ﷺ kutokana na mateso waliyokuwa wanafanyiwa Waislamu pale Makkah.

Zaynab bint Khuzaymah رضي الله عنها alikuwa mama aliyelelewa vema na kufundishwa maadili mazuri na tabia njema. Tabia yake njema ikaja kuzidishwa na mafundisho na nuru ya Uislamu aliyoipokea. Athari ya vitu hivi viwili na kujitolea kwake katika kuupeleka mbele Uislamu vikamfanya awe mwenye kutajwa kwa wema wakati wake na katika zama zote. Wakati wa uhai wake, mama huyu alikuwa mtu mwenye wingi wa huruma, mkarimu na aliyependa kutoa sana sadaka na zawadi mbalimbali na kuwasaidia watu. Ni kutokana na tabia hii ya kuuacha mkono wake wazi kuwasaidia watu wenye shida na kuwatendea wema, mama huyu, Zaynab bint Khuzaymah رضي الله عنها akapata kuitwa "Mama wa mafakiri na masikini". Hakika alikuwa akiishi kwa kufuata maneno na dua ya Mtume ﷺ pale aliposema: "Ewe Allah, nifanye niishi kama mtu masikini, nifanye nife hali ya kuwa ni masikini na unifufue nikiwa ndani ya kundi la watu masikini!" 'Abdullah رضي الله عنه alikuwa binamu yake Mtume ﷺ, jina la mama yake ni Umaamah bint 'Abdul-Muttalib.

Maisha ya Zaynab bint Khuzaymah رضي الله عنها na mume wake 'Abdullah, yalikuwa yamejaa mapenzi, utiifu na kujitolea kwa hali ya juu katika kutimiza wajibu wake kama mke ndani ya nyumba. Hadhi na mwenendo wa mume wake ulimfanya Zaynab bint Khuzaymah رضي الله عنها ampende zaidi mume wake. Mapenzi yao yalizidi kutokana na Allah na Mtume ﷺ. Hii ina maana kuwa, walijikuta wakipendana zaidi kutokana na kila mmoja kufanya jitihada kubwa katika kuutumikia Uislamu huku akitekeleza wajibu wake kama mke au mume katika familia yake. Hakukuwa na kuvutana au kubishana au mtu kuhangaika na kutaka afanyiwe hili au lile, bali kila mmoja alikuwa akiamini anafanya kwaajili ya Allah na Uislamu.

Pamoja na jitihada katika maisha ya kifamilia, katu haikuwapotezea malengo makuu, ambayo ni kuupeleka mbele Uislamu kwa mali zao na nafsi zao. Daima kulikuwa hakuna kulega lega katika kuutumikia Uislamu.

Al-Baghawi anasimulia kutoka kwa Ishaaq ibn Sa'd ibn Abi Waqqaas رضي الله عنه ambaye anasema:

"Baba yangu aliniambia kwamba, siku ya vita vya Uhud 'Abdullah ibn Jahsh alimwambia, "Unaonaje tukikaa pembeni kidogo na kuomba dua?"

Anasema, "Kisha tulisogea pembeni kidogo na Sa'd akaomba dua akisema, "Ewe Mola wangu! Tutakapokutana na adui zetu leo nakuomba unikutanishe na mmoja kati ya mashujaa wakubwa na mpiganaji hodari miongoni mwao ambaye nitapambana naye kwa ajili yako. Kisha nipe ushindi dhidi yake ili nimuuwe na nichukue silaha zake."

'Abdullah ibn Jahsh akaitikia dua ile kwa kusema, Aameen! Kisha 'Abdullah ibn Jahsh naye akaomba dua akisema, "Ewe Allah! Nijaaliye nikutane na mpiganaji hatari katika maadui zetu ambaye nitamkabili na kupambana naye na ujaaliye adui huyo anishinde na anikate pua yangu na masikio yangu, ili nitakapokutana Nawe Allah niseme, "Hakika hali hii (ya kukatwa pua na masikio) ni katika kupigana katika njia yako na Mtume wako, na wewe Allah useme: 'Umesema kweli mja Wangu'"

Sa'd رضي الله عنه anasema, "Dua ya 'Abdullah ilikuwa bora kuliko yangu. Nilimuona baadaye siku hiyo pua na masikio yake yakiwa yamekatwa na yakining'inia."

Zubayr ibn Bakr anasimulia kuwa:

'Abdullah ibn Jahsh alikuwa akiitwa 'aliyekatwa masikio katika njia ya Allah.' Upanga wake ulivunjika katika vita vya Uhud na Mtume wa Allah ﷺ akampa fimbo nyembamba aitumie kama upanga, na hakika ulikuwa upanga mkali wakati akiitumia fimbo ile. Baada ya hapo alipewa jina la utani la 'fimbo nyembamba'. Upanga huu ulibakia kuwepo kama kumbukumbu mpaka ulipouzwa kwa mturuki aliyefahamika kwa jina la Bagha, kwa thamani ya Dinaar mia mbili."

Ilikuwa siku ya jumapili, katika mwaka wa tatu baada ya kufanyika Hijrah, siku ambayo 'Abdullah رضي الله عنه aliuwawa shahidi. Iwe kwa Muislamu mwanamke au kwa Muislamu mwanaume, bado anayo ya kujifunza katika historia hii, hasa kwa wale wenye dhamira ya kutafuta radhi za Allah.

Baadaye Mtume ﷺ akapata habari kuhusu huzuni na unyonge aliokuwa nao Zaynab رضي الله عنها kutokana na kubaki mjane baada ya mumewe kuuwawa katika njia ya Allah. Ili kumsaidia na kumliwaza, Mtume ﷺ alipeleka posa ili amuoe. Zaynab bint Khuzaymah رضي الله عنها aliipokea posa ya Mtume ﷺ kwa furaha kubwa, na hivyo kuolewa na Mtume ﷺ na kuwa mmoja kati ya mama wa Waumini. Bila shaka, kuwa mama wa Waumini (Kuwa mke wa Mtume) ni hadhi ya juu kabisa ambayo mtu angeweza kuipata. Sasa hakuwa tena na jina la mama wa masikini na mafakiri peke yake, bali pia mama wa Waumini.

Miezi minane (8) tu baada ya Zaynab bint Khuzaymah رضي الله عنها kuolewa na Mtume ﷺ, Zaynab bint Khuzaymah رضي الله عنها, mama wa Waumini na mama wa masikini na mafakiri akauguwa na kuwa mgonjwa sana; maradhi haya yakaja kuwa sababu ya kifo chake.

Huyu ndiye mke pekee wa Mtume ﷺ aliyefariki wakati Mtume ﷺ akiwa hai ukiacha Khadijah. Hii ina maana kuwa, Zaynab bint Khuzaymah na Khadijah, ndio wake wawili wa Mtume ﷺ ambao walifariki na kumuacha Mtume ﷺ akiwa hai; Mtume ﷺ aliwazika wake hawa, wake wengine wa Mtume ﷺ walifariki baada ya Mtume ﷺ kufariki. Mtume ﷺ aliingiwa na huzuni sana kutokana na kifo chake na alimuomba Allah amsamehe na siku zote Mtume ﷺ alibakia akikumbuka uwezo mkubwa wa mama huyu katika kuwa na subira, imani thabiti na msimamo usioyumba.

# Maria al-Qibtiyya

## Mimi ni Zawadi Maalum kwa Mtume ﷺ

Baada ya Mtume ﷺ kuingia makubaliano na makafiri wa Makkah, makubaliano ambayo yanafahamika kwa jina la 'mkataba wa Hudaybiyyah', Mtume ﷺ aliwaandikia barua viongozi wa mataifa mbalimbali ya kiarabu na yasiyokuwa ya kiarabu akiwalingania na kuwataka wasilimu na kuingia katika Uislamu. Miongoni mwa viongozi na mataifa ambayo Mtume ﷺ aliwaandikia barua ni Mfalme Najashi wa Ethiopia, Harith Ghassani aliyekuwa gavana wa Syria, Munzir ibn Sawa Al-Tamimi aliyekuwa gavana wa Bahrain na Muqauqis aliyekuwa anatawala Misri. Kwa kuwa mama huyu, Maria al-Qibtiyya anatokea katika nchi ya Misri, tutajihusisha na namna gani alikuja kuwa mke wa Mtume ﷺ, na bila shaka tutazungumza kwa uchache habari za mtawala wa huko, Muqauqis.

Muqauqis alikuwa na taarifa juu ya kuja kwa Mtume ﷺ katika bara Arabu. Ushahidi wa jambo hili ni kwamba, kabla ya kuingia katika Uislamu, Mughira ibn Shu'ba alifanya mazungumzo na Muqauqis na kiongozi huyu alimuuliza mambo kadhaa kuhusiana na Mtume ﷺ. Mughira ibn Shu'ba anasimulia kuwa:

Wakati fulani nilikwenda Ikulu ya Muqauqis ambaye aliniuliza kuhusu familia ya Mtume ﷺ. Nilimfahamisha kuwa, yeye (Mtume ﷺ) anatoka katika ukoo na familia yenye kuheshimika miongoni mwetu. Muqauqis akasema kuwa, 'Mitume wote hutokea katika familia zenye kuheshimika'. Kisha aliniuliza ikiwa ninafahamu chochote juu ya ukweli wake. Nikamwambia kuwa, siku zote yeye husema kweli, na kwamba pamoja na kwamba tunampinga, tunamwita 'Mkweli'. Muqauqis akasema, 'Mtu ambaye hasemi uongo kwa watu, anawezaje kusema uongo juu ya Mwenyezi Mungu?' Kisha aliniuliza aina ya watu waliokuwa wafuasi wake na wayahudi wanasema nini juu yake? Nikamjibu kuwa, 'wafuasi wake wengi ni watu masikini, lakini wayahudi

walikuwa ndio maadui zake wakubwa.' Muqauqis akasema kuwa, 'Mwanzoni wafuasi wengi wa Mitume mara nyingi huwa ni watu masikini, na kwamba lazima huyo atakuwa ni Mtume wa Mwenyezi Mungu'. Kisha akaongeza kusema kwamba, 'Mayahudi wanamchukia na kumpiga vita kwa sababu ya wivu, vinginevyo wangekuwa wa mwanzo kuthibitisha ukweli, na kwamba wao pia walikuwa wakisubiri kutokea kwa Mtume. Yesu aliwaambia wafuasi wake kwamba, kumfuata na kumtii Mtume atakayekuja ni jambo la lazima; na sifa alizonazo Mtume Muhammad ﷺ ni sifa za mitume waliotangulia'.

Mazungumzo haya yalifanyika kabla ya Mughira ibn Shu'ba hajaingia katika Uislamu, na Mtume ﷺ hajatuma barua kwenda kwa watawala mbalimbali kama tulivyodokeza hapo kabla. Mwaka wa 6 Hijiriyah, Mtume ﷺ akampa barua mmoja katika maswahaba wake, Hatib ibn Balta'ah na kumtaka aipeleke kwa Muqauqis. Sehemu ya barua hiyo ya Mtume ﷺ ilikuwa na maneno yafuatayo: *"Bismillahir Rahmanir Rahiim. Barua hii inatoka kwa Muhammad mtumwa na Mtume wa Allah kwenda kwa Muqauqis kiongozi wa Misri. Amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya kila anayefuata Muongozo (wa Mwenyezi Mungu). Nakualika na kukutaka ujisalimishe kwa Mwenyezi Mungu (Usilimu na kuwa Muislamu): Kwa kujisalimisha kwako (kwa kuwa kwako Muislamu) utakuwa na amani na Mwenyezi Mungu atakupa ujira mara mbili. Na kama utakataa kujisalimisha (kuwa Muislamu) basi utabeba madhambi ya kuwapoteza watu*.

قُلْ يَٰٓأَهْلَ ٱلْكِتَٰبِ تَعَالَوْا۟ إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَآءٍۭ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا ٱللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِۦ شَيْـًٔا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ ٱللَّهِ ۚ فَإِن تَوَلَّوْا۟ فَقُولُوا۟ ٱشْهَدُوا۟ بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٦٤﴾

***"Sema, Enyi watu mliopewa kitabu (cha Mwenyezi Mungu, Mayahudi na Wakristo)! Njooni katika neno lililo sawa baina yetu na baina yenu: ya kwamba tusimwabudu yoyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe (Mwenyezi Mungu) na chochote; wala baadhi yetu tusiwafanye wengine kuwa waungu badala ya Mwenyezi mungu (au pamoja na Mwenyezi mungu). Wakikengeuka, semeni: "Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu, (tumenyenyekea amri za Mwenyezi Mungu)."***

Haya ndiyo maneno yaliyokuwa ndani ya barua aliyoituma Mtume wa Allah kwenda kwa Muqauqis, mtawala wa Misri. Baada ya kupokea barua hii, kiongozi wa Misri Muqauqis aliamuru barua ile ihifadhiwe vizuri katika sehemu salama. Kisha aliandika barua ya majibu iliyosomeka:

'Kutoka kwa Muqauqis Nimesoma barua yako na kuelewa vizuri kile kilichoandikwa. Nafahamu kuwa kunatazamiwa kutokea (kuja) kwa Mtume. Lakini nilidhani Mtume huyo atazaliwa Syria – Nimempokea na kumtendea wema na kumpa heshima ya juu kabisa mtu uliyemtuma ujumbe huu. Nakutumia zawadi ya watumishi wawili wa kike. Watumishi hawa wawili (Maria al-Qibtiyya na dada yake Sirin) wanatoka katika familia yenye kuheshimika sana miongoni mwetu. Pamoja na zawadi hiyo, nakutumia pia nguo na farasi aliye bora kabisa. Namuomba Mwenyezi Mungu akulinde'.

Haya ndiyo yalikuwa majibu ya Muqauqis. Wakiwa njiani kuelekea Madinah, Maria al-Qibtiyya na dada yake Sirin waliongozana na swahaba wa Mtume ﷺ, Hatib ibn Balta'ah رضي الله عنه. Walistaajabishwa na kushangazwa na namna ambavyo swahaba huyu alivyokuwa na nidhamu na akiwaheshimu sana mabinti hawa. Walifikia hatua wakaamini kuwa haiwezekani mtu wa kawaida amfundishe mtu na awe na nidhamu kwa kiasi kile. Hivyo waliamini kuwa bila shaka mtu aliyemfundisha nidhamu na heshima ya kiasi kile Hatib ibn Balta'ah alikuwa ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, hivyo wakasilimu kabla hata hawajafika Madinah kwa Mtume ﷺ.

Walipofika Madinah kwa Mtume ﷺ, Mtume ﷺ, alimuoa Maria al-Qibtiyya na Sirin akamuozesha kwa swahaba wake Hassan ibn Thabit ambaye alizaa naye mtoto mmoja aliyemwita 'Abd al-Rahman ibn Hassan.

Katika mwaka wa 9 Hijiriyah, Maria al-Qibtiyya alijifungua mtoto wa kiume na Mtume ﷺ, alimwita mtoto huyu Ibrahim. Huu ni mwaka ambao pia Zainab mtoto wa Mtume ﷺ, alifariki. Kwa bahati mbaya, mtoto huyu alipofikisha umri wa miezi minane (8), akawa mgonjwa sana na hatimaye akafariki. Mtume ﷺ alikuwa akibubujikwa na machozi kufuatia kifo cha mtoto huyu. Maswahaba walipomuuliza Mtume ﷺ, kwanini alikuwa analia, aliwajibu kuwa: *"Hii ni hali ya kibinadamu"*

Ikatokea kuwa, wakati mtoto wa Mtume ﷺ, Ibrahim akizikwa, jua lilipatwa na kiza kikatanda. Baadhi ya watu wakadhani kuwa kupatwa huku kwa jua kulikuwa na uhusiano na kufariki kwa mtoto wa Mtume, Ibrahim.

Mtume ﷺ akafuta fikra hizi kwa kuwaambia kuwa: *"Jua na Mwezi ni alama mbili za Mwenyezi Mungu. Havipatwi kwa sababu ya kuzaliwa au kufa kwa yeyote. Mtakapoona dalili hizi mbili (kupatwa kwa jua au kupatwa kwa mwezi), basi zidisheni kumkumbuka Allah katika Swala."*

Pamoja na kuwa makafiri walikuwa wakimteta Mtume Muhammad ﷺ kuwa hana mtoto wa kiume, jambo hilo lilikomeshwa pale Mwenyezi Mungu Aliposhusha Ayah zifuatazo:

مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَآ أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رَّسُولَ ٱللَّهِ وَخَاتَمَ ٱلنَّبِيِّـۧنَ ۗ وَكَانَ ٱللَّهُ بِكُلِّ شَىْءٍ عَلِيمًا ﴿٤٠﴾

***"Hakika Tumekupa kheri nyingi. Basi Swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (kwa ajili ya Mola wako). (Na kila utakalolifanya lifanye kwaajili ya Mola wako, siyo mizimu wala mapango wala makaburi). Hakika adui yako ndiye atakayekuwa mkiwa (atakatika na kila kheri)" .*** **(108:1-3)**

إِنَّآ أَعْطَيْنَٰكَ ٱلْكَوْثَرَ ﴿١﴾ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنْحَرْ ﴿٢﴾ إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ ٱلْأَبْتَرُ ﴿٣﴾

***"Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa Mitume, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu".*** **(33:40)**

Hivi ndivyo Maria al-Qibtiyya alivyokuja kuingia katika orodha ya wake wa Mtume ﷺ na hivyo kuwa mama wa Waumini. Maria al-Qibtiyya aliishi na Mtume ﷺ kwa muda wa miaka mitatu (3) tu, Mtume ﷺ akafariki dunia.

Baada ya hapo, mama wa Waumini Maria al-Qibtiyya, aliendelea kutekeleza Uislamu wake na muda mwingi alikuwa akikaa ndani ukiachia muda mchache aliotoka kwa sababu maalum ikiwemo kulizuru (kulitembelea) kaburi la Mtume ﷺ au la mwanae Ibrahim. Yeye pia hakuishi miaka mingi baada ya kufariki Mtume ﷺ, kwani alifariki baada ya miaka mitano tu baada ya kufariki Mtume ﷺ na alizikwa katika makaburi ya Baqi. Makaburi ambayo walizikwa wachamungu wengine kama tulivyoona huko nyuma na kama tutakavyoona hapo baadaye. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amuwie radhi na amridhie mama yetu, mama wa Waumini - Maria al-Qibtiyya.

## Mabinti wa Mtume ﷺ

**Zainab bint Muhammad**

**Ruqayyah bint Muhammad**

**Ummu Kulthum bint Muhammad**

**Fatmah bint Muhammad**

# Zainab bint Muhammad

## Ewe Abu Al'As, Hujatukumbuka hata kidogo?

Zainab bint Muhammad, huyu alikuwa binti mkubwa wa Mtume ﷺ, mmoja kati ya watoto ambao Mtume ﷺ alijaaliwa kuwapata kutoka kwa mama wa waumini, Khadijah رضي الله عنها.

Mume wa mama huyu, Zainab bint Muhammad رضي الله عنها, alikuwa ni Abu al-'As ibn Rabi' na alikuwa akipendwa sana na Mtume ﷺ. Siku moja, Abu al-'As ibn Rabi' alikwenda kwa Mtume ﷺ kabla Mtume ﷺ hajapewa Utume na kumwambia baba wa Zainab kuwa: "Naomba ridhaa nimuoe mwanao mkubwa". Mtume ﷺ akamjibu kuwa: "Lazima nimuulize kwanza yeye mwenyewe". Mtume ﷺ akaenda kwa Zainab na kumuuliza: "Binamu yako amekuja kwangu na amesema anataka kukuoa, je, unamkubali awe mume wako?" Uso wake ukabadilika rangi na kuwa mwekundu kwa furaha na akatabasamu Zainab.

Hivi ndivyo Zainab رضي الله عنها alivyoolewa na Abu al-'As ibn Rabi', na kuanza kwa safari yao ya Maisha! Katika maisha yao, wawili hawa walijaaliwa kupata watoto wawili na kuwaita; Ali na Uma'mah. Baadaye Muhammad ibn Abdullah akapewa Utume na Allah. Wakati huo Abu al-'As ibn Rabi' hakuwepo Makkah. Aliporejea, alimuona mkewe, Zainab amekuwa Muislamu. Alipofika tu, mkewe akamwambia, "Nina habari njema kwa ajili yako". Alisimama na kuondoka huku akimuacha Zainab pale. Zainab alishangaa na alimfuata huku akisema, "Baba yangu amekuwa Mtume, na mimi nimekuwa Muislamu".

Abu al-'As ibn Rabi' akajibu kuwa, "Kwanini hukuniambia kwanza (habari hizi kabla hujachukua uamuzi wowote)?" Hivyo mgogoro mkubwa ukazuka baina yao; Tatizo kubwa likiwa ni dini na imani. Zainab akamwambia kuwa, "Katu siwezi kuacha kumfuata baba na ujumbe wa Uislamu aliokuja nao, baba

yangu hakuwahi kuwa muongo, na si muongo katika hili pia. Yeye ni mkweli na muaminifu". Na mimi si Muislamu peke yangu; mama yangu na dada zangu wote wamekuwa Waislamu, binamu yangu Ali ibn Abi Talib amekuwa Muislamu pia, binamu yako Uthman ibn Affan amekuwa Muislamu, na hata rafiki yako mkubwa Abu Bakr amekuwa pia Muislamu". Abu al-'As ibn Rabi' akajibu, "Sawa lakini mimi sitaki watu waje waseme 'aliacha dini na imani ya wazee wake ili kumridhisha mke wake'. Na mimi sithubutu kumsema au kumtuhumu vibaya baba yako kwa lolote". Kisha mume wa Zainab رضي الله عنها, Abu al-'As ibn Rabi' akasema, "Unaweza kunielewa na kunisamehe (kwa hilo)?" Zainab bint Muhammad رضي الله عنها akamjibu kuwa, "Unadhani nani anaweza kukuelewa na kukuridhia kama sio mimi?" Mimi nitasimama na wewe na kukusaidia mpaka uufahamu na kuufikia ukweli." Na alidumu na kusimama katika ahadi yake kwa muda wa miaka ishirini (20)!

Abu al-'As ibn Rabi' alibakia kuwa kafiri, na ikafika wakati wa Hijirah. Zainab bint Muhammad, akaenda kwa baba yake na kumuomba ruhusa yeye (Zainab) abaki Makkah na mume wake. Mtume ﷺ akamjibu, "Baki na mume wako na watoto wenu".

Hivyo Zainab رضي الله عنها akabaki Makkah wakati Waislamu wanahama kwenda Madinah na alibakia huko mpaka vita vya Badr vikatokea. Mume wa Zaynab alikuwa apigane akiwa ndani ya jeshi la makafiri wa Kiquraishi dhidi ya Waislamu. Kwa Zainab, hii ilimaanisha kuwa, mume wake atakuwa anapigana na baba yake Zainab, Mtume Muhammad ﷺ, jambo ambalo Zainab رضي الله عنها alikuwa muda wote akichelea lisije kutokea. Muda wote alikuwa akilia na kumuomba Allah akisema: "Ewe Allah, siku moja jua linaweza kuchomoza na wanangu wakabaki yatima, au nikampoteza baba yangu". Vita vikaanza, na Waislamu wakapata ushindi mkubwa sana. Mume wa Zainab رضي الله عنها, Abu al-'As ibn Rabi' alikamatwa na kuchukuliwa mateka na Waislamu na habari juu ya kukamatwa kwake zikawafikia watu wa Makkah.

Zainab رضي الله عنها akauliza, "Nini kimemtokea baba yangu?" Wakamjibu kuwa, "Waislamu wameshinda vita". Zainab رضي الله عنها akamshukuru Allah. Kisha Zainab رضي الله عنها akauliza: "Nini kimemtokea mume wangu?" wakamjibu: "Mume wako amekamatwa mateka". Zainab رضي الله عنها akasema, "Nitatuma fedha kumkomboa mume wangu". Wakati huo Zainab alikuwa hamiliki chochote cha thamani kubwa, hivyo akachukua mkufu wa marehemu mama

yake na kumkabidhi shemeji yake (kaka wa mume wake) ili aupeleke mkufu ule kwa Mtume ﷺ kama kikomboleo cha mume wake.

Wakati Mtume ﷺ akiwa amekaa na kupokea fidia kutoka kwa watu mbalimbali waliokuja kulipa fidia ili watu wao waliotekwa waachiwe, Mtume ﷺ aliuona mkufu wa marehemu mkewe, Khadijah. Aliinua uso na kuuliza: "Malipo haya ni kwa ajili ya mateka yupi?" Wakamjibu kuwa: "Malipo haya ni kwa ajili ya Abu Al'As ibn Rabi". Mtume ﷺ akapaza sauti akisema, "huu ni mkufu wa Khadijah". Mara tu Mtume ﷺ alipouona mkufu ule wa marehemu mke wake, Khadijah, aliingiwa na simanzi na kumbukumbu za mkewe zikamjia. Maswahaba waliokuwepo katika eneo lile wakapigwa na butwaa kuona hali ya huzuni iliyokuwa imempata Mtume ﷺ. Baada ya kimya cha muda mrefu, Mtume ﷺ akasimama na kusema, "Mtu huyu (Abu al-'As ibn Rabi') ni mkwe wangu. Je, nimuachie? Na je, mnakubali nimrudishie mkufu huu mwanangu?" Maswahaba wakajibu kwa pamoja, "Ndiyo ewe Mtume wa Allah".

Mtume ﷺ akamkabidhi mkufu ule Abu Al'As na kumwambia: "Mwambie mwanangu Zainab, asitoe mkufu wa Khadijah". Kisha Mtume ﷺ akasema, "Naomba kuongea na wewe faragha ewe Abu Al'As." Mtume ﷺ akamchukua bwana yule na kwenda nae pembeni na kumwambia, "Allah Ameniamuru kuwatenganisha Waislamu na makafiri, je, unaweza kunirejeshea binti yangu?" Huku akisita sita, Abu Al'Ass akakubali.

Zainab رضي الله عنها akasimama katika lango la mji (njia ya kuingilia mjini) akisubiri kuwasili kwa Abu Al'As. Alipofika, Abu Al'As akasema, "Naondoka kwenda mbali". Zainab akamuuliza "Unakwenda wapi?" Akajibu, "Sio mimi ninayekwenda, bali wewe. Unakwenda kwa baba yako. Lazima tuachane kwa sababu wewe ni Muislamu". Zainab رضي الله عنها akamuuliza; "Utasilimu na kuongozana na mimi?" Abu Al'As Akakataa.

Hivyo Zainab رضي الله عنها akawachukua watoto wake na kusafiri kwenda Madinah, na kwa muda wa miaka sita (6) alikataa kuolewa na mwanamume mwingine, akitarajia kwamba siku moja Abu Al'As anaweza kusilimu. Baada ya miaka hiyo sita, Abu al-'As ibn Rabi' alikuwa anasafiri katika msafara uliokuwa ukitoka Makkah kwenda Syria. Wakiwa safarini, walikutana na kukabiliana na maswahaba wa Mtume ﷺ. Abu al-'As ibn Rabi' akafanikiwa kutoroka na kuulizia nyumbani kwa Zainab رضي الله عنها. Abu al-'As akagonga mlango muda mfupi kabla

ya Swala ya Magharib. Zainab akafungua mlango na kumuuliza, “Umesilimu?” Alijibu kwa kunong’ona, “Hapana, nimekuja kuomba hifadhi”. Zainab akamuuliza, “Unaweza kusilimu?” Abu al-‘As akajibu, “Hapana”. Zainab akamwambia, “Usiwe na wasiwasi,” karibu ewe baba wa watoto wangu.

Baada ya Mtume ﷺ kumaliza kuswali Swala ya Magharib kwa jamaa msikitini, walisikia sauti nyuma ya msikiti ikisema: “Nimemuacha huru Abu Al’As ibn Rabi”. Zainab رضي الله عنها amempa uhuru. Mtume ﷺ akawauliza maswahaba, “Mmesikia nilichokisikia mimi?” Wote wakasema, “Ndiyo, ewe Mtume wa Allah”. Zainab رضي الله عنها anasema, “Yeye (Abu al-‘As) ni baba wa watoto wangu nimemuacha huru”.

Mtume ﷺ akasimama na kusema, “Enyi watu, nathibitisha kuwa mtu huyu alikuwa mkwe mwema, hakuwahi kuvunja ahadi yake, na hakuwahi kusema uongo. Kama mtakubali, nitamrejeshea mali zake na kumuacha aondoke. Kama mtakataa, hiyo ni hiari yenu wala sitowalaumu kwa kukataa kwenu.” Maswahaba wakakubali, na kusema: “Tutampa mali na fedha zake”.

Hivyo, Mtume ﷺ akamwambia Zainab, “Ewe Zainab, tumemuacha huru yule ambaye wewe umemuacha huru.” Kisha Mtume ﷺ akamwendea Zainab رضي الله عنها na kumwambia, “...usiruhusu akusogelee, hakika yeye (kwa kuwa kwake kafiri) ameharamishwa kwako”. Zainab akamjibu baba yake, “Niamini baba, nitafanya vile ulivyonielekeza”.

Zainab رضي الله عنها aliingia ndani na kumwambia Abu al-‘As’, “Ewe Abu Al’As, hivi hujatukumbuka hata kidogo? Huwezi kuwa muislamu na ukakaa na sisi?” Lakini Abu al-‘As alikataa. Abu Al’As akachukua mali na pesa zake na kurejea Makkah.

Aliporejea, alisimama na kutangaza hadharani kuwa, “Mali na fedha zenu hizi hapa. Je, kuna chochote ambacho hakikurejeshwa?”

Wakajibu, “Hapana, ewe Abu Al’As, hakuna chochote kilichosalia au kukosekana, asante sana.” Kisha Abu Al’As akasema, “Nakiri kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na Muhammad ni Mtume wake.”

Kisha akarejea tena Madinah, na alipofika alienda moja kwa moja kwa Mtume wa Allah na kumwambia, “Ewe Mtume wa Allah, jana uliniacha huru, na leo nakubali kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na wewe ni Mtume Wake.”

Kisha Abu Al'As akamuuliza Mtume ﷺ, "Je, unaweza kunipa ruhusa nirejee kuishi na Zainab?" Mtume ﷺ akatabasamu, kisha akamwambia "Nifuate"; Mtume ﷺ akaongozana na Abu Al'As mpaka nyumbani kwa Zainab رضي الله عنها na kugonga mlango. Baada ya Zainab kufungua mlango, Mtume ﷺ akamwambia, "Ewe Zainab, mume wako amekuja na kuniomba ruhusa kama anaweza kurejea na kuishi na wewe". Kama ilivyokuwa miaka takriban ishirini iliyopita, uso wake ulijawa na furaha na tabasamu.

Ni bahati mbaya iliyoje? Mwaka mmoja tu baada ya kutokea tukio hili, Zainab رضي الله عنها alifariki dunia. Abu Al'As alilia sana kwa uchungu kufuatia kifo cha mke wake Zainab bint Muhammad, binti wa Mtume ﷺ; hali iliyowafanya watu wote waliokuwepo pale waangue kilio kwa simanzi. Mtume ﷺ alikuja huku macho yake yakibubujika machozi na moyo wake ukiwa umejawa na huzuni.

Kifo cha mwanae Zainab رضي الله عنها, kilimkumbusha kifo cha mke wake kipenzi, mama wa kwanza wa Waumini, Khadijah رضي الله عنها, Mtume ﷺ aliwaambia wanawake waliokusanyika na kuuzunguka mwili wa Zainab رضي الله عنها: *"Muosheni mara tatu na mtumie kafuri katika josho la tatu."*

Mtume ﷺ aliongoza swala ya jeneza la mwanae na akashiriki katika kumzika. Abu Al'Ass akarejea nyumbani kwa watoto wake, Ali na Uma'mah. Alikuwa akiwabusu huku amewakumbatia na akibubujikwa machozi kwa kumkumbuka marehemu mke wake, Zainab bint Muhammad رضي الله عنها.

Abu Al'Ass alikuwa akilia sana kiasi kwamba watu walikuwa wakimuona Mtume ﷺ akim-bembeleza na kumtuliza. Abu Al'As alikuwa akisema, "Naapa kwa jina la Allah, siwezi kuishi muda mrefu bila kuwa na Zainab." Na ndivyo ilivyokuwa. Abu Al'As, mume wa Zainab bint Muhammad naye alifariki mwaka mmoja tu baada ya kufariki Zainab.

Tunamuomba Allah amridhie Zainab, mtoto wa Mtume ﷺ na Amruzuku Pepo ya juu kabisa (Jannatul-Firdaus) kwa subira aliyoionesha na jitihada aliyoifanya kwa ajili ya Allah. Amin.

# Ruqayyah bint Muhammad

## Kwa ajili ya Uislamu niliachwa na Mume wangu

Ruqayyah bint Muhammad رضي الله عنها, ni mtoto wa pili wa Mtume ﷺ. Kama ilivyokuwa kwa watoto wote wa Mtume wa Allah ﷺ, mtoto huyu pia alizaliwa na mama wa Waislamu, Khadijah bint Khuwaylid ibn Asad رضي الله عنها. Mtoto huyu wa Mtume ﷺ alizaliwa miaka mitatu baada ya kuzaliwa mtoto wa kwanza wa Mtume ﷺ, Zaynab bint Muhammad رضي الله عنها

Kabla ya Mtume ﷺ kukabidhiwa Utume, Ruqayyah bint Muhammad رضي الله عنها aliolewa na bwana mmoja akiitwa Utbah ibn Abu Lahab. Lakini baada ya baba wa Ruqayyah (Mtume Muhammad – ﷺ) kukabidhiwa Utume, Abu Lahab na mkewe Ummu Jamil wakawa maadui wakubwa wa Uislamu na wakifanya kila wanaloliweza kuhakikisha wanazima nuru ya Allah. Baadaye Allah Akashusha Ayah zikiwabashiria mwisho mbaya (moto) wote wawili, Abu Lahab na mkewe Ummu Jamil. Ayah zenyewe ni hizi:

تَبَّتْ يَدَآ أَبِى لَهَبٍ وَتَبَّ ۝١ مَآ أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُۥ وَمَا كَسَبَ ۝٢ سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ ۝٣ وَٱمْرَأَتُهُۥ حَمَّالَةَ ٱلْحَطَبِ ۝٤ فِى جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍۭ ۝٥

***"Pana kuangamia mikono miwili ya Abu Lahab! Naye amekwisha angamia. Hayatamfaa mali yake wala alivyovichuma. (Atakapokufa) atauingia Moto wenye mwakao (mkubwa kabisa). Na mkewe, mchukuzi wa kuni (za fitina), (fattani anayefitinisha watu wasiingie katika dini, atauingia na yeye Moto huo). (Kama kwamba) shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa (atakayochukulia kuni za fitina hizo)".***

Abu Lahab na mkewe Ummu Jamil wakakasirika sana na kuwaamuru watoto wao wawili ambao kila mmoja alikuwa amemuoa mtoto mmoja wa

Mtume ﷺ kuwaacha mara moja. Watoto hawa wa Mtume ﷺ waliachwa katika siku moja, baada ya waume zao kupokea amri ya kuwaacha kutoka kwa wazazi wao. Baadaye mtoto huyu wa Mtume Ruqayyah رضي الله عنها aliolewa na mmoja katika maswahaba wa kweli na waaminifu wa Mtume ﷺ, Uthman ibn 'Affan, ambaye baadaye alikuja kuwa Khalifa wa tatu wa Waislamu.

Baada ya mateso kuwa makali na Waislamu kufanyiwa kila aina ya uadui na mateso, Mtume ﷺ akawaruhusu baadhi ya maswahaba zake kuhamia Uhabeshi (Ethiopia). Miongoni mwa maswahaba waliohamia Ethiopia alikuwemo Uthman ibn 'Affan na mkewe Ruqayyah رضي الله عنهما. Wakiwa wanaondoka kuelekea Uhabeshi, Allah Akawajaalia kupata mtoto wa kiume na wakamwita mtoto yule Abdullah. Kwa bahati mbaya mtoto huyu hakuishi muda mrefu, kwani alifariki akiwa na umri wa miaka sita (6) tu.

Baada ya kuishi muda mrefu Uhabeshi (Ethiopia), Uthman ibn 'Affan na mkewe Ruqayyah bint Muhammad رضي الله عنها, wakarejea Makkah, na baadaye wakawa miongoni mwa maswahaba waliohamia Madinah. Ni kutokana na kuhama kwake kwenda Uhabeshi na kuhamia Madinah, Ruqayyah bint Muhammad hufahamika kama 'Mwanamke aliyehama mara mbili'. Waliendelea kuishi Madinah wakitekeleza Uislamu wao vizuri na kwa mapenzi makubwa. Wakati wote huo, makafiri wa Makkah waliendelea kuwachokoza Waislamu. Walikuwa wakitoka Makkah na kuja Madinah kuwavamia na kuwashambulia. Hatimaye vikatokea vita vya Badr.

Muda mfupi kabla ya kutokea vita vya Badr, Ruqayyah رضي الله عنها, aliugua. Hivyo, Mtume Muhammad ﷺ akamshauri Uthman ibn 'Affan رضي الله عنه asitoke pamoja na msafara uliokuwa ukielekea Badr, na badala yake abaki akimuuguza mkewe.

Anasimulia ibn Umar رضي الله عنه kwamba:

Uthman hakushiriki vita vya Badr kwa sababu alikuwa amemuoa mmoja katika watoto wa Mtume ﷺ na mkewe alikuwa mgonjwa. Mtume ﷺ akamwambia, "Utapata ujira (thawabu) na mgao wa ngawira (kutoka katika vita) sawa na yule ambaye ameshiriki katika vita vya Badr."

Ruqayyah bint wa Mtume, alifariki siku ile ile ambayo Waislamu walipata ushindi katika vita vya Badr; na ilikuwa takriban miaka miwili toka Waislamu wahamie Madinah. Kwa kuwa Mtume ﷺ alikuwa hajarejea kutoka vitani,

hakujaaliwa kushiriki mazishi ya mwanae. Ruqayyah bint Muhammad, alizikwa katika makaburi ya Al-Baqi katika mji wa Madinah. Na huyu alikuwa mtoto wa kwanza wa kike wa Mtume ﷺ kufariki dunia.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Amridhie na kumuingiza katika rehema zake - Amin

# Ummu Kulthum bint Muhammad

## Ningekuwa na watoto wengine kumi Ningewaozesha kwa Uthman

Ummu Kulthum bint Muhammad رضي الله عنها, alikuwa ni mtoto wa tatu wa kike wa Mtume wetu, Muhammad ﷺ aliyemzaa kwa mama wa waumini Khadijah bint Khuwaylid رضي الله عنها. Binti huyu alizaliwa mwaka wa 603, na alikuwa mdogo kwa dada yake Ruqayyah, kwa kiasi cha mwaka mmoja.

Watoto wawili wa Mtume ﷺ, Ummu Kulthum na Ruqayyah waliishi maisha yanayofanana sana. Wote walizaliwa na kulelewa na baba mmoja na mama mmoja (Muhammad na Khadijah); mwanzoni wote waliolewa katika familia moja, familia ya Abu Lahab; Waliingia katika Uislamu siku moja; wote waliachwa na waume zao siku moja baada ya waume zao kupokea amri kutoka kwa wazazi wao; na wote kwa nyakati tofauti waliolewa na Uthman ibn 'Affan!

Kabla ya kuja kwa Uislamu, Ummu Kulthum bint Muhammad alikuwa ameolewa na bwana mmoja akiitwa Utaybah ibn Abu Lahab. Lakini baada ya baba wa Ummu Kulthum (Mtume Muhammad ﷺ) kukabidhiwa Utume, Abu Lahab na mkewe Ummu Jamil wakawa maadui wakubwa wa Uislamu na wakifanya kila wanaloliweza kuhakikisha wanazima nuru ya Allah. Baadaye Allah akashusha Ayah zikiwabashiria mwisho mbaya (moto) wote wawili, Abu Lahab na mkewe Ummu Jamiil. Ayah zenyewe ni hizi:

تَبَّتْ يَدَآ أَبِى لَهَبٍ وَتَبَّ ﴿١﴾ مَآ أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُۥ وَمَا كَسَبَ ﴿٢﴾ سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ
لَهَبٍ ﴿٣﴾ وَٱمْرَأَتُهُۥ حَمَّالَةَ ٱلْحَطَبِ ﴿٤﴾ فِى جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍۭ ﴿٥﴾

***"Pana kuangamia mikono miwili ya Abu Lahab! Naye amekwisha angamia. Hayatamfaa mali yake wala alivyovichuma.***

***(Atakapokufa) atauingia Moto wenye mwako (mkubwa kabisa). Na mkewe, mchukuzi wa kuni (za fitina), (fattani anayefitinisha watu wasiingie katika dini, atauingia na yeye Moto huo). (Kama kwamba) shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa (atakayochukulia kuni za fitina hizo)".***

Abu Lahab na mkewe Ummu Jamil wakakasirika sana na kumuamuru mtoto wao Utaybah ibn Abu Lahab kumuacha mke wake Ummu Kulthum bint Muhammad mara moja. Hivyo, Ummu Kulthum na Ruqayyah, watoto wa Mtume ﷺ waliachwa katika siku moja, baada ya waume zao kupokea amri ya kutakiwa kuwaacha kutoka kwa wazazi wao. Mara baada ya kuachwa, Ummu Kulthum alirudi nyumbani na kuendelea kuishi na wazazi wake, Mtume Muhammad ﷺ na mama wa Waumini, Khadijah رضي الله عنها,.

Baadaye makafiri wa Makkah wakawawekea vikwazo vya kiuchumi na kijamii Waislamu waliokuwa wachache na wanyonge. Waislamu walikabiliwa na hali ngumu sana, kiasi cha kuwalazimu baadhi ya maswahaba kula majani ya miti na nyasi kunusuru maisha yao. Mama wa waumini na mke kipenzi wa Mtume ﷺ na mama wa Ummu Kulthum na watoto wengine wa Mtume ﷺ alifariki muda mfupi tu baada ya kuondolewa kwa vikwazo. Kifo cha mama yake, kilimuachia Ummu Kulthum huzuni kubwa na unyonge. Hata hivyo, Ummu Kulthum aliyakabili maisha haya yaliyojaa misukosuko na msiba wa mama yake kwa ujasiri mkubwa. Alijikuta akilazimika kusimama imara kwa sababu baada ya kufariki mama yake mzazi, Khadijah, alitakiwa sasa kusimamia na kuiangalia familia ikiwemo kumuangalia mdogo wake aliyekuwa mdogo wakati huo, Fatmah رضي الله عنها,.

Mwaka 622, Mtume Muhammad ﷺ alihama kutoka Makkah na kwenda kuanza maisha yake katika mji wa Madinah. Baadaye Mtume ﷺ alimuagiza Zayd ibn Harith رضي الله عنه awapeleke Madinah watoto wake, Ummu Kulthum na Fatmah رضي الله عنها,. Maisha ya Madinah kwa ujumla yalikuwa maisha mazuri. Ummu Kulthum رضي الله عنها alipata bahati ya kushuhudia ushindi wa Waislamu katika vita vya Badr, lakini kwa bahati mbaya ni katika siku hiyo hiyo ambayo Waislamu walipata ushindi, Ummu Kulthum رضي الله عنها alipata taarifa za msiba wa dada yake, Ruqayyah رضي الله عنها,.

Baada ya kifo cha Ruqayyah, 'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alimwendea

Uthman ibn 'Affan رضي الله عنه na kumuomba amuoe mwanae Hafsah bint 'Umar رضي الله عنها. Wakati huo, Hafsah alikuwa amefiwa na mume wake ambaye aliuwawa katika vita vya Badr. Lakini 'Uthman رضي الله عنه akakataa. 'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alikwenda kwa Mtume ﷺ akilalamika juu ya Uthman ibn 'Affan kukataa kumuoa mwanae Hafsah bint Umar ibn Khattab رضي الله عنها. Ni katika wakati huu, Mtume ﷺ alimwambia 'Umar ibn Khattab; Mwenyezi Mungu Akipenda, atampa Hafsah mume bora kuliko Uthaman ibn 'Affan رضي الله عنه, na atampa 'Uthman رضي الله عنه mke bora kuliko Hafsah. Baadaye, Hafsah bint Umar ibn Khattab رضي الله عنها aliolewa na Mtume ﷺ; na Mtume ﷺ akamuozesha Ummu Kulthum kwa Uthman. Kwa hakika, mume wa Hafsah ambaye ni Mtume wa Allah ﷺ alikuwa bora kuliko Uthman, na Ummu Kulthum mtoto wa Mtume ﷺ alikuwa mke bora kwa Uthman kuliko Hafsah.

Ni kutokana na kuozeshwa watoto wawili wa Mtume ﷺ katika nyakati tofauti, Uthman ibn 'Affan akaitwa *"Dhu al-Nurayn*" (Mwenye nuru mbili), kwa sababu alioa watoto wawili wa Mtume Muhammad ﷺ.

Ummu Kulthum رضي الله عنها aliishi na mume wake Uthman ibn 'Affan kwa miaka sita (6), hata hivyo hawakujaaliwa kupata mtoto katika ndoa yao. Mama huyu alishuhudia na kushiriki matukio mbalimbali katika historia ya Uislamu katika maisha yake. Miongoni mwa matukio hayo ni misukosuko na mateso waliyokabiliana nayo Waislamu wakiwa bado wako Makkah, tukio la Waislamu kuwekewa vikwazo vya kiuchumi na kijamii, Waislamu kuhamia Madinah na kukombolewa kwa Makkah katika mwaka wa nane (8) Hijiriyah.

Mama huyu alifariki katika mwezi wa Shaaban katika mwaka wa tisa (9) Hijiriyya, mwaka mmoja baada ya kukombolewa kwa Makkah. Alifariki akiwa na umri wa miaka ishirini na tisa (29). Mama huyu alioshwa na mama wawili wacha-mungu, Asma bint Umays na Shafiah bint Abdul Muttalib. Akiwa mwenye huzuni kubwa, Mtume Muhammad ﷺ aliongoza Swala ya jeneza.

Mwili wa Ummu Kulthum uliwekwa juu ya jeneza lililotengenezwa kwa magogo ya mtende. Wakati wa kumzika Ummu Kulthum, Mtume ﷺ akiwa amekaa pembeni ya kaburi la mwanae Ummu Kulthum رضي الله عنها huku akiwa mwenye huzuni kubwa, aliuliza: "Nani kati yenu hakushiriki tendo la ndoa na mke wake usiku wa kuamkia leo?" 'Abu Talhah رضي الله عنه akasema, "Mimi (sikushiriki tendo la ndoa usiku wa kuamkia leo) ewe Mtume wa Allah." Kisha

Mtume ﷺ akamwambia Abu Talhah, "Ingia ndani ya kaburi". Hivyo Abu Talha akaingia na kumzika Ummu Kulthum.

Ummu Kulthum alizikwa pembeni na mahala alipozikwa ndugu yake, Ruqayyah bint Muhammad. Kisha Mtume ﷺ akasema, "Kama ningekuwa nina watoto (wengine) kumi wa kike, bado ningewaozesha kwa Uthman."

# Fatmah bint Muhammad

## Kinachonifurahisha kinamfurahisha Mtume wa Allah ﷺ.

Huyu alikuwa ni mtoto mdogo kabisa kwa umri ukimlinganisha na watoto wengine wa Mtume Muhammad ﷺ, na alikuwa kwa hakika akipendwa sana na Mtume wa Allah ﷺ. Binti huyu aliolewa na binamu yake, 'Ali bin Abi Talib na alikuwa ni mama wa wajukuu vipenzi wa Mtume ﷺ, Hassan na Hussein. Mama huyu alizaliwa katika mji wa Makkah, miaka michache kabla baba yake (Mtume Muhammad ﷺ hajapewa Utume. Pamoja na kuwa wote wawili, Mtume Muhammad ﷺ na Khadijah رضي الله عنها walikuwa tayari wana watoto wengine watatu wa kike kabla ya Fatmah, bado walifurahia sana kuzaliwa kwake. Mama yake alikwenda kinyume na utaratibu uliozoeleka, hakumpeleka mwanae kwenda kunyonyweshwa katika kijiji chochote cha jirani, bali aliamua kukaa na mwanae mchanga na kumnyonyesha yeye mwenyewe. Bi Khadija alikuwa akimpenda sana mwanae, kiasi kwamba alishindwa kumuamini yeyote na kumkabidhi mwanae amlee. Baada ya kupita miaka kadhaa, baba wa Fatmah (Muhammad ﷺ) alipewa Utume na kuwa Mtume wa Mwisho. Binti huyu (Fatmah bint Muhammad), mama yake (Bi Khadijah) na dada zake watatu Zaynab, Ruqayya, na Ummu Kulthum wakaukubali Uislamu. Bi Fatmah alitumia muda na miaka yake ya utoto akiwa chini ya malezi na uangalizi wa wazazi wake.

Kabla ya Mtume Muhammad ﷺ hajatangaza wazi kuwa yeye ni Mtume wa Allah na Mtume wa mwisho, alikuwa ni mtu maarufu sana; mtu aliyekuwa akipendwa na kuheshimiwa na kila mtu miongoni mwa Maquraishi. Lakini mara tu alipoweka wazi kuwa yeye ni Nabii na Mtume wa Mwenyezi Mungu, ghafla maisha yalibadilika. Njia alizokuwa akipita kwa furaha zilizokuwa zenye wasaa, zilianza kuwekewa miba na alikuwa akitupiwa taka kutoka paa za nyumba

zilizokuwa kando ya barabara. Mikakati mbalimbali ilipangwa ili kumuuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Vituko hivi walivyokuwa wakimfanyia Mtume vilikuwa na athari ya kisaikolojia kwa familia ya Mtume Muhammad ﷺ. Fatmah aliishi katika maisha yake ya utoto katika mazingira haya, lakini alionesha ukomavu na aliweza kuvumilia shida na udhalilishaji aliokuwa akifanyiwa baba yake na hata vituko alivyofanyiwa yeye mwenyewe kwa kuwa kwake mtoto wa Mtume kwa ustahmilivu na subira ya hali ya juu.

Fatmah bint Muhammad رضي الله عنها alikuwa binti jasiri aliyekuwa akisimama kumuhami baba yake dhidi ya mashambulizi ya maadui zake. Alikuwa akisimama kumkinga na mashambulizi ya wale waliokusudia kumletea madhara Mtume wa Allah ﷺ wakiwemo Abu Jahl, 'Utbah na Shaybah.

Katika tukio moja, Mtume ﷺ akiwa na maswahaba zake, walikwenda katika eneo lililohifadhiwa katika mji wa Makkah na kuanza kuswali. Wakati huo, makafiri walikuwa wamemaliza kuchinja ngamia. Matumbo na uchafu mwingine wa ngamia aliyechinjwa ulikuwa bado uko katika eneo walilomchinja ngamia yule. Abu Jahl akaingiwa na wazo la kishetani. Akawauliza rafiki zake ni nani kati yao angependa na yuko tayari kubeba uchafu wote ule na kumwagia mgongoni Mtume Muhammad ﷺ. 'Uqbah bin Abi Mu'it, mmoja kati ya rafiki zake wa mbali, aliyekuwepo katika eneo lile akainuka huku akitikisa mabega yake kwa kiburi na ujahili uliopitiliza, huku akisema yeye yuko tayari kufanya kazi ile. Aliinua matumbo na uchafu wote uliotoka tumboni mwa ngamia na kuutupa juu ya mgongo wa Mtume ﷺ wakati Mtume ﷺ akiwa katika hali ya kusujudu kwa ajili ya Allah. Wote kwa pamoja wakaangua kicheko kwa furaha iliyotokana na ujinga walioufanya.

Habari za tukio hili la kusikitisha zilipomfikia Fatmah رضي الله عنها, Fatmah alikimbia haraka kwenda katika eneo lile ambalo tukio hili lilikuwa limetokea. Alijitahidi kuondoa uchafu ule kwa mikono yake midogo, huku akiwa na hasira kutokana na kitendo cha kinyama alichofanyiwa baba yake. Aliwaonya makafiri juu ya kitendo walichokifanya. Mtume ﷺ alipomaliza kuswali, aliinua mikono yake juu na kumuomba Allah huku akimshitakia juu ya wanne hawa Abu Jahl ibn Hisham, Shaybah ibn Rabi'ah, 'Uqbah ibn Abi Mu'it na Umayyah ibn Khalaf. Mashetani hawa wakashikwa na hasira sana, kwa sababu walikuwa wakifahamu kuwa dua iliyoombwa katika viwanja vitukufu vya Makkah, tena iliyoombwa na Mtume ﷺ ilikuwa inajibiwa na Allah.

Siku moja Abu Jahl alikuwa amekaa pamoja na makafiri wengine mbele ya Ka'bah, makafiri hawa walikuwa wanapanga mikakati jinsi gani wanaweza kumuuwa Mtume ﷺ kwa kosa la kuyakataa masanamu yao. Walimchukia sana kwa kutangaza na kueneza ujumbe wa Mwenyezi Mungu mmoja apasaye kuabudiwa kwa haki na kwa kutangaza kuwa yeye (Muhammad ﷺ) ni Mtume wa mwisho ﷺ. Wakati wakiendelea na majadiliano yao, Fatmah akapita eneo lile na aliweza kusikia kile walichokuwa wakikipanga dhidi ya baba yake. Fatmah alipata wasiwasi juu ya kile kinachoweza kumtokea baba yake, hivyo alikimbia haraka sana. Huku akilia alimueleza baba yake kuwa, makafiri walikuwa wameapa kwa jina la mungu wao kuhakikisha kuwa wanamuuwa Mtume ﷺ. Walikuwa wamekubaliana wote kwa pamoja wamshambulie pindi atakapotoka nyumbani kwake. Fatmah رضي الله عنها alimuuliza baba yake, 'nini wanaweza kufanya juu ya njama hizi za kishenzi na kinyama?' Mtume ﷺ alimjibu kuwa, 'awe na imani na Mwenyezi Mungu, na kwamba hakika yeye Allah ndiye Mlinzi wa baba yake.'

Katika tukio jingine, Fatmah alikutana na Abu Jahl ibn Hisham njiani; bila sababu yeyote, Abu Jahl alimnasa kibao usoni bi Fatmah bint Muhammad رضي الله عنها. Bi Fatmah رضي الله عنها alienda moja kwa moja kulalamika juu ya uonevu huu kwa kiongozi wa Maquraishi wa wakati huo, Abu Sufyan. Abu Sufyan aliongozana na Fatmah mpaka eneo ambalo Abu Jahl alikuwa bado amekaa. Abu Sufyan alimuamuru Fatmah na yeye amnase kibao sawasawa na alivyopigwa yeye hapo awali. Fatmah aliporudi na kumsimulia tukio hili baba yake ﷺ alifurahishwa sana na uadilifu na haki aliyoionesha Abu Sufyan katika tukio hili. Mtume ﷺ akamuombea dua kwa Allah, ili Allah Amjaalie na kumuongoza kuutambua Uislamu na kuukubali kama dini ya kweli na ya haki. Dua ya Mtume ﷺ ilikubaliwa na baadaye Abu Sufyan alisilimu na kuchukua ahadi ya utii kwa Mtume Muhammad ﷺ.

Miaka saba ilipita toka Mtume ﷺ aweke wazi kuwa yeye ni Mtume wa Allah. Pamoja na jitihada na vitimbi walivyokuwa wakifanya wakubwa na waheshimiwa wa Makkah, bado walikuwa wameshindwa kumfanya Mtume ﷺ aache kazi ya kufikisha ujumbe au japo kuzuia ujumbe wenyewe usiwafikie watu na kuwafanya wamuunge mkono Mtume ﷺ. Watu waliokuwa wameukubali Uislamu na kusilimu, walikuwa wakipokea mateso na manyanyaso ya kila aina kutoka kwa makafiri. Wakati wanasilimu Hamzah ibn

'Abdul Muttalib na 'Umar ibn Khattab رضي الله عنهما, watu wote wa mji wa Makkah walipatwa na mshituko mkubwa. Watu walianza kuwataka viongozi wao kuchukua hatua. Hatua waliyoichukua viongozi wa makafiri ilikuwa kuwawekea vikwazo Waislamu, kiuchumi na kijamii. Walizuiliwa hata kupata maji na chakula. Vikwazo hivi walivyokabiliana navyo Waislamu katika *Shi'b* Abi Talib vilidumu kwa muda wa miaka mitatu.

Mama aliye tajiri kuliko wanawake wote katika Makkah, Khadijah, na wanae wakasimama imara mithili ya mwamba imara kumuunga mkono baba yao. Walikuwa wako tayari kutoa maisha yao na uhai wao kwa ajili ya harakati za baba yao. Na hivi ndivyo ilivyokuwa kwa binti mdogo kwa umri wakati huo, Fatmah رضي الله عنها. Msingi huu imara uliweza kuathiri na kujenga msingi imara wa akili yake, imani yake na afya ya mwili wake kwa muda wote wa maisha yake.

Baada tu ya vikwazo kuondolewa, Mtume ﷺ, Fatmah رضي الله عنها na dada zake wakaingia katika majonzi makubwa ya kufiwa na mama yao kipenzi – Bi Khadijah رضي الله عنها. Si muda mrefu kutoka hapo, wakampoteza tena mtu aliyekuwa akiwapa nguvu na kuwaunga mkono, mtu muhimu katika maisha yao, baba yao mdogo, Abi Talib. Fatmah رضي الله عنها alikuwa akikabiliana na matukio haya mazito na magumu huku akiendelea kumuunga mkono na kusimama na baba yake. Ni katika muda huu pia, Mtume ﷺ alikwenda katika mji wa Ta'if kupeleka ujumbe wa Allah (Uislamu) kwa wakazi wa huko. Wenyeji wa mji ule walimkaribisha kwa kumshambulia na mawe na aliondoka huku amejeruhiwa huku akitokwa na damu kutokana na mashambulizi. Hata hivyo, alimuomba Allah awaongoze watu wale katika njia iliyonyooka, njia iliyokuwa ya sawasawa.

Ummu Kulthum na Fatmah رضي الله عنهما walianza kulia kwa uchungu mara walipomuona baba yao akiwa katika hali ile. Kwa mapenzi makubwa, Mtume ﷺ aliwafuta machozi na kuwabembeleza. Aliwaambia kuwa, ilikuwa ni jambo lisiloepukika na kwamba Allah Atamsaidia katika kueneza dini yake na kuifanya izishinde dini zote zisizokuwa sahihi. Wakati mwepesi utakuja baada ya kupitia hali ngumu na ya misukosuko. Mara ziliwafikia habari njema, balozi wa Mtume ﷺ katika mji wa Madinah, Mus'ab ibn 'Umair alikuwa anafanya kazi yake vizuri na kwamba watu wengi walikuwa wanaukubali na kuingia katika Uislamu. Walimualika na kumuomba Mtume Muhammad ﷺ ahamie na kuishi katika

mji wao wa Madinah, huku wakimuahidi kuwa watafanya kila linalowezekana kumsaidia kazi ile ya kueneza Uislamu. Baada ya kupata maelekezo na ruhusa kutoka kwa Allah, Mtume ﷺ akakubali mwaliko na kuhamia Madinah. Wakati anahamia Madinah, Mtume ﷺ aliwaacha watoto wake wawili wa kike wakiwa na mama yao (Mke wa Mtume ﷺ) Sawdah bint Zam'ah رضي الله عنها.

Baadaye, aliagiza nao wahamie Madinah; hivyo wanawake hawa watatu ni miongoni mwa Waislamu waliopata ujira wa kuhama kwa ajili ya Allah. Hata hivyo, makafiri hawakuvumilia na kukubali kuwaona wote watatu wakihama kwa pamoja. Baadhi ya makafiri walienda kuwasubiri na kuwavizia nje ya mji wa Makkah. Mmoja kati ya vijana washenzi katika Maquraishi, Huwayrith ibn Naqith akaanza kumfanyia fujo ngamia aliyekuwa amewabeba mabinti wa Mtume ﷺ, na ngamia yule akawaangusha mabinti wale wawili, watoto wa Mtume ﷺ. Huwayrith ibn Naqith alivyoona vile, akakimbia.

Walipofika walikokuwa wakielekea (Madinah), Mtume ﷺ aliwapokea. Alifurahi sana kuwaona wamefika na kuwapokea wakiwa salama. Wale ambao Allah Amewahifadhi, hakuna mwenye uwezo wa kuwadhuru.

Fatmah رضي الله عنها alipofikisha umri wa miaka kumi na nane (18), watu wengi maarufu walitaka kumuoa. Hata hivyo, Mtume ﷺ alisema alikuwa anasubiri maelekezo kutoka kwa Allah. Siku moja 'Ali ibn Abi Taalib رضي الله عنه alikuja nyumbani kwa Mtume ﷺ, alikuwa akionekana kama mtu mwenye aibu na kana kwamba kulikuwa kuna kitu kinamzuia asiseme kile alichokusudia kusema. Lakini Mtume ﷺ alifahamu kile alichokidhamiria na akamuuliza kama alikuwa amekuja kwa ajili ya kumposa Fatmah. 'Ali رضي الله عنه akajibu, 'Ndiyo'. Mtume ﷺ akamuuliza Fatmah رضي الله عنها alikuwa ana maoni gani kuhusu posa ile kutoka kwa Ali ibn Abi Taalib رضي الله عنه. Fatmah رضي الله عنها alianza kulia kimya kimya (bila kutoa sauti). Mtume ﷺ alimwambia Fatmah kuwa, 'Ali رضي الله عنه alikuwa ni mwanazuoni, mtu rahimu na kijana mwenye busara. Fatmah akakubali uamunzi wa baba yake. Mtume ﷺ akamuuliza 'Ali kama ana fedha za kutoa kama mahari ya Fatmah. 'Ali رضي الله عنه alijibu kuwa, bila shaka Mtume ﷺ anayafahamu maisha yake kuanzia mwanzo mpaka mwisho; hivyo Mtume ﷺ anafahamu hali ya ki-uchumi aliyonayo Ali. Kisha Mtume ﷺ akamuuliza ilipo ngao yake, na kumwambia kuwa, hiyo ndiyo itakuwa mahari ya Fatmah. 'Ali رضي الله عنه alimtuma msaidizi wake kwenda kuiuza ngao ile sokoni na akapata Dirham mia nne kutokana na kuuza ngao ile. Alimkabidhi fedha zile Mtume ﷺ

na Mtume ﷺ akamwambia Ali رضي الله عنه azihifadhi fedha zile na azitumie kununulia mahitaji ya nyumbani na manukato au uturi kwa ajili ya harusi. Kisha aliwaalika maswahaba wahudhurie sherehe ya ndoa.

Ali رضي الله عنه akatoa hotuba fupi, akasema: 'Sifa zote njema zinamsahiki Allah. Tunamshukuru kwa neema zake na baraka zake. Nashuhudia kuwa, hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, Tunamuomba Allah Atuzidishie neema zake na baraka zake. Mtume ﷺ ameniozesha binti yake, Fatmah na mahari yake ni Dirham Mia Nne. Wote mliohudhuria msikilizeni Mtume ﷺ kile atakachokisema na muwe mashahidi.'

Baada ya hapo, Mtume ﷺ akamuhimidi na kumshukuru Allah na kusoma hotuba ya ndoa, baada ya kuomba idhini kwa mwanae Fatmah. Alitangaza kiwango cha mahari na akawaambia wale wote waliohudhuria kuwa, Allah Amemuamuru amuozeshe Fatmah رضي الله عنها kwa 'Ali رضي الله عنه. Baada ya hapo aliwaombea dua na kuwatakia maharusi maisha mema katika ndoa yao.

Mahitaji muhimu yalinunuliwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani walikokuwa wanakwenda kuanza maisha ya pamoja, 'Ali na Fatmah. Kitanda, mto uliojazwa na majani makavu ya mtende, sahani, kikombe, chombo cha kuhifadhia maji na jiwe la kusagia. Hivi ndio vitu vichache ambavyo mtoto wa Mtume ﷺ aliondoka navyo kwenda kuanza maisha na mumewe. Naam! Hakika zawadi bora ni ucha-Mungu! Sio mali wala vitu vya thamani na vya kifahari.

Nyumba yao ilikuwa mbali kidogo na ulipokuwa msikiti wa Mtume ﷺ. Mtume ﷺ alitamani mwanae aishi karibu na alipokuwa akiishi yeye Mtume ﷺ, ili aweze kuwa anamuona mara kwa mara. Swahaba mmoja, Harithah ibn Nu'man Ansari, alipofahamu hamu ya Mtume ﷺ kuishi karibu na mwanae, akiwa mwenye unyenyekevu, heshima na adabu, alienda kwa Mtume ﷺ, na kumwambia kuwa yeye (Harithah ibn Nu'man) ana nyumba kadhaa zilizokuwa jirani na Msikiti wa Mtume na kumwambia Mtume ﷺ achague nyumba yeyote aitakayo. Mtume ﷺ akafurahi sana kwa zawadi hii, na akachagua nyumba moja kwa ajili ya mwanaye Fatmah رضي الله عنها; hivyo, 'Ali na Fatmah رضي الله عنها wakahamia katika nyumba ile na kuendelea na maisha ya kawaida. Ilikuwa ni jambo la kawaida kabisa kwa Fatmah kusaga ngano kwa mikono yake, kuchota maji kutoka kisimani na kupika chakula kwa ajili yao.

Huku akiwa ameathirika sana na vikwazo walivyowekewa Waislamu kwa

takriban miaka mitatu, Fatmah رضي الله عنها hakuwa mwenye afya njema sana. Hivyo alikuwa akichoka sana kutokana na kazi hizi ngumu. Katika tukio moja baada ya vita, jeshi la Waislamu lilikusanya ngawira nyingi vikiwemo, fedha, mapambo yenye thamani na mateka (wanaume kwa wanawake). 'Ali رضي الله عنه akapendekeza kwamba, aende kwa Mtume ﷺ na kumuomba mjakazi wa kumsaidia.

Fatmah رضي الله عنها alikubali na kwenda kwa baba yake na kumuomba mjakazi mmoja wa kumsaidia. Alipofika, hakumkuta baba yake nyumbani, hivyo akaacha ujumbe wake kwa mama wa Waumini, Aishah. Usiku kabla ya kwenda kulala, baba yake alikwenda kumjulia hali mwanae Fatmah رضي الله عنها. Mtume ﷺ akamwambia Fatmah kuwa, atampa kilichokuwa bora zaidi kuliko mjakazi. Kisha Mtume ﷺ akamfundisha maneno katika kumtukuza Mwenyezi Mungu Mtukufu, na akamwambia kuwa maneno yale ni bora kuliko mjakazi yeyote. Kisha alimfundisha kusema *Subhanallah* (Ametakasika Allah) mara thelathini na tatu, *Alhumdulillah* (Sifa zote njema ni zake Allah) mara thelathini na tatu, na *Allah-u-Akbar* (Mwenyezi Mungu ni Mkubwa) mara thelathini na tatu.

Fatmah رضي الله عنها akatumia maisha yake yote kwa ajili ya Allah na katika kumtumikia Allah. Siku zote alikuwa mwenye subira na mwingi wa shukurani kwa Muumba wake. Hata siku moja hakuwahi kutoa maneno ya kulalamika, bila kujali mazito na magumu kiasi gani alikuwa akipitia au alikuwa akikabiliana nayo. Hakukuwa na kitu chochote katika dunia kilichokuwa chenye kumvutia au kumshawishi. Kauli mbiu yake siku zote ilikuwa 'kuutumikia Uislamu'. Katika vita, Fatmah alikuwa mstari wa mbele katika kuwahudumia majeruhi na wagonjwa katika jeshi la Waislamu. Baba yake alipojeruhiwa katika vita vya Uhud, ni mwanae Fatmah رضي الله عنها aliyeunguza majani makavu na kutumia majivu yake kudhibiti damu isiendelee kutoka. Kuna hadithi katika Sahih Al-Bukhari inayosimulia kuwa, Mtume ﷺ alipoulizwa anampenda nani zaidi duniani, alimtaja binti yake huyu mdogo, Fatmah رضي الله عنها.

Akimzungumzia Fatmah رضي الله عنها, Aishah رضي الله عنها anasema, alikuwa akifanana sana na baba yake. Sio tu kwamba alikuwa anafanana nae kwa sura, bali uzungumzaji wake, kukaa kwake, kusimama kwake na kutembea kwake pia; uchache wa maneno ni kwamba alikuwa akifanana naye kwa tabia na mwenendo, vyote vilikuwa vinafanana na Mtume ﷺ. Kila baba yake alipomtembelea, Fatmah رضي الله عنها alikuwa akimpokea na kumbusu paji lake

la uso kwa heshima kubwa. Fatmah na baba yake walikuwa watu wa karibu sana na wakipendana. Fatmah رضي الله عنها alipomtembelea baba yake, baba yake alikuwa akisimama na kumpokea. Mtume ﷺ alikuwa akimuona Fatmah ana huzuni, basi Mtume رضي الله عنها pia alikuwa akiingiwa na huzuni, na alikuwa akimuona Fatmah رضي الله عنها akiwa mwenye furaha, basi na yeye Mtume ﷺ alikuwa mwenye furaha.

Siku moja Mtume ﷺ alipata taarifa kuwa kulikuwa na kutoelewana baina ya 'Ali na Fatmah رضي الله عنها. Akiwa njiani kuelekea nyumbani kwao, Mtume ﷺ alionekana mtu aliyetatizika na mwenye huzuni. Na alipokuwa akitoka nyumbani kwao (Fatmah na Ali رضي الله عنهما), alionekana mwenye furaha. Baadhi ya maswahaba wakamuuliza juu ya hili; Mtume ﷺ akajibu akisema, aliweka sawa baadhi ya tofauti baina ya watoto wake wawili awapendao na furaha yao imemfanya nae awe mwenye furaha.

Siku moja 'Ali ibn Abi Taalib رضي الله عنه alikusudia kumuoa binti wa Abu Jahl. Fatmah رضي الله عنها akapata habari juu ya dhamira hii na akamwambia baba yake (Mtume ﷺ) kuwa 'Ali رضي الله عنه ana mpango wa kuoa katika familia ya Abu Jahl; Mtume ﷺ hakufurahishwa na taarifa ile. Mtume ﷺ alikwenda msikitini na akatoa hotuba akisema, Fatmah رضي الله عنها ni sehemu ya moyo wake na kwamba kila kinachomfanya asiwe na furaha yeye hakifurahii. Kisha Mtume ﷺ akasema, binti wa Mtume wa Allah ﷺ na binti wa adui yake hawawezi kuolewa na mtu mmoja. Ali ibn Abi Taalib رضي الله عنه akafuta dhamira yake na kumuomba radhi Fatmah kwa usumbufu na machungu yeyote ambayo huwenda amemsababishia.

Siku moja 'Ali رضي الله عنه alimuuliza Mtume ﷺ nani alikuwa mtu wake wa karibu zaidi, yeye Ali au Fatmah? Mtume ﷺ akamjibu kuwa: "Nampenda zaidi Fatmah, lakini wewe ('Ali رضي الله عنه) ni wa karibu zaidi kwangu." Ilikuwa kana kwamba Mtume ﷺ alikuwa akitumia diplomasia kuwaridhisha wote, lakini ukweli ni kwamba Mtume ﷺ alikuwa akiwapenda wote sana.

Mtoto wao wa kwanza alizaliwa mwaka wa tatu baada ya kufanyika kwa Hijrah baada ya Mtume ﷺ kuhamia Madinah. Mtume ﷺ alipopata habari, alifurahi sana na mara moja akaondoka na kwenda kumuona mtoto. Alimpa jina la Hassan na kumuadhinia. Siku ya saba kichwa cha mtoto yule (Hassan) kilinyolewa nywele, na nywele zile zilipimwa uzito wake. Thamani ya fedha sawa na uzito wa nywele zile ilitolewa sadaka kwa watu mafakiri na masikini.

Katika mwaka wanne (4) wa Hijirah, mtoto wa pili alizaliwa. Mtume ﷺ akamwita mtoto yule Hussein, na kwa mtoto huyu pia akamuadhinia katika masikio yake kama alivyofanya kwa mtoto wa kwanza. Inasemekana mtoto wa tatu alizaliwa na kuitwa Muhsin, hata hivyo mtoto huyu alifariki akiwa bado mchanga. Mtume ﷺ aliwapenda sana watoto hawa wawili. Mtume ﷺ alikuwa akisema, Hassan na Hussein ni kama maua na watakuwa viongozi wa vijana Peponi. Usamah ibn Zayd رضي الله عنه anasema, alimuona Mtume ﷺ akiwa amebeba kitu alichokihifadhi kwa kukizunguushia ndani ya kitambaa. Usamah akamuuliza Mtume ﷺ alikuwa amebeba nini, Mtume alifungua kitambaa kile. Usamah aliona nini? Walikuwa ni watoto hawa wawili waliokuwa wamebebwa kwa pamoja katika mikono ya babu yao.

Katika mwaka wa 5 baada ya Hijrah, mtoto wa kike alizaliwa nyumbani kwa 'Ali na Fatmah; Mtume ﷺ akamwita mtoto huyu Zaynab رضي الله عنها; mwaka wa 7 baada ya Hijirah, mtoto mwingine wa kike akazaliwa, na Mtume ﷺ akamwita mtoto huyu Ummu Kulthum. Zaynab bint 'Ali رضي الله عنهما alipokuwa mkubwa, aliolewa na 'Abdullah Ibn Ja'far Ibn Abi Talib رضي الله عنهما. Na Ummu Kulthum aliolewa na 'Umar Ibn Khattab رضي الله عنهما., na wakajaaliwa kupata watoto wawili Zayd na Ruqayyah رضي الله عنهما. Wakati fulani Imam Ahmad aliulizwa kuhusu maoni yake juu ya 'Ali رضي الله عنه na watu wa familia yake; Alijibu akisema, hadhi yao katika historia ya Uislamu haiwezi kulinganishwa. Kwa mujibu wa Qur'an, Mwenyezi Mungu Ameitakasa familia hii kutokana na kila aina ya machafu, madhambi ya kutokuwa na imani, kutomtii Allah na Mtume wake na madhambi mengine.

Ibn 'Abdullah رضي الله عنه anasema, kila Mtume ﷺ aliporejea kutoka safari au kila akirejea kutoka katika vita, alikuwa kwanza akienda msikitini kwake Madinah na kuswali rakaa mbili, kisha alimtembelea na kumjulia hali Fatmah رضي الله عنها kisha akienda kwa wake zake.

Kuna tukio limesimuliwa katika kitabu *Al-Bidayah wa An-Nihayah*, kwamba Fatmah aliwahi kuandaa chakula, mkate na nyama iliyochomwa. Fatmah رضي الله عنها aliweka chakula hiki katika sahani na kufunika chakula kile vizuri kwa kitambaa. Kisha alituma ujumbe kumwita baba yake aje kula. Baba yake alipofika, Fatmah رضي الله عنها aliondoa kitambaa kile alichokitumia kufunika chakula. Alipoondoa kitambaa kile alishtuka na kushangaa kuona sahani ile ilikuwa imejaa mkate na nyama nyingi sana tofauti na alivyokuwa ameandaa.

Hata hivyo alifahamu vema kuwa, chakula kile kingi kilikuwa kimetoka kwa Allah. Alimshukuru Allah kwa rehema zake, kisha alianza kugawa chakula kile baada ya kutamka jina la Allah. Mtume ﷺ alipoona chakula ni kingi sana, alitabasamu na kumuuliza mwanae Fatmah رضي الله عنها, nani alimletea chakula chote kile? Fatmah رضي الله عنها akajibu chakula kile amepewa na Allah; na kwamba hakika Allah humruzuku (humtosheleza) amtakaye bila ya hesabu. Mtume ﷺ akatabasamu na kula chakula yeye, binti yake na familia yao yote. Hata hivyo bado chakula kingi sana kilibakia, ambacho Mtume ﷺ aliagiza kipelekwe kwa wake zake Mtume ﷺ mama wa waumini. Nao walikula mpaka wakatosheka, na chakula kikagawiwa kwa majirani.

## Wanawake ambao Maisha yao Yanalandana na Maisha ya Mtume ﷺ

**Fatmah Bint Al - Khattaab**

**Sumayyah Bint Khayyaat**

**Al-Khansaa, Tamadur binti Amr ibn Shareed**

**Ash - Shifaa binti 'Abdullah**

**Ar-Rumaysa binti Milhan (Ummu Sulaym) Al-Ansariyyah**

**Asmaa binti Abu Bakr As-Siddiiq**

**Asma binti Umays**

**Asmaa binti Yaziid**

**Atika Binti Zaid**

**Khawlah Bint Al-Azwari**

**Nusaybah binti Ka'b - Ummu 'Umarah**

**Safiyyah Binti Abdul Muttalib**

**Lubabah binti al-Harith, Ummu Fadl**

**Ummu Hani, Fakhita binti Abi Taalib**

**Ummu Hiram binti Milhan**

# Fatmah Bint Al - Khattaab

## Dada wa Khalifa Umar ibn Al-Khattab

Fatmah bint al-Khattab رضي الله عنها anasimulia kuwa: Nilimsikia Mtume wa Allah ﷺ akisema: *"Ummah wangu utaendelea kubakia katika kheri kwa muda wote ambao watu hawatozidiwa na mapenzi katika kuipenda dunia, na katika muda ambao Ummah wangu utakuwa umesalimika na wanazuoni waovu, wasomaji wa Qur'an wasiofahamu na kuizingatia maana yake na kuwepo kwa viongozi madhalimu. Ikiwa haya (kuipenda sana dunia, kuwa na wanazuoni waovu, wasomaji wa Qur'an wasiojua maana yake na viongozi madhalimu) vitatokea miongoni mwao, basi nachelea Allah anaweza kuwajumuisha wote katika adhabu."*

Lakini ni nani hasa muhusika aliyepokea na kusimulia hadithi hii tukufu ya Mtume Muhammad ﷺ?. Kaka wa mama huyu ni 'Umar ibn al-Khattab رضي الله عنه, Khalifa wa pili wa Waislamu na Kamanda wa Waumini. Moja katika heshima aliyokuwa nayo Fatmah bint al-Khattab ni kwamba, habari zake hutajwa kila inapozungumzwa kusilimu kwa kaka yake 'Umar ibn al-Khattab رضي الله عنه. Kila ambapo jina la mume wake, Sa'eed ibn Zayd رضي الله عنه ambaye ni mmoja kati ya maswahaba wakubwa wa Mtume ﷺ waliobashiriwa Pepo linapotajwa, basi jina la mama huyu pia hutajwa. Kila linapotajwa jina la Khabbaab ibn al-Aratt, swahaba mkubwa, msomaji mkubwa wa Qur'an na mwalimu wa Waislamu, basi jina la mama huyu pia hutajwa. Kila inaposomwa Surah Ta-Ha, bila shaka Fatmah bint al-Khattab رضي الله عنها pia hukumbukwa. Kutajwa kwake kunatokana na athari ya kusomwa kwa Surah hii na namna ilivyobadilisha hasira alizokuwa nazo kaka yake, Umar ibn Khattab رضي الله عنه na hatimaye kuukubali Uislamu na kusilimu na hivyo kubadili kabisa historia yake na kwa hakika historia ya Uislamu. Hii ni kutokana na fadhila zake Allah

na dua aliyoiomba Mtume ﷺ pale aliposema: *"Ewe Allah! Upe nguvu Uislamu kutokana na yeyote umpendaye miongoni mwa 'Umar wawili: 'Umar ibn al-Khattab na 'Amr ibn Hishaam."*

Ili kujua mchango wake halisi alioutoa wakati wa Mtume ﷺ, ni lazima turudi nyuma kidogo katika historia ili kujua msingi ambao ulijengwa na familia hii ya Kiislamu katika zama za mwanzo za Uislamu, familia ya Fatmah bint al-Khattaab رضي الله عنها.

Baba wa mume wa Fatmah رضي الله عنها alikuwa ni Zayd ibn 'Amr ibn Nawfal. Kabla hata ya kuja kwa Uislamu, bwana huyu alijitenga na njia (mfumo wa maisha) waliokuwa wakiufuata Maquraishi. Hivyo hakuwa akiamini na kuabudu yale waliyokuwa wakiamini Maquraishi.

Asmaa' bint Abu Bakr رضي الله عنها anasimulia kuwa, alimuona na kumsikia Zayd ibn 'Amr ibn Nawfal akiwa ameegemea ukuta wa Ka'bah akisema,

"Enyi Maquraishi! Naapa kwa Yule ambaye anamiliki roho yangu (uhai wangu)! Hakuna yeyote katika ninyi ambaye anafuata dini na imani ya Ibrahiim isipokuwa mimi."

Al-Bukhari, an-Nasaai na al-Baghawi pia wamesimulia kuwa Zayd alikuwa akiwanusuru watoto wa kike waliozaliwa wasizikwe wakiwa hai na alikuwa akimwambia kila aliyetaka kumuuwa mtoto wake wa kike kwamba:

"Usimuuwe mwanao, Mimi nitalipa gharama zote za kumlea mtoto huyo mpaka atakapo kuwa mkubwa."

Ibn Is-haaq anaongeza kusema kuwa: Na alikuwa akisema: "Ewe Mwenyezi Mungu! Kama ningeifahamu njia sahihi ya kukuabudu, basi ningekuabudu kupitia njia hiyo. Lakini siifahamu njia hiyo. Kisha alikuwa akisujudu kwenye mtende wake."

Mussa ibn U'qbah anasimulia katika simulizi zake kuwa: "Nilimsikia mmoja kati ya wale ninaowaamini akisema kuwa, Zayd ibn Amr alikuwa akiwashutumu na kuwalaumu watu waliokuwa wakichinja mnyama kwa ajili ya asiyekuwa Mwenyezi Mungu."

Bukhari anasimulia hadithi aliyoipokea kutoka kwa Saleem ibn 'Abdullah ibn 'Umar, ambaye aliipokea kutoka kwa baba yake akisema: "Zayd ibn 'Amr

alikwenda Syria akitafuta dini ya kweli. Mayahudi na Wakristo wakamfahamisha kuwa dini ya kweli ni dini ya Ibrahiim na yeye (Zayd) hakuwa Myahudi wala Mkristo. Aliinua mikono yake na kusema: "Ewe Mwenyezi Mungu! Nakufanya kuwa shahidi kuwa mimi nafuata dini ya Ibrahiim."

Pia anasimulia hadithi maarufu juu ya yeye kukutana na Myahudi ambaye alimwambia kuwa: "Usifuate dini yetu usije ukapatwa na hasira za Mwenyezi Mungu", na alikutana na Mkristo aliyemuambia kuwa, "Usifuate dini yetu usije ukapata laana kutoka kwa Mwenyezi Mungu".

Al–Fakihi pia anasimulia kutoka kwa 'Amr ibn Rabii'ah ambaye anasema kwamba: "Nilikutana na Zayd ibn 'Amr wakati akiwa nje ya Makkah akiwa njiani kuelekea Hira, na akaniambia kuwa,

"Amr, mimi nimeachana na njia wanayoifuata watu wangu na kufuata dini ya Ibrahiim na Ismaa'eel. Ibrahiim alikuwa akiswali akielekea nyumba ile (akimaanisha Ka'bah). Na ninatarajia kuja kwa Mtume kutokana na kizazi cha Ismaa'eel na kutoka katika kizazi cha 'Abdul-Muttalib. Siamini kama nitakuwa hai mpaka atakapotokea Mtume huyu ili nimuamini na kumfuata na kuthibitisha ukweli wake kuwa kwa hakika yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu."

'Amr ibn Rabee'ah anaongeza kusema kuwa, "Nilipoingia katika Uislamu, nilifikisha salamu zake kwa Mtume ﷺ. Naye (Mtume ﷺ) alimrejeshea salamu na kumuombea dua kwa Allah Amrehemu. Kisha Mtume ﷺ akasema, "Nilimuona akiwa Peponi akiburuza koti lake."

Al–Baghawi anasimulia kutoka kwa Ibn 'Umar رضي الله عنه ambaye anasema kwamba: Saeed ibn Zayd na 'Umar رضي الله عنهما walimuuliza Mtume wa Allah ﷺ kama ilikuwa ni sahihi kumuombea msamaha Zayd ibn 'Amr na alijibu ndiyo.

At–Tayalisi anasimulia katika kitabu chake kwamba Sa'eed ibn Zayd alimuuliza Mtume ﷺ: "Baba yangu alikuwa kama ulivyomuona na kama ulivyojulishwa na Allah. Je, naweza kumuombea msamaha?" Mtume ﷺ akajibu: *"Ndiyo, na atafufuliwa siku ya Kiyama akiwa peke yake kama Ummah au taifa linalojitegemea."*

Ni kutokana na msingi huu madhubuti, Sa'eed aliibuka na kukua kama pambo lenye thamani kubwa kutokana na malezi aliyopata. Alikuwa miongoni

mwa watu waaminifu na wa kweli kwa Mola wao; watu waliojitolea mali zao na nafsi zao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wakitafuta radhi Zake.

Fatmah bint Al–Khattab رضي الله عنها alikuwa mama wa Kiislamu mwenye moyo safi na ambaye nafsi yake iliepuka kila aina ya upotofu na ujinga. Ucha-Mungu wake uliendana kabisa na ucha-Mungu aliokuwa nao Saeed رضي الله عنه, kisha wacha-Mungu hawa wawili wakaunganishwa na ndoa, ndoa ambayo ilizaa familia halisi ya Kiislamu. Familia iliyokuwa na imani thabiti ambayo hapo baadaye ilikuja kuzaa matunda.

Inatosha kuwa heshima kwao, kwa Allah kuwafanya wao kuwa sababu ya ‘Umar ibn Khattab رضي الله عنه kuukubali Uislamu na kusilimu. ‘Umar ibn Khattab, swahaba madhubuti ambaye baadaye alikuja kuwa Khalifa wa pili na Kamanda wa Waislamu. Hakika Allah humuongoza amtakaye katika njia iliyokuwa ya sawa.

Hatutoweza kuelezea historia yote kama ilivyo, hata hivyo tutajitahidi kugusa na kuzungumzia baadhi ya nukta na matukio muhimu kwa lengo la kuwezesha msomaji aweze kuchota mafunzo na mazingatio kutoka kwa mama huyu. Ni muhimu sana kuzingatia kuwa, kuukubali Uislamu na kusilimu kwa ‘Umar ibn Khattab hakukuwa tukio la kawaida.

Umar ibn Khattab رضي الله عنه aliukubali Uislamu na kusilimu siku chache baada ya kusilimu kwa Hamzah. Baadhi ya mapokezi yanasema ilikuwa kiasi kama cha siku tatu toka kusilimu kwa Hamzah au zaidi ya hapo kidogo tu.

Mtu akipewa uwezo wa kuusimamisha moyo usifanye kazi au mapigo ya moyo yasimame kwa muda, basi mtu huyo huwa na uwezekano mkubwa wa kuweza kuurejesha moyo katika utendaji wake wa kawaida na kusukuma damu kwa namna inavyopaswa! Hii ina maana kuwa, adui hatari anayekufahamu vema anaweza kuwa mtu wa msaada kwako ikiwa atabadilika na kuwa upande wako. Kwa maoni yetu, kusilimu kwa Hamzah na ‘Umar kuliwatikisa sana Maquraishi. Hata hivyo nguvu ya shetani iliyokuwa imejikita katika nyoyo zao, iliwafanya wazidi kufuru na kukanusha ukweli badala ya kutafakari na kuitambua haki.

‘Umar alikuwa amekaa chini katika viwanja vya Ka’bah akijadiliana mambo mbalimbali na viongozi wa Kiquraishi. Walikuwa wanatatizwa na kuzidi kuenea kwa Uislamu, kuongezeka kwa wafuasi wa Muhammad ﷺ na msimamo

wao thabiti. Walikuwa wakiwachukia kwa kiwango cha juu kabisa kwa kukataa kwao kuendelea kuamini masanamu, mfano wa masanamu ya al-Laat, al-'Uzza, al-Manaat na wengineo. Wakati huo, 'Umar alikuwa bado hajasilimu. Umar akashikwa na hasira sana. Alisimama ghafla kwa hasira na kuamua kuwa, sasa alikuwa yuko tayari kwenda kumuuwa Muhammad ﷺ na kuwanusuru Maquraishi kutokana na tabu ambayo Muhammad ﷺ na dini yake walikuwa wakiwapa Maquraishi.

Akiwa njiani kuelekea kwa Mtume ﷺ, alikutana na mtu mmoja kutoka kabila la Banii Makhzum, ambaye aliweza kuona sura ya 'Umar na kujua kuwa alikuwa mtu mwenye hasira na aliyehamaki. Yule mtu akamuuliza 'Umar ibn Khattab , wapi alikuwa anaelekea? 'Umar akajibu kuwa, "Nakwenda kwa Muhammad ibn 'Abdillah! Nataka nimuuwe na kuwafanya Waarabu waepuke fitina aliyokuja nayo!" Yule mtu akamwambia: "Hivi unadhani ukoo wa 'Abd al-Manaaf watakuacha ubakie salama ikiwa utamuuwa Muhmmad ﷺ?!... Safisha nyumba yako kwanza!"

'Umar akapatwa na mshangao na kumuuliza yule mtu kwa mshangao mkubwa, "Una maana gani kusema hivyo, na unamkusudia nani?" Yule bwana akamjibu kuwa: "Dada yako Fatmah na shemeji yako Sa'eed ibn Zayd. Wote wamemuamini Muhammad ﷺ na wanamfuata."

'Umar ibn Khattab akasema kwa hasira, "Ole wao niwatie mkononi!"

Umar ibn Khattab akabadili muelekeo na kuamua kuelekea nyumbani kwa dada yake Fatmah, akiwa ameshika upanga wake huku akilizunguusha hewani kama ng'ombe dume aliyejeruhiwa huku akiunguruma kama simba kwa hasira.

Mpaka wakati huo, kazi ya kulingania Uislamu ilikuwa bado inafanywa kwa siri ukiacha Waislamu wachache ambao walikuwa wakiitangaza imani yao hadharani kama vile Abu Bakr رضي الله عنه, kijana mdogo 'Ali ibn Abu Taalib, Sa'd ibn Abi Waqqas, na Zubayr ibn Awwaam رضي الله عنه. Mtume wa Allah ﷺ aliruhusu dini kutangazwa kwa siri wakati huo ili kulinda imani, kulinda uhai wa Waislamu wapya na kuepuka vikwazo ambavyo vingeweza kukwamisha kazi ya Da'wah katika hatua zake za mwanzo. Hili lilikuwa ni jambo la lazima ili kufikia mafanikio yaliyokuwa yanakusudiwa.

Mmoja kati ya watu waliokuwa wakieneza mafundisho haya ya Mtume ﷺ alikuwa ni Khabbaab ibn Al-Aratt. Huyu alikuwa anahusika katika kufanya

mawasiliano na Sa'eed na Fatmah. Alikuwa akikusanya mafundisho ya Uislamu kutoka kwa Mtume ﷺ na alikuwa akiwafundisha kila alichokuwa amefundishwa au kukisikia kutoka kwa Mtume ﷺ.

'Umar ibn Khattab alipowasili nyumbani kwa dada yake na shemeji yake, akiwa bado ndio kwanza amefika mlangoni, alisikia minong'ono lakini hakuweza kuyaelewa vizuri maneno yaliyokuwa yakizungumzwa. Aligonga mlango kwa fujo huku akipaza sauti afunguliwe.

Mara moja Khabbaab akakimbilia katika moja ya kona za nyumba ile na kujificha. Fatmah bint Khattab akaficha maandiko ya Qur'an waliyokuwa wakisoma na mume wake akaenda haraka kufungua mlango na kumruhusu 'Umar aingie. Walitambua kuwa aliyekuwa anagonga alikuwa ni 'Umar ibn Khattab kutokana na namna alivyogonga mlango kwa fujo na walitambua kuwa alikuwa amekuja akiwa na hasira na kwamba alikuwa amekuja akiwa amejiandaa kwa shari kutokana na sauti yake na vurugu.

Umar akawauliza, "Minong'ono niliyoisikia ilikuwa ni ya nini?"

Walikanusha kuwa, kulikuwa hakuna minong'ono yeyote.

Kisha akaongea nao kwa ukali tena kwa kufoka na huku akiwatisha kuwa atawatia matatani na watapata madhara makubwa ikiwa atabaini kuwa walikuwa wanafuata dini ya Muhammad ﷺ.

Ilikuwa katika hatua hii, ambapo Fatmah bint Khattab alimkabili wazi kaka yake na kumwambia wazi bila woga kuwa yeye na mume wake walikuwa wameukubali Uislamu na kusilimu na kukiri kuwa Hapana Mola Apasaye Kuabudiwa kwa Haki isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah. Kusikia hivyo, 'Umar ibn Khattab akaanza kumpiga Sa'eed na kumuangusha chini kwa hasira. Fatmah alipojaribu kwenda kumtetea na kumsaidia mume wake, Umar akampiga kofi la nguvu sana Fatmah, na Fatmah akaanza kububujikwa na damu.

Ni kutokana na damu iliyokuwa ikibubujika kwa Fatmah ndiyo ilimfanya 'Umar apoe na nuru ianze kupenya katika moyo wa 'Umar na kuondoa hisia za ukafiri katika moyo wake. Umar akamsogelea Sa'eed na kumuinua kutoka chini alipokuwa amemuangusha, kisha akamsogelea dada yake na kuanza kumfuta damu iliyokuwa ikitoka usoni kwake. Alianza kuongea na Sa'eed na dada yake

Fatmah kwa namna ya urafiki na mapenzi mpaka Fatmah akatoa maandiko ya Qur'an waliyokuwa wakisoma, maandiko yaliyokuwa na Ayah za mwanzo za Surat Ta Ha.

'Umar ibn Khattab alipotaka kushika maandiko yale ya Qur'an, Fatmah alimkatalia na kumtaka ajisafishe kwanza kabla ya kushika Qur'an. 'Umar alifanya alivyoelekezwa. Imani thabiti, ucha-Mungu, busara na ujasiri wa Fatmah unaonekana kwa namna alivyohusika katika tukio hili na namna alivyokabiliana na vitisho vya kaka yake - 'Umar ibn al-Khattaab.

Kisha 'Umar ibn al-Khattab akawauliza, "Yuko wapi Muhammad?" Fatmah na Sa'eed wakaingiwa na hofu ndani ya nyoyo zao, wakidhani kuwa huwenda 'Umar bado anadhamira ya kumdhuru Mtume ﷺ. Lakini 'Umar aliwaondoa hofu na kuwahakikishia kuwa alichohitaji ni kwenda mbele ya Mtume Muhammad ﷺ kusilimu. Fatmah bint Al-Khattab na Sa'eed wakamwambia kuwa, Mtume ﷺ alikuwa yuko nyumbani kwa Arqam katika eneo la Safa.

Ilikuwa ni katika wakati huu, ndipo Khabbaab akatoka alikokuwa amejificha na kumwambia 'Umar, "Furaha iliyoje ewe 'Umar! Wewe ndiye uliyechaguliwa na Allah kutokana na dua aliyoiomba Mtume ﷺ. Hakika nilimsikia Mtume ﷺ akimuomba Allah aupe nguvu kwa kusilimu kwako."

Maneno haya yalimuongezea 'Umar ibn Al-Khattab imani, kujiamini na mapenzi yake kwa Mtume ﷺ. Dada yake Umar رضي الله عنه, Fatmah bint Al-Khattab naye alijawa na furaha sana, kwani kwa muda mrefu alikuwa anamuomba Mwenyezi Mungu Amuongoze kaka yake.

Kuna jambo moja ni muhimu kulisisitiza hapa.Watu wengi hudhania na hata kuamini kuwa Khabbab رضي الله عنه alikimbia na kwenda kujificha kutokana na woga au hofu. Lakini ukweli ni kwamba, alifanya vile ili kuepuka kuweka wazi mafundisho ya Uislamu ambayo kwa wakati huo yalikuwa yanaendeshwa kwa siri na huo ndio ulikuwa msingi wa harakati na Da'wah katika masiku ya mwanzo ya Uislamu. Ili kuthibitisha haya, ni vema kila mtu akasoma historia ya swahaba huyu wa Mtume ﷺ kama tulivyomuelezea katika kitabu chetu tulichokiita "Wanaume waliomzunguuka Mtume ﷺ". Allah Akipenda utaweza kuona ni kwa kiasi gani swahaba huyu alikuwa jasiri na mpambanaji. Itoshe kusema hapa kuwa, baadhi ya wanahistoria wamemtaja Khabbaab kama mtu

wa sita kusilimu na miongoni mwa watu wa mwanzo kabisa kuthubutu kutangaza Uislamu wao hadharani na hivyo kupata mateso makali kutoka kwa makafiri. Huyu alikuwa swahaba aliyekuwa na imani thabiti kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Muhammad ﷺ.

Baada ya hapo, 'Umar ibn Al-Khattab akaondoka na kuelekea nyumbani kwa Arqam. Safari hii ilikuwa na umuhimu mkubwa katika historia binafsi ya Umar ibn Al-Khattab na Uislamu kwa ujumla. Umar ibn Al-Khattab, kutoka kuwa adui mkubwa wa Uislamu na Waislamu mpaka kuja kuwa Khalifa wa pili wa Waislamu na Kamanda wa Waumini! 'Umar alifika nyumbani kwa Arqam na kugonga mlango. Mmoja kati ya maswahaba alichungulia kupitia ufa wa mlango ili kujua ni nani alikuwa akigonga mlango, na alipomuona kuwa aliyekuwa akigonga mlango alikuwa ni Umar ibn Al-Khattab, aliingiwa na wasiwasi. Huku akiwa amechanganyikiwa na mwingi wa hofu, swahaba yule alisema, "Ewe Mtume wa Allah! Anayegonga mlango ni mtoto wa Al-Khattaab!"

Kupitia Nuru ya Utume, Mtume ﷺ aliweza kuthibitisha maneno yale kuwa ni kweli, kuwa aliyekuwa akigonga mlango alikuwa ni 'Umar ibn Al-Khattab, na ilikuwa si muda mrefu toka Mtume ﷺ alipomaliza kuomba dua Allah aupe nguvu kutokana na kusilimu kwa mmoja kati ya 'Umar wawili. Mwenyezi Mungu Anasema katika Qur'an kuwa:

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي
وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ﴿١٨٦﴾

***"Na waja wangu watakapokuuliza hakika Yangu, (waambie kuwa) Mimi niko karibu nao. Naitika maombi ya mwombaji anaponiomba. Basi nawaniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka."* (2:186)**

Mtume wa Allah ﷺ aliamuru mlango ufunguliwe na 'Umar aruhusiwe aingie. Mlango ulipofunguliwa kwa ujasiri na Ibn 'Abbaas, na Mtume ﷺ akamsogelea 'Umar ibn Khattab huku maswahaba wengine waliokuwepo wakati huo nao wakisogea na wakimfuata Mtume ﷺ nyuma yake. Mtume ﷺ alimwambia 'Umar: *"Ewe mtoto wa Al-Khattaab! Unasubiri nini? Bila shaka*

*huu ni muda muafaka kwako kuingia katika Uislamu!"*

Huku akiwa mnyonge na aliyepoa, 'Umar ibn Al-Khattab alitamka, "Nakiri kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah! Na wewe Muhammad ﷺ ni Mtume wa Allah." Waislamu waliokuwepo wakati tukio hili likitokea, walijawa na furaha sana na wakawa wakimtukuza Allah kwa kusema *Takbeer*! Mvumo wa Takbeer ulitoka nje ya nyumba ile na hakika ulikwenda mbali kiasi cha kuwafikia waliokuwa jirani na Ka'bah kwa wakati ule.

Hakika kusilimu kwa 'Umar ibn Al-Khattab رضي الله عنه ilikuwa ni ushindi kwa Uislamu na Waislamu. Allah Akampa nguvu 'Umar kutokana na kusilimu kwake, na Akaupa nguvu Uislamu kupitia kwa 'Umar. Baada ya kusilimu 'Umar ibn Khattab رضي الله عنه, kazi ya kulingania Uislamu ikatoka kuwa ya siri na kuanza kufanyika hadharani na Mwenyezi Mungu Akabainisha na Kuweka wazi baina ya haki na batili. Mtume wa Allah ﷺ akampa 'Umar ibn Al-Khattab رضي الله عنه jina la '*Al-Faarooq*' (Jina ambalo linamaana ya mwenye kubainisha haki na batili) na kumpa jina la 'Abu Hafs'.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Amuwie radhi Fatmah bint al-Khattab na Amridhie. Kwa hakika Allah Alimchagua yeye (Fatmah) kuwa sababu ya kaka yake – 'Umar ibn Al-Khattab رضي الله عنه – Khalifa wa pili wa Waislamu na Kamanda wa Waumini, kuukubali Uislamu na kusilimu. Nyumbani kwa mama huyu ikawa ndio sehemu ya kuanzia mabadiliko ya nafsi ya 'Umar na safari iliyopelekea kuupa nguvu Uislamu.

Tuseme kama walivyosema Waislamu waliokuwepo wakati 'Umar ibn Al-Khattab رضي الله عنه anasilimu kwa Mtume ﷺ: *Takbirr - Allahu Akbar*!

# Sumayyah Bint Khayyaat

## Shahidi wa Kwanza Katika Uislamu

Inawezekana kabisa ndani ya familia yako au miongoni mwa rafiki zako akawepo mtu anayeitwa Sumayyah. Je, ni nani hasa mwanamke huyu? Basi hii ndio historia itakayokuwezesha kumjua vema mama huyu.

Sumayyah bint Khayyat رضي الله عنها alikuwa na mwanzo mwema. Mama huyu alikuwa ni mtumwa hapo mwanzo na baadaye akaachiwa huru. Toka akiwa binti mdogo, mama Sumayyah رضي الله عنها alikuwa anafahamika kwa tabia njema, busara na mtu mwenye hisia za utu na mwingi wa huruma.

Mama huyu alikuja kuolewa na Yasir رضي الله عنه ambaye baadaye alikuja kuwa miongoni mwa maswahaba wa Mtume ﷺ wenye hadhi kubwa. Mama Sumayyah na mumewe Yasir waliishi maisha yenye furaha katika ndoa yao, na walijaaliwa kuzaa watoto watatu. Watoto wao hao waliwaita Ammar, Abdullah na Harith. Sumayyah رضي الله عنها alikuwa mama mwenye bidii kubwa katika kuwalea watoto na kuhakikisha wanapata malezi bora na kila kilichokuwa muhimu mtoto kukipata kutoka kwa wazazi wake. Hili lilijionesha wazi miongoni mwa watoto wake, kwani watoto wake Ammar na Abdullah walikuja kuwa miongoni mwa watu wenye tabia njema na wenye kuheshimika miongoni mwa vijana wa Makkah pamoja na kuwa wote wawili walizaliwa na familia iliyokuwa na asili ya utumwa. Kwa bahati mbaya mtoto wao Harith aliuwawa kabla ya kuja kwa Uislamu – hakika hili lilikuwa ni jambo la kuhuzunisha sana kwa mama Sumayyah رضي الله عنها na familia yake kwa ujumla. Hata hivyo huzuni hii ilikuwa ni sehemu ya maisha ya mwanadamu ambayo kwa vyovyote vile haiwezi kuwa jambo la kufanya maisha yasiendelee na yeye mama Sumayyah رضي الله عنها kushindwa kutekeleza wajibu wake kama mama.

Baada ya muda Mtume ﷺ alianza kuwalingania watu kumjua Mwenyezi Mungu aliye wa haki na kuwataka watu waingie katika dini ya Allah – Dini ya Kiislamu. Sumayyah رضي الله عنها akaukubali Uislamu na kuwa miongoni mwa watu saba (7) wa mwanzo kuukubali Uislamu na kuchukua ahadi ya utii na kumuunga mkono Mtume ﷺ katika kazi yake ya da'wah. Hii inaweza kuwa na maana kuwa busara ya mama Sumayyah رضي الله عنها limfanya auone ukweli wa dini hii mapema na hivyo kuikubali na hakuwa na uzito wala kuona shida kuukubali Uislamu – dini pekee ya haki kwa mwanadamu. Hivyo mama huyu ana heshima ya pekee sana katika historia ya Uislamu na alikuwa na hadhi kubwa na pekee miongoni mwa maswahaba wa Mtume ﷺ na hakika katika kundi lile maalum la Waislamu wa mwanzo. Waislamu wa mwanzo kabisa ni pamoja na Khadijah bint Khuwaylid, Abu Bakr, Ali ibn Abu Talib, Bilal ibn Abi Rabiah, Zaid ibn Harith, yeye mwenyewe – Summayah na mwanae Ammar Ibn Yasir رضي الله عنهم.

Maquraishi walikuwa hawana uwezo wa kumtesa na kumdhuru Mtume ﷺ yeye mwenyewe moja kwa moja kutokana na hadhi na heshima aliyokuwa nayo baba yake mdogo Abu Talib, japo hili halikuwafanya waache kujaribu kumdhuru kwa njia nyingine isiyokuwa ya moja kwa moja na kujaribu kukwamisha ujumbe aliokuja nao usienee. Abu Bakr رضي الله عنه alikuwa akilindwa na hadhi yake mwenyewe na nguvu ya kabila lake na hivyo ilikuwa vigumu kumkabili na kumfanyia udhalilishaji au unyanyasaji kama waliokuwa wakifanyiwa maswahaba wengine رضي الله عنهم. Ukiachia Waislamu hawa waliokuwa na hadhi maalumu wao au makabila yao na hivyo kutoteswa, Waislamu wengine walikuwa hawako salama na daima walikuwa wakiteswa.

Waislamu wa mwanzo walikuwa wachache wasiozidi hata thelathini, lakini Maquraishi ambao ndio kwa wakati ule walikuwa wakitawala Makkah walikuwa wakihisi utawala wao uko mashakani. Hii ina maana Waislamu thelathini tu tena wasiokuwa na silaha na wanyonge wakiwemo watumwa, waliwafanya watawala wahisi utawala wao uko mashakani! Kwanini wahisi hivi wakati Waislamu walikuwa wachache na dhaifu? Bila shaka hili ni somo muhimu sana kwa Waislamu wa leo ambao wingi wetu umekuwa hauna msaada wowote wala hauna faida. Pamoja na idadi yetu kuwa kubwa bado tunaweza kudhalilishwa na makafiri wachache. Maquraishi kwa kuhofia kupoteza utawala wao, walikuwa wakiwatesa Waislamu wa mwanzo kwa

mateso makali sana wakiamini Muislamu huyo atarudi nyuma na kuiacha dini yake au itasaidia kuwatisha wengine wasiukubali Uislamu.

Mama Sumayyah رضي الله عنها mume wake Yasir رضي الله عنه na mtoto wao Ammar رضي الله عنه kama ilivyokuwa kwa Waislamu wengine wanyonge wa mwanzo, walikuwa walengwa wakuu wa mateso haya ya Maquraishi. Walikuwa ni walengwa kwa sababu wao hawakuwa matajiri wala walikuwa hawatoki katika familia yenye nguvu ambayo ingeweza kuwalinda. Mtume ﷺ alikuwa akiwaombea du'a familia hii. Alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu aiihifadhi familia hii na kuwanusuru na adhabu ya moto. Alikuwa akiwatembelea na kuwaambia *"Kuweni wenye subira enyi familia ya Yasir! Kwani kwa hakika mwisho wenu utakuwa Peponi".*

Wakati fulani Ammar alifanikiwa kutoroka mateso na kwenda kwa Mtume ﷺ Ammar akamuuliza Mtume ﷺ ni lini mateso dhidi ya Waislamu wanyonge yatamalizika (yataisha). Hisia zake zilikuwa zinaonesha ni kwa kiasi gani Waislamu wa mwanzo walikuwa wanakabiliwa na wakati mgumu pale Makkah. Waislamu walipojaribu kuyakimbia makazi yao walifuatwa wakatekwa na kuteswa vikali sana na kwa hakika waliishi katika maisha ya hofu kubwa na mashaka makubwa juu ya hatima yao. Hakika Waislamu wa mwanzo walijaribiwa imani zao na wakatikiswa. Lakini pamoja na hayo walibakia kuwa imara; si mateso wala udhalilishaji vilivyoweza kutikisa imani zao thabiti juu ya Mola wao. Ujasiri wao katika kuyakabili matatizo na nyakati ngumu katika mazingira tofauti inatosha kutoa mazingatio kwetu na kujifunza na sisi kuwa Waislamu wenye kujitoa, wenye subira na watiifu kwa Mola wetu. Waislamu wa mwanzo walijua kuwa maisha haya ni mtihani kwao, kwa vyovyote vile mtihani ambao mtu akifaulu atakwenda Peponi hauwezi kuwa mtihani rahisi hata kidogo.

Zaidi ya yote walifahamu na kuamini kwa dhati kuwa maisha ya hapa duniani ni maisha mafupi sana na wala si ya kudumu. Lakini zaidi ya hayo, walijua kuwa maisha ya Akhera ndio yenye kudumu na yasiyo na mwisho. Basi kwanini Muislamu asijinyime usingizi, akafunga na kuswali na kukubali kuikabili misukosuko ya muda mfupi ili apokelewe na Mwenyezi Mungu hali ya kuwa Amemridhia? Akakutane na Mtume ﷺ na maswahaba na Waislamu wengine waliotangulia ndani ya Pepo Aliyowaandalia Mola wao Insha-Allah.

Abu Jahl alikuwa miongoni mwa viongozi wa Maquraishi wa Makkah na alikuwa adui mkubwa wa Uislamu na Waislamu aliyejitoa kwa ajili ya kuulinda na kuupigania ukafiri kwa mali na nguvu zake zote. Bwana huyu alikuwa akimpa adhabu kali sana mama Sumayyah رضي الله عنها. Aliyafanya haya bila kujali kuwa mama huyu alikuwa mtu mzima. Mama ambaye alikuwa amejaaliwa kuzaa na kulea vijana ambao nao walikuwa wanayakabili mateso, bila shaka hakuwa binti bali mama mtu mzima. Unaweza kuvuta hisia ni mateso magumu kiasi gani aliyokuwa akiyapata mama huyu katika umri wa utu uzima kwa kosa la kusema mimi ni Muislamu na ninamuamini Mwenyezi Mungu – Mola wa Walimwengu wote. Lakini pamoja na umri mkubwa aliokuwa nao, pamoja na mateso makali aliyopewa na kusababisha maumivu makali katika akili na mwili wake, mama huyu hakuyumba wala kutetereka imani yake wala kutafakari kinyume chake. Alibakia kuwa imara kama mlima na alibakia kuishi ndani ya kalima tukufu ya - *La ilaha illa Allah Muhammad ur-rasulullah* – Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na Muhammad ni Mtume wake.

Abu Jahl alitumia mbinu mbalimbali kumfanya mama Summayah رضي الله عنها arudi nyuma na kuachana na dini yake, alitumia vitisho, nguvu, ahadi na hata rushwa ili mama Sumayyah رضي الله عنها aukane Uislamu, lakini alikataa vikali kabisa kufanya hivyo. Angeweza hata kumkubalia kwa mdomo ili kusitisha mateso aliyokuwa akiyapata na wala kufanya hivi kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu sio kosa wala mtu hawezi kupata dhambi kwa kukanusha Uislamu au kutamka maneno katika ulimi wake na wala maneno hayo hayatoki katika dhati ya nafsi yake kwa lengo la kuepuka kupata madhara. Hili linakubalika katika misingi ya sheria za Kiislamu. Hata hivyo, Bi Sumayyah رضي الله عنها alichagua njia ngumu zaidi – njia aliyoamini ina malipo zaidi. Ni kwa namna hii, Bi Sumayyah رضي الله عنها pamoja na umri wake mkubwa aliweza kuwatia moyo Waislamu wengine kuvumilia mateso na kubakia wenye subira. Hapa ndipo tunapata somo muhimu katika *da'wa*. Je, tunawafundisha watu kuishi kwa huruma, imani thabiti na ucha-Mungu kwa kuwahubiria kwa maneno au tunakuwa mfano kwa vitendo vyetu ili watamani kuishi vile tunavyotaka waishi? *Da'awa* ya maneno mara nyingi huonekana ni mambo yasiyotekelezeka na ile ya vitendo huonekana mfano wa kuigwa – Matendo hukidhi haja maridhawa kuliko maneno. Ikiwa tunataka watu waamini na kuishi tunavyotaka, basi tuwe mfano wa maisha hayo.

Abu Jahl hakuamini kuwa mama Sumayyah angeweza kuhimili mateso kiasi kile. Kwa hasira na chuki iliyopitiliza alimchoma mkuki sehemu za siri na hili likawa tukio la mwisho na hatimaye Bi Sumayyah bint Khayyat رضي الله عنها akawa ameuwawa. Bi Sumayyah رضي الله عنها akawa ameutoa uhai wake kwa ajili ya Uislamu. Muda huu ambao Bi Sumayyah aliuwawa alipata bahati ya kufa shahidi katika dini ya Allah, lakini zaidi ya yote akawa shahidi wa kwanza kufa kwa ajili ya dini ya Kiislamu. Hivyo mtu wa kwanza kufa kwa ajili ya dini ya Allah alikuwa mwanamke na si mwingine isipokuwa ni mama Sumayyah bint Khayyat رضي الله عنها na mtu wa kwanza kumuua Mwislamu kwa sababu ya dini yake alikuwa ni Abu Jahl.

Bi Sumayyah رضي الله عنها anatuachia mfano bora na somo muhimu kwa wale wenye kutaka kuipata Pepo ya Allah kuwa wanahitaji kufanya bidii kwa ajili ya dini ya Allah, wawe tayari kujitoa muhanga na kuwahimiza watu kuwa na msimamo thabiti kwa wao wenyewe kuwa mfano bora. Mwenyezi Mungu Anasema:

أَمْ حَسِبْتُمْ أَن تَدْخُلُوا۟ ٱلْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُم مَّثَلُ ٱلَّذِينَ خَلَوْا۟ مِن قَبْلِكُم ۖ مَّسَّتْهُمُ ٱلْبَأْسَآءُ
وَٱلضَّرَّآءُ وَزُلْزِلُوا۟

***"Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, na hali hamjajiwa na mfano wa (yale yaliyowajia) wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa....."* (2:214)**

Bi Sumayyah رضي الله عنها alikuwa mfano halisi wa watu waliozungumzwa ndani ya Ayah hii:

وَلَنَبْلُوَنَّكُم بِشَىْءٍ مِّنَ ٱلْخَوْفِ وَٱلْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ ٱلْأَمْوَٰلِ وَٱلْأَنفُسِ وَٱلثَّمَرَٰتِ ۗ وَبَشِّرِ
ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿١٥٥﴾ ٱلَّذِينَ إِذَآ أَصَٰبَتْهُم مُّصِيبَةٌ قَالُوٓا۟ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيْهِ رَٰجِعُونَ ﴿١٥٦﴾

***"Na Tutakutieni katika msukosuko wa (baadhi ya mambo haya); hofu na njaa na upungufu wa mali na wa watu na wa matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri. Ambao uwapatapo msiba husema: "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake Yeye tutarejea (Atatupa jaza Yake)."* (2:155-156)**

Yapo mengi ya kuanzia na kutukurubisha kwa Mola wetu. Haya ni pamoja na kudumisha Swala za faradhi na kuziswali ndani ya wakati tena kuhakikisha tunajifunza na kuziswali kwa usahihi, kufunga Swaumu za Sunnah, kuacha usingizi na kusimama usiku na kuswali na kutaka msamaha kwa Mola wetu, kuzidisha kumtaja Allah, kusoma Qur'an, kuwasaidia wenye shida, kuwalisha wenye njaa, kuwavalisha wasio kuwa na nguo, kuwa wakarimu kwa ndugu na jamaa zetu kwa kutaraji malipo kutoka kwa Allah, kukaa chini kutafakari na kutumia uwezo wetu wa elimu, maarifa na mali na kufanya kila linalowezekana kuupeleka mbele Uislamu. Mwanamke huyu shujaa na shahidi wa kwanza katika Uislamu - Sumayyah bint Khayyat رضي الله عنها alifariki miaka saba (7) kabla *Hijrah* (Kabla ya Waislamu kuhamia Madinah). Mume wake Yasir ﷺ naye aliteswa mpaka akauwawa na Maquraishi kwa ajili ya Uislamu na hivyo naye kufa shahidi. Baada ya wazazi wake wote wawili kuuwawa, Ammar رضي الله عنه akawa miongoni mwa maswahaba waliopendwa sana na Mtume ﷺ. Kinyume na ilivyokuwa desturi kwa wakati ule kuwaita watoto kwa ubini wa baba zao, Mtume ﷺ alikuwa akimwita Ammar ibn Sumayyah (Ammar mtoto wa Sumayyah) – ili kutunza kumbukumbu na hisia juu ya mama huyu pamoja na kumpa heshima. Mtume ﷺ alikuwa akiitaja familia hii kwa kuipa hadhi ya juu na kuitaja kwa wema.

Baada ya miaka mingi, baada ya Mtume ﷺ kufariki dunia na Makhalifa watatu wa mwanzo (Abu Bakr, 'Umar Ibn Khattab na 'Uthaman Ibn Affan رضي الله عنهم), Ammar رضي الله عنه aliuwawa katika vita maarufu, vita vya Siffin. Ammar رضي الله عنه aliuwawa akiupigania Uislamu na hivyo kufa shahidi kama walivyokufa wazazi wake. Familia hii ilijitolea kila walichokuwa nacho ikiwemo uhai wao kwa ajili ya kuutetea Uislamu – dini ya haki – dini ya Allah na wao kulipwa Pepo. Ni kwa watu mfano wa mama Sumayyah bint Khayyat رضي الله عنها, Allah Anasema:

۞ إِنَّ ٱللَّهَ ٱشْتَرَىٰ مِنَ ٱلْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَٰلَهُم بِأَنَّ لَهُمُ ٱلْجَنَّةَ

***"Mwenyezi Mungu Amenunua kwa Waislamu nafsi zao na mali zao (watoe nafsi zao na mali zao katika kupigania dini) ili na yeye awape Pepo..."* (9:111)**

# Al-Khansaa, Tamadur binti Amr ibn Shareed

## Mtakeni msaada Allah dhidi ya adui zake

Mtume ﷺ alikuwa mtu aliyethamini sana vipaji vya watu na kutoa fursa ya matumizi ya vipaji hivyo katika kuutumikia Uislamu. Moja katika fani za wakati huo alizozikubali na kuzipa nafasi, ni matumizi ya mashairi katika kuupigania na kuuhami Uislamu. Na hii ni kwa sababu Mtume ﷺ alifahamu athari ya matumizi ya sanaa hii. Aliwaruhusu Hassan ibn Thaabit, Ka'b ibn Maalik رضي الله عنه. na Abdullah ibn Rawaahah kutumia vipaji vyao katika kujenga hoja dhidi ya ukafiri na kuwaruhusu kuingia vitani baina ya haki na batili kwa njia ya mashairi.

Imesimuliwa kuwa, 'Abdullah ibn Rawahah رضي الله عنه. alisoma shairi mbele ya Mtume ﷺ wakati wa 'Umrah, muda mfupi kabla ya Mtume ﷺ hajaingia Makkah. Pamoja na mambo mengine, inaelezwa kuwa,sehemu ya shairi alilosoma lilikuwa na maneno yaliyokuwa na maana ifuatayo:

"Enyi watoto wa makafiri! Mwachieni njia ﷺ;

Leo tutapigana kwa nguvu kabisa kiasi kwamba kichwa kitakatwa
na kutenganishwa na mwili; na mtu atatengana na rafiki yake!

Sisi ndio tuliokupigeni kwa ahadi ya Qur'an; kama tulivyokupigeni
wakati ikishushwa!

Allah Ametufunulia katika kitabu Chake kuwa njia bora ya kufa ni
kufa katika njia Yake!

Ewe Allah! Mimi namwamini kiongozi uliyemtuma Kitabu (Qur'an),
na ninaamini kuwa njia pekee iliyo sahihi ni kumuamini yeye!"

‘Umar ibn Khattab رضي الله عنه aliposikia maneno haya, alihamaki na kutaka kumzuia ‘Abdullah asiendelee kusoma mashairi zaidi. ‘Umar ibn Khattab رضي الله عنه alipaza sauti na kusema, “Ewe Rawahah, unasoma mashairi mbele ya Mtume ﷺ tena katika ardhi Tukufu ya Allah (Makkah)?!” ‘Umar ibn Khattab رضي الله عنه alihofia kuwa huwenda jambo hili la kuimba au kusoma mashairi likamchukiza Mtume ﷺ. Lakini Mtume ﷺ akamjibu na kumtoa hofu ‘Umar ibn Khattab رضي الله عنه kwa kumwambia kuwa: *“Muache aendelee ‘Umar. Kwani mashairi yake yanawaumiza sana makafiri kuliko kuwarushia mshale.”*

Pamoja na kuwa Mtume ﷺ hakuwa mshairi wala hakuwahi kutunga au kujaribu kutunga shairi lolote, lakini tumeona ni namna gani Mtume ﷺ aliyaridhia na kuyapenda mashairi yenye mafunzo ya Kiislamu na yale ambayo yanaeneza ujumbe wa Kiislamu kama njia moja wapo ya sanaa.

Sasa tuyaangazie na kujifunza kutoka katika maisha ya mshairi hodari wa kike, mama wa Kiislamu, Al-Khansa’ رضي الله عنها. Al-Khansa ni nani, na ana mchango gani katika Uislamu na harakati za Mtume ﷺ kwa ujumla?

Al-Khansa رضي الله عنها anatoka katika kabila la Bani Sulaym; Mama huyu alikuwa mwanamke mrembo sana, mwanamke aliyelelewa na kujipamba kwa tabia njema na aliyekuwa fasaha katika kuongea. Al-Khansa رضي الله عنها alianza kusoma mashairi akiwa na umri mdogo kabisa. Mwanzoni alikuwa hasomi zaidi ya mistari miwili au mitatu ya mashairi kisha alikuwa haendelei. Huzuni iliyotokana na kifo cha kaka yake, Sakhr kulimfanya aanze kutunga na kusoma mashairi marefu.

Alikuwa akiimba mashairi marefu akiomboleza kifo cha kaka yake Sakhr, lakini pia kifo cha kaka yake Mu‘aawiyah رضي الله عنه. Wanazuoni na mabingwa wa lugha na mashairi wamekubaliana kuwa, hakuna mwanamke mwingine yeyote aliyewahi kufikia kiwango au uwezo wa Al-Khansa رضي الله عنها katika kutunga na kusoma mashairi.

Katika kumlilia kaka yake, alisema (maneno yaliyokuwa na maana kuwa):

“Ewe macho yangu! Mwaga sana machozi!
Na kwanini usimlilie Sakhr, mtu mkarimu?!

Kwanini usimwage machozi kumlilia kijana mrefu, mtanashati na jasiri

Mtu aliyekuwa na sifa za uongozi na akiwaongoza watu wake?!”

Al-Khansa alikuja Makkah akiongozana na msafara kutoka katika kabila lake la Bani Sulaym. Alisilimu na kuingia katika Uislamu. Alichukua kiapo cha utii kwa Mtume ﷺ na kuwa mwaminifu na mkweli juu ya kiapo chake. Siku moja, Mtume ﷺ alimsikia akisoma shairi na kumtaka aendelee kusoma (asome zaidi). Mtume ﷺ aliyapenda mashairi yake, na hii ni moja ya ishara kuwa alikuwa karibu na Mtume ﷺ. Al-Khansa رضي الله عنها alitokea katika familia yenye kuheshimika na alikuja kuzaa matunda yenye kuheshimika pia. Utukufu na ubora wa mama huyu na kizazi chake tunaushuhudia siku ya vita vya Qaadisiyah. Ni katika vita hivi, mama huyu Al-Khansa رضي الله عنها alifikia kilele cha ucha-Mungu na kufanya matendo ambayo mpaka leo anabakia katika vitabu vya historia ya Kiislamu. Na hivyo kuacha somo muhimu kwa wazazi, wanawake na wanaume.

Hadhi na heshima yake inabebwa na mambo makubwa mawili:

1) Usia wake kwa watoto wake wanne (4) waliokuwa wanaingia katika Jihad na

2) Kauli aliyoitoa baada ya kupata taarifa ya kuuwawa watoto wake wote wanne (4).

Enyi akina mama wa Kiislamu! Enyi wanawake wa Kiislamu! Hakika mnayo mambo mazito na muhimu ya kujifunza kutoka kwa mama huyu wa Kiislamu, Al-Khansa رضي الله عنها. Pengine baada ya kusoma historia hii fupi ya mama huyu mnaweza kuona namna gani mmewaandaa watoto wenu na vipi mnayapokea mambo mazito yanapowafika au yanapowafika watoto wenu. Kwa namna gani mnawahimiza watoto wenu katika kuihangaikia dunia na wala hamtumii nafasi yenu kuwahimiza kuitafuta Akhera! Vipi mnawahimiza ushujaa wa kuikabili dunia na si ushujaa kwa ajili ya dini yao na Akhera yao! Soma maneno ya Al-Khansa رضي الله عنها na yakuzindue ewe mama wa Kiislamu.

Ibn 'Abdul-Barr anasimulia tukio zito linalomuhusu mama huyu katika kitabu *Al-Istee'ab*: "Al-Khansa' bint 'Amr alikuwa miongoni mwa Waislamu walioshuhudia vita vya Qaadisiyah, yeye na wanaye wanne (4). Mama huyu Al-Khansa رضي الله عنها, aliwausia watoto wake muda mfupi kabla ya kuanza kwa vita akiwaambia kuwa: "Enyi watoto wangu! Mliingia katika Uislamu na kuhama kutoka Makkah kwenda Madinah kwa hiari yenu. Naapa kwa jina la Allah, ambaye hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, ninyi ni

watoto wa baba mmoja kama mlivyokuwa watoto wa mama mmoja. Sikuwahi kumuendea kinyume au kumfanyia hiyana baba yenu. Wala sikuwahi kumletea huzuni mjomba wenu, kuwavunjia heshima au kuharibu mahusiano. Mnafahamu vizuri malipo makubwa yasiyokuwa na mfano ambayo Allah Ameyaandaa kuwalipa Waislamu wanaopambana dhidi ya makafiri. Fahamuni ya kwamba, hakika maisha ya Akhera ni bora na ya kudumu kuliko maisha haya ya mpito. Allah Anasema:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱصْبِرُوا۟ وَصَابِرُوا۟ وَرَابِطُوا۟ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٢٠٠﴾

***"Enyi mlioamini! Subirini na muwashinde makafiri (katika kusubiri), na kuweni imara (nyoyo zenu) na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufaulu (kufuzu)".* (3:200)**

Allah Akipenda, mtakapoamka kesho asubuhi mkiwa na afya njema, nendeni mkapigane kwa ujasiri dhidi ya maadui zenu (makafiri) mkiwa na yakini na mtakeni msaada Allah dhidi ya adui zake. Mtakapoona vita imekuwa ngumu, basi piganeni kwa ushujaa tena kwa ukakamavu na ujasiri mkubwa ili mpate malipo na heshima katika maisha ya Akhera."

Huu ndio ulikuwa usia wa Al-Khansa رضي الله عنها kwa watoto wake wanne (4) siku moja kabla ya vita!. Msimuliaji anaendelea kusimulia: "Watoto wale wanne (4) wakaondoka hali ya kuwa wamepokea na kukubali usia wa mama yao na wakiwa wamejiandaa kuutekeleza usia ule siku inayofuata. Asubuhi ilipowadia, watoto wale waliondoka asubuhi sana na kuwahi katika uwanja wa vita.Vita ilipoanza, watoto hawa walipigana kwa ujasiri mkubwa na kishujaa mpaka walipouwawa wote, mmoja baada ya mwingine."

Haikuchukua muda mrefu, habari juu ya kuuwawa kwa watoto wote wanne wa Al-Khansa zilimfikia mama yao! Al-Khansa رضي الله عنها alipokea vipi taarifa za kuuwawa watoto wake wote? Je, alisema nini mama huyu wa Kiislamu?

Hapa ndipo ucha-mungu na subira ya Al-Khansa رضي الله عنها inapojidhihirisha na kuthibitika waziwazi. Fikiria kama mzazi mwenye watoto wakubwa uwapendao, kisha unapokea taarifa ya watoto wako wote wanne kuuwawa kwa wakati mmoja. Vipi ungepokea taarifa nzito namna hii?.

Al-Khansa رضي الله عنها alipopokea taarifa kuwa watoto wake wote wanne wameuwawa, alisahau habari ya mashairi, alisahau hadhi yake katika jamii na uzuri aliokuwa nao. Hakukumbuka chochote zaidi ya Allah! Mola wa Walimwengu wote. Alikumbuka ahadi za Allah kwa waja wake na mitihani ambayo itawafika Waumini katika dunia hii. Al-Khansa رضي الله عنها akasema maneno yafuatayo baada ya kupokea taarifa ya kuuwawa kwa watoto wake wote katika uwanja wa vita: "Sifa zote njema zinamstahiki Allah! Aliyenipa heshima kubwa kwa watoto wangu wote kuuwawa mashahidi. Nataraji Mola wangu Atanifanya na mimi niungane nao katika maisha ya Akhera nikiwa ndani ya Rehema Zake!"

Ni muhimu sana kufahamu kuwa, haikutokea kwa bahati mama huyu kutoa usia huu kwa wanae au kutamka maneno haya baada ya kupata taarifa za kuuwawa watoto wake wote. La hasha! Hii ni kutokana na msingi imara wa imani aliokuwa tayari ameujenga kutokana na ibada mbalimbali na kumuamini na kumtegemea Allah ukweli wa kumuamini na kumtegemea. Hayatokei haya kwa mtu ambaye maisha yake anaishi apendavyo kinyume na Atakavyo Allah.

Pengine yaweza kuwa muhimu kufahamu kuwa, Kamanda wa waumini, 'Umar Ibn al-Khattab رضي الله عنه, alikuwa akimpa Al-Khansa' رضي الله عنها kiasi cha Dirham mia mbili kwa mwaka kutokana na watoto wake kuuwawa mashahidi. Aliendelea na utaratibu huu mpaka Al-Khansa رضي الله عنها alipofariki dunia.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Amuwie radhi Al-Khansa, mshairi wa kike; Mwenyezi Mungu Amridhie mama huyu mwenye subira na mcha-Mungu! Mwenyezi Mungu Amuinue daraja kama alivyowainua watoto wake waliokuwa wacha-Mungu. Amin!

# Ash - Shifaa binti 'Abdullah

## Daktari, Mwalimu na Afisa Masoko

Mtume wa Allah ﷺ aliingia wakati (Ash-Shifaa) akiwa amekaa pamoja na Hafsa, Mtume ﷺ akasema, *"Kwanini usimfundishe huyu (Hafsah) dawa ya magonjwa ya ngozi kama ulivyomfundisha kuandika."* (Dawud 28:3878)

Jina halisi la mama huyu ni Laylah bint Abdullah ibn Abdshams na jina la mama yake ni Fatmah bint Wahb. Hata hivyo alifahamika zaidi kwa jina la Al-Shifa (daktari au tabibu) kutokana na ujuzi mkubwa wa elimu ya tiba aliokuwa nao mama huyu. Katika zama zake, alikuwa miongoni mwa watu wachache sana (takriban watu ishirini tu) katika mji wa Makkah waliokuwa na elimu na ujuzi wa kusoma na kuandika. Mama huyu alikuwa anatoka katika ukoo wa Adi katika kabila la Kiquraishi katika mji wa Makkah. Mama huyu aliolewa na Abu Hathma ibn Hudhayfa na kujaaliwa kupata watoto wawili, ambao waliwaita Sulayman na Masruq. Kupitia kwa mwanae Sulayman, mama huyu alijaaliwa kupata wajukuu wawili - Abu Bakr na Uthman رضي الله عنهما.

Katika mambo ya kuvutia na kujifunza kutoka kwake ni kwamba, mama huyu alikuwa mtu aliyependa sana kuwaelimisha na kuwafundisha watu wengine elimu aliyokuwa nayo, na hivi ndivyo alivyofanya kwa mke wa Mtume ﷺ, Hafsah bint Umar رضي الله عنها.

Al-Shifa aliingia katika Uislamu mwanzoni kabla ya Mtume ﷺ hajafanya *Hijrah* (hajahamia Madinah), na alikuwa miongoni mwa Waislamu wa mwanzo waliohama kutoka Makkah na kwenda Madinah. Mama huyu alichukua ahadi na kiapo cha utii *(Bay'ah)* kwa Mtume ﷺ na kuahidi kuwa mtiifu kwake katika wakati ambao kufanya hivyo (kula kiapo cha utii kwa Mtume) ilikuwa ni jambo la hatari kutokana na uadui, chuki na mateso waliyokuwa wakifanyiwa Waislamu wa mwanzo.

Kutokana na taaluma aliyokuwa nayo ya udaktari, alikuwa pia akitoa kinga dhidi ya wadudu wanaong'ata kabla ya kuja Uislamu (Kabla ya kuja kwa Mtume ﷺ.) Baada ya *Hijrah*, mama huyu alikwenda kwa Mtume wa Allah ﷺ na kumwambia, "Ewe Mtume wa Allah, mimi nilikuwa nikitoa kinga dhidi ya wadudu wanaong'ata kabla ya kuja kwa Uislamu, na ningependa kukuonesha vipi nilikuwa nafanya."

Mtume ﷺ akasema, "Nioneshe." Ash-Shifa رضي الله عنها anasema, "Nikamuonesha Mtume ﷺ namna ninavyofanya, na Mtume ﷺ akasema endelea kufanya hivyo (kutoa kinga), na mfundishe ujuzi huu Hafsah رضي الله عنها (Mke wa Mtume ﷺ)". Katika mapokezi mengine Mtume ﷺ alisema, "Kwanini usimfundishe huyu (Hafsah) dawa ya magonjwa ya ngozi kama ulivyomfundisha kuandika".

Mama huyu alikua na nyumba yake baina ya msikiti wa Mtume ﷺ na soko. Mtume ﷺ alikuwa akimtembelea nyumbani kwake mara kwa mara, kiasi kwamba mama huyu aliandaa zulia maalum ambalo Mtume ﷺ alikuwa akikalia alipokwenda kumtembelea. Mama huyu alikuwa mtu mcha-Mungu na alidumu katika kufanya ibada na kutoa huduma ya tiba mpaka alipofariki.

Ni kutokana na ucha-Mungu aliokuwa nao na bidii katika kuwatumikia watu, Khalifa 'Umar Ibn Khattab رضي الله عنه alimteua kuwa afisa masoko katika mji wa Madinah. Yawezekana alikuwa mwanamke wa kwanza kuteuliwa kushika uongozi wa kijamii katika Ummah wa Kiislamu.

# Ar-Rumaysa binti Milhan (Ummu Sulaym) Al-Ansariyyah

## Aliyepewa zawadi na Allah

Mtume ﷺ anasema: *"Nilipoingia Peponi, nilisikia nyayo za mtu akitembea ndani ya Pepo – nilifahamishwa kuwa mtu huyo alikuwa ni Ar-Rumaysa' bint Milhan."*

Mama huyu anatoka katika familia iliyojaaliwa ucha-Mungu, familia iliyojitolea kila kitu kwa ajili ya Uislamu. Mtoto wa mama huyu alikuwa ni mmoja katiya maswahaba wakubwa na maarufu wa Mtume ﷺ Anas Ibn Malik na kaka wa mama huyu pia alikuwa swahaba wa Mtume ﷺ- Haram Ibn Milhan. Ndoa yake ya kwanza haikuwa ndoa yenye furaha; kulikuwa na migogoro mingi katika ndoa yake hii ya kwanza baina yake na mume wake, na sababu kubwa ya ugomvi baina yao ilikuwa mama huyu kuingia katika Uislamu. Mume wa mama huyu - Malik Ibn Nadhar, alifanya kila linalowezekana kuhakikisha mke wake (mama huyu) anaachana na dini yake mpya, dini ambayo alikuwa amekula kiapo cha utii. Lakini hakufanikiwa, kwani mama huyu alibakia kuwa mtiifu na mwaminifu kwa dini yake hii mpya – dini ya Kiislamu. Kwa upande mwingine, mama huyu aliendelea kumshawishi mwanae Anas akubali na kuingia katika Uislamu. Jitihada na ushawishi wake hatimaye vilizaa matunda, kwani mwanae Anas alitamka shahada na kuingia katika Uislamu.

Kulikuwa na matukio mengi ya ugomvi katika nyumba yao, hata hivyo mama huyu alibakia kuwa na msimamo imara, thabiti na mwenye subira na utulivu. Hatimaye mume wake alimuacha na mume wake huyo akahamia Syria ambako huko aliuwawa. Watu wa Ansari walikuwa wakimwita mama huyu kwa majina tofauti tofauti kama Sehlah, Ghumiysa', Rumiysa' Ramlah na Sahlah, lakini hatimaye alikuja kufahamika kwa jina la Ummu Sulaym رضي الله عنها.

Baada ya kuuwawa kwa mume wake nchini Syria, mama huyu alimtoa mwanae Anas رضي الله عنه kwa ajili ya kumtumikia Mtume ﷺ. Anas akaishi miaka kumi akimtumikia Mtume wa Allah ﷺ, na kwa hakika hii ilikuwa miaka bora na yenye faida kubwa kabisa katika umri wake. Ummu Sulaym رضي الله عنها alimuomba Mtume ﷺ amuombee dua mwanae Anas رضي الله عنه kwa Allah ili amruzuku elimu na mali na amneemeshe duniani na Akhera. Na Allah akajibu dua yake; Anas aliishi miaka mia moja na tatu na alijaaliwa kuwa na watoto wanane. Alikuwa na nyumba nzuri sana katika mji wa Basrah na alimiliki pia shamba kubwa na zuri. Alikuwa mtu mtanashati aliyependa kuvaa vizuri na kuzipamba nywele zake kwa kuzitia hina. Miongoni mwa wanae, wengi wao walikuja kuwa wanazuoni wakubwa. Baada ya kufariki dunia alikuja kuwa miongoni mwa wakazi wa moja ya bustani za Pepo.

Katika mji wa Madinah kulikuwa na kijana mmoja mtanashati sana akiitwa Abu Talhah رضي الله عنه, kijana huyu alikuwa kiongozi wa kabila lake. Wakati huo alikuwa bado hajasilimu na kuingia katika Uislamu, lakini alikuwa anafahamu kuwa mjane, Ummu Sulaym رضي الله عنها alikuwa na sifa nyingi zilizokuwa njema. Uaminifu wake, utiifu wake na ujasiri, zote hizi zilikuwa miongoni mwa sifa nzuri alizokuwa nazo mama huyu aliyekuwa mjane. Abu Talhah رضي الله عنه akatuma posa ili kumuoa mama huyu. Mama huyu alimjibu kuwa jambo hilo (la yeye kuolewa na Talhah) lilikuwa haliwezekani kwa sababu yeye alikuwa ni Muislamu na yeye Talhah alikuwa si Muislamu. Pale alipoona Abu Talhah رضي الله عنه akisisitiza kuwa lazima amuoe mama huyu, mama huyu alimuuliza yeye ni mwanaume wa aina gani; wakati mwingine alikuwa akiabudu miti inayoota katika ardhi, wakati mwingine akiabudu masanamu yaliyochongwa kutokana na mawe. Mama huyu alimuuliza kama Abu Talhah aliwahi kujiuliza kama vitu hivi vilikuwa na uwezo wa kutatua shida na matatizo yake wakati vyenyewe vilikuwa havina uwezo wa kujisaidia.

Abu Talhah رضي الله عنه aliposikia hoja zile, hakuwa na jibu. Aliendelea kujaribu kumshawishi, lakini mama huyu alikuwa mtu mwenye msimamo thabiti na usioyumba. Mama huyu alimjibu kuwa, katika hali ya kawaida, posa kutoka kwa mtu mwenye hadhi kama yake huwa haikataliwi, lakini imani yake ilikuwa na thamani na kamwe hawezi kuiacha. Alijitolea maisha yake kwa ajili ya Uislamu na kwa hakika alitimiza malengo yake. Kwa muda wote huo, Abu Talhah aliendelea kujinyima fadhila za kuwa Mwislamu. Hatimaye Abu Talhah

alimuuliza Ummu Sulaym kama atakubali kuolewa na yeye ikiwa ataingia katika Uislamu. Kusikia hivi, Ummu Sulaym رضي الله عنها alifurahi sana na kwa hili; Ummu Sulaym رضي الله عنهما alimwambia kuwa, mahari yake itakuwa yeye kukubali na kuingia katika Uislamu, na akamwambia mwanae Anas afanye maandalizi ya ndoa ya Ummu Sulaym رضي الله عنها (mama yake).

Mtume ﷺ alikuwa akimtembelea mara kwa mara na akimuombea dua kwa Allah Amzidishie neema na baraka Ummu Sulaym رضي الله عنها, Ummu Sulaym alikuwa mwenye furaha sana katika ndoa hii ya pili kwake, na haikuchukua muda walijaaliwa kupata mtoto katika ndoa yao na wakamwita mtoto yule Abu 'Umair. Siku moja Mtume ﷺ alitembelea nyumbani kwa familia hii (familia ya Abu Talhah na Ummu Sulaym رضي الله عنها) na kumkuta Abu 'Umair akiwa hana furaha. Mtume ﷺ akauliza kwanini mtoto yule alikuwa hana furaha. Ummu Sulaym alimjulisha Mtume ﷺ kuwa ndege wake aliyekuwa akimpenda na akipenda kucheza naye alikuwa amefariki. Mtume ﷺ alimpa pole na kum-bembeleza akimuonesha hisia na mapenzi ya hali ya juu.

Baada ya muda kupita, Abu 'Umair رضي الله عنه aliugua, na usiku mmoja joto la mwili wake lilipanda sana na hatimaye alifariki dunia. Wakati mtoto wao anafariki, mume wake (ambaye ndiye baba mzazi wa mtoto), hakuwepo nyumbani. Ummu Sulaym رضي الله عنها alionesha subira na ustahmilivu wa hali ya juu na kudhibiti hisia zake juu ya msiba huu. Hakumjulisha yeyote msiba huu wala hakupaza sauti akilia kutokana na uchungu wa kufiwa na mwanae. Mume wake aliporejea, hakutaka kumsumbua na kumtia simanzi mume wake aliyekuwa amerudi akiwa amechoka kutokana na kazi ngumu za mchana kutwa. Mume wake aliporejea, aliuliza juu ya hali ya mtoto wake na Ummu Sulaym alimjibu mume wake kuwa mtoto alikuwa anaendelea vizuri kuliko alivyokuwa hapo kabla. Kisha Ummu Sulaym رضي الله عنها akampakulia na kumkaribisha chakula cha jioni na akawa anaongea naye mambo mengine wakati mumewe akila. Baada ya mume wake kumaliza kula na kufurahia chakula na mazungumzo mazuri kutoka kwa mkewe, Ummu Sulaym رضي الله عنها alimuuliza mume wake, "Ikiwa mtu amepewa amana na mtu fulani, kisha mtu huyo akaja kuchukua amana yake, je inampasa mtu aliyepewa amana kurudisha amana aliyopewa?" Mume wake (Abu Talhah رضي الله عنه) akajibu, "Bila shaka anapaswa kurejesha amana ile bila kuwa na kinyongo chochote". Kisha Ummu Sulaym alimchukua mume wake na kuongozana naye mpaka chumbani ambapo mtoto

wao alikuwa amelala akiwa amefariki na kumwambia kwa sauti ya kutetema: “Allah Amemchukua mtoto aliyekuwa ametukabidhi kama amana ili tumlee.” Asubuhi walikwenda kuonana na Mtume ﷺ na Mtume ﷺ aliwaombea dua kwa Allah ili Allah Awajaalie na kuwapa baraka katika ndoa yao na maisha yao. Haikuchukua muda mrefu mtoto mwinine akazaliwa na wacha-Mungu hawa. Anas akam-beba mtoto huyu (mdogo wake) kwa mikono yake mpaka kwa Mtume wa Allah ﷺ; Mtume ﷺ akatafuna na kuilainisha tende na kumpa mtoto aliyezaliwa na akampa jina mtoto huyu, ‘Abdullah. Alimuombea dua mtoto huyu ili Allah amjaaliye mafanikio. Na kwa uwezo wake Allah, mtoto huyu alipokuwa alioa mke na kujaaliwa kupata watoto tisa wa kiume; na wote walihifadhi Qur’an kwa ukamilifu wake.

Anas anasimulia kuwa, mama yake alikuwa anamiliki mbuzi. Siku moja mama yake alitengeneza siagi kutokana na maziwa ya mbuzi huyu na kuihifadhi ndani ya chombo kidogo kilichotengenezwa kwa ngozi. Kilipojaa, alimuagiza mtoto wake wa kumlea aipeleke kwa Mtume ﷺ kama zawadi. Mtume ﷺ aliwaagiza watu wa nyumbani mwake waimimine na kumrejeshea chombo kile binti aliyeagizwa. Alirejea na chombo kile na alipofika alikining’iniza chombo kile kwenye msumari uliokuwa katika ukuta jikoni kwa Ummu Sulaym.

Ummu Sulaym alipokiona chombo kikiwa bado kimening’inizwa katika msumari na kukikagua, alikuta bado kimejaa na zaidi ya hapo kilikuwa kimejaa kiasi cha kukaribia kumwagika. Ummu Sulaym akamuuliza binti yake kwanini hakutekeleza maagizo aliyomwachia (hakupeleka siagi kwa Mtume ﷺ). Binti yule alijibu kuwa alipeleka siagi ile kwa Mtume ﷺ kama alivyomuagiza na kurejea akiwa na chombo kitupu na kukining’iniza katika msumari. Ummu Sulaym رضي الله عنها alishangazwa na muujiza huu.

Ummu Sulaym رضي الله عنها aliondoka na kwenda kwa Mtume ﷺ na kumsimulia miujiza iliyotokea. Mtume ﷺ akamjibu kuwa, hakika binti alimletea zawadi ambayo aliikubali na kuipokea na kumrejeshea chombo kikiwa kitupu.

Ummu Sulaym رضي الله عنها akaapa kwa jina la yule aliyemleta Mtume ﷺ na dini ya haki kuwa, hakika chombo kile kilikuwa bado kimejaa mpaka wakati huo. Mtume ﷺ akamwambia Ummu Sulaym رضي الله عنها kuwa hapaswi kushangaa; yeye alituma zawadi kwa mtume wa Allah ﷺ, na Allah amemtumia zawadi yeye Ummu Sulaym. Anapaswa kuitumia (kuila) na kuwalisha wengine.

Ummu Sulaym anasema, aliiweka siagi hii ndani ya chombo kikubwa, walikaa wakiitumia siagi hii yeye na watu wengine kwa muda wa miezi miwili.

Anas رضي الله عنه anasimulia kuwa, siku moja Abu Talhah alikuja nyumbani na kumwambia mkewe Ummu Sulaym kwamba Mtume ﷺ anaonekana kuwa dhaifu, na kwamba yawezekana alikuwa mwenye njaa. Alimwambia kwamba, ikiwa wana chakula chochote itakuwa ni kheri kubwa kwao ikiwa watakitoa na kumpelekea Mtume wa Allah ili ale. Ummu Sulaym رضي الله عنها akajibu kuwa, kulikuwa na mkate uliokuwa umehifadhiwa kwa kuzunguushwa ndani ya kitambaa. Abu Talhah رضي الله عنه aliondoka na kwenda msikitini na kumuomba Mtume ﷺ aongozana nae.

Mtume ﷺ alikubali na kuwaita watu waliokuwa wamekaa naye waongozane kwenda nyumbani kwa Abu Talhah. Watu wote walisimama na kuongozana na Mtume ﷺ. Abu Talhah رضي الله عنه alipoona hali hii, aliingiwa na wasiwasi, kwa sababu hakuwa na chakula cha kuwatosha watu wengi kiasi kile. Alipofika nyumbani, Abu Talhah رضي الله عنه alimueleza hofu aliyokuwa nayo mke wake - Ummu Sulaym رضي الله عنها. Ummu Sulaym رضي الله عنها alitabasamu na kumwambia mumewe asiwe na wasiwasi wowote; watakachokifanya ni kutoa chakula chote walicho nacho ndani ya nyumba yao. Na hiki ndicho alichokifanya mama huyu - Ummu Sulaym رضي الله عنها. Mtume ﷺ akaingia na akakiombea dua chakula kile. Kisha Mtume ﷺ akamuagiza Abu Talhah awaite watu kumi waingie ndani kula chakula. Hivyo watu kumi wakaingia kula chakula mpaka wakatosheka. Walipomaliza alimuagiza tena Abu Talhah awaite wengine kumi. Na akaendelea kwa utaratibu huu mpaka kiasi cha watu sabini (70) au themanini (80) wakawa wamekula na kutosheka kabisa, na bado kulikuwa na chakula kingi kimesalia!!

Mtume ﷺ alipomuoa Zaynab bint Jahash رضي الله عنهما, Ummu Sulaym aliandaa chakula maalum (tende na siagi) na kutuma mtu akipeleke kama zawadi. Na baada ya vita maarufu, vita vya Khaybar ambapo Mtume ﷺ alimuoa Safiyyah, ni mama huyu Ummu Sulaym رضي الله عنها ndiye aliyemuandaa na kumpamba bi harusi – Safiyyah, mama wa waumini na mke wa Mtume ﷺ. Mama huyu Ummu Sulaym رضي الله عنها pia alishiriki kikamilifu katika vita mbalimbali ambavyo Waislamu walikabiliana navyo. Anas anasimulia kuwa, katika vita vya Uhud mama yake ambaye ndiye Ummu Sulaym na mama Aishah رضي الله عنهما walikuwa wakijaza maji katika vyombo vilivyotengenezwa kwa

ngozi na kuwapa wapiganaji wa Kiislamu wenye kiu waliokuwa wamejeruhiwa. Wakati huo, Ummu Sulaym رضي الله عنها alikuwa mjamzito. Lakini hali hii ya ujauzito haikumzuia kwa namna yeyote kushiriki kikamilifu. Ummu Sulaym alishiriki kikamilifu katika vita vya Hunayn pia. Ummu Sulaym alibeba mkuki na mumewe Abu Talhah alipomuona katika hali hii, alimwambia Mtume ﷺ juu ya jambo hili. Mtume ﷺ akamuuliza Ummu Sulaym رضي الله عنها, "Kwanini umebeba mkuki?". Ummu Sulaym رضي الله عنها akajibu kuwa, "Ili kama askari wa jeshi la maadui atapita mbele yangu au karibu na mimi niweze kumuua. Mtume ﷺ akatabasamu na kufurahi.

Anas anasimulia kuwa, Mtume ﷺ alikuwa akiwatembelea mara kwa mara. Pale mtu alipomuuliza sababu ya yeye kuwatembelea mara kwa mara, Mtume alijibu kuwa alikuwa akijisikia huzuni toka kaka yake Ummu Sulaym رضي الله عنها - Haram Ibn Milhan رضي الله عنها alipouliwa na 'Amar ibn at-Tufayl akiwa miongoni mwa wasomaji Qur'an wengine wa Kiislamu. Haram Ibn milhan wakati anaaga dunia alitamka maneno ambayo mpaka leo yamebakia katika kumbukumbu ya vitabu vya historia ya Uislamu. Haram Ibn Milhan wakati akimaliza uhai wake na kufariki, alitamka maneno haya:

"Naapa kwa jina la yule anayeitosheleza Ka'bah hakika nimefanikiwa."

Kaka yake Ummu Sulaym رضي الله عنها (Ar-Rumaysa bint Milhan) aitwaye Sulaym Ibn Milhan pia aliuwawa shahidi katika vita hivi.

Siku moja Mtume alipowatembelea, Ummu Sulaym رضي الله عنها alimpa Mtume ﷺ tende na siagi. Mtume ﷺ akamwambia kuwa, aviweke mbali kwani siku hiyo Mtume ﷺ alikuwa amefunga. Mtume ﷺ alisimama katika moja ya kona za nyumba na kuswali, kisha alitumia muda mrefu kuomba dua kwa ajili ya familia hii ili Allah aibariki familia hii hapa duniani na kesho Akhera. Kisha Ummu Sulaym akamuomba amuombee dua mwanae. Alimuombea dua ndefu sana Anas ili Mwenyezi Mungu amjaalie yaliyokuwa ya kheri hapa duniani na kesho Akhera. Anas anaamini kuwa lazima Mtume ﷺ alimuombea kila kilichokuwa kizuri kwake hapa duniani na kesho Akhera.

رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنۡهُمۡ وَرَضُواْ عَنۡهُۚ

***"Mwenyezi Mungu Amewaridhia, nao wameridhika..."*** **(98:8)**

# Asmaa binti Abu Bakr As-Siddiiq

## Mama Aliyebashiriwa Pepo

Mtume ﷺ anasema: *"Utalipwa mikanda miwili (Peponi) kwa (mkanda) mmoja ulioutoa."*

Mama huyu alikuwa na uhusiano na Mtume ﷺ, kutokana na Mtume wa Allah kumuoa dada wa mama huyu, mama wa Waumini, Aishah رضي الله عنها. Baba wa mama huyu alikuwa ni Abu Bakr As-Siddiq ambaye alikuwa swahaba na rafiki mkubwa wa Mtume Muhammad ﷺ. Bibi wa mama huyu alikuwa akiitwa Ummu Al-Khayr Salma bint Sakhr. Shangazi zake walikuwa wafuasi waaminifu wa Mtume ﷺ kama vile Fardah, Qaribah na Ummu 'Amer. Babu wa Asma bint Abu Bakr رضي الله عنها alikuwa Abu Quhafah. Mume wa mama huyu alikuwa ni Zubayr Ibn 'Awwaam, ambaye pia alikuwa miongoni mwa maswahaba na mashujaa wakubwa katika historia ya Uislamu. Mwanae wa kiume, 'Abdullah ibn Zubayr, pia alikuwa mmoja kati ya maswahaba wacha-Mungu na waaminifu wa Mtume wa Allah ﷺ ambao walitoa maisha yao na uhai wao kwa ajili ya Uislamu. Kwa hakika historia ya mama huyu - Asma' bint Abu Bakr As-Siddiq رضي الله عنها, ni historia muhimu sana kwa mtu kuisoma na kujifunza kutoka kwake, kama ilivyokuwa kwa akina mama wengi walioishi wakati wa Mtume ﷺ.

Asma' bint Abu Bakr رضي الله عنها, alizaliwa miaka ishirini na saba (27) kabla ya Mtume ﷺ kuhamia Madinah (Kabla ya *Hijrah)*. Jina la mama yake ni Qatilah bint 'Uza na jina la baba yake ni Abu Bakr. Wazazi hawa walifunga ndoa kabla ya kuja kwa Uislamu; Asma' رضي الله عنها alizaliwa wakati mama yake akiwa na umri wa miaka ishirini na moja (21) tu. Asma' رضي الله عنها na 'Abdullah رضي الله عنه ni watoto wawili waliozaliwa katika ndoa hii. Kwa muda mrefu sana, mama wa Asma' رضي الله عنها alikataa kuukubali Uislamu; lakini baadaye baada ya

Makkah kukombolewa, mama yake alikubali Uislamu, akasilimu na kuchukua ahadi ya utii kwa Mtume ﷺ. Asma' رضي الله عنها aliukubali na kuingia katika Uislamu kutokana na ushawishi na kulinganiwa na baba yake – Abu Bakr رضي الله عنه. Ucha-Mungu, msimamo thabiti, imani ya kweli, busara na ujasiri na kwa hakika sifa zote njema zinazoelezwa na Uislamu zilikuwa zinapatikana kwa mama huyu Asma' bint Abu Bakr رضي الله عنها. Wakati ambapo Mtume ﷺ na baba yake walipojihifadhi na kupumzika katika pango la Thawr, baada ya kuondoka Makkah wakielekea katika mji wa Madinah, ni mama huyu Asma' bint Abu Bakr رضي الله عنها aliyekuwa akiwapelekea chakula wakati huo akiwa bado ni binti mdogo. Baada tu ya kuondoka, Abu Jahl alikwenda nyumbani kwa Abu Bakr As-Siddiq رضي الله عنه kuwatafuta akiwa amejawa na hasira na chuki ya hali ya juu. Alimuuliza Asma baba yake yuko wapi? Asma رضي الله عنها alijibu kuwa alikuwa hafahamu baba yake yuko wapi. Alithibitisha ukorofi na ukatili aliokuwa nao kwa kumtandika Asma kofi kwa nguvu sana; lakini ili asifichue siri aliyokuwa nayo moyoni, Asma رضي الله عنها alimkabili kwa ujasiri mkubwa na uvumilivu.

Asma' رضي الله عنها alikuja kufahamika kwa jina la *Dthat An-Nitaqayn*. Kuna simulizi ya kusisimua na ya kufurahisha sana juu ya namna gani alikuja kupewa jina hili. Mkanda unaovaliwa na wanawake kiunoni kwa kiarabu unaitwa *Nitaq*. Wakati Mtume ﷺ na Abu Bakr As-Siddiq walipokuwa wakijiandaa kuondoka kuelekea Madinah, Asma' aliweka vyakula katika mkoba wa ngozi, lakini kulikuwa hakuna kamba ambayo angeweza kuitumia kufunga sehemu ya juu ya mkoba ule. Hivyo aliupasua mkanda wake vipande viwili na kutumia vipande vile kuufunga mkoba ule uliotengenezwa kwa ngozi. Mtume ﷺ akamuombea dua na kumwambia badala ya mkanda huu mmoja alioutoa hapa duniani, Allah Atamlipa mikanda miwili Peponi. Hii ilimaanisha kuwa mama huyu alibashiriwa Pepo. Katika namna hii, Mtume ﷺ alikuwa akiwabashiria habari njema (Pepo) maswahaba wake.

Baada ya Mtume ﷺ na baba yake Asma, Abu Bakr رضي الله عنه kuondoka, Asma' aliachwa na babu yake ambaye alikuwa kipofu, Abu Quhafah. Mzee huyu Abu Quhfah alipofahamu kuwa mwanae Abu Bakr amehama aliingiwa na huzuni sana. Pia alikuwa na wasiwasi kama mwanae atakuwa ameacha fedha yeyote kwa ajili ya matumizi. Asma anasimulia kuwa, walikuwa na kiasi kama cha Dinari elfu nne au tano hivi, na fedha zote hizo alikuwa amezichukua

baba yao na kuondoka nazo kwa ajili ya matumizi ya njiani wakiwa safarini kuelekea Madinah. Hata hivyo, alimkabili babu yake na kumfahamisha kuwa kulikuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi, na kwamba kulikua hakuna mapungufu yeyote. Ili kumridhisha juu ya kuwepo kwa fedha za kutosha, Asma alikusanya vijiwe vilivyokuwa na umbile la Dinar na kuvisambaza juu ya kitambaa kisha akamuongoza babu yake kwa kumshika mkono na kupapasa vijiwe vile; Abu Quhafah alifurahi sana kuona kuwa mtoto wake Abu Bakr رضي الله عنه hakuwapuuza na kuwaacha katika mazingira magumu. Asma alifanya hivi kumfanya babu yake awe na amani katika nafsi; Lakini ukweli ni kuwa, akiwa na imani thabiti juu ya Allah, Abu Bakr As-Siddiq رضي الله عنه alikuwa amechukua mali zote na kwenda kuzitumia katika njia ya Allah na Mtume wake ﷺ.

Mume wa Asma Bint Abu Bakr رضي الله عنها alikuwa anaitwa Zubayr ibn 'Awwaam رضي الله عنه; huyu pia alikuwa rafiki na swahaba mkubwa wa Mtume ﷺ na alikuwa mtoto wa Safiyyah bint 'Abdul Muttalib. Alipohamia katika mji wa Madinah, alimiliki nyumba ambayo aliitumia kama makazi yake, alimiliki pia upanga na farasi. Ilikuwa ni jukumu la Asma kumtunza na kumlisha farasi huyu. Siku moja Mtume ﷺ alimuona Asma akitembea kuelekea nyumbani kwake huku akiwa amebeba mzigo wa nyasi kavu kwa ajili ya farasi. Mara moja Mtume ﷺ alimfanya ngamia wake alale chini ili kumpa nafasi Asma رضي الله عنها kupanda juu yake. Hata hivyo, Asma رضي الله عنها aliona aibu sana na alihisi kufanya hivyo kutamuhuzunisha sana mume wake, mtu aliyekuwa mwenye furaha sana kwa nafasi yake. Asma رضي الله عنها alikuwa mwanamke mtiifu na mwaminifu sana kwa mume wake. Jambo lolote ambalo alihisi litamfedhehesha au kumfanya mume wake asiwe mwenye furaha alijiepusha nalo. Hivyo alikataa fursa aliyopewa na Mtume ﷺ na akapendelea kuendelea kutembea kuelekea nyumbani kwake. Alipomsimulia mume wake, mume wake alimwambia kuwa alipaswa kukubali na kupanda juu ya ngamia, kwa kufanya hivyo ilikuwa ni jambo bora kuliko kukataa na kuamua kutembea na mzigo wa nyasi kichwani.

Asma' aliondoka Makkah kuelekea Madinah akiwa mjamzito. Alipofika katika bonde la Quba alianza kujisikia uchungu na akajifungua mtoto wa kiume, waliyemwita 'Abdullah ibn Zubayr. Hakika hili lilikuwa ni tukio muhimu sana kwa Waislamu. Kwa muda mrefu hakukuwa na mtoto aliyezaliwa miongoni

mwa Waumini. Makafiri walikuwa na furaha na wakijisifu kwa hali hii ya kutozaliwa mtoto yeyote miongoni mwa waumini. Walikuwa wakitamba kuwa muda si mrefu kizazi cha Waislamu kitafutika. Waislamu wote wakawa wenye furaha kama alivyokuwa mwenye furaha Mtume ﷺ. Alimbeba mtoto aliyezaliwa kwa mikono yake na kuwapongeza wazazi wake. Kisha alimung'unya tende kwa mdomo wake na kumlisha mtoto yule. Tendo hili lilikuwa jambo la heshima kubwa sana, jambo ambalo liliwafanya wanafamilia wote wawe wenye furaha na kujihisi wamepewa heshima ya hali ya juu.

Alipoinukia na kuwa mkubwa, 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه alikuwa mtu mwenye uelewa mkubwa, msomi (mwanazuoni) na mtu jasiri. Baadaye mama yake alikuja kuishi naye. Abdullah alipoondoka kuelekea Makkah, Asma aliongozana naye.

Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه hakuwahi kuwakubali Banu Umayyah kuwa Makhalifa, bali aliendelea kufanya jitihada za kuanzisha Ukhalifa wake; alifanikiwa kuwashawishi na kuungwa mkono na watu wengi sana na hii ni kwa sababu watu wengi walimuamini kuwa alikuwa mtu mwenye nguvu, mwanazuoni (mtu mwenye elimu kubwa), mcha-Mungu na mtu mwenye busara. Hata hivyo, pale 'Abdul Malik Ibn Marwan alipokuja kuushambulia mji wa Makkah, alifanikiwa kuviteka baadhi ya vitongoji. 'Abdul Malik Ibn Marwan akamtuma Hajjaj Ibn Yusuf kama muwakilishi wake katika mji wa Hijaz (ambayo leo ndio Makkah). Hajjaj akayaongoza majeshi ya Syria na kuizingira Hijjaz yote huku akiushambulia mji kutoka pande zote; vita vikali vikaanza baina ya majeshi ya pande mbili. Wakati huo, Hijjaz (Makkah) ilikuwa chini ya uongozi wa 'Abdullah ibn Zubayr, ambaye kama tulivyosema hapo kabla, hakuwahi kusalimu amri na kuukubali utawala wowote uliotokana na Banu Umayyah.

Katika wakati mzito na mazingira magumu ya vita, 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه alikwenda kuonana na kuongea na mama yake, ambaye ndiye Asma bint Abu Bakr رضي الله عنها. Pale mama yake alipomwambia kuwa yeye Asma alikuwa anaumwa, 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه alimwambia mama yake kuwa, mwanadamu hupata amani na kupumzika baada ya kufa kwake tena akiwa ametenda matendo yenye kumridhisha Allah. Mama yake (Asma رضي الله عنها) alitabasamu na kumuuliza kwa maskhara ikiwa alikuwa anataka yeye (Asma) afariki. Mama alimwambia mwanae kuwa angependa yeye aendelee kuishi kwani alitamani kuona mwisho wa jitihada za mwanae. Ikiwa atauwawa

shahidi, yeye atalipokea tukio hilo la kuuwawa kwa mwanae kwa subira na uvumilivu; na kama atamshinda adui yake katika vita hivyo bila shaka atakuwa mtu mwenye furaha.

Vita ngumu na kali ilikuwa inaendelea katika mji wa Makkah na jeshi la 'Abdullah ibn Zubayr ibn Awwaam lilikuwa linaelekea kushindwa. 'Abdullah ibn Zubayr alimuuliza mama yake ikiwa yeye 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه anaweza kusalimu amri katika vita vile. Asma رضي الله عنها alimwambia mwanae 'Abdullah ibn Zubayr kuwa, ikiwa anaamini kuwa yuko katika haki, basi hapaswi kuogopa kufa. 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه alimwambia mama yake kuwa, anahofia kuwa maadui wataukata kata mwili wake baada ya yeye kuwa wamemuuwa. Mama yake alimjibu kuwa ilikuwa haina maana yeyote kwa kile watakachokifanya juu ya mwili wake baada ya kuwa amefariki. Mama yake aliongeza kumwambia mwanae kuwa, baada ya mbuzi kuchinjwa, kuchunwa ngozi yake hakuwezi kusababisha maumivu yeyote. Mama huyu aliongeza kumwambia mwanae kuwa, kifo hakipaswi kuwa tishio kwa mtu shujaa na jasiri. Na kwamba kifo chenye heshima ni bora kuliko uhai na maisha ya amani yasiyokuwa na heshima au kuheshimiwa. Na kwamba maisha ya kidhalili na yasiyokuwa na heshima hayakuwa kitu kilichomfaa kijana shujaa kama yeye. Hivyo 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه alirejea katika uwanja wa vita na kuendelea na mapambano akiwa na nguvu na ari mpya. Alipambana kwa ujasiri mkubwa, hata hivyo, kwa kuwa wapiganaji wake walikuwa wamebaki wachache kwa idadi, 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه aliuwawa shahidi katika mapigano yale. Mtu katili Hajjaj ibn Yusuf aliuning'iniza mwili wa 'Abdullah ibn Zubayr ili kila mmoja ashuhudie kuwa 'Abdullah bn Zubayr ameuwawa. Hata baada ya siku tatu, bado Hajjaj Ibn Yusuf hakuushusha mwili wa 'Abdullah ibn Zubayr. Siku ya tatu, mama wa 'Abdullah ibn Zubayr - Asma Bint Abu Bakr As-Siddiq رضي الله عنها , ambaye kwa wakati huo alikuwa ni mzee wa takriban miaka tisini na saba (97) alikwenda kujaribu kutaka apewe mwili wa marehemu mwanae. Kwa kuwa alikuwa amepoteza uwezo wa kuona mbali kutokana na umri kuwa mkubwa, aliweza kuifahamu njia kwa taabu. Kwa uchungu mkubwa, aliuliza ikiwa muda haujafika kwa mwili wa marehemu mwanae kushushwa chini.

Hajjaj alipomuona mama wa 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه akiwa amesimama pembeni ya mwili wa marehemu mwanae, Hajjaj alimuamuru

mtu aende na kumchukua mama yule na kumpeleka kwake. Kwa ujasiri mkubwa, Asma bint Abu Bakr رضي الله عنها, mama wa 'Abdullah ibn Zubayr alisema kuwa hawezi kwenda kumuona muuaji wa mwanae. Hajjaj Ibn Yusuf alipopelekewa majibu ya mama yule, alishikwa na hasira na kumtuma tena yule mtu akamwambie mama wa 'Abdullah ibn Zubayr – Asma bint Abu Bakr رضي الله عنها kuwa, ikiwa hatoenda mwenyewe kwa Hajjaj ibn Yusuf, basi atakokotwa kwa nywele zake kupelekwa kwa Hajjaj. Kama ambavyo Asma bint Abu Bakr رضي الله عنها alivyosimama imara dhidi ya Abu Jahl miaka mingi iliyopita, mama wa Kiislamu, mama wa 'Abdullah ibn Zubayr – Asma bint Abu Bakr رضي الله عنها alimjibu kwa ujasiri mkubwa kuwa, yeye Asma bint Abu Bakr رضي الله عنها na mama wa 'Abdullah ibn Zubayr hawezi kwenda kumuona mtu asiyestahili kuheshimika na mwenye kudharaulika; haya yalikuwa ndio majibu ya mwisho na msimamo wa Asma bint Abu Bakr – mama wa 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنهما kwa kiongozi wa majeshi. Unaweza kuona ni kwa kiasi gani mama huyu alikuwa na imani ya kweli na msimamo thabiti. Hajjaj alipoona kuwa vitisho vyake havikusaidia kitu na mama Asma bint Abu Bakr رضي الله عنها ameshikilia msimamo wake, aliamua kwenda yeye mwenyewe alipokuwa amesimama Asma bint Abu Bakr رضي الله عنها. Hajjaj alimuuliza Asma kama ameona jinsi alivyomfanya mwanae. Mama Asma bint Abu Bakr رضي الله عنهما alimjibu Hajjaj kuwa yeye (Hajjaj) amekuwa sababu ya kumaliza uhai wa mwanae hapa duniani, lakini mwanae alikuwa ameyaanza maisha matukufu na yaliyokuwa bora, maisha ya kudumu, maisha ya Peponi. Kisha Asma akaongeza kumwambia Hajjaj - kiongozi wa majeshi kuwa, yeye (Asma) alimsikia Mtume ﷺ akisema kuwa: *"Kuna mtu atakuja kutoka katika kabila la Banu Thaqif ambaye atakuwa muongo, katili na muovu sana".*

Na kwamba leo alikuwa amemuona kwa macho yake mwenyewe, ambaye ni Hajjaj ibn Yusuf. Kusikia vile, Hajjaj ibn Yusuf akaondoka kimya kimya bila kusema kitu.

Siku moja mama huyu (Asma bint Abu Bakr رضي الله عنهما ) alipokwenda katika msikiti Mtukufu wa Makkah, alimsikia Hajjaj ibn Yusuf akiwahutubia watu akiwa juu ya mimbari. Pamoja na kwamba alikuwa mzee sana, lakini bado alikuwa hajapoteza nguvu kubwa ya imani yake aliyokuwa nayo; alikwenda na kusimama karibu kabisa na Hajjaj. Hajjaj alipomuona mama yule, Hajjaj alisema, mwanae 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه ameeneza upotofu na

unafiki katika nyumba ya Allah hivyo aliamua kumpa adhabu kali kabisa. Hapo hapo Asma' (mama wa 'Abdullah ibn Zubayr ibn Awaam رضي الله عنهما) akamjibu kuwa: "Mwanangu hakuwa mtu mnafiki; mwanangu alikuwa mtu mcha-Mungu, mwanazuoni mkubwa ambaye muda wote alikuwa akimuabudu Mola wake na akifanya kazi kwa bidii katika kuutumikia Ummah wa Kiislam. Alikuwa kielelezo kizuri cha uaminifu na uadilifu. Kwa upande mwingine, wewe Hajjaj ni mtu unayejulikana kuwa wewe ni mtu muongo, mnafiki na mtu fitina. Unapaswa kumuhofu Mwenyezi Mungu na adhabu zake ambazo humfika mtu katika wakati ambao mtu hakutarajia kuwa zitamfika". Hajjaj akajifanya hajamsikia, akaendelea na hotuba yake; kisha kwa sauti kubwa, akawaamuru watu wasimame na wajiandae kwa Swala. Katika mkusanyiko ule, alikuwepo pia 'Abdullah ibn 'Umar ibn Khattab رضي الله عنهما, akapaza sauti na kusema, "Ewe Hajjaj! Nikikwita muongo na mnafiki ntakuwa sijasema tofauti na ukweli. Naapa kwa jina la Mola wa Walimwengu wote – Allah, kuwa katika maisha yake yote 'Abdullah ibn Zubayr ibn Awwaam رضي الله عنهما, hata siku moja hajawahi kwenda japo hatua moja kinyume na mafundisho ya Allah. Sasa nakiri na kushuhudia hadharani kuwa 'Abdullah ibn Zubayr alikuwa mtu mcha-Mungu aliyefunga mchana na kusimama usiku kuswali. Siku zote alikuwa akiijua haki na akiisimamia na kuipigania haki.

Kisha Abdullah ibn Umar ibn Khattab aliondoka na kwenda ulipokuwa mwili wa 'Abdullah Ibn Zubayr رضي الله عنهما, ambao mpaka wakati huo ulikuwa bado umening'inizwa. Kwa sauti nzito na yenye kutetema, Abdullah Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, "Assalam Alaykum ewe Abu Khubaib; Assalam Alaykum Abu Khubaib." (Amani iwe juu yako ewe Abu Khubaib; Amani iwe juu yako Abu Khubaib)

Khubaib lilikuwa jina la ukoo la 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنهما. Huku akiwa anauangalia mwili wa 'Abdullah (marehemu) aliionya nafsi yake isijihusishe na kupigania madaraka. Watu wenye kuheshimika na wenye hadhi kubwa, mara nyingi hupoteza heshima zao na hadhi zao katika kupigania madaraka. Kisha alimuomba Allah ampe nafasi 'Abdullah ibn Zubayr ibn Awwaam katika Pepo yake Tukufu. Baada ya siku chache baada ya hapo, Hajjaj aliutupa mwili wa marehemu 'Abdullah ibn Zubayr ndani ya kaburi kwa maelekezo aliyopewa na 'Abdul Malik ibn Marwan. Mama Asma' alipopata habari juu ya tukio hili la kutupwa mwanae, aliagiza watu wakauchukue mwili

wa marehemu mwanae. Aliuosha mwili wa mwanae, Waislamu wakauswalia mwili wa 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه, kisha mama akaruhusu mwili wa marehemu mwanae uzikwe; na 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنه alizikwa kwa taratibu na heshima zote alizostahili kupewa kama Muislamu.

Hajjaj Ibn Yusuf akapokea amri kutoka kwa gavana nchini Syria. Amri hiyo ilimtaka yeye mwenyewe Hajjaj aende kwa Asma' bint Abu Bakr رضي الله عنها na amuulize ikiwa alikuwa na ombi lolote au alikuwa anahitaji kitu chochote na kwamba serikali ilikuwa iko tayari kumtekelezea kile akitakacho. Hajjaj akaenda nyumbani kwa Asma kufikisha salam na ujumbe kutoka kwa gavana 'Abdul Malik Ibn Marwan. Asma' alimfukuza kwa hasira; kwa sauti kali kabisa, alimwambia Hajjaj kuwa yeye alikuwa hana haja ya kitu chochote na kumuamuru kuwa aondoke ndani ya nyumba yake mara moja; alikataa fursa aliyokuwa amepewa mbele ya macho ya Hajjaj. Alimuuliza Hajjaj ikiwa yeye (Hajjaj) mtu asiyekuwa na aibu alikuja kwa nia ya kutonesha kidonda na machungu ya marehemu mwanae 'Abdullah ibn Zubayr. Asma - mama wa 'Abdullah ibn Zubayr رضي الله عنهما akamwambia Hajjaj kuwa kwa hakika Hajjaj alikuwa mzigo katika ardhi ya Allah, na kwamba anamuona kama mtu muovu na mtu asiyefaa kuwepo.

Asma' رضي الله عنها alikuwa akiswali kwa unyenyekevu mkubwa sana. Zubayr ibn 'Awwaam رضي الله عنه anasimulia kuwa, siku moja alikwenda nyumbani kwake na kumkuta akiswali huku akilia; alikuwa akirudia rudia maneno haya kutoka katika Qur'an:

فَمَنَّ ٱللَّهُ عَلَيْنَا وَوَقَىٰنَا عَذَابَ ٱلسَّمُومِ ﴿٢٧﴾

***"Basi Mwenyezi Mungu ametufanyia ihsani, (Ametutia Peponi) na ametuokoa na adhabu ya pepo za Moto."* (52:27)**

Zubayr Ibn Awwaam رضي الله عنه alipomuona Asma bint Abu Bakr akiwa amezama katika kumkumbuka Allah, aliondoka nyumbani na kuelekea sokoni. Aliondoka na kurejea baada ya muda mrefu sana na kumkuta akiwa bado yumo ndani ya Swala na akiwa katika unyenyekevu wa hali ya juu.

Asma' رضي الله عنها alikuwa mtu mwenye kumbukumbu nzuri sana. Alikuwa akisikia jambo hata mara moja, basi alikuwa akitunza kumbukumbu ya jambo hilo na katu alikuwa halisahau. Kama ilivyokuwa kwa mama Aishah, Ummu

Salamah na Asma' bint Yazid ibn as-Sakan al-Ansariyyah رضي الله عنهما, mama huyu (Asma) alipokea hadithi nyingi za Mtume ﷺ. Maswahaba wengi wa Mtume ﷺ na Waislamu waliowafuatia maswahaba walikuwa wakienda kwake kwa ajili ya kuomba muongozo na kuthibitisha usahihi wa hadithi walizokuwa wakizisikia au kuzipokea. 'Abdullah ibn Zubayr ibn Awwaam رضي الله عنه, 'Urwah ibn Zubayr ibn Awwaam, 'Abdullah ibn 'Abbas رضي الله عنهما, Fatmah bint Mundhir ibn Zubayr na 'Abdullah ibn Kisan رضي الله عنهم ni miongoni mwa maswahaba waliokuwa wakifanya hivyo.

Asma' bint Abu Bakr As-Siddiq رضي الله عنها alifariki dunia mwaka wa 73 Hijiriya. Wakati anafariki, alikuwa na umri wa takriban miaka mia moja (100), lakini hata wakati alipokuwa na umri mkubwa kiasi hicho, alikuwa bado ana meno yake kamili (alikuwa hajang'oa jino hata moja) na akiwa na kumbukumbu nzuri kabisa.

رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنۡهُمۡ وَرَضُواْ عَنۡهُ

***"Mwenyezi Mungu Amewarirdhia, nao wameridhika."* (98:8)**

# Asma binti Umays

## Mke wa Maswahaba Watukufu

Kuwa miongoni mwa watu waliohama kutoka Makkah kwenda Madinah kwa ajili ya Allah na Mtume wake ﷺ ilikuwa ni jambo lenye heshima na hadhi kubwa. Baadhi ya maswahaba walielewa kuwa dhana na tendo la Hijrah ni makhususi na maalum kwa ajili ya kuhama kutoka katika mji wa Makkah na kwenda katika mji wa Madinah tu na si vinginevyo. Hivyo huchukulia kuwa, wale waliohamia Uhabeshi (Ethiopia ya leo) na kukaa huko mpaka wakati wa vita vya Khaybar hawana malipo yeyote kutokana na kuhama kwao.

Fikra hizi na maoni haya yalimfanya Asma رضي الله عنها kuwa mtu mwenye simanzi, hivyo aliondoka haraka na kwenda kwa Mtume ﷺ na kumuuliza juu ya kile ambacho baadhi ya maswahaba walikuwa wakisema. Katika majibu yake juu ya jambo hili, Mtume ﷺ alijibu kuwa, *"Wewe umehama mara mbili na watu wengine wamehama mara moja."*

Maneno ya Mtume ﷺ hayakuwa maneno yaliyokusudia kumfanya Asma رضي الله عنها aondokane na unyonge na kuwa mwenye furaha. Bali yalikuwa ni maneno yaliyoendana na ukweli halisi, na yalikuwa maneno yaliyolenga kuondoa utata katika jambo ambalo lilikuwa likiwatatiza watu. Walithibitisha kuwa wale walioondoka Makkah na kwenda Uhabeshi (Ethiopia) ili kuhifadhi imani na dini yao kwa hakika walikuwa wamefanya Hijrah kwa ajili ya Allah. Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

أَلَمْ تَكُنْ أَرْضُ ٱللَّهِ وَٰسِعَةً فَتُهَاجِرُوا۟ فِيهَا

***"...Ardhi ya Mwenyezi Mungu haikuwa na wasaa na nyinyi kuhamia humo?"* (4:97)**

Watu waliofanya Hijrah kwenda Uhabeshi (Ethiopia) walikuwa wahamiaji waliokuwa wakipenda na wakitamani siku moja wawe pamoja na mtu

waliyempenda – Mtume wa Allah ﷺ na maswahaba zake. Walipopata habari kuwa Mtume ﷺ amehamia katika mji wa Madinah na sasa alikuwa mwenye nguvu, waliondoka haraka sana kwenda kuungana na kuishi na mtu waliyempenda kuliko yeyote na kuliko chochote – Mtume Muhammad ﷺ. Walipofika Madinah wakiwa wamechoka kutokana na safari ya muda mrefu wakikatiza majangwa na jua kali, waliambiwa kuwa, Mtume Muhammad ﷺ na maswahaba zake wameondoka na kwenda katika vita vya Khaybar. Pamoja na kuwa ndio kwanza walikuwa wamefika wakiwa wamechoka sana kutokana na safari ngumu na ndefu kutoka Uhabeshi, miguu yao ilitii tamaa na matakwa ya nyoyo zao, hivyo wote wakaanza safari kuelekea Khaybar.

Walipofika Khaybar, walikuwa wamechelewa; vita vilikuwa vimemalizika na Khaybar ilikuwa tayari imekombolewa. Mtume wa Allah ﷺ akasema: *"Sifahamu nifurahie nini zaidi, kuikomboa Khaybar au kuwasili kwa Ja'far na ndugu zake waliowasili wakitokea Uhabeshi (Ethiopia)!"*

Asma bint Umays رضي الله عنها aliingia katika Uislamu mapema sana, yeye pamoja na mume wake Ja'far. Kwa hakika walikuwa ndio kwanza wametoka kufunga ndoa siku si nyingi walipoanza safari kuhamia Uhabeshi (Ethiopia ya leo) kwa ajili ya Allah. Kuwa kwao maharusi hakukuwazuia wao kuhama kwa ajili ya Allah, kwa sababu tayari nafsi zao zilikuwa zimeingiwa na kujawa na imani ya kweli, imani ya Kiislamu. Badala ya kukaa Makkah na kufurahia masiku ya mwanzo ya ndoa yao (fungate), wao walikuwa katika mapambano ya kunusuru imani yao na dini yao. Hili kwa muumini wa kweli anayemuamini Allah na Mtume wake ﷺ, lilikuwa jambo bora na lenye thamani kwa kuwa linaambatana na ujira bora na mkubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mlezi.

Asma bint Umays رضي الله عنها alikuwa mtu mcha-Mungu sawa na alivyokuwa mume wake Ja'far ibn Abi Talib رضي الله عنه. Alikuwa mwanamke mwenye uelewa mkubwa na mwenye kujua wajibu wake. Ushahidi wa haya unaweza kuonekana wazi katika tabia zake, mwenendo wake na imani yake. Mtume ﷺ alifikia kumwita kuwa yeye (Asma bint Umays رضي الله عنها) alikuwa mmoja kati ya "Dada wenye imani".

Ikiwa mtu atahesabu idadi ya miaka ambayo wahamiaji wa Kiislamu waliishi katika ardhi ya Uhabeshi (Ethiopia) wakiwa katika ardhi ya ugenini, na kama mtu atazingatia pia mbinu chafu za Maquraishi zilizokuwa zikipangwa

dhidi yao, ataweza kuona ni kwa kiwango gani waumini hawa walikuwa na subira na msimamo thabiti. Kwa sababu muda walioishi Uhabeshi (Ethiopia) haukuwa muda mfupi. Bali Asma bint Umays رضي الله عنها aliishi Uhabeshi kwa miaka kumi na tano (15), na ni katika muda huo baadhi ya watoto wake walizaliwa. Mtume ﷺ alikuwa akiwasiliana nao mara kwa mara kwa kuwatumia mjumbe ambaye aliwapelekea habari kuhusu hali na maendeleo ya Mtume ﷺ na Waislamu wengine. Walikuwa pia wakifahamishwa kuhusu Ayah mpya zilizoshushwa na shariah mbalimbali ambazo zilikuwa zimeshushwa na hivyo kutakiwa kuzifuata. Miongoni mwa watu waliokuwa wakitumwa huko Uhabeshi alikuwa ni swahaba Amar ibn Umayyah ad-Damri رضي الله عنه.

Asma bint Umays alipoondoka Uhabeshi (Abyssinia), aliondoka akiwa ameongozana na watoto wake akiwemo ‘Abdullah na Muhammad. Hata hivyo hakufahamu mtihani mzito ambao ulikuja kumkabili muda mfupi baadaye. Baada ya muda, Mtume ﷺ alimtuma mume wake pamoja na maswahaba wengine katika vita vya Mu’tah. Mume wa Asma bint Umays alitakiwa kushika uongozi wa jeshi ikiwa Zayd Ibn Haarith atauwawa shahidi. Vita hivi vya Mu’tah vilikuwa vita vya kwanza vya aina yake baina ya Waislamu na Warumi katika historia ya Uislamu. Jeshi la Waislamu lilikuwa na wapiganaji wapatao elfu tatu (3000) na wapinzani wao (jeshi la Warumi) walikuwa na wapiganaji wapatao laki moja (100,000). Sababu ya kutokea vita ilikuwa ni kutokana na Mtume ﷺ kumtuma Al-Harith ibn ‘Umayr al Azdi رضي الله عنه kwa mfalme wa Basrah akiwa na barua ya kumtaka mfalme yule asilimu. Al-Harith alishambuliwa na kuuwawa na Shurahbeel ibn ‘Amr al–Ghassani, ambaye alikuwa rafiki na akiwaunga mkono Warumi. Mtume ﷺ alikasirishwa sana na tukio hili. Hivyo aliwakusanya Waislamu na kuwataka kwenda kulipa damu ya Al–Harith. Mtume ﷺ aliwapa maelekezo kuwa, ikiwa kamanda wa kwanza wa Waislamu atauwawa shahidi, basi kamanda wa pili alipaswa kushika nafasi ya uongozi wa jeshi; na kama kiongozi wa pili wa jeshi la Waislamu atauwawa shahidi, basi kamanda wa tatu atatakiwa kushika uongozi wa majeshi ya Waislamu. Na kama kiongozi wa tatu wa jeshi la Waislamu naye atauwawa, basi Waislamu watatakiwa kukubaliana nani awe kiongozi wa jeshi lao kutoka miongoni mwao.

Makamanda hao watatu walikuwa: Zayd ibn Haarithah, Ja’far ibn Abu Talib na Abdullah ibn Rawaahah رضي الله عنهم. Makamanda wote watatu

waliuwawa wakiwa mashahidi katika vita hivi, akiwemo mume wa Asma bint Umays رضي الله عنه. Baada ya hapo Waislamu wakamchagua Khaalid ibn al–Waleed رضي الله عنه kuwa kamanda wa jeshi la Waislamu. Kutokana na mbinu za kijeshi alizokuwa nazo na umahiri mkubwa aliokuwa nao, aliwaongoza Waislamu na kuwashinda Warumi pamoja na majeshi ya Ghassan aliyekuwa akiwaunga mkono. Alirejea na wapiganaji wa Kiislamu wakiwa washindi, katika vita ambavyo jeshi la maadui lilikuwa kubwa sana na lenye nguvu.

Msiba kwa Waislamu ulikuwa mkubwa, kwa sababu makamanda wao watatu walikuwa wameuwawa wakiwa mashahidi. Vita vya Mu'tah ilikuwa ni vita ya kwanza na ya mwisho aliyoshiriki Ja'far Ibn Abittalib رضي الله عنه dhidi ya maadui wa Mwenyezi Mungu na akipigana katika njia ya Allah.

Kama ulivyokuwa mkubwa mchango wa Ja'far رضي الله عنه kule Uhabeshi (Abyssinia) mbele ya mfalme Najashi, Ja'far alikuwa na mchango mkubwa pia katika uwanja wa vita. Alipoona kuwa farasi wake alikuwa akimfanya ashindwe kupambana kwa uhuru zaidi katika uwanja wa vita, aliamua kushuka kutoka juu ya farasi, na kumjeruhi farasi yule ili maadui wasiweze kumtumia na kisha akaingia katikati ya uwanja wa vita. Mkono wake ulishambuliwa na kukatwa akiwa amebeba bendera na hivi ndivyo alivyokuja kuuwawa akiwa shahidi na hivi sasa anaruka juu ya bustani za Pepo. Tunafahamu kuwa anaruka katika bustani za Peponi kwa sababu baadae Mtume ﷺ aliwaambia maswahaba رضي الله عنهم kuwa Allah Alibadili mikono miwili ya Ja'far iliyokatwa katika uwanja wa vita kwa mbawa mbili ambazo alikuwa sasa anazitumia kuruka kwenda popote apendapo katika Pepo ya Allah.

Baada ya Ja'far رضي الله عنه kufariki, mke wake Asma bint Umays رضي الله عنها alishikwa na huzuni kubwa baada ya kupata taarifa juu ya kifo cha mume wake. Alikuwa akitokwa na machozi mengi kutokana na uchungu na huzuni kubwa aliyokuwa nayo. Walikuwa wapenzi na wasaidizi wa kweli kwa maana halisi. Machozi ya Asma رضي الله عنها hayakukauka na wala hakuacha kulia mpaka pale Mtume wa Allah ﷺ alipomtembelea siku ya tatu na kumpa pole. Aliomba watoto wote wa marehemu Ja'far waitwe, na wote waliitwa na kufika pale mara moja.

Abdullah ibn Ja'far رضي الله عنه (Mmoja kati ya watoto wa Asma bint Umays na Ja'far) anasimulia kuwa: "Mtume wa Allah ﷺ aliwapa muda familia ya Ja'far

رضي الله عنه kuhuzunika juu ya kifo chake kisha aliwatembelea na kuwaambia kuwa: *“Msimlilie tena kaka yangu baada ya siku ya leo.”* Kisha akasema: *“Waleteni watoto wa ndugu yangu kwangu.”*

Kisha tulileta mbele ya Mtume ﷺ kama ndege wadogo. Kisha Mtume ﷺ akasema, ‘Niitieni kinyozi!’ na kinyozi alikuja na kutunyoa nywele zetu kichwani.

Kisha Mtume ﷺ akasema, “Ama kuhusu Muhammad (Mmoja kati ya watoto wa Ja’far), anafanana na baba yetu Abu Talib, na kuhusu ‘Abdullah anafanana na mimi. Ewe Allah! Kuwa msaidizi wa familia ya Ja’far na mpe baraka ‘Abdullah (mwanae) katika kazi atakazozifanya kwa mikono yake.” Mtume ﷺ alirudia dua hii mara tatu.

Kisha mama yetu alizungumza kwa huzuni kuwa sasa watoto wake walikuwa ni yatima na kuanza kulia. Mtume ﷺ akamwambia mama yetu, “Asmaa’ unahofia umasikini kwa watoto wako ilhali mimi (Mtume ﷺ) ndiye mlezi wao hapa duniani na kesho Akhera?”

Baada ya hapo, Asma bint Umays رضي الله عنها akatumia muda wake mwingi katika kuwalea watoto wake na yeye mwenyewe. Aliwafundisha na kuwapa malezi mazuri na Mtume ﷺ hakumsahau Asma bint Umays رضي الله عنها na watoto wake kama alivyokuwa karibu na akiwajali waumini kuliko alivyokuwa akijithamini yeye mwenyewe. Alikuwa akiwatembelea kila alipopata fursa ya kufanya hivyo; alikuwa akiwaulizia na kutaka kujua hali zao na alikuwa akiwatendea wema na kuwa mkarimu sana kwao kwa kuwapa zawadi.

Hali iliendelea namna hii mpaka vilipokuja kutokea vita vya Hunayn. Kutokana na simulizi, mke wa Abu Bakr رضي الله عنه, Ummu Roomaan رضي الله عنها, akafariki, hivyo Mtume ﷺ akamuozesha Asma bint Umays رضي الله عنها (Mjane wa Ja’far).

Abu Bakr رضي الله عنه alikuwa mtu wa kwanza kuingia katika Uislamu. Alikuwa na Mtume ﷺ pangoni (walipokuwa safarini kuelekea Madinah), wakiwa wawili peke yao. Alikuwa rafiki mkubwa na swahaba aliyeaminiwa na Mtume kuliko maswahaba wote. Alikuwa ni swahaba aliyetumia mali zake zote kwa ajili ya Uislamu. Asma bint Umays رضي الله عنها pia alikuwa miongoni mwa watu walioukubali na kuingia katika Uislamu katika siku za mwanzo.

Alikuwa mtu mwenye maarifa makubwa na mcha-Mungu aliyefanya Hijrah mara mbili. Aliwahi pia kuwa mke wa Ja'far, shahidi ambaye sasa alikuwa akipaa na kuruka kwenda atakako katika Pepo ya Mwenyezi Mungu. Asma bint Umays aliishi ndani ya nyumba ya Abu Bakr رضي الله عنه akiwa mtu aliyeridhika, mwenye heshima na mwanamke mwenye kufahamu na kutimiza wajibu wake ipasavyo. Alikuwa akifahamu haki zake na alikuwa akifanya jitihada kubwa kutekeleza wajibu wake. Asma bint Umays رضي الله عنها alijaaliwa kupata mtoto akiwa mke wa Abu Bakr رضي الله عنه, mtoto ambaye walimwita Muhammad. Mapenzi makubwa baina yao, na kiwango cha namna gani Asma bint Umays alifurahia maisha yake na mume wake - Abu Bakr رضي الله عنه, yalikuja kudhihirika wakati Abu Bakr alipokuwa mgonjwa katika masiku yake ya mwisho akielekea kuyakabili mauti. Abu Bakr aliagiza kuwa, pindi atakapofariki, basi Asma bint Umays amuoshe. Hii ilikuwa ni ishara ya wazi kuwa juu ya mapenzi aliyokuwa nayo Abu Bakr kwa mkewe na namna alivyokuwa akimuamini.

Baadaye Asma bint Umays alikuja kuolewa na 'Ali ibn Abi Taalib رضي الله عنه baada ya kifo cha Abu Bakr رضي الله عنه na walijaaliwa kupata mtoto waliyemwita 'Awn. Asma bint Umays رضي الله عنها akaishi katika nyumba ya 'Ali ibn Abi Taalib رضي الله عنه kama mama mcha-Mungu na mwanamke mwenye hadhi na heshima kubwa. Mwanamke aliyekuwa akitekeleza wajibu wake kikamilifu bila kujilegeza wala kuzembea hata katika nyakati ngumu.

Imesimuliwa kuwa, watoto wake wawili Muhammad ibn Ja'far na Muhammad ibn Abu Bakr رضي الله عنه walikuwa wakitambiana, kila mmoja akimtambia mwenzake akisema kuwa yeye alikuwa bora na baba yake alikuwa bora kuliko baba wa mwenzie. 'Ali alikuwepo wakati wa tukio hilo na akamtaka Asma bint Umays aamue ushindani ule.

Swali linakuja: Je, 'Ali ibn Abi Taalib رضي الله عنه alikuwa akitaka kupima busara alizokuwa nazo Asma bint Umays au alitaka kujua ni mtoto yupi aliyekuwa akipendwa zaidi na mama huyu? Hapa ndipo mama huyu alipodhihirisha busara ya hali ya juu na kutoa somo muhimu kwa kila Mwanamke wa Kiislamu, kwa kila mke mcha-Mungu! Alitoa somo kwa kila msichana, kila mwanamke na kila mke na kwa kila mama mwenye kutaka kujifunza. Alijibu bila kusita wala bila kupendelea: "Sikuwahi kumuona kijana bora kuliko alivyokuwa Ja'far, na sikuwahi kumuona mwanaume mwenye umri wa kati aliyekuwa bora kuliko alivyokuwa Abu Bakr."

Vijana wale wawili wakakaa kimya na kuacha kujisifu na kutambiana.

Ni katika hatua hii, tena katika namna ya utani, 'Ali ibn Abi Taalib رضي الله عنه akamuuliza, ikiwa ndiyo hivyo basi sisi wengine umetuachia nafasi gani?" Bila shaka Asma bint Umays رضي الله عنها alikuwa akimpenda sana pia mume wake wa wakati huo 'Ali ibn Abi Taalib.

Safari ya kuondoka duniani ya mama huyu - Asma bint Umays رضي الله عنها ilianza mara tu baada ya kupata taarifa juu ya kifo cha mwanae Muhammad ibn Abi Bakr kilichotokea huko Misri. Alikwenda katika sehemu aliyokuwa akiitumia kwa ajili ya kuswalia ndani ya nyumba yake. Akaswali Swala ndefu kupita kiwango huku akilia sana kwa uchungu. Yote haya (kuswali Swala ndefu kupita kiasi na kulia sana) yalikuwa mambo yenye athari kubwa kwa mwili wake hasa ukizingatia kuwa tayari alikuwa na umri mkubwa na alikuwa dhaifu. Alianza kutokwa na damu nyingi kifuani na hatimaye alifariki dunia na kurejea kwa Mola wa Walimwengu wote. Hivi ndivyo Asma bint Umays alivyoondoka duniani na kuanza maisha ya Peponi.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Amuwie radhi mama yetu - Asma bint Umays! Amin.

# Asmaa binti Yaziid

## Muwakilishi wa Wanawake

Mwanamke mmoja alikuja kwa Mtume ﷺ wakati Mtume ﷺ akiwa amekaa na maswahaba zake. Mama yule akasema: Ewe Mtume wa Allah! Hakika mimi nimeagizwa kwa niaba ya kundi la wanawake ambao kwa pamoja tuna fikra zinazofanana na tuna jambo linalotutatiza sote. Allah amekutuma kwetu sote, wanaume na wanawake. Sisi tumekuamini na tunakufuata. Pamoja na hayo, sisi wanawake tunapaswa kubakia nyumbani. Sisi tupo kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wanaume na tunalea watoto wao. Lakini wanaume wamependelewa, kwa mfano: Wao wamefaradhishwa Swala ya Ijumaa, wanaruhusiwa kuhudhuria mazishi na kwenda kupigana vita kwa ajili ya Allah. Wanapoondoka na kwenda vitani, sisi hubakia tukiangalia mali zao na kulea watoto wao. Ewe Mtume wa Allah! Je, sisi tunapata ujira wowote kwa kufanya haya?"

Mtume ﷺ akageuka na kuwaangalia maswahaba zake na kuwauliza: "Je, mlipata kumsikia mwanamke fasaha zaidi katika kujenga hoja au kuuliza jambo juu ya dini au imani yake?" Maswahaba wakasema: "Hatukujua kama mwanamke anaweza kujieleza kwa ufasaha kiasi hiki". Mtume ﷺ akamjibu mama yule: "Asmaa, nenda kawaambie wanawake wenzako kwamba, mwanamke yeyote atakayekuwa mke bora, atakayemfanya mume wake aishi vizuri na kujiepusha na misuguano na mumewe, basi atapata malipo sawa na yale wapatayo wanaume kwa hayo yote uliyoyasema (Swala ya Ijumaa, kuhudhuria mazishi na kushiriki vita kwa ajili ya Allah)". Mama yule aliondoka huku akimuhimidi na akimtukuza Allah. Mama huyu hakuwa mwingine ila alikuwa Asmaa bint Yazeed ibn Al-Sakan رضي الله عنها. Huyu alikuwa mama wa kupigiwa mfano miongoni mwa akina mama wa Kiislamu kutoka kwa watu wa Ansar.

Mama huyu anatokana na ukoo wa Abd Al-Ashhal katika kabila la Aws, kabila ambalo kiongozi wao (Chifu) alikuwa ni Saad ibn Mu'adh رضي الله عنه. Mama huyu (Asmaa bint Yazeed) na Kabshah bint Rafi, ambaye alikuwa mama mzazi wa Saad, walikuwa wanawake wa kwanza kutoka kundi la Ansar kuchukua ahadi ya utii kwa Mtume ﷺ mara tu alipowasili katika mji wa Madinah.

Simulizi tuliyomaliza kuisimulia juu ya swali alilomuuliza Mtume ﷺ linatuonesha wazi kuwa, mama huyu alikuwa mzungumzaji na alikuwa na uwezo mkubwa wa kujieleza, vitu ambavyo viliambatana na ujasiri. Hili linaweza kuashiria kuwa, mama huyu alikuwa mtu aliyeelimika. Kwa hakika alikuwa miongoni mwa watu bora katika kupokea hadithi za Mtume ﷺ, na alipokea si chini ya hadithi themanini na moja (81), jambo linalomfanya awe miongoni mwa watu wa juu kabisa miongoni mwa wanawake wa Ansari waliopokea hadithi, kama si mwanamke wa kwanza. Katika moja ya mapokezi yake, anazungumzia kushushwa kwa sura ya tano (5) katika Qur'an - Al-Ma'idah. Anasimulia kuwa: "Nilikuwa nimeshikilia hatamu za ngamia aitwaye Al-Adbaa, ngamia wa Mtume ﷺ wakati Surah Al-Ma'idah ilipokuwa ikishushwa yote. Ilikuwa nzito mno kiasi kwamba ilikaribia kumvunja miguu ngamia yule jike". Hii ni uthibitisho kuwa, wakati wa kupokea *Wahyi* ilikuwa ni wakati mzito kwa Mtume ﷺ, kwa kuwa ilihusisha mawasiliano baina yake na Malaika Jibril.

Asmaa bint Yazeed رضي الله عنها alikuwa anatoka katika familia ya watu jasiri na shupavu katika vita na mapigano. Katika vita vya Uhud, wakati jeshi la Waislamu liliposambaratika, kaka wa mama huyu, Imarah ibn Yazeed رضي الله عنها, alikuwa miongoni mwa watu wachache waliobaki wakiwa imara wakimlinda na kumuhami Mtume ﷺ mpaka Imarah ibn Yazeed alipouwawa. Baba yake Asmaa bint Yazeed رضي الله عنها na mjomba wake, wote wawili pia waliuwawa katika vita hivi. Ujasiri waliokuwa nao katika familia ulimfanya Asmaa bint Yazeed رضي الله عنها nae afuate mwenendo wa wazazi na ndugu zake. Asmaa bint Yazeed رضي الله عنها alitoka na kuongozana na jeshi la Waislamu katika matukio mbalimbali ya vita wakati wa uhai wa Mtume ﷺ. Alikuwa pia pamoja na Mtume ﷺ na maswahaba zake wakati ambao Mtume ﷺ alikusudia kwenda Makkah kwa ajili ya ibada ya Umrah, lakini Maquraishi waliokuwa wakiupinga na kuupiga vita Uislamu wakawazuia. Katika hatua fulani, Mtume ﷺ aliwataka maswahaba kuchukua ahadi ya kuwa tayari kupigana mpaka tone la mwisho ikiwa watalazimishwa kufanya hivyo. Asmaa bint Yazeed رضي الله عنها alikuwa miongoni mwa Waislamu waliochukua ahadi hiyo kwa Mtume ﷺ .

Miaka mitatu baada ya kufariki kwa Mtume ﷺ, Asmaa bint Yazeed aliungana na jeshi la Waislamu lililokuwa likielekea Syria kupambana na jeshi la Warumi. Mama huyu رضي الله عنها alishiriki kikamilifu katika vita. Alitumia nguzo ya hema kujilinda na kuwalinda wanawake wenzake waliokuwa pamoja. Asmaa bint Yazeed رضي الله عنها aliweza kuwauwa askari tisa (9) wa maadui! Baada ya vita na baada ya Syria kuwa chini ya uongozi wa dola ya Kiislamu, Asmaa bint Yazeed alibaki na kuishi nchini Syria, akiwafundisha wanawake wenzake dini ya Kiislamu. Asmaa bint Yazeed رضي الله عنها aliishi mpaka kufikia katika umri wa utu uzima. Kulingana na simulizi sahihi, mama huyu (Asmaa bint Yazeed) alifariki katika mji wa Damascus katika mwaka wa 69 Hijiriya; hii ina maana kuwa mama huyu alifariki akiwa na miaka takriban tisini (90). Asmaa bint Yazeed رضي الله عنها alizikwa katika makaburi ya Bab Al-Sagheer katika mji wa Damascus.

# Atika Binti Zaid

## Mfano Bora kwa Wapendanao

Atika رضي الله عنها alikuwa mtoto wa Zaid Ibn Amr Ibn Nawfal. Zaid bin Amr alikuwa ni mjomba wa 'Umar ibn Khattab. Kwa maana hiyo, Atika bint Zaid رضي الله عنه alikuwa ni binamu wa 'Umar Ibn Khattab رضي الله عنه.

Wakiwa katika mji wa Madinah, Atika bint Zaid رضي الله عنها aliolewa na Abdullah mtoto wa swahaba Abu Bakr رضي الله عنه. Abu Bakr رضي الله عنه ambaye baadaye alikuja kuwa Khalifa wa kwanza wa Waislamu. Atika bint Zaid رضي الله عنها alikuwa bint mrembo na mwenye kuvutia sana na Abdullah رضي الله عنه alivutiwa na kumpenda sana binti huyu. Abdullah رضي الله عنه alishikwa kimapenzi na Atika bint Zaid رضي الله عنها kiasi kwamba ilifikia mahala akawa hawezi kushiriki misafara na vita ambavyo Waislamu walishiriki. Ilifikia mahala akawa haendi kuswali Swala za jamaa msikitini, kisa? Atika bint Zaid رضي الله عنها!

Mapenzi baina ya Abdullah na Atika yakawa makubwa na hayakuwa ya kawaida. Abdullah رضي الله عنه alikuwa akihisi kuwa, Atika bint Zaid رضي الله عنها alikuwa mwenye thamani kuliko kila kitu katika dunia. Abu Bakr رضي الله عنه alipopata habari kuwa mwanae Abdullah رضي الله عنه hakushiriki katika misafara mbalimbali na imefikia mahala anapuuza Swala za jamaa msikitini, alimwita mwanae na kumtaka atoe maelezo kwanini amefikia hatua ile. Abdullah رضي الله عنه alikuwa hana sababu yeyote ya maana ambayo angeweza kumwambia na kumridhisha baba yake – Abu Bakr رضي الله عنه. Ukweli ilikuwa ni kwamba, Abdullah رضي الله عنه alikuwa amezidiwa na mapenzi ya mkewe Atika bint Zaid رضي الله عنها kiasi kwamba alikuwa hawezi kutekeleza majukumu yake mengine.

Abu Bakr رضي الله عنه alimwambia mwanae kwa maneno yaliyokuwa wazi bila kuficha kuwa, mwanae Abdullah رضي الله عنه alikuwa amefanya makosa

makubwa mno ambayo yasingeweza kuachwa yaendelee. Abdullah رضي الله عنه alimuomba radhi sana baba yake, na Abu Bakr رضي الله عنه akamuamuru mwanae Abdullah رضي الله عنه ampe talaka Atika bint Zaid رضي الله عنها ndani ya siku tatu. Abdullah رضي الله عنه alikuwa amewekwa njia panda. Upande mmoja alihisi kuwa ana wajibu wa kuwa mkweli juu ya mapenzi yake kwa mke wake, Atika bint Zaid رضي الله عنها. Na upande wa pili aliona wazi kuwa, amri aliyopewa na baba yake ilikuwa lazima aitekeleze kwa gharama yeyote. Baada ya siku tatu, Abdullah رضي الله عنه alimuacha na kumpa talaka mke wake Atika bint Zaid رضي الله عنها. Uamuzi huu ulimfanya Abdullah رضي الله عنه akose mwelekeo na kujihisi kuchanganyikiwa. Abdullah رضي الله عنه akawa hawezi kula wala kunywa. Abdullah رضي الله عنه akawa mtu wa kujitenga, akiimba mashairi ya huzuni akielezea uchungu na huzuni aliyokuwa nayo kwa kumpoteza mpenzi wake.

Kupewa talaka kwa Atika bint Zaid رضي الله عنها ikawa habari iliyotawala mji mzima wa Madinah. Mtume ﷺ alipopata habari juu ya jambo hili, alimuonea huruma sana Abdullah. Mtume ﷺ akaifuta talaka, na wapenzi wawili – Abdullah bin Abu Bakr na Atika bint Zaid رضي الله عنهما wakarejea na kuishi pamoja kama mume na mke kama walivyokuwa hapo awali.

Kuanzia wakati huo, Abdullah رضي الله عنه alikuwa makini sana kuhakikisha kuwa, mapenzi yake kwa Atika bint Zaid رضي الله عنها hayakumfanya apuuzie au ashindwe kutekeleza wajibu wake kwa Mola wake. Kuanzia wakati huo, kila msafara na mapigano yaliyoongozwa na Mtume ﷺ, Abdullah رضي الله عنه alikuwa mstari wa mbele kushiriki kikamilifu na alikuwa akipambana kwa nguvu na kwa ushujaa mkubwa. Katika vita vya Taif, Abdullah رضي الله عنه alijeruhiwa na baadaye alifariki akiwa Madinah kutokana na majeraha aliyokuwa ameyapata katika vita vile. Atika bint Zaid رضي الله عنها alihuzunika sana kufuatia kifo cha mume wake kipenzi Abdullah رضي الله عنه, huku akiwa na huzuni kubwa, Atika bint Zaid رضي الله عنها akasoma shairi lililokuwa na maneno yenye maana hii:

"Naapa Abdullah رضي الله عنه kuwa macho yangu hayotoacha kukulilia;

Na mwili wangu utabakia ukiwa umejaa vumbi."

Atika bint Zaid رضي الله عنها aliamua kuwa, baada ya kufariki mume wake – Abdullah رضي الله عنه, hatoolewa na na mtu mwingine yeyote. Alidumu katika kiapo chake hicho kwa miaka minne au mitano. 'Umar ibn Khattab رضي الله عنه akamuonea huruma. Alimuona kuwa, binti mdogo na mrembo kiasi kile ilikuwa

haifai kubakia ndani ya huzuni na unyonge kwa muda mrefu kama mjane. ‘Umar رضي الله عنه akamshauri Atika bint Zaid رضي الله عنها aolewe. ‘Umar ibn Khattab رضي الله عنه alipokuwa Khalifa, alijitolea yeye mwenyewe kumuoa Atika bint Zaid رضي الله عنها. Baada ya kusita sita, Atika bint Zaid رضي الله عنها akakubali kuolewa na ‘Umar ibn Khattab رضي الله عنه . Baada ya kukamilisha taratibu zote na ndoa kufungwa baina ya ‘Umar ibn Khattab na Atika bint Zaid رضي الله عنهما, Ali ibn Abi Taalib رضي الله عنه alimpongeza ‘Umar رضي الله عنه, kisha akamuomba ruhusa aongee na bibi harusi. ‘Umar رضي الله عنه akamruhusu, na Ali رضي الله عنه akamkumbusha Atika juu ya ahadi na kiapo chake kuwa hatoolewa na mtu yeyote baada ya kufariki Abdullah رضي الله عنه. Kusikia maneno yale, Atika akaangua kilio (akalia sana). ‘Umar Ibn Khattab رضي الله عنه akam-bembeleza huku akimwambia Atika bint Zaid رضي الله عنها kuwa: “Usihuzunike Atika. Wanawake wote hufanya hivyo (huapa kuwa hawatoolewa tena baada ya kufariki waume zao). Allah Akubariki, kwa kuolewa tena umeenda sawasawa na mafundisho ya Uislamu.”

Akiwa na ‘Umar ibn Khattab رضي الله عنه kama mume wake, Atika bint Zaid رضي الله عنها alijaaliwa kupata mtoto mmoja ambaye walimwita Ayaz.

# Hamnah binti Jahsh

## Mama wa Kiislamu wa Kupigiwa Mfano

Hamnah رضي الله عنها ni mama wa Kiislamu aliyeishi wakati wa Mtume ﷺ, na alisilimu na kuukubali Uislamu na hivyo kuchukua ahadi ya utii kwa Mtume Muhammad ﷺ. Mama huyu alikuja kuolewa na swahaba maarufu na balozi wa kwanza wa Mtume ﷺ Mus'ab ibn Umair رضي الله عنه. Bila shaka swahaba huyu anafahamika vema na mchango wake alioutoa katika kuujenga Uislamu na hususan katika kuandaa mazingira mazuri ya Mtume ﷺ kufika na kupokelewa Madinah. Mama wa swahaba huyu alikuwa Khunas bint Malik رضي الله عنها, mama tajiri na aliyesifika kwa wingi wa mali alizomiliki, na mali hizi zilimuwezesha mama huyu kumpa maisha ya anasa na starehe mwanae, Mus'ab ibn Umair رضي الله عنه. Ama kuhusu maisha aliyowahi kuishi Mus'ab ibn Umair رضي الله عنه akiwa kwa mama yake, baada ya muda mrefu toka Mtume ﷺ kukabidhiwa Utume; Mtume ﷺ aliwahi kusema: *"Sikuwahi kumuona mtu yeyote katika Makkah aliyekua na nguo ya thamani au yenye mapambo yenye kuvutia zaidi ya Mus'ab ibn Umair."*

Hata hivyo, aliposilimu, mama yake alijitahidi sana kumshawishi aachane na imani yake mpya - Uislamu na kurejea katika ukafiri, lakini Mus'ab ibn Umair رضي الله عنه alikataa kabisa. Mama yake alikata huduma zote ikiwemo kumpa chakula kizuri na mavazi mazuri ya thamani, hata hivyo Mus'ab ibn Umair رضي الله عنه hakujali kupoteza vitu hivyo. Alibakia kuwa mmoja kati ya maswahaba wake waaminifu na watiifu.

Mama huyu, Hamnah bint Jahsh رضي الله عنها, baada ya kuolewa na Mus'ab ibn Umair رضي الله عنه, walijaaliwa kupata mtoto wa kike, na wakamwita mtoto yule Zaynab.

Mtume ﷺ na maswahaba zake walipohamia Madinah (wakati wa Hijirah), mama huyu Hamnah na mume wake walikuwa miongoni mwa

Waislamu waliofanya hivyo kwa ajili ya Allah, na hivyo wanaingia katika kundi maalum la watu waliopata ujira mkubwa kwa kuhama pamoja na Mtume ﷺ kutoka Makkah kwenda Madinah kwa ajili ya Allah na Mtume wake ﷺ kama ilivyokuwa kwa familia nyingine za Kiislamu. Hawa ni Waislamu wakweli ambao walitoa uhai wao na maisha yao kwa ajili ya Allah, Mtume ﷺ na dini yao. Biashara, mifugo, kilimo na mfano wa hayo, havikuwadanganya kutoka kwa ajili ya Mola wao.

Baada ya maswahaba na Mtume ﷺ kuhamia Madinah na kuanza maisha ya kawaida huku wakiutangaza Uislamu, makafiri wa Makkah hawakutulia wala kuridhika na hali ile. Kila siku walikuwa wakipanga mipango ya kumuhujumu Mtume ﷺ na dini ya Allah, na kwa hakika kuwahujumu Waislamu wanyonge waliohama kutoka katika miji yao wakitafuta radhi za Mola wao. Ni katika mazingira ya namna hii, Maquraishi walianzisha na kudumu kuwachokoza Waislamu kwa kuwashambulia tena kwa kuwafuata katika mji wa Madinah wakiwa na lengo la kuwadhoofisha Waislamu na hata kuidhoofisha dola ya Kiislamu ambayo kwa wakati ule ilikuwa bado ndio kwanza inajengwa.

Wakati wa vita mbalimbali ambavyo Waislamu walipigana, mama huyu Hamna bint Jahsh alikuwa miongoni mwa akina mama wa Kiislamu waliotoka pamoja na jeshi la Waislamu na kufanya kazi kubwa ya kuwatibu wapiganaji waliojeruhiwa na kuwapa maji askari wa Kiislamu waliokuwa na kiu.

Katika vita vya Uhud, Waislamu walishindwa vibaya, huku takriban Waislamu sabini (70) wakiuwawa mashahidi katika uwanja wa vita. Mama huyu Hamnah bint Jahsh رضي الله عنها alikuwa pamoja na jeshi la Waislamu katika vita hivi. Hata hivyo hakujua ni askari gani wa Kiislamu walikuwa wameuwawa. Baada tu ya vita kumalizika, Hamnah bint Jahsh رضي الله عنها alikutana na Mtume ﷺ na Mtume wa Allah akampa pole na kumtaka apokee taarifa ya msiba kwa subira. Hamnah bint Jahsh رضي الله عنها akamuuliza Mtume ﷺ alikuwa anakusudia msiba gani? Mtume ﷺ akamjibu: "*Mjomba wako, Hamzah.*"

Hamnah رضي الله عنها akasema: "*Inna lillahi Wainna ilayhi Rajiuun* - Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake (Mwenyezi Mungu) sisi sote tutarejea. Mwenyezi Mungu amuwie radhi na amuingize katika rehema zake. Hakika yeye amejaaliwa kufa shahidi na kuingia Peponi."

Mtume ﷺ akaanza tena kumwambia kuwa apokee taarifa ya msiba kwa subira. Hamnah رضي الله عنها alipomuuliza Mtume ﷺ alikuwa anamaanisha msiba gani, Mtume ﷺ akajibu: "Kaka yako Abdullah." Hamnah رضي الله عنها alirudia kutamka maneno yale yale aliyotamka alipopewa taarifa ya kifo cha mjomba wake, Hamzah - "*Inna lillahi Wainna ilayhi Rajiuun* - Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake (Mwenyezi Mungu) sisi sote tutarejea. Mwenyezi Mungu amuwie radhi na amuingize katika rehema zake. Hakika yeye amejaaliwa kufa shahidi na kuingia Peponi." Na Mtume aliendelea kumtajia msiba mwingine, na alipouliza ni wa nani, Mtume ﷺ alimtajia wa mume wake, Mus'ab ibn Umair رضي الله عنه. Mara hii, alipaza sauti na kusema,: "Hasara iliyoje kwangu! Oh, huzuni iliyoje kwangu!" Mtume ﷺ akamwambia: "Mume na mke wana nafasi ya pekee, hakuna yeyote mwingine anaweza kuziba nafasi zao."

Baadaye Mtume ﷺ akamuuliza Hamnah رضي الله عنها, kwanini huzuni zilizidi kupita kiasi. Hamnah bint Jahsh رضي الله عنها akajibu kuwa: "Ewe Mtume wa Allah! Nilikumbuka kuwa, watoto wake sasa ni yatima." Kimsingi watoto wale walikuwa bado ni wadogo kwa sababu, wakati Mus'ab anafariki, alikuwa na umri wa takriban miaka thelathini na tano (35) tu. Mtume ﷺ akamuombea dua yeye Hamnah bint Jahsh na watoto wake, huku akitaja katika dua yake kuwa, Allah Awajaalie wawe waja wema na wakarimu.

Baadaye Hamnah رضي الله عنها alikuja kuolewa na Talhah ibn Ubaydillah. Talhah ibn Ubaydillah ni miongoni mwa maswahaba kumi waliobashiriwa Pepo na Mtume ﷺ. Hamnah bint Jahsh رضي الله عنها alijaaliwa kuzaa mtoto mmoja wa kiume na Talhah ibn Ubaydillah رضي الله عنه. Hamnah alimbeba mwanae na kwenda naye kwa Mtume ﷺ na kumuomba Mtume ﷺ amchagulie jina mwanae. Mtume ﷺ akamwita mtoto huyu Muhammad na kumpa jina la utani (lakabu) Abu Al-Qasim. Talhah ibn Ubaydillah رضي الله عنه alikuwa mwema na mkarimu mno kwa watoto aliowalea (watoto waliozaliwa na Hamnah wakati akiwa mke wa Mus'ab).

Hamnah bint Jahsh رضي الله عنها amepokea hadithi kadhaa za Mtume ﷺ, moja kati ya hadithi hizo ni ile inayotoa maelekezo nini mwanamke afanye kuhusu Swala za faradhi anapokuwa katika hedhi mfululizo, zaidi ya hali ya kawaida (inapokuwa siku zimezidi sana). Yeye Hamnah alikabiliwa na tatizo hilo, na hakuona aibu kumuuliza Mtume ﷺ ili kujua yeye anatakiwa afanye nini. Mtume ﷺ alimpa majibu fasaha tena ya kina kabisa, na majibu hayo yanaendelea kutumiwa na kila mwanamke mwenye tatizo hilo.

# Khawlah Bint Al-Azwari

## Mwanamke mchungu kwa Makafiri

Khawlah رضي الله عنها alikuwa binti wa mmoja kati ya viongozi wakuu wa kabila la Bani Asad. Historia inaonesha kuwa, familia ya mama huyu waliukubali Uislamu na kusilimu katika masiku ya mwanzo. Kuna kutofahamika au kutokubaliana juu ya jina halisi la baba yake. Baadhi wanasema jina halisi la baba yake lilikuwa Malik Ibn Aws, huku wengine wakisema alikuwa Tariq Ibn Aws. Al-Azwar lilikuwa jina la utani la baba yake ambalo ndilo lilikuja kuwa jina maarufu zaidi. Kaka wa mama huyu, Dirar رضي الله عنه, alikuwa mtu shujaa na bingwa wa mashairi katika kabila lake, na alikuwa akifahamika sana na kuheshimika kutokana na busara zake. Dirar رضي الله عنه alikuwa anamuamini na alikuwa akimpenda sana dada yake, Khawlah رضي الله عنها.

Kwa ujumla, dada na kaka hawa walikuwa marafiki waliopendana vilivyo kiasi kwamba walikuwa wakitembea pamoja. Dirar رضي الله عنه alimfundisha dada yake mbinu zote za kupigana kwa kutumia upanga kiasi ambacho Khawlah رضي الله عنها naye alifikia kuwa mjuzi wa hali ya juu katika mapigano ya aina hii. Mbali na hayo, Khawlah رضي الله عنها alifahamu vizuri sanaa ya mashairi. Kwa muonekano wake, Khawlah رضي الله عنها alikuwa binti mwenye nywele ndefu na nyeusi, mrefu, mwembamba na mrembo wa kuvutia. Jina lake kwa kiasi kikubwa halikuwa mashuhuri, mpaka baada ya vita vya Ajnadin, vita ambavyo vilipiganwa si mbali sana kutoka ilipo Jerusalem.

Ni katika vita hivi kaka wa Khawlah رضي الله عنها, Dirar رضي الله عنه alipoteza mkuki wake na kuanguka kutoka juu ya farasi na hatimaye akachukuliwa mateka na maadui zake. Mama huyu, Khawlah رضي الله عنها, alivaa kama wanavyovyaa mashujaa wanaume, akabeba silaha zake na kupanda juu ya farasi na kuchanja mbuga akizivuka safu za askari wa kirumi. Alikuwa akitumia

upanga wake kwa ujuzi mkubwa kwa kila aliye jaribu kutaka kumzuia. Askari wa jeshi la Waislamu wakiongozwa na kamanda wao Khalid ibn Al-Walid رضي الله عنه, walimuangalia kwa kustaajabu huku akipambana na kusonga mbele kana kwamba alikuwa mwanaume.

Mwanahistoria wa Kiarabu, Al Waqidi, anasimulia tukio hili katika kitabu chake alichokiita 'Kukombolewa kwa Sham (Syria)' kwamba: "Katika vita vilivyotokea katika mji wa Bayt Lahyah jirani kabisa na Ajnadin, Khalid رضي الله عنه alimuona askari shujaa, aliyevalia nguo nyeusi, akiwa amejizungushia kitambaa chenye rangi ya kijani kuzunguka kiuno chake na huku akiwa amefunika kifua chake. Shujaa yule alikuwa akipenya safu za askari wa Kirumi kama (mithili ya) mshale. Huku wakiwa wameshangazwa na kutomfahamu shujaa yule, Khalid ibn Al-Walid na askari wengine walimfuata na kuungana naye katika vita".

Rafe' Ibn Umayrah Al-Ta'if رضي الله عنها alikuwa mmoja kati ya wapiganaji. Mpiganaji huyu anaelezea namna ambavyo shujaa huyu alivyo sambaratisha ngome za askari wa maadui, na kutokomea kati kati yao. Shujaa yule alirudi kuonekana wakati akirejea huku mkuki wake ukiwa umelowa na ukiwa unatiririka damu. Askari shujaa yule alirudia mara kadhaa kuingia na kuendesha mapambano makali sana dhidi ya askari wa Kirumi. Askari na wapiganaji wa Kiislamu waliingiwa na hofu juu ya usalama wa mpiganaji yule. Rafe' na wapiganaji wengine walidhani mpiganaji yule alikuwa Khalid ibn Al-Walid رضي الله عنه, mtu aliyekuwa mahiri sana katika mipango na operesheni za kijeshi. Lakini ghafa Khalid ibn Al-Walid رضي الله عنه akatokea akiwa ameambatana na mashujaa wengine. Rafe' akamuuliza kiongozi wa majeshi ya Waislamu, Khalid ibn Al-walid رضي الله عنه, "Shujaa yule ni nani? Naapa kwa jina la Allah, mpiganaji yule amekuwa akipambana vikali bila kujali usalama wake!"

Khalid Ibn Al-Walid رضي الله عنه akajibu kuwa alikuwa hamfahamu mpiganaji huyo, pamoja na kuwa alikuwa akivutiwa na ujasiri na ushujaa aliokuwa akiuonesha katika uwanja wa vita. Ghafla walimuona mpiganaji na shujaa yule akitokea huku akikimbizwa na wapiganaji wa Kirumi. Alikuwa akikimbia na ghafla akigeuka na kumuuwa askari wa kirumi aliyekuwa ametangulia mbele katika waliokuwa wakimkimbiza na kuanza mashambulizi upya!

Hatimaye Warumi wakashindwa vita na kukimbia. Khalid Ibn Al-Walid رضي الله عنه akamtafuta shujaa yule mpaka akamuona. Wakati huo akiwa amelala

chini na huku anatiririkwa na damu. Alimsifu kwa ushujaa na umahiri wake aliouonesha na kumtaka atoe kitambaa alichojifunika ili wamtambue mpiganaji yule alikuwa nani miongoni mwa Waislamu. Lakini shujaa yule hakujibu chochote, na akawa anajaribu kuondoka. Lakini askari wa Kiislamu hawakumruhusu aondoke, na kila mmoja akawa anamtaka bwana yule ajitambulishe alikuwa nani.

Baada ya shujaa yule kubaini kuwa kulikuwa hakuna uwezekano wa yeye kuondoka bila kufahamika, alijibu swali lile kwa sauti ya kike akisema: "Ewe kiongozi wangu, nilishindwa kujibu kwa sababu mimi ni mtu mwenye aibu. Hakika wewe ni kiongozi mkubwa, na mimi ni mwanamke tu, mwanamke ambaye moyo wake umejaa huzuni." Bado Khalid ibn Al-Walid akaendelea kumuuliza, 'wewe ni nani?" "Mimi ni Khawlah Bint Al-Azwar رضي الله عنها. Nilikuwa pamoja na wanawake wengine walioongozana na jeshi la Waislamu, nilipofahamu kuwa maadui wamemkamata na kumchukua mateka kaka yangu, nilijikuta nikifanya yale niliyofanya."

Khalid ibn Al-Walid رضي الله عنه akatoa amri kwa jeshi la Waislamu kuwafuata na kuwakimbiza jeshi la warumi lililokimbia huku Khawlah رضي الله عنها akiongoza mashambulizi, na huku akiangalia huku na kule kujaribu kumtafuta kaka yake bila mafanikio. Ilipofika mchana, Waislamu walipata ushindi mkubwa sana na wanajeshi wengi wa kirumi walikuwa wameuwawa.

Huku akijua kuwa lazima mateka wawe wamehifadhiwa mahala fulani, kiongozi wa vikosi vya jeshi la Waislamu Khalid ibn Al-Walid رضي الله عنه akamtuma Khawlah رضي الله عنها akiongozana na idadi kadhaa ya wapiganaji wa Kiislamu kuwatafuta. Baada ya kuwakimbiza kwa muda mrefu, walifanikiwa kulifikia kundi la askari wa kirumi waliokuwa wakiwapeleka mateka makao makuu yao. Mapigano mapya yakaanza, na walinzi wote wa kirumi wakauwawa na mateka wakakombolewa.

Katika vita nyingine iliyotokea Ajnadin, mkuki wa Khawlah رضي الله عنها ulivunjika na mnyama aliyekuwa akimtumia katika vita aliuwawa, na akajikuta amechukuliwa mateka. Lakini alishangazwa kuona askari wa kirumi wakishambulia kambi ya wanawake na kuwateka wanawake kadhaa. Kiongozi wao aliwakabidhi mateka wale wanawake kwa askari wao, na kutoa amri Khawlah apelekwe katika hema lake. Khawlah alishikwa na hasira sana, na

aliamua kuwa kufa itakuwa heshima kwake kuliko kuishi huku akidhalilishwa. Khawlah رضي الله عنها alisimama katikati ya akina mama wengine waliokuwa wamekamatwa mateka na kupaza sauti akiwataka wapambane kutetea uhuru wao na heshima yao au wafe ikiwa italazimu. Wanawake wote waliingiwa na morali kutokana na hamasa ile aliyoiibua Khawlah رضي الله عنها. Walichukua nguzo za kujengea hema na kuwashambulia walinzi wa kirumi, huku wakiwa wamewazingira barabara kama alivyokuwa amewaelekeza Khawlah رضي الله عنها.

Khawlah رضي الله عنها aliongoza mashambulizi yale, na kumuuwa mlinzi wa kwanza kwa nguzo ya kujengea hema, na mwanamke mwingine akafanikiwa kumuuwa mlinzi mwingine. Kwa mujibu wa mwanahistoria wa kiarabu, Al-Waqidi, akina mama wale walifanikiwa kuwauwa askari kiasi cha thelathini (30) wa kirumi, huku Khawlah رضي الله عنها akiwahamasisha wanawake wale kwa mashairi yake, kitu ambacho kilifanya damu ya askari wa maadui kuchemka.

Kiongozi wa majeshi ya warumi alishitushwa na kustaajabishwa na kile kilichotokea, na akaamua kuongoza kundi la wapiganaji wa kirumi kupambana na wanawake wale, lakini alijaribu kwanza kujaribu kuwahadaa na kuwapa ahadi mbalimbali. Alimwambia Khawlah kwamba, yeye kiongozi wa majeshi anakusudia kumuoa Khawlah na kumfanya *first lady* wa Damascus. Lakini Khawlah alimjibu kwa utulivu, tena kwa kujiamini: “Siwezi kukubali wewe uwe japo mchunga ngamia wangu! Unawezaje kutarajia mimi kujishusha na kuishi na wewe? Naapa kuwa mimi ndiye nitakayekata kichwa chako kwa kiburi chako.”

Kabla ya kuanza mapigano na jeshi hili, akina mama hawa wa Kiislamu walitiana moyo na kupeana maelekezo nini cha kufanya. Kwa kutumia nguzo ndefu za kujengea mahema, waliwazuia askari wa kirumi wasiwasogelee na kuwashambulia. Ghafla, Khalid ibn Al-Walid رضي الله عنه na jeshi lake wakaingia katika uwanja wa vita. Katika mapigano haya, zaidi ya askari wa kirumi elfu tatu (3000) waliuwawa. Wanawake walioshiriki vita hivi walikuwa wakijisifu na kusema kuwa, Khawlah رضي الله عنها peke yake alifanikiwa kuwauwa askari wa kirumi wapatao watato (5), akiwemo kiongozi wao aliyemtolea lugha ya matusi na kujaribu kumdhalilisha.

Katika vita nyingine waliyopigana wapiganaji wa Waislamu dhidi ya majeshi ya warumi, majeshi ya Waislamu yalistushwa na kuingiwa na hofu

kutokana na kuona ukubwa wa vikosi vya maadui. Askari wengi wa Kiislamu walikimbia, lakini hawakufika mbali. Mama wa Kiislamu, Khawlah رضي الله عنها akiwa na wanawake wengine wa Kiislamu walikutana na askari wa Kiislamu waliokuwa wakikimbia, wakawahoji juu ya ushujaa na ujasiri wao na kuwalazimisha askari wale wa Kiislamu kurudi katika uwanja wa vita. Kabla askari wale wa Kiislamu hawajafanya maamuzi nini wafanye, walimuona Khawlah رضي الله عنها akichomoa upanga wake na kuongoza mapambano dhidi ya maadui. Wanaume nao wakageuza farasi wao na kurejea kuendelea na vita, vita ambayo hatimaye Waislamu walishinda.

Mpiganaji wa Kiislamu aliyekuwepo siku ile alisema: "Wanawake walikuwa wakali zaidi kwetu kuliko walivyokuwa askari wa kirumi (kirumi). Tulifikia hatua ya kuona kuwa, kurudi katika uwanja wa vita kupigana na kufa, ilikuwa ni rahisi kuliko kukabiliana na hasira za akina mama wale hapo baadaye".

Khawlah Bint Al-Azwar رضي الله عنها alibakia kielelezo bora cha ushujaa wa wanawake wa Kiislamu wakati wa uhai wake, na amebakia kuwa kielelezo bora mpaka hii leo. Khawlah Bint Al-Azwar رضي الله عنها amekuwa na atabakia mfano bora kwa wanawake na wanaume kuwa, Muislamu ni lazima awe tayari kutetea na kupigania kile anachokiamini, na hata siku moja hapaswi kukubali kushindwa au kurudi nyuma kwa kukata tamaa.

# Nusaybah binti Ka'b - Ummu 'Umarah

## Rafiki na Jirani wa Mtume Peponi

Jina kamili la mama huyu ni: Nusaybah bint Ka'b ibn 'Amr ibn 'Awf Al-Khazrajy Al-Ansariyah رضي الله عنها. Ummu 'Umarah ni mama wa ki-Ansar, na alikuwa akitokea katika ukoo wa Banu Najjar. Kaka wa mama huyu 'Abdullah Ibn Ka'b, aliuwawa shahidi katika vita maarufu, vita vya Badr. Mama huyu alikuwa maarufu na alijulikana kwa ushujaa wake katika uwanja wa vita na mapambano. Alikuwa mama mtiifu na mwaminifu, mama mwenye mapenzi ya kweli kwa familia yake; na alikuwa mama mwenye subira na uvumilivu wa hali ya juu sana. Mama huyu pia alikuwa na elimu kubwa ya Qur'an na Hadith.

Nusaybah na mume wake Zayd Ibn 'Asim" رضي الله عنهما walikuwa miongoni mwa watu wa mwanzo kuukubali na kuingia katika Uislamu katika miaka ya mwanzo kabisa. Katika siku ile ya tukio maarufu na kubwa la Al-'Aqaba, ambapo Waislamu sabini na nne (74) walichukua ahadi ya utii, wawili (2) kati yao walikuwa wanawake. Mama huyu alikuwa miongoni mwa wanawake hao waliokuwepo na kushuhudia tukio hilo, na wao kuchukua ahadi ya utii kwa Mtume ﷺ. Mama mwingine alikuwa Ummu Muni' Asma' bint 'Amr Ibn 'Adi.

Nusaybah bint Ka'b رضي الله عنها anasimulia kuwa, mume wake, Ghazyah Ibn 'Amr, alimwambia Mtume ﷺ kuwa, wanawake hawa wawili pia wanataka kuchukua kiapo cha utii. Mtume ﷺ akakubali, na utaratibu ulikuwa sawa kwa wanaume na wanawake katika kuchukua ahadi ya utii. Isipokuwa Mtume ﷺ alikuwa akiwapa mkono Waislamu wanamume wakati wanachukua kiapo cha utii, lakini hakuwapa mkono Waislam wanawake. Katika vitabu vya historia ya Uislamu, tukio hili la kuchukua ahadi ya utii siku ile limeitwa *Bay'atul-'Aqabah Ath-Thaniyah* (kiapo cha pili 'Aqabah). Aliporudi Madinah baada ya kuchukua ahadi ya utii, Ummu 'Umarah alijitolea katika kuwaelimisha wanawake wa Kiislamu dini yao.

Mama huyu alishuhudia matukio mengi makubwa na ya kihistoria akiwa na Mtume ﷺ. Miongoni mwa matukio hayo, Nusaybah رضي الله عنها alishuhudia vita vya Uhud, *Bay`at Ar-Ridhwan*, vita vya Hunayn, vita vya Yamamah, kutiwa saini makubaliano ya mkataba wa Hudaybiyah na Umrah aliyoifanya Mtume ﷺ. Katika matukio yote haya, mama huyu alikuwa tayari kujitoa yeye mwenyewe, nafsi yake, mali yake na kila kitu kwa ajili ya kuupeleka mbele Uislamu.

Kama tulivyozungumza hapo mwanzo, Ummu ‘Umarah رضي الله عنها aliolewa kwa mara ya kwanza na Zaid Ibn ‘Asim Al-Mazni. Na alijaaliwa kuzaa nae watoto wawili wa kiume, ambao waliwaita Abdullah na Habib na watoto wote hawa walikuwa miongoni mwa maswahaba wa Mtume ﷺ. Mtoto mwingine wa kiume aliyeitwa Tamim, na mtoto mwingine wa kike waliyemwita Khawlah, walizaliwa katika ndoa ya pili ya mama huyu, ambapo aliolewa na Ghazyah Ibn ‘Amr Mazni.

Ummu ‘Umarah - Nusaybah bint Ka`b رضي الله عنها, alikuwa mwanamke hodari na mpambanaji mwenye maarifa makubwa katika uwanja wa vita. Uwezo wake na ujuzi aliokuwa nao katika kupigana kwa kutumia upanga ulikuwa unastaajabisha kabisa. Wale waliomshuhudia katika uwanja wa vita siku ile ya vita vya Uhud, walimshangaa, ni vipi mwanamke anaweza kuwa jemedari na hodari vitani kiasi kile. Mtume ﷺ anasema, kila upande aliogeuka yeye (Mtume ﷺ) katika uwanja wa vita, alikuwa akimuona Ummu ‘Umarah - Nusaybah bint Ka`b رضي الله عنها akipambana na kumlinda Mtume ﷺ. huyu ndiye mama wa Kiislamu, Ummu ‘Umarah - Nusaybah bint Ka`b.

Ni muhimu kuzingatia kuwa, katika siku ya vita vya Uhud, Nusaybah bint Ka‘b رضي الله عنها alimuomba Mtume ﷺ amuombee dua kwa Allah, ili yeye (Nusaybah bint Ka‘b رضي الله عنها) na watoto wake wawe na Mtume ﷺ Peponi. Mtume ﷺ akamuomba Allah akisema: “Ewe Allah! Wafanye kuwa jirani zangu Peponi.” Baada ya dua hii, Nusaybah bint Ka‘b رضي الله عنها akasema, “Kuanzia leo, sito shawishika na anasa yeyote ya ki-dunia”.

Mwenyewe Nusaybah bint Ka‘b رضي الله عنها anasimulia wakati ulivyokuwa mgumu kabisa wakati wa vita vya Uhud. Anasema wapiganaji wa Kiislamu (Mujahidin) walikuwa katika wakati mgumu sana na walikuwa wanaelekea kushindwa vita, na walikuwa katika hali ya kusambaa na kupoteana. Nusaybah

bint Ka'b akiwa na watoto wake wawili na mume wake walijaribu kumzunguuka Mtume ﷺ ili kumuhami na kukabiliana na hatari yeyote itakayotokea ya kujaribu kumdhuru Mtume ﷺ. Nusaybah bint Ka'b رضي الله عنها alikuwa amekamata upanga kwa mkono wake mmoja na ngao kwa mkono wake wa pili kwa ajili ya kujihami. Kama maadui wangejaribu kuwasogelea wakiwa wanatembea kwa miguu na hawako juu ya farasi, basi wangewauwa adui wote.

Mmoja katika maadui alimshambulia Nusaybah bint Ka'b رضي الله عنها, mama huyu alijilinda na mashambulizi yale kwa kutumia ngao yake; kisha alivuta hatamu za farasi yule na kumgeuza, kisha alitumia fursa ile kumchoma kwa kutumia upanga yule farasi. Farasi aliyejeruhiwa alianguka chini, na Nusaybah bint Ka'b رضي الله عنها alianza kupambana na askari aliyekuwa akiendesha farasi yule. Mtume ﷺ alipoona vile, alipaza sauti kumwita 'Abdullah Ibn Ummu 'Umarah رضي الله عنه ili aje kumsaidia mama yake. Kwa pamoja, 'Abdullah Ibn Ummu 'Umarah رضي الله عنه na mama yake wakammaliza askari na mpiganaji wa maadui.

'Abdullah Ibn Ummu 'Umarah رضي الله عنه anasimulia jinsi hali ilivyokuwa wakati wa vita vya Uhud na namna ambavyo maadui walivyowashambulia. Mujahidina walisambaratika, yeye na mama yake wakasogea karibu na Mtume ﷺ na kumuhami kutoka kila upande asipatwe na madhara. Mtume ﷺ alimwita 'Abdullah Ibn Ummu 'Umarah رضي الله عنه ili amshambulie adui. 'Abdullah Ibn Ummu 'Umarah رضي الله عنه alirusha jiwe kumshambulia kafiri yule; na jiwe lile lilimpata farasi aliyekuwa anatumiwa na kafiri yule katika vita, na farasi yule akaanguka chini. Alirusha jiwe jingine kwa nguvu na jiwe lile lilimpata yule kafiri na alikufa pale pale na Mtume ﷺ akaonekana mwenye furaha. Kisha akamuona Ummu 'Umarah akiwa anabubujikwa na damu katika mabega yake; Mtume ﷺ akamwambia 'Abdullah رضي الله عنه akifunge kidonda cha mama yake na Mtume ﷺ akasema hakika hii ilikuwa familia bora. Mtume ﷺ akamuomba Mwenyezi Mungu Aifanye familia hii kuwa marafiki na jirani zake Peponi.

Wote, Nusaybah bint Ka'b (Ummu 'Umarah رضي الله عنها) na mwanae 'Abdullah رضي الله عنه walifurahi sana waliposikia Mtume ﷺ akiwaombea dua hii kwa kinywa chake. Dua hii pia ya Mtume ﷺ iliwazidishia ari na morali na hivyo wakarejea katika mapambano wakiwa na nguvu kubwa zaidi. Baada ya kurejea vitani na kuendelea na mapambano, Abdullah alijeruhiwa na adui yake katika mkono wake wa kushoto, na damu nyingi ilikuwa inatoka katika jeraha lile.

Mtume ﷺ akamwambia Abdullah رضي الله عنه alifunge jeraha lile haraka. Ummu 'Umarah alipomuona mwanae akibubujikwa na damu katika jeraha, Nusaybah bint Ka'b alimfunga mwanae jeraha lile huku akimwambia mwanae asirudi nyuma wala kuvunjika moyo, bali aongeze nguvu katika kukabiliana na adui zake na adui wa Mwenyezi Mungu. Mtume ﷺ alipoona ushujaa na ujasiri wa mama Nusaybah bint Ka'b na mwanae Abdullah, akatabasamu na kusema: "Ewe Ummu 'Umarah! Wapi mtu anaweza kupata ujasiri kama mliokuwa nao?'

Katika tukio lingine, Nusaybah bint Ka'b (Ummu 'Umarah) alikuwa amesimama mbele ya Mtume ﷺ akiwa ameshika upanga ukiwa wazi, mara akaja adui na Mtume ﷺ akasema kumwambia Nusaybah رضي الله عنها huyu ndiye kafiri aliyemjeruhi mwanao. Mama Nusaybah رضي الله عنها alimshambulia kafiri yule kwa pigo moja kali sana kwa kutumia upanga wake na akaukata mguu wa kafiri yule. Kafiri yule alianguka huku uso wake ukiwa chini, na wapiganaji wengine wa Kiislamu walifika na kumuuwa kabisa. Mtume ﷺ alifurahishwa sana kwa nguvu na ujasiri aliouonesha mama huyu wa Kiislamu, Nusaybah bint Ka`b رضي الله عنها. Mtume ﷺ akamshukuru Allah Aliyempa mafanikio yake Nusaybah bint Ka`b رضي الله عنها na kumfanya amalize machungu kutokana na kujeruhiwa vibaya mwanae kwa kumfanya Nusaybah رضي الله عنها ashuhudie kifo cha kafiri aliyemjeruhi mwanae mbele ya macho yake.

Katika vita hivi, Nusaybah bint Ka'b رضي الله عنها alipata majeraha makubwa takriban kumi na mbili; moja katika majeraha hayo ni jeraha alilolipata begani, ambalo liliingia sana ndani na kusababisha kutokwa na damu nyingi sana mpaka akaanguka chini na kupoteza nguvu na fahamu. Ilichukua mwaka mzima kupona jeraha hili. Alipopata fahamu swali lake la kwanza, alitaka kujua hali ya Mtume ﷺ, badala ya kutaka kujua hali za watoto wake au mume wake. Alipoambiwa kuwa Mtume ﷺ alikuwa yuko salama, alimshukuru Allah. Mbali ya vita, Nusaybah bint Ka'b رضي الله عنها alishiriki pia katika ukombozi wa Makkah na vita dhidi ya Musaylamah - muongo. Katika vita hivi alipata majeraha kumi na moja na mkono wake ulikatwa.

Baada ya vita vya Uhud na majeshi ya Waislamu kurudi Madinah chini ya uongozi wa Mtume ﷺ, Mtume ﷺ aliwatangazia Waislamu kuwa wanatakiwa kujiandaa kwenda katika sehemu iitwayo Hamra' Al-Asad رضي الله عنها, kuwakimbiza makafiri wa huko. Wapiganaji wa Kiislamu walitumia usiku mmoja tu wakiwa Madinah. Ummu 'Umarah - Nusaybah bint Ka`b رضي الله عنها alisimama

na yeye kuungana na jeshi la wapiganaji wa Kiislamu, akiwa amejawa na hamasa na ari kubwa ya kupambana na washirikina na makafiri. Hata hivyo hakuweza kufanya hivyo kutokana na udhaifu aliokuwa nao uliotokana na majeraha makubwa aliyokuwa ameyapata. Mara tu baada ya kurejea Mtume ﷺ akamuuliza kaka wa Nusaybah رضي الله عنها, ‘Abdullah Ibn Ka’b kuhusu hali ya dada yake. Mtume ﷺ alipofahamishwa kuwa alikuwa anaendelea vizuri na vidonda vilikuwa vinapona, alimshukuru Allah kwa neema Zake na fadhila Zake.

Ummu ‘Umarah - Nusaybah bint Ka`b رضي الله عنها na wanawake wengine walishiriki pia vita dhidi ya Banu Quraydhah. Mtume ﷺ aliwapa sehemu ya ngawira zilizopatikana wakati wa vita hivi. Hivi ndivyo Mtume ﷺ alivyokuwa akitenda haki. Mama huyu pia alishiriki na alikuwa na mchango mkubwa wakati wa kutiwa saini kwa mkataba wa Hudaybiyah. Mwenyewe Nusaybah رضي الله عنها anasimulia jinsi walivyotoka Madinah kuelekea Makkah kwa ajili ya kufanya ibada ya ‘Umrah wakiongozwa na Mtume ﷺ. Walizuiliwa na makafiri katika eneo la Hudaybiyah. Makafiri wa ki-quraishi walikuwa hawataki Waislamu waingie katika mji wa Makkah. ‘Uthman Ibn ‘Affan رضي الله عنه aliteuliwa kuwa mjumbe wa Waislamu, na aliagizwa kwenda Makkah kufanya mazungumzo na makafiri. ‘Uthman Ibn ‘Affan رضي الله عنه alichelewa kurejea na kukawa na tetesi zilizoenea kuwa, ‘Uthman Ibn ‘Affan رضي الله عنه ameuwawa. Baada ya kupokea amri kutoka kwa Allah, Mtume ﷺ alikaa chini ya mti na kuanza kupokea ahadi ya utii kwa Allah na Mtume wake ﷺ kutoka kwa maswahaba. Wale waliokuwa na silaha wakazishika silaha zao barabara. Wengi katika maswahaba walikuja bila silaha yeyote. Hii ni kwa sababu walikuja wakiwa wamekusudia kufanya ‘Umrah tu, na si kupigana vita. Ummu ‘Umarah. anasema, yeye alikuwa na fimbo na alikuwa amechomeka kisu katika mkanda wake ili kuvitumia ikiwa maadui watawavamia. Baadae ilikuja kugundulika kuwa tetesi juu ya kuuwawa kwa ‘Uthman Ibn ‘Affan رضي الله عنه zilikuwa ni tetesi za uongo. Na makubaliano yalifanyika na maadui, makubaliano ambayo yalikuja kufahamika mpaka leo kama makubaliano au mkataba wa Hudaybiyah. Makubaliano haya yanatajwa ndani ya Qur’an katika ayah ifuatayo:

۞ لَّقَدْ رَضِيَ ٱللَّهُ عَنِ ٱلْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ ٱلشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِى قُلُوبِهِمْ
فَأَنزَلَ ٱلسَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَٰبَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿١٨﴾ وَمَغَانِمَ كَثِيرَةً يَأْخُذُونَهَا ۗ وَكَانَ ٱللَّهُ عَزِيزًا
حَكِيمًا ﴿١٩﴾

***“Kwa hakika Mwenyezi Mungu Amewaridhia Waislamu walipofungamana nawe chini ya mti; na alijuwa yaliyo nyoyoni mwao. Basi Akateremsha utulivu juu yao, na Akawapa kushinda kwa zama za karibu. Na ngawira (nyara) nyingi watakazozichukua, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu (na) Mwenye Hikima*. (48:18-19)**

Wanawake wapatao ishirini walishiriki katika vita vya Khaybar; miongoni mwa wanawake hao alikuwa ni Ummu ‘Umarah رضي الله عنها. Baada ya jeshi la Waislamu kupata ushindi katika vita hivi, wanawake wa Kiislamu pia walipewa mgao wao wa ngawira. Ummu ‘Umarah رضي الله عنها peke yake, alipata nguo nzuri tena zenye thamani kubwa, mapambo pamoja na Dinar mbili.

Katika vita vya Hunayn, Ummu ‘Umarah رضي الله عنها alifanya kazi kubwa na kuchangia kubadili matokeo ya vita, kutoka hali ya kushindwa mpaka kupata ushindi mkubwa. Yeye mwenyewe Nusaybah bint Ka‘b رضي الله عنها anasimulia kazi aliyoifanya katika vita hivi: “Katika siku ya vita vya Hunayn, wakati Waislamu wakiwa wameshindwa vibaya, nilichomoa upanga wangu na kupaza sauti nikasema “Enyi Ansar, kwanini mnakimbia? Sio tabia yenu kukimbia vita.” Kisha anaongeza kusema kuwa, “Nilimfuata kafiri mmoja aliyekuwa akiwakimbiza Waislamu. Nikapambana naye, akaanguka chini, nikachukua upanga wake na kuingia katika uwanja wa vita.” Hivi ndivyo alivyoshiriki kwa kuwahamasisha wapiganaji wa Kiislamu na yeye mwenyewe kushiriki kikamilifu katika uwanja wa vita. Mtu mmoja kutoka kabila la Banu Hawazin aliingia katika uwanja wa vita akiwa juu ya ngamia, akipeperusha bendera. Nusaybah bint Ka‘b رضي الله عنها alimshambulia kwa nguvu sana ngamia yule na ngamia yule aliumia na kuanguka chini, kisha mama wa Kiislamu, Ummu ‘Umarah - Nusaybah bint Ka‘b رضي الله عنها alimshambulia mtu yule asiweze tena kupona. Katika vita hivi, Ummu ‘Umarah alipata mgao wake wa ngawira pia.

Wakati Mtume ﷺ akiwa hai, kulitokea makafiri waliodai kuwa na wao ni mitume sawa na alivyokuwa Mtume wa Allah! Mmoja kati ya makafiri hao alikuwa Musaylamah. Mtume ﷺ akamtuma mtoto wa Ummu ‘Umarah ﷺ, Habib Ibn Zaid kama muwakilishi wake kwenda kwa Musaylamah muongo, ili kumpa nasaha na kumtaka arudi katika njia ya haki na kuachana na madai yake ya uongo kuwa na yeye ni Mtume. Huku akivunja kanuni iliyokuwepo ya kidiplomasia, ambapo mjumbe alikuwa hakamatwi wala kuadhibiwa,

Musailamah alimkamata na kumfunga Habib. Kisha Musailamah muongo akawaita watu waje washuhudie kile kilichoitwa masiku ya kukumbukwa. Mjumbe wa Mtume ﷺ, Habiib Ibn Zaid, aliletwa. Kwa namna alivyoonekana na majeraha aliyokuwa nayo, ilikuwa wazi kabisa kuwa alikuwa amedhalilishwa, ameteswa sana na kufanyiwa kila aina ya ukatili na uovu. Walikuwa wanaamini kuwa wanaweza kumuondoa ujasiri na ukakamavu wote aliokuwa nao na hivyo aonekane mbele ya mkusanyiko ule wa watu akiwa dhalili na myonge. Walikuwa wakiamini kuwa baada ya hapo, atampa heshima na kumkubali Musailamah na kukubali utume wake wa uongo mbele za watu waliokusanywa, hivyo muongo mkubwa atakuwa ameweza kufanya alichokiona maajabu na hivyo kuzidi kuwadanganya wale aliokuwa akiwahadaa.

Hivyo Musailamah akamuuliza Habiib Ibn Zaid رضي الله عنه, "Je, unaamini kuwa Muhammad ﷺ hakika ni Mtume wa Allah?" Habiib Ibn Zaid رضي الله عنه akaitika kwa ujasiri kabisa, "Ndiyo, nashuhudia kuwa Muhammad ﷺ hakika ni Mtume wa Allah." Uso wa Musailamah ukabadilika rangi na kuwa mweupe kwa hasira na udhalilifu lakini bado akaendelea kuuliza, "Je unashuhudia kuwa mimi ni Mtume wa Allah?" Habiib Ibn Zaid رضي الله عنه akamjibu kwa dharau, "Upuuzi!"

Muongo Musailamah akadhalilika na uso wake ukawa mweusi karibu arukwe na akili. Mpango wake ulikuwa umefeli. Mateso yake kwa Habiib Ibn Zaid رضي الله عنه hayakuzaa matunda. Akadhalilika sana mbele ya umati wa watu ambao yeye mwenyewe aliwaita na kuwakusanya ili washuhudie kile alichokiita miujiza. Aibu hii ilikuwa ni kubwa mno kiasi kwamba ilivunja heshima yake mwanzo na mwisho. Ghafla akawa mkatili wa kupitiliza kama tembo aliyejeruhiwa, akamwita mtesaji wake ambae alifika haraka na kuanza kumshambulia Habiib Ibn Zaid رضي الله عنه kwa panga mwilini mwake. Alikuwa akimsukuma na kumkata mwili wake vipande vidogo vidogo, kiungo kimoja baada ya kingine. Habiib Ibn Zaid رضي الله عنه hakupiga kelele yoyote zaidi ya kutamka kwa ukakamavu, "Hapana Mola wa haki isipokuwa Allah na Muhammad ni Mtume wake."

Taarifa juu ya kuuwawa kikatili ziliwafikia Waislamu kupitia kwa Mtume. Mama wa Kiislamu, Nusaybah رضي الله عنها alionesha ustahamilivu na ujasiri wa kupigiwa mfano pale alipopata habari za kukatwa katwa na kuuwawa kwa mwanae, Habib ibn Zayd رضي الله عنه, kwa kukataa kuwa mfuasi wa Musailama –

muongo na kuukanusha utume wake wa uongo hadharani. Mama wa Kiislamu, Nusaybah رضي الله عنها, alipopata taarifa juu ya msiba huu alitamka maneno haya: "Nilimuandaa mwanangu kufa kwa ajili ya Allah, namuomba Allah Ampokee kama shahidi."

Haikupita muda mrefu toka kifo cha Habib ibn Zayd رضي الله عنه, vikatokea vita vya Al-Yamama; Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه akaandaa jeshi na kutoka kwenda kukabiliana na jeshi la Musaylamah muongo. Ummu 'Umarah رضي الله عنها alikuwa miongoni mwa wapiganaji waliotoka pamoja na jeshi la Waislamu; Mama huyu wakati huo alikuwa na umri wa miaka takriban sitini (60)! Na mwanae 'Abdullah Ibn Zaid رضي الله عنه alikuwa pamoja na mama yake katika vita hivi; na alikuwa miongoni mwa watu ambao hatimaye walimuuwa Musaylamah. Pamoja na kwamba alikuwa na umri wa miaka sitini (60), Nusaybah alishiriki katika vita hivi kwa ujasiri mkubwa sana na alikuwa akipaza sauti muda wote akisema: "Ewe adui wa Allah Musaylimah, jitokeze." Katika jitihada zake za kutaka kumuuwa Musaylimah, mama huyu alijeruhiwa majeraha kumi na moja (11), na mkono wake mmoja ulikatwa. Mwisho wa vita, Musaylimah aliuliwa na mwanae, `Abdullah baada ya kuanguka chini kutokana na shambulizi la Wahshi ibn Harb رضي الله عنه, mtu aliyemuuwa swahaba na mjomba wa Mtume ﷺ, Hamzah. Vita hivi vya Yamamah vilikuwa vita vya mwisho ambavyo Ummu `Umarah رضي الله عنها alivishuhudia na kushiriki.

Wakati wa Ukhalifa wa 'Umar Ibn Khattab رضي الله عنه, mashuka mazuri na yenye thamani yalitumwa kwa Nusaybah رضي الله عنها. Baadhi ya mashuka haya yalikuwa makubwa na mazuri sana. Baadhi ya maswahaba wakapendekeza mashuka yale yapelekwe kwa Safiyyah Ibn 'Ubayd رضي الله عنها, mke wa 'Abdullah Ibn 'Umar. Lakini 'Umar Ibn Khattab akasema, "Ninamfahamu aliye bora kuliko yeye (Safiyyah رضي الله عنها), na aliyesifiwa na Mtume ﷺ kuliko yeye." Kisha aliagiza mashuka yale yapelekwe kwa Ummu 'Umarah - Nusaybah رضي الله عنها.

Siku moja Ummu 'Umarah رضي الله عنها alimwambia Mtume ﷺ kuwa, katika Qur'an Tukufu, mara nyingi wamekuwa wakitajwa wanaume na wanawake mara nyingi hawapewi nafasi; Mara moja Ayah ifuatayo ilishushwa:

إِنَّ ٱلْمُسْلِمِينَ وَٱلْمُسْلِمَٰتِ وَٱلْمُؤْمِنِينَ وَٱلْمُؤْمِنَٰتِ وَٱلْقَٰنِتِينَ وَٱلْقَٰنِتَٰتِ وَٱلصَّٰدِقِينَ

وَٱلصَّٰدِقَٰتِ وَٱلصَّٰبِرِينَ وَٱلصَّٰبِرَٰتِ وَٱلْخَٰشِعِينَ وَٱلْخَٰشِعَٰتِ وَٱلْمُتَصَدِّقِينَ وَٱلْمُتَصَدِّقَٰتِ

وَٱلصَّٰٓئِمِينَ وَٱلصَّٰٓئِمَٰتِ وَٱلۡحَٰفِظِينَ فُرُوجَهُمۡ وَٱلۡحَٰفِظَٰتِ وَٱلذَّٰكِرِينَ ٱللَّهَ كَثِيرٗا وَٱلذَّٰكِرَٰتِ أَعَدَّ ٱللَّهُ لَهُم مَّغۡفِرَةٗ وَأَجۡرًا عَظِيمٗا ﴿٣٥﴾

***"Bila shaka Wanaume wenye kufuata vizuri nguzo za Uislamu, na wanawake wenye kufuata vizuri nguzo za Uislamu, na wanaume wanaoamini vizuri nguzo za Imani, na wanawake wanaoamini vizuri nguzo za Imani, na wanaume wanaotii, na wanawake wanaotii, na wanaume wasemao kweli, na wanawake wasemao kweli, na wanaume wanaosubiri, na wanawake wanaosubiri, na wanaume wanaonyenyekea na wanawake wanaonyenyekea, na wanaume wanaotoa (Zaka na) sadaka na wanawake wanaotoa (Zaka na) sadaka, na wanaume wanaofunga na wanawake wanaofunga, na wanaume wanaojihifadhi tupu zao, na wanawake wanaojihifadhi, na wanaume wanaomtaja Mungu kwa wingi, na wanawake wanaomtaja Mwenyezi Mungu (kwa wingi), Mwenyezi Mungu Amewaandalia msamaha na ujira mkubwa.*** **(33:35)**

Ummu 'Umarah رضي الله عنها alikuwa na nafasi muhimu sana miongoni mwa maswahaba wanawake, na ameacha somo zito kwa akina mama wa Kiislamu na hata wanaume kwa zama zote. Mtume ﷺ alipoona namna ushujaa na kujitoa muhanga kwa familia yote - mume, mke na watoto – katika wakati mgumu na hatari, wakati wa vita vya Uhud, Mtume ﷺ alimuomba Allah Airehemu familia ile.

Nusaybah bint Ka'b رضي الله عنها, ambaye pia ndiye Ummu 'Umarah رضي الله عنها, alitumia muda wake wote uliosalia akimuabudu Allah, na baada ya miaka mingi ya kuutumikia Uislamu kwa mali zake, nafsi yake na watoto wake, roho ya mama shujaa, Nusaybah bint Ka'b رضي الله عنها – ilirejea kwa Mola wake katika mwaka wa 13 baada ya Hijjirah.

Mtoto wake mwingine, 'Abdullah Ibn Zaid رضي الله عنه aliuwawa shahidi katika vita vya Hurrat. Vita hivi vilitokea mwaka wa 63 baada ya Hijjrah, mashariki mwa mji wa Madinah. 'Abdullah Ibn Zaid رضي الله عنه alikuwa miongoni mwa maswahaba wakubwa wa Mtume ﷺ na alishiriki pia katika vita dhidi ya Musaylamah – muongo (Aliyedai kuwa na yeye ni Mtume).

Mwenyezi Mungu Amrehemu mama huyu; Mama wa Kiislamu, Ummu 'Umarah - Nusaybah bint Ka'b رضي الله عنها!

# Safiyyah Binti Abdul Muttalib

## Nataka kutoa Mwanaume wa kweli Kutokana na Mtoto Huyu

Mama huyu alikuwa mama mzazi wa Zubayr ibn Awwaam رضي الله عنه na dada halisi wa shujaa na shahidi, Hamzah ibn Abdul Muttalib رضي الله عنه. Inasemekana mama huyu alikuwa ndiye shangazi wa pekee wa Mtume ﷺ ambaye aliingia katika Uislamu na alikuwa miongoni mwa Waislamu waliohamia Madinah. Alikuwa mama mkakamavu na mkali kwa kiasi fulani.

Kwa mara ya kwanza, mama huyu aliolewa na Al-Harith ibn Umayyah. Bwana huyu alikuwa ni kaka wa Abu Sufyaan. Al-Harith ibn Umayyah alifariki kabla wawili hawa hawajajaaliwa kupata mtoto. Kisha mama huyu aliolewa na Al-'Awwam ibn Khuwaylid, ambaye alikuwa kaka wa mama yetu, mama wa waumini, Khadijah bint Khuwaylid رضي الله عنها. Wakiwa na bwana huyu, Safiyah alijaaliwa kuzaa watoto wawili, As-Sa'ib na Zubayr ibn Awwaam رضي الله عنه. Bwana huyu (Al-'Awwam ibn Khuwaylid) alipofariki, Safiyah رضي الله عنها aliamua kutumia muda wake mwingi kuwalea watoto wake wawili ambao walikuwa ni yatima, na zaidi mwanae mdogo, Zubair ibn Al-Awwaam رضي الله عنه. Kila mwanae huyu (Zubayr ibn Awwaam) aliporudi nyumbani akilia au kulalamika kuwa ameonewa au kupigwa na wenzake, Safiyah رضي الله عنها alikuwa akimfokea, akimfunga kamba na kumuadhibu ili awe imara na jasiri.

Siku moja, mtu mmoja kutoka katika familia ya marehemu mume wake alipita na kukuta Safiyah رضي الله عنها akimuadhibu vikali mwanae; bwana yule alimtaka Safiyah awe na huruma na awatendee wema watoto wale yatima. Safiyah Bint Abdul Muttalib رضي الله عنها akamjibu kuwa: "Nataka kutoa mwanaume wa kweli kutokana na mtoto huyu. Mwanaume ambaye hatokubali kushindwa wala kuonewa. Mwanaume ambaye hata siku moja hatosalimu

amri kwa kiumbe yeyote wa Allah". Haya yalikuwa ndiyo majibu ya Safiyah Bint Abdul Muttalib رضي الله عنها.

Inasemekana siku moja Zubayr ibn Awwaam رضي الله عنه alipigana na mtu mmoja ambaye alikuwa amemtukana au kumtolea lugha isiyofaa. Zubayr رضي الله عنه alikuwa mkakamavu mno kiasi kwamba alimvunja mkono yule bwana aliyemtukana na akampiga sana. Huku akiwa na maumivu makali, bwana huyu aliletwa kwa Safiyah Bint Abdul Muttalib. Safiyah رضي الله عنها akamuuliza yule bwana nini kimemtokea? na Safiyah Bint Abdul Muttalib رضي الله عنها akaambiwa kuwa: "Amepigana na mwanao Zubayr رضي الله عنه, na Zubayr akamfanya kile ambacho unakiona."

Bi Safiyah Bint Abdul Muttalib رضي الله عنها aliposikia maneno yale, alifurahi sana na kuimba shairi hili:

Unamuonaje Zubayr?
Umemuona mshamba, laini kama siagi au tende?
Au umemkuta shujaa na mkali kama tai mkubwa?

Si mtu rahisi kumshinda au kama chakula rahisi unachoweza kula
bila kutokwa jasho!

Safiyah Bint Abdul Muttalib رضي الله عنها alikuwa amefanikiwa kupata alichokihitaji; Zubayr alikuwa imara kimwili na kiimani.

Katika mambo ambayo historia wakati mwingine inastaajabisha, ni kumuona mtu akimuandaa mwenzake na aliyeandaliwa akaifikia kheri kabla ya aliyekuwa anamuandaa. Na hivi ndiyo ilivyokuwa kwa familia hii. Zubayr aliukubali Uislamu na kusilimu kabla ya mama yake, Safiyah رضي الله عنها; Pamoja na kumpa malezi mazuri na ya kijasiri, Safiyah رضي الله عنها alikuwa akijadiliana na mwanae juu ya dini mpya na wakivutana sana. Lakini Safiyah alikuwa hana la kufanya kwa sababu wakati huu, Zubayr ibn Awwaam رضي الله عنه hakuwa mtoto tena na alikuwa na uwezo wa kufanya maamuzi yake. Hivyo Safiyah alikuwa hana udhibiti tena kwa Zubayr رضي الله عنه ukiachia kuheshimiwa na kutiiwa kama mama. Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها hakuingia katika Uislamu, mpaka siku ambayo kaka yake Hamza ibn Abdul Muttalib رضي الله عنه, alipoukubali na kuingia katika Uislamu. Hivyo, Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها aliukubali Uislamu na kusilimu, baada ya mwanae Zubayr ibn Awwaam رضي الله عنه kuukubali Uislamu na kusilimu.

Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها alikuwa na sifa na mambo mengi ya kujifunza kutoka kwake, mambo ambayo yametajwa katika historia ya Mtume ﷺ. Moja katika mambo haya ni mchango wake na kazi aliyoifanya wakati wa vita vya Khandaq. Mtume ﷺ aliwaweka wanawake na wanaume katika ngome ili kuwahifadhi na kuwalinda dhidi ya majeshi ya ushirika wa makafiri wakiwemo mayahudi wa Banu Quraydhah. Safiyah رضي الله عنها alikuwa ndani ya ngome iliyojulikana kama 'Fari' wakiwa chini ya uangalizi wa swahaba Hassan ibn Thabit رضي الله عنه. Hassan ibn Thabit رضي الله عنه alipewa jukumu la kuwalinda wanawake na hakwenda kupigana.

Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها anasema: "Mtume ﷺ alipotoka kwenda kwenye vita vya Khandaq, aliwaweka wanawake ndani ya ngome iitwayo Fari', na akamkabidhi Hassan ibn Thabit رضي الله عنه jukumu la kutuangalia. Kisha myahudi mmoja akaja na kuanza kupanda ukuta wa ngome mpaka akaweza kutuona. Nilimwambia Hassan ibn Thabit رضي الله عنه asimame na kumuuwa myahudi yule, lakini akasema yeye hawezi, na kama angekuwa anaweza mambo ya kupigana, basi angekuwa ametoka na Mtume ﷺ na wala asingekuwa amepewa jukumu la kubaki akiwaangalia wanawake. Basi nilisimama mimi mwenyewe (Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها), nikamuuwa myahudi yule na kumkata kichwa chake.

Kisha nilimwambia Hassan ibn Thabit رضي الله عنه akirushe kichwa cha myahudi yule nje ya ngome ambapo kulikuwa na wayahudi wengine waliokuwa wakikusudia kutuvamia ili kuwatisha. Hassan ibn Thabit رضي الله عنه aliapa kwa jina la Allah kuwa hawezi kufanya hivyo. Hivyo nikachukua kichwa kile mimi mwenyewe na kukirusha kwa mayahudi. Mayahudi waliokuwa nje walipokiona kichwa kile walisema, 'Sisi tulijua, mtu huyu (wakimaanisha Mtume ﷺ) hawezi kuiacha familia yake bila kuweka mtu au watu wa kuiangalia'. Wakakimbia ....."

Hili ni moja kati ya matukio ambayo yanaonesha ni kwa namna gani Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها, mama wa Kiislamu tunayemzungumzia alivyokuwa jasiri kiimani, kimwili na mkakamavu. Mama huyu (Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها) alikuwa na mchango mkubwa sana pia katika vita vya Uhud. Waislamu walipohisi kuwa wameshindwa, yeye alisonga mbele na pale watu waliporudi nyuma, yeye alizidi kusonga mbele! Hammad anasimulia kutoka kwa Hisham kwamba, 'Urwah anasema:

"Safiyah رضي الله عنها alikuja siku ya vita vya Uhud wakati Waislamu wakiwa wamesambaratishwa akiwa ameshika mkuki mkononi mwake huku akiwashambulia makafiri kwa kutumia mkuki ule. Mtume ﷺ alipomuona (Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها), Mtume ﷺ alimwita mwanae Safiyah, Zubayr ibn Awwaam رضي الله عنه ili amzuie vinginevyo angeweza kudhurika, na yeye alikuwa shangazi yake Mtume ﷺ."

Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها alipopata habari juu ya kuuwawa kwa kaka yake, Hamzah ibn Abdul Muttalib رضي الله عنه, kaka yake ambaye yeye (Safiyah) alimpenda sana, alisonga kwenda mbele kuangalia namna gani kaka yake alikuwa ameuwawa huku akiwa amepasuliwa tumbo. Mwanae Zubayr ibn Awwaam رضي الله عنه alimzuia huku akimwambia kuwa, "Mama yangu, Mtume wa Allah anakuamuru urudi ulikotoka!" Hapa ndipo unaweza kumtofautisha Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها na wanawake wengine; hapa ndio unaweza kuona ujasiri, imani, ukakamavu vinapokutana na kujitokeza kwa pamoja. Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها alimwambia, "Vipi naweza kurejea nilikotoka ilhali nimesikia kuwa kaka yangu ameuwawa shahidi katika njia ya Allah? Si jambo zuri lililotokea lakini nitalipokea kwa ustahamilivu na uvumilivu na ninataraji kupata malipo ya subira na uvumilivu wangu kutoka kwa Allah Akipenda."

Zubayr ibn Awwaam رضي الله عنه akarudi kwa Mtume ﷺ na kumfahamisha kile ambacho mama huyu (Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها) alikuwa amemjibu. Kisha Mtume ﷺ akasema, "Muache aende (akamuone kaka yake)." Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها alikwenda ulipokuwa mwili wa shujaa Hamzah رضي الله عنه na kusimama pembeni ya mwili wake. Alitokwa na machozi, na kuomba msamaha kwa Allah na kusema: "*Inna lillahi wa inna ilahi raaji'un* (Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake Allah tutarejea)."

Huyu ni mama wa Kiislamu, aliyefahamu kuwa:

وَلَنَبْلُوَنَّكُم بِشَيْءٍ مِّنَ ٱلْخَوْفِ وَٱلْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ ٱلْأَمْوَٰلِ وَٱلْأَنفُسِ وَٱلثَّمَرَٰتِ ۗ وَبَشِّرِ ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿١٥٥﴾ ٱلَّذِينَ إِذَآ أَصَٰبَتْهُم مُّصِيبَةٌ قَالُوٓا۟ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيْهِ رَٰجِعُونَ ﴿١٥٦﴾ أُو۟لَٰٓئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَٰتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ ۖ وَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُهْتَدُونَ ﴿١٥٧﴾

***"Na Tutakutieni katika msukosuko wa (baadhi ya mambo haya); hofu na njaa na upungufu wa mali na wa watu na wa matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri. Ambao uwapatapo msiba husema: "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake Yeye tutarejea (atatupa jaza yake). Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao na rehema; na ndio wenye kuongoka".*** **(2:155-157)**

Kutokana na ujasiri na imani thabiti aliyokuwa nayo, mama huyu hakuwahi kutamka neno lolote la kujuta kutokana na kifo cha mtu wake yeyote wa karibu isipokuwa kifo cha Mtume ﷺ. At-Tabarani anasimulia kuwa, Mtume ﷺ alipofariki, Bi Safiyah رضي الله عنها alitoka akikung'uta nguo zake huku akisema:

Mambo mengi yametokea baada yako,

Kama ungekuwa hai na ukayashuhudia, basi madhara yake yasingetufikia kwa kiwango hicho kikubwa.

Ibn Ishaaq ameandika baadhi ya mistari ya mashairi ambayo Safiyah aliisoma akimlilia Mtume ﷺ. Sehemu ya mistari hiyo ni hii hapa:

Hii ndiyo siku tuliyotokwa na Mtume wa Allah!

Ewe macho yangu, lia na umwage machozi ya kutosha!

Imepokelewa pia kuwa aliwahi kusema mama Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها kuwa:

Siku ya kifo chako hakika ni siku nzito,

Siku ambayo jua lilikuwa gizani japo hutoa nuru!

Hakuna mwanahistoria yeyote anayepinga kuhusishwa mistari hii ya mashairi na Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها aliishi mpaka wakati wa Ukhalifa wa 'Umar رضي الله عنه. Ilikuwa wakati wa Ukhalifa wa 'Umar رضي الله عنه, mama huyu alifariki dunia.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu amridhie mama shujaa, Safiyah bint Abdul Muttalib رضي الله عنها – Aamin!.

# Lubabah binti al-Harith, Ummu Fadl

## Mama wa Mwanazuoni wa Ummah huu

Jina kamili la mama huyu ni Lubabah bint Al-Harith Ibn Huzn bin Bajir Ibn Hilaliyah رضي الله عنها. Mama huyu alifahamika pia kwa jina la Ummu Fadhl Ummu Fadhl رضي الله عنها ni mmoja kati ya wanawake wanne ambao Mtume ﷺ aliwaita 'wanawake waumini'. Wanawake hawa wanne ni Maimunah رضي الله عنها, Ummu Fadhl رضي الله عنها, Asma رضي الله عنها 'na Salma رضي الله عنها.

Maimunah رضي الله عنها, yeye ni mama wa Waumini na alikuwa ni ndugu wa Ummu Fadhl رضي الله عنها. Asma' na Salma رضي الله عنها ni dada wawili, watoto wa Umays. Ummu Fadhl رضي الله عنها, yeye alikuwa mke wa Abbas, mjomba wa Mtume ﷺ, na alikuwa mama wa watoto sita watukufu na wacha-Mungu, lakini alikuwemo pia mwanamke ambaye alikuja kuzaa watoto bora mfano wao. Watoto hawa ni Fadhl رضي الله عنه, Abdullah al-Faqih رضي الله عنه, Ubaidullah al-Faqih رضي الله عنه, Ma'bad رضي الله عنه, Qatsam رضي الله عنه na Abdurrahman رضي الله عنه.

Ama kuhusu huyu Ummu Fadhl رضي الله عنها, Abdullah Ibn Yazid anasema: "Hakuna mtu aliyezaa watoto bora, wenye thamani kubwa kuliko watoto aliozaa Ummu Fadhl".

Ummu Fadhl رضي الله عنها alisilimu kabla ya kufanyika kwa Hijrah. Mama huyu alikuwa mwanamke wa pili kusilimu baada ya Bi Khadijah رضي الله عنها (Mke wa Mtume ﷺ na mama wa Waumini) kama anavyosema mwanae Abdullah Ibn Abbas kuwa, "Mimi na mama yangu ni miongoni mwa wanawake na watoto waliopata mateso."

Ummu Fadhl رضي الله عنها alikuwa mwanamke mwenye hadhi na heshima kubwa miongoni mwa Wanawake wenye hadhi kubwa. Mtume ﷺ alikuwa akimtembelea na wakati mwingine akipumzika na akipata usingizi nyumbani kwa mama huyu.

Katika tukio moja, Ibn Ishak anasimulia kutoka kwa Ikrimah kwamba, “Abu Rafi anasema, yeye alikuwa ni mtumwa wa Abbas رضي الله عنه, Uislamu ulipokuja, Abbas رضي الله عنه aliingia katika Uislamu akifuatiwa na Ummu Fadlh رضي الله عنها. Pamoja na madhila na mateso waliyokuwa wakifanyiwa Waislamu, bado Abbas رضي الله عنه alikuwa akiheshimiwa na watu katika jamii.”

Abu Lahab yeye hakuongozana na Maquraishi wenzake kwenda katika vita vya Badr, lakini aliwakilishwa na Ash Ibn Hisham Ibn Mughirah, na hivi ndivyo ilivyokuwa. Kama mtu hawezi kwenda vitani, basi ilimlazimu kutafuta mtu wa kumuwakilisha.

Zilipotujia habari za ushindi wa Waislamu na namna Allah Alivyowadhalilisha makafiri katika vita vya Badr, tulijihisi wenye furaha na wenye nguvu. Lakini Abu Lahab alipatwa na uchungu sana baada ya kupokea taarifa ile. Wakati huo mimi nilikuwa mtu mnyonge, nilikuwa nikikata majani pembeni ya miamba jirani na kilipo kisima cha Zam Zam.

Nilikuwa nimekaa jirani na mahala alipokuwa amekaa Ummu Fadhl رضي الله عنها, lakini tulikuwa hatuna ukaribu au uhusiano wowote. Mara akaja Abu Lahab na kukaa sehemu tuliyokuwepo. Watu wakasema, “Abu Sufyan ibn al-Harith amewasili kutoka Badr”. Abu Lahab akasema, “Sogea karibu ewe Abu Sufyan, hakika nilisubiri sana habari njema kutoka kwako.” Kisha Abu Jahl alisimama na watu wakamzunguuka. Abu Lahab akasema, “Ewe mtoto wa kaka yangu, tusimulie vipi hali za watu zilikuwa (katika uwanja wa vita vya Badr)?” Abu Sufyan akasema, “Naapa, kwa jina la Mungu, tulipowaona, hawakupumzika kuvishambulia vikosi vyetu; walitushambulia na kuuwa wapiganaji wetu kadri walivyotaka. Hata tulipoinua majeshi yetu, tuliwashuhudia wapiganaji waliokuwa juu ya farasi weupe na weusi wakiwa katikati ya wapiganaji wa Kiislamu. Wapiganaji hao wa ajabu hawakushuka wala kukanyaga chini.”

Abu Rafi’ anasema, “Niliinua jiwe juu kwa mkono wangu, na kusema, “Naapa kwa jina la Allah! Wapiganaji hao (wa ajabu uliowaona) ni Malaika.” Ghafla Abu Lahab akanipiga pigo la nguvu, kwa sababu nilikuwa nimemchukiza, kisha alinikwida na kuniangusha chini, kisha alianza kunipiga na kuniadhibu vikali huku mimi nikiwa mtu mnyonge nisiyekuwa na mtetezi. Ghafla akasimama Ummu Fadl رضي الله عنه na kuchukua nguzo na kumpiga nayo kwa

nguvu kichwani Abu Lahab na kumuumiza vibaya. Ummu Fadhl رضي الله عنها akasema, “Ni lazima nimdhoofishe na kuvunja hadhi yake.”

Kisha Abu Lahab aliinuka akiwa mnyonge na aliyedhalilika. Kwa uwezo wa Allah, Abu Lahab hakuishi muda mrefu baada ya hapo, kwani jioni ile Mwenyezi Mungu Alimpa maradhi ya kidonda ambacho kilikuwa ndiyo sababu ya kifo chake.”

Ibn Sa’d ameeleza katika kitabu *At-Tabaqat al-Kubra* kuwa, Ummu Fadhl رضي الله عنها aliota ndoto ya ajabu mchana, hivyo haraka alikwenda kumsimulia ndoto ile Mtume ﷺ, Ummu Fadhl رضي الله عنها akasema, “Ewe Mtume wa Allah! Nimeota kwamba umati mkubwa katika familia yako uko ndani ya nyumba yangu”. Mtume ﷺ akamjibu kuwa, hiyo ni ndoto nzuri. Siku moja Fatmah atazaa mtoto, mtoto ambaye utamnyonyesha maziwa ambayo utamnyonyesha na mwanao (Mtoto huyo wa Ummu Fadhl ﷺ alikuja kuwa Qatsam). Haikuchukua muda mrefu, Fatmah bint Muhammad رضي الله عنها akamzaa Hasan ibn Ali, ambaye alililelewa na Ummu Fadhl رضي الله عنها.

Ummu Fadhl رضي الله عنها anasema, “Nilipokuja kwa Mtume ﷺ, kumpeleka mtoto, Mtume ﷺ alimchukua mtoto na kum-busu, lakini ghafla mtoto akamkojolea Mtume ﷺ, Mtume ﷺ akasema, “Ewe Ummu Fadhl, mchukue mtoto kwa sababu amekojoa.”

Ummu Fadhl رضي الله عنها anasema, “Nilimchukua mtoto nikamuadhibu kiasi kwamba akawa analia, nikasema, ‘Umemfanyia maudhi Mtume ﷺ kwa sababu umemkojolea”. Mtume ﷺ alipomuona mtoto analia, Mtume ﷺ akasema, “Ewe Ummu Fadhl, sasa unaniudhi kwa kumfanya mtoto huyo alie”. Kisha Mtume ﷺ akaomba aletewe maji na kuyanyunyuzia maji yale katika eneo lililoathirika (lililofikiwa na mkojo), kisha akasema: “Ikiwa ni mtoto wa kiume, basi nyunyuzieni maji; na kama ni mtoto wa kike paosheni.”

Miongoni mwa matukio ya kukumbukwa ya mwana mama huyu wa Kiislamu, Ummu Fadhl رضي الله عنها Lubabah bint al-Haris, ni pale watu wengi walipomfuata na kumuuliza kama Mtume ﷺ alikuwa anafunga siku ya Arafa au alikuwa hafungi? Ili kuondoa shaka kwa Waislamu, Ummu Fadhl رضي الله عنها alimwita mmoja kati ya watoto wake kisha akamtuma ampelekee glass ya maziwa Mtume ﷺ wakati akiwa Arafa. Mtume ﷺ alipoona anaonekana na kila mmoja, aliipokea glass ile ya maziwa na kunywa maziwa yale.

Kwa upande mwingine, Ummu Fadl رضي الله عنها alipokea na kuhifadhi Hadith za Mtume ﷺ. Miongoni mwa watu waliopokea hadithi kutoka kwake ni mwanae Abdullah ibn Abbas رضي الله عنه, Tamam (aliyekuwa mtumwa) na Anas Ibn Malik رضي الله عنه. Mama huyu, Lubabah bint Al-Harith رضي الله عنها, Ummu Fadhl رضي الله عنها, alifariki wakati wa Ukhalifa wa 'Uthman ibn Affan رضي الله عنه baada ya kuacha mfano bora kwa akina mama na Waislamu kwa ujumla. Alikuwa ni mfano bora wa watu waliosimama kutetea wanyonge na katu hakuwaruhusu makafiri kutamba kwa ajili ya nafasi zao katika jamii au utukufu wao; na hili lilikuwa wazi pale alipothubutu kumpiga na kumuumiza Abu Lahab, mtu aliyekuwa anaheshimika miongoni mwa Maquraishi na yeye alikuwa mwanamke wa kawaida tu. Na zaidi ya yote baada ya kujaaliwa kuzaa mtoto mwenye daraja kubwa na mwanazuoni mkubwa ambaye Mtume ﷺ alimtaja kuwa mwanazuoni wa Ummah huu, Abdullah ibn Abbas رضي الله عنه, mama huyu alizidi kuwa mwingi wa shukurani kwa Mola wake.

# Ummu Hani, Fakhita binti Abi Taalib

## Israa na Miraj

Kwa wale wanaosoma vitabu vya Hadith za Mtume ﷺ, mfano vitabu vya Bukhari, Muslim, na Riyad as-Saliheen; jina la Ummu Hani رضي الله عنها ni jina ambalo watakuwa wamekutana nalo mara nyingi. Kulikuta jina lake likijitokeza mara kadhaa katika vitabu vya Hadith za Mtume ﷺ, inatosha kuwa sababu ya kupata hamu kutaka kujua, ni nani hasa huyu Ummu Hani رضي الله عنها, Fakhita bint Abi Talib رضي الله عنها, na vipi amekuwa mtu muhimu sana kisi cha kutajwa katika vitabu vya Hadithi. Kwa wale ambao hawajawahi kusikia jina hili hapo kabla, hakika huyu ni mwanamke mwenye umuhimu mkubwa katika historia ya Uislamu. Anahesabiwa kama mmoja wa maswahaba wa kike (sahabiyyah) wa Mtume Muhammad ﷺ.

Jina lake halisi ni Fakhitah, binti wa baba yake mdogo Mtume Muhammad ﷺ, Abu Talib. Mama huyu alikuwa dada mkubwa wa mashujaa wawili wakubwa katika historia ya Uislamu, Ali Ibn Abi Talib na Jaafar Ibn Abi Talib رضي الله عنهما. Wakati Mtume ﷺ akiwa bado mdogo, na baada ya kuwa mtoto yatima na babu yake kufariki, Mtume ﷺ alilelewa na baba yake mdogo, Abu Talib. Mtume ﷺ alikuwa akipendwa sana katika familia hii, na Abu Talib alimpenda na kumuhudumia kama mwanae.

Mtume Muhammad ﷺ alikuwa mtu muungwana na mkarimu sana na aliishi kwa mapenzi makubwa sana na ndugu zake katika familia hii ya mzee Abu Talib. Alikuwa akimuheshimu sana baba yake mdogo na alikuwa akijitahidi sana kusaidia kazi za nyumbani na kazi alizokuwa akifanya baba yake mdogo kwa kadri alivyoweza kufanya hivyo. Alikuwa pia akionesha uaminifu wa hali ya juu pale aliposhiriki shughuli za kibiashara alizokuwa akifanya Abu Talib.

Mtume Muhammad ﷺ aliomba kumuoa Fakhitah bint Abi Talib رضي الله عنها, hata hivyo mjomba wake alimkatalia na akakubali kumuozesha

Fakhitah رضي الله عنها kwa Hubayra Ibn Abi Wahb. Hubayra alikuwa anatoka katika ukoo wa Makhzoum. Ukoo huu ulikuwa umemuozesha binti yao mmoja katika ukoo wa Abi Talib katika siku za nyuma. Hii kwa namna fulani ilikuwa kama kulipa fadhila za wema waliotendewa. Hili lilikuwa jambo la kawaida na utamaduni uliozoeleka kwa waarabu kulipa fadhila baina ya koo na kudumisha udugu kwa kumuozesha binti yao katika ukoo ambo na wao wameoa kutoka ukoo ule.

Hivi ndivyo Fakhitah bint Abi Talib alivyokuja kuolewa na Hubayra. Wanandoa hawa waliishi Makkah na walijaaliwa kupata watoto wanne (4). Mtoto mkubwa walimuita Hani, na hapa ndipo Fakhitah رضي الله عنها alipofahamika pia kama Ummu Hani, yaani mama wa Hani رضي الله عنها.

Wakati Mtume Muhammad ﷺ alipopewa Utume, baba yake mdogo huyu alimuunga mkono Mtume ﷺ na kumuhami kutokana na njama na vitimbi vya Maquraishi, lakini hakuingia katika Uislamu. Pamoja na kuwa hakusilimu, watoto wake wote walisilimu pamoja na mama yao – mke wa Abi Talib.

Ummu Hani رضي الله عنها akasilimu na kuwa Muislamu, lakini mume wake hakusilimu, na wala hakumuadhibu Fakhitah mke wake kwa kuingia katika Uislamu. Fakhitah رضي الله عنها na mume wake walikuwa na nyumba kubwa na nzuri ambayo waliishi wao na watoto wao, na walikuwa wakimkaribisha Mtume ﷺ nyumbani kwao.

Baada ya kufariki mke kipenzi wa Mtume ﷺ Bi Khadijah, Mtume ﷺ alikuwa mwenye huzuni na mara nyingi alikuwa anakwenda nyumbani kwa Ummu Hani. Familia hii ilijitahidi kumfariji katika wakati huu wa majonzi.

Huyu ndiye Ummu Hani رضي الله عنها, mwanamke na mama muhimu katika historia ya Uislamu. Ni katika nyumba ya Ummu Hani رضي الله عنها, moja kati ya miujiza mikubwa ulitokea; lazima tuamini kuwa nyumbani kwa Ummu Hani kulikuwa kuna baraka. Mtume Muhammad ﷺ alikwenda nyumbani kwa Ummu Hani رضي الله عنها, akaswali Swala za usiku, kisha akalala. Usiku ule, Malaika Jibril akashuka kwa Mtume Muhammad ﷺ ndani ya nyumba ya Ummu Hani; kisha Jibril aliondoka na Mtume ﷺ kwenda safari ya mbali, Jerusalem na baadaye kupanda naye mbinguni, safari ambayo leo tunaifahamu kwa jina la Israa na Miraj. Kufika asubuhi, Mtume ﷺ alikuwa tayari karejeshwa ndani ya nyumba ya Ummu Hani رضي الله عنها. Ndiyo kusema, safari ya Israa na Miraj aliyokwenda

Mtume ﷺ ilianzia na kuishia nyumbani kwa mama huyu, Fakhitah bint Abi Talib, Ummu Hani.

Ilipofika asubuhi, Mtume ﷺ alimuhadithia Ummu Hani رضي الله عنها kile kilichotokea. Yeye (Ummu Hani رضي الله عنها) alikubali na alimuamini, hata hivyo alimuomba Mtume ﷺ asimwambie mtu yeyote katika Maquraishi kwa sababu alichelea kuwa hawatomuamini na badala yake watamtukana, watamkashifu na kumdhuru.Hata hivyo ilikuwa ni wajibu wa Mtume ﷺ kufikisha ujumbe wa Allah kama ulivyo bila kuficha kitu chochote. Watu wa Makkah hawakumuani, na walijaribu kumuuliza maswali ili kuthibitisha habari aliyokuwa amewaambia. Walimtaka Mtume ﷺ awaambie jinsi msikiti wa Aqsa uliopo Jerusalem namna ulivyo, huku wakiwa wana uhakika kuwa Mtume Muhammad ﷺ hajawahi kufika huko Jerusalem, na wao Maquraishi wamekuwa wakienda huko katika misafara yao ya kibiashara. Mtume Muhammad ﷺ akawaelezea namna msiikiti ule ulivyo kwa kina tena kwa usahihi kabisa na kuwaeleza hata alama ndogo ndogo kwa namna ambayo haikuacha shaka kuwa kwa hakika ameuona msikiti ule wa Aqsa. Kimsingi waliridhika kuwa ameuelezea msikiti na kujibu maswali yao kwa usahihi japo waliendelea kupinga kuwa Mtume ﷺ hakwenda safari hiyo na hawakumdhuru.

Mtume Muhammad ﷺ na Waislamu walipohamia Madinah, Ummu Hani رضي الله عنها, yeye hakuhama. Alibakia Makkah akiishi na familia yake na akiendelea kuutekeleza Uislamu.

Baada ya kupita miaka mingi na matukio mengi, Waislamu wakiwa Madinah, waliongezeka kwa idadi yao na nguvu zao kuwa kubwa. Jeshi la Waislamu likiongozwa na Mtume Muhammad ﷺ liliingia na kuukomboa mji wa Makkah bila kumwaga damu.

Wakati wa ukombozi wa Makkah, makafiri wawili waliokuwa wamekataa kusilimu walikimbia kujificha ndani ya nyumba ya Ummu Hani رضي الله عنها, huku wakimuomba awahifadhi. Ummu Hani رضي الله عنه alikuwa ni mtu mwenye busara, mtu mwenye uoni wa mbali na mwingi wa huruma. Ummu Hani رضي الله عنها alikubali kuwapa hifadhi waliyokuwa wameiomba kwake. Kaka yake Fakhitah (Ummu Hani رضي الله عنها ), Ali Ibn Abi Talib رضي الله عنه, akagundua na akaja nyumbani kwa Ummu Hani رضي الله عنها ili awauwe makafiri wale. Pamoja na nguvu na ushujaa wa Ali Ibn Abi Talib رضي الله عنه, Ummu Hani رضي الله عنها

akamkabili na kumzuia asiwafikie makafiri wale. Fakhitah alimwambia Ali Ibn Abi Talib رضي الله عنه kuwa, "Nimekwisha waahidi hifadhi!"

Mtume Muhammad ﷺ akasikia sauti za watu wakizozana na akaenda haraka ili kutatua mzozo uliokuwepo. Mtume ﷺ akaunga mkono rai na msimamo wa Ummu Hani رضي الله عنها juu ya watu wale na kusema: "Tutampa hifadhi kila ambaye Ummu Hani amempa hifadhi."

Wale makafiri wawili waliokuwa wamejificha nyuma ya Ummu Hani walishuhudia kile kilichotokea. Walivutiwa sana na msimamo na huruma aliyoionesha Ummu Hani رضي الله عنها na Mtume ﷺ, na wote wakaingia katika Uislamu.

Hata baada ya kukombolewa kwa Makkah, mume wa Ummu Hani bado alikataa kuingia katika Uislamu, na alikimbia kutoka Makkah, na kumuacha Ummu Hani رضي الله عنها na wanae. Ummu Hani رضي الله عنها, akiwa na wanae, aliamua kuhamia Madinah ili kuishi na kumalizia muda wa uhai wake wote uliuobaki katika mji mkuu wa dola ya Kiislamu. Aliwalea watoto wake vema akiwa peke yake. Akiwa Madinah, Ummu Hani رضي الله عنها akawa mfuasi mkubwa na muhimu wa Uislamu na alikuwa chanzo muhimu cha maarifa ya Uislamu. Fakhitah رضي الله عنها akawa mwanazuoni mkubwa wa Hadithi za Mtume Muhammad ﷺ na historia ya maisha ya Mtume ﷺ. Kwa kufanya kazi hii, kumemfanya kubakia katika kumbukumbu za vitabu vikubwa vya elimu ya Kiislamu, hususan elimu ya Sharia na Hadithi za Mtume ﷺ.

Huyu ndiye Ummu Hani, Fakhita bint Abi Talib رضي الله عنها; ndani ya nyumba yake, safari ya Israa na Miraj ilianzia na kuishia. Allah Amuwie radhi Fakhita bint Abi Talib رضي الله عنها.

# Ummu Hiram binti Milhan

## Mwanajeshi katika jeshi la Wanamaji wa Kiislamu

Siku moja Mtume ﷺ alisema: *"Katika Ummah wangu, jeshi litatembea (kwenda katika jihad) juu ya bahari kama mfalme anavyokaa juu ya kiti chake cha enzi."*

Ummu Hiram رضي الله عنها akamuuliza Mtume ﷺ, "Je na mimi nitakuwa miongoni mwa jeshi hilo?" Mtume ﷺ akamwambia, "*wewe utakuwa miongoni mwa watu wa mstari wa mbele katika jeshi hilo*."

Mapokezi mengine yanasema: Siku moja Mtume ﷺ alimtembelea Ummu Hiram رضي الله عنها nyumbani kwake. Ummu Hiram رضي الله عنها alimuandalia chakula kizuri Mtume ﷺ, kisha Mtume ﷺ alikwenda katika moja ya sehemu ya nyumba hiyo na kujipumzisha. Alipoamka, Mtume ﷺ alikuwa mwenye furaha. Ummu Hiram رضي الله عنها akamuuliza Mtume ﷺ kwanini alikuwa mwenye furaha? Mtume ﷺ akajibu, *"Nimeona katika Ummah wangu, jeshi litatembea (kwenda katika jihad) juu ya bahari kama mfalme anavyokaa juu ya kiti chake cha enzi."* Ummu Hiram رضي الله عنها akatumia fursa ile kumuomba Mtume ﷺ amuombee kwa Allah ili na yeye awe miongoni mwao, Mtume ﷺ akamwambia: *"Wewe utakuwa miongoni mwa watu wa mstari wa mbele katika jeshi hilo."*

Ummu Hiram رضي الله عنها anatoka familia yenye hadhi kubwa. Dada wa Ummu Hiram رضي الله عنها ndiye mama wa Anas Ibn Malik رضي الله عنه. Kaka zake wawili mama huyu, Hiram Ibn Milhan رضي الله عنه na Salim Ibn Milhan رضي الله عنه, walikuwa miongoni mwa maswahaba walioshiriki na kutoa mchango mkubwa katika vita vya Badr na vita vya Uhud.

Kutokana na ndoa, alikuwa pia na uhusiano na Abu Talhah رضي الله عنه, ambaye pia ni mmoja kati ya maswahaba wakubwa wa Mtume ﷺ. Mume wa

mama huyu alikuwa 'Amr Ibn Quays Ibn Zayd رضي الله عنه, na mwanae wa kiume alikuwa Quays Ibn 'Amr Ibn Quays رضي الله عنه – ambao wote wawili, baba na mtoto, walikuwa maswahaba waaminifu wa Mtume ﷺ, na wote wawili waliuwawa mashahidi katika vita vya Badr. Baada ya kufariki kwa mume wake, mama huyu aliolewa na 'Ubadah Ibn Samit رضي الله عنه, aliyekuwa mmoja kati ya makamanda wakubwa wa majeshi ya Waislamu. Mwenyezi Mungu Alimjaalia kupata mtoto katika ndoa hii pia, na mtoto huyu walimwita Muhammad Ibn 'Ubadah Ibn Samit رضي الله عنه.

Ukarimu, kujitolea na kujitoa kwa ajili ya Allah ilikuwa sehemu ya maumbile na maisha ya mama huyu. Lengo lake kubwa siku zote, lilikuwa kufa kwa ajili ya Allah, na hivyo kufa shahidi. Na katika kutafuta kufikia lengo hili, alifanya jitihada na kuitumia kila fursa iliyojitokeza mbele yake. Aliishi nje kidogo ya mji wa Madinah, katika mji mdogo wa Qubah.

Mtume ﷺ alipokuwa njiani akihamia Madinah, alipofika Qubah alisimama kwa muda kabla ya kuendelea na safari. Mama huyu (Ummu Hiram) sio tu kwamba alikuwa mwanamke wa kwanza wa Ki-Ansar kuukubali Uislamu, bali kuutangaza pia hadharani. Alifanya hivyo kabla hata ya Mtume ﷺ kuhamia Madinah. Ummu Hiram alikuwa mwanamke mwenye busara, mcha-Mungu na aliyejibidisha katika kuitakasa nafsi yake. Alikuwa mwanamke mwenye hadhi ya juu miongoni mwa wanawake wa Ki-Ansar. Mtume ﷺ alikuwa akimtembelea nyumbani kwake na wakati mwingine alikuwa anapumzika nyumbani kwa mama huyu ikiwa Mtume ﷺ amechoka. Mtume alikuwa akienda kumtembelea au kusimama kwa muda katika nyumba yake, basi alikuwa akimuachia baraka nyingi; na mama huyu alichukulia kupata fursa ya kumuhudumia Mtume ﷺ kama heshima kubwa aliyopewa.

Anas Ibn Malik رضي الله عنه anasimulia kuwa, siku moja alikuwa nyumbani kwake, Mtume ﷺ akaja. Mtume ﷺ aliwapa zawadi kubwa. Aliwaambia watawadhe na kisha yeye Mtume ﷺ atawaongoza katika Swala maalum; haikuwa wakati wa Swala yeyote ya faradhi. Baada ya Swala Mtume ﷺ aliwaombea dua kwa Allah Airehemu na kuipa baraka familia ile duniani na kesho Akhera.

Mume wa mama huyu, 'Ubadah Ibn Samit رضي الله عنه alikuwa na bahati ya kuwa katika misafara yote miwili iliyokwenda Makkah ikitokea Madinah,

kwenda kula kiapo na kuchukua ahadi ya utii kwa Mtume ﷺ kabla Mtume ﷺ hajahamia Madinah. Alikuwa mfano bora wa mume, na mfano bora wa baba wa familia. Alikuwa baba aliyempenda na kumpa malezi mazuri mwanae 'Abdullah Ibn 'Amr رضي الله عنه, mtoto aliyezaliwa na mkewe Ummu Hiram kutoka kwa mume wake wa kwanza. Malezi na mapenzi aliyokuwa akiwapa watoto wake, ni yale yale aliyokuwa akiwapa watoto aliozaa mke wake kutoka katika ndoa nyingine. Wakati Ayah iliyoamuru kubadili muelekeo wa Qiblah wakati wa kuswali, kutoka walikokuwa wakielekea hapo awali Masjid- al-Aqsa na kuanza kuelekea Ka'bah, Muhammad Ibn 'Ubadah alikuwa miongoni mwa watu waliokuwepo katika Swala ile. Hivyo, mtoto wao Muhammad Ibn 'Ubadah alipata bahati ya kuelekea Qibla zote mbili ndani ya Swala hii moja.

Hadithi zilizopokelewa na mama huyu, Ummu Hiram رضي الله عنها zimenukuliwa na maswahaba wengi wakubwa wa Mtume ﷺ. Miongoni mwa maswahaba hao ni 'Ubadah Ibn Samit رضي الله عنه, Anas Ibn Malik رضي الله عنه, 'Umair Ibn Aswad رضي الله عنه, 'Ata Ibn Yasirرضي الله عنه na Ya'la Ibn Shaddad Ibn Aws رضي الله عنه. Hisia na mapenzi ya mama huyu, Ummu Hiram رضي الله عنها kwa Mtume ﷺ yalikuwa ni makubwa na ya kiwango cha juu kabisa. Mtume ﷺ alipotembelea nyumbani kwa Ummu Hiram رضي الله عنها au kutembelea nyumbani kwa dada yake mama huyu, Ummu Sulaym, walikuwa wakifurahi sana. Walikuwa wakimuandalia chakula kizuri kadri walivyoweza na kumuandalia kitanda ili apumzike. Kwa hali ilivyokuwa na mazingira yalivyokuwa, yalimfanya Mtume ﷺ naye ajisikie furaha na amani anapoitwa na mama huyu, Ummu Hiram رضي الله عنها. Mtume ﷺ alipoulizwa kama alikuwa na sababu yeyote ya msingi ya kutembelea nyumba ya mama huyu (Ummu Hiram رضي الله عنها) mara kwa mara, Mtume ﷺ alijibu kuwa, toka alipowaona kaka zake wawili wakiuwawa mashahidi katika vita na kwamba toka wakati huo, amekuwa akienda kujua mahitaji yao na kuwaliwaza. Watu wa Ansar walikuwa wakifahamika vema kwa nyoyo zao za kujitoa muhanga kwa ajili ya Allah na ukarimu wa hali ya juu; na Ummu Hiram رضي الله عنها alikuwa amejengwa katika misingi hii muhimu katika kuutumikia Uislamu.

وَٱلَّذِينَ تَبَوَّءُو ٱلدَّارَ وَٱلْإِيمَـٰنَ مِن قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِى صُدُورِهِمْ
حَاجَةً مِّمَّآ أُوتُوا۟ وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ ۚ وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِۦ
فَأُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ ﴿٩﴾

***"Na (pia wapewe) wale waliofanya maskani yao hapa (yaani Madinah) na wakautakasa Uislamu (wao barabara) kabla ya (kuja) hao (Muhajiri huko Madinah) na wakawapenda hao waliohamia kwao, wala hawapati, hawaoni dhiki nyoyoni mwao kwa hayo waliyopewa (hao Muhajiri), na wanawapendelea kuliko nafsi zao ingawa wenyewe wana hali ndogo. Na waepushwao na ubakhiri wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kweli kweli."*** **(59:9)**

Mwenyezi Mungu alifurahishwa na kuridhishwa na moyo wa ukarimu, huruma na kujitoa muhanga kwa kiwango kilichooneswa na watu wa Ansar kwa ndugu zao waliohama kwa ajili ya Allah na Mtume wake ﷺ kutoka Makkah; akaamua kuhifadhi sifa zao ndani ya Qur'an ili watu wazisome mpaka mwisho wa dunia. Sifa hizi njema za huruma, ukarimu na kujitolea zilikuwa kwa watu wote wa Ansar, wanaume na wanawake. Ilikuwa ni jambo la dhahiri kuwa, mama huyu, Ummu Hiram رضي الله عنها alikuwa amejaaliwa ziada ya sifa hizi. Zaidi ya yote, familia hii ilipata bahati ya kuwa na baraka za Mtume ﷺ. Mtu anaweza kutaka nini tena, zaidi ya kuwa na baraka za Mtume? Wakati Mtume ﷺ anafariki dunia, alikuwa amemridhia mama huyu kutokana na ukarimu aliokuwa akiuonesha na kwa wema aliokuwa akimtendea Mtume wa Allah ﷺ.

Wakati wa Ukhalifa wa 'Uthman Ibn 'Affan رضي الله عنه, katika mwaka wa 27 baada ya Hijrah, Mu'awiyah Ibn Abu Sufyan رضي الله عنه alipewa ruhusa ya kukikomboa kisiwa cha Cyprus. Ili kufika huko, ililazimu kuwa na kikosi cha askari wanamaji (*naval force*). Hii ilikuwa ni mara ya kwanza katika historia ya Uislamu, Waislamu kuandaa jeshi la askari wanamaji. 'Ubadah Ibn Samit رضي الله عنه aliongozana na mke wake, Ummu Hiram رضي الله عنها; wakiwa pamoja na kamanda wa majeshi, Mu'awiyah رضي الله عنه na mke wake Fakhtah bint Qurdhah.

'Umair Ibn Aswad 'Ansi anaandika kuwa, alimtembelea 'Ubadah aliyekuwa akiishi eneo la pwani ya Hamas. Alikutana na Ummu Hiram ambaye (Ummu Hiram رضي الله عنها) alimwambia kuwa, alimsikia Mtume ﷺ akisema: *"Katika Ummah wangu, jeshi litatembea (kwenda katika jihad) juu ya bahari kama mfalme anavyokaa juu ya kiti chake cha enzi."* Nikamuuliza, 'Je na mimi nitakuwa miongoni mwa jeshi hilo?' Mtume ﷺ, "*akakubali kuwa mimi nitakuwa miongoni mwao*".

Ummu Hiram رضي الله عنها alifurahishwa sana na maneno yale ya Mtume ﷺ kwa sababu alikuwa na hamu sana na yeye siku moja ashiriki jihad kwa ajili ya Allah. Kwa rehema Zake Allah, Waislamu walipata ushindi. Baada ya kusafiri kwa bahari, Ummu Hiram رضي الله عنها akapanda juu ya mnyama ili atembee juu yake katika ardhi. Kwa bahati mbaya mnyama yule akatishwa na kitu na yeye (Ummu Hiram) akaanguka chini. Aliumia sana shingo, na hii ikawa sababu ya kifo chake. Hivyo alipata bahati ya kufa shahidi akitokea vitani, jambo ambalo siku zote alikuwa akiliomba, na alizikwa Cyprus. Katika vita hivi, swahaba mkubwa na hodari, Abu Talhah رضي الله عنه alikufa shahidi katika vita hivi.

Ummu Hiram رضي الله عنها alikuwa ni mwanamke mwenye bahati sana, mmoja kati ya wanawake wa Kiislamu walioshiriki katika jeshi hili la wanamaji la kwanza katika historia ya Uislamu, na kufa shahidi akiupigania Uislamu, na kustahili kuwa na nafasi yake ndani ya Pepo ya Mwenyezi Mungu.

Aliishi maisha yake ya kicha-Mungu na ya kupigiwa mfano, na akapata mwisho mwema kwa kufa shahidi katika jeshi la kwanza la wanamaji la Waislamu, jeshi la kwanza la wanamaji katika historia ya Uislamu.

رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا۟ عَنْهُ

***"...Mwenyezi Mungu Amewaridhia, nao wameridhika...."* (98:8)**

# Ummu Mihjan

## Sababu ya Nuru kwa Wengine

Mama mmoja alikuwa na kawaida ya kusafisha msikiti, kwa leo tunaweza kumwita muhudumu wa msikiti. Akijihusisha na kufanya shughuli zote za usafi msikitini. Zikapita siku kadhaa bila Mtume ﷺ kumuona mama huyu. Mtume wa Allah ﷺ, akawauliza maswahaba zake, 'yuko wapi Ummu Mihjan رضي الله عنها (mama aliyekuwa na kawaida ya kufanya usafi msikitini)?' Mtume ﷺ aliuliza hivi kwa sababu ilikuwa ni jambo la kawaida kumuona mama huyu takriban kila siku. Kukosekana kwake kwa siku kadhaa kulimaanisha huwenda mama huyu akawa anaumwa au ana tatizo jingine. Maswahaba wakamwambia kuwa mama huyo (Ummu Mihjan رضي الله عنها) ameshafariki. Mtume ﷺ akawauliza maswahaba wale, *"Kwanini hamkunifahamisha juu ya kifo chake?"* Inawezekana maswahaba si kwa nia mbaya, waliona kifo cha mama yule halikuwa jambo kubwa kiasi cha kumpa taarifa Mtume ﷺ, jambo ambalo lingemshughulisha. Kisha Mtume ﷺ akawaambia: *"Nionesheni kaburi lake."*

Alipooneshwa kaburi lile, alimswalia Swala ya maiti akasema: *"Makaburi ya watu hawa yalikuwa yamejaa giza, na Allah Ameyaangazia nuru kutokana na dua niliyowaombea."* (Muslim)

Pamoja na mapokezi mengine, wanazuoni wengi wamekubaliana kuwa mtu aliyetajwa katika hadithi hii au kuhusika na hadithi hii si mwingine ila ni mama huyu, Ummu Mihjan رضي الله عنها, mama wa Kiislamu aliyekuwa na kawaida ya kusafisha msikiti.

Yapo mengi tunayoweza kujifunza katika tukio hili na hadithi hii. Miongoni mwa mambo haya ni kutopuuza au kudharau tendo au matendo mema bila kujali tendo hili ni dogo kiasi gani, hasa linapofanywa kwa nia ya kutafuta radhi za Allah. Pili ni kuheshimu na kuthamini mchango wa kila mmoja wetu katika

kuupeleka mbele Uislamu. Mama huyu hakuwa miongoni mwa wapiganaji wa Kiislamu, lakini alikuwa na nafasi ndogo tu ya kusafisha msikiti, lakini kwa Allah na Mtume wake alikuwa anafanya jambo kubwa na alistahili heshima kubwa na Mtume ﷺ alilithibitisha hilo.

Pengine somo muhimu tunalojifunza ni kutoka katika hadithi ya Mtume ﷺ kuwa anasema: *"Amali (ibada) bora na inayopendwa zaidi na Allah ni ile ya kudumu, hata kama ibada hiyo ni ndogo."* (Muslim)

# Zaynab, Ummu Rooman

## Mfano wa Wanawake wa Peponi

Mtume ﷺ anasema: *"Yeyote mwenye kutaka kumuona mwanamke mrembo na bikira wa Peponi, amuangalie Ummu Rooman."*

Mama huyu alikuwa mke wa swahaba wa Mtume ﷺ na Khalifa wa kwanza wa Waislamu, Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه, ambaye pia ndio mama wa Aishah رضي الله عنها. Hivyo mama huyu alikuwa ni mama mkwe wa Mtume ﷺ. Mwanae mwingine ni Asma bint Abu Bakr رضي الله عنها, ambaye tayari tumekwisha mzungumza huko nyuma. Mwanae wa kiume alikuwa 'Abdur-Rahman Ibn Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه, shujaa na mwendesha farasi hodari na jemedari wa vita. Mama huyu alimfundisha mwanae 'Abdur-Rahman Ibn Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه, maana ya mtu kuwa shujaa na jasiri.

Jina halisi la mama huyu alikuwa ni Zaynab رضي الله عنها, lakini alikuja kufahamika zaidi kwa jina la ukoo wake. Alikuwa mama mtulivu na mwingi wa subira asiyekurupuka na kutoa majibu ya haraka na ya jumla jumla, bali alikuwa akiyatafakari na kuyachambua mambo kwa umakini na kwa kina kabisa. Sifa hii ilijidhihirisha wazi pale wanafiki na watu wenye ndimi silizokosa stara walipoeneza tuhuma za zinaa za uzushi juu ya mwanae Aishah رضي الله عنها.

Pale mume wake Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه, alipomueleza mafundisho ya Uislamu na hukumu juu ya jambo lile, mama huyu hakuonesha shaka wala wasiwasi na kuchelea hukumu ya Kiislamu kupita juu ya mwanae. Aliuona ubora wa Uislamu na alikubali mara moja. Mtume ﷺ alipoona msimamo wa mwili na roho wa mama huyu, alimfananisha na wanawake wa Peponi.

Imeandikwa katika *Tabaqat* Ibn Sa'd kwamba Ummu Rooman رضي الله عنها aliukubali na kuingia katika Uislamu siku za mwanzo kabisa wakiwa Makkah.

Alichukua ahadi ya utii kwa Mtume ﷺ na kuwa miongoni mwa kundi la Waislamu lililohama kutoka Makkah kwenda Madinah kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah. Alipokuwa akishuhudia mateso na unyanyasaji wa kupita kiasi uliokuwa ukifanywa na Maquraishi kwa Waislamu wanyonge, alikuwa akiwaonea huruma Waislamu na kulia kwa uchungu kwa kuwa alikuwa hana namna ya kuwasaidia; lakini alijawa na morali na furaha baada ya kuona namna ambavyo mume wake, Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه alivyokuwa tayari kujitolea kwa kiwango cha juu kabisa kwa ajili ya Uislamu. Alikuwa akimuhimiza mume wake na akimtia moyo katika kuutumikia Uislamu.

Mtume ﷺ alikuwa pia akiwahimiza Waislamu wasikate tamaa kutokana na misukosuko na mateso, bali wabakie imara na kumtegemea Allah na wasiache kuhifadhi imani yao na kwamba kwa subira yao, wao watakuwa wenye kulipwa Pepo. Maswahaba walikuwa ni watu wenye imani thabiti ya kweli. Hawakuwa wakiyumba au kutetereka imani zao hata kama itawalazimu miili yao kukatwa vipande viwili kwa msumeno. Mtume ﷺ alipoona namna familia ya Yasir ilivyokuwa ikikabiliwa na mateso makali, Mtume ﷺ alisema: *"Enyi Familia ya Yasir! Kuweni wenye subira, mwisho wenu na makazi yenu yatakuwa Peponi."*

Katika muda wote, Ummu Rooman رضي الله عنها alibakia kuwa kielelezo cha utulivu na ustahamilivu na ujasiri. Alitumia muda wake mwingi katika kufanya ibada na dua kwa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote. Alipomuona mume wake akijitolea kwa hali na mali tena kwa kiwango cha juu katika kuupeleka mbele Uislamu, alimuunga mkono na kumtia moyo azidi kufanya hivyo. Na si kumvunja moyo au kumtisha kutokana na hofu ya umasikini na vitu kama hivyo. Alitumia muda wake vema katika kuwalea watoto wake katika misingi ya Uislamu na kuwafundisha kuijua dini yao na kumjua Mola wao. Mtume ﷺ alikuwa na kawaida ya kumtembelea rafiki yake na mfuasi wake mwaminifu, Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه. Mtume ﷺ alikuwa akimshauri na akimuhimiza Ummu Rooman رضي الله عنها kuendelea kumtia moyo mume wake, Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه katika kuutumikia Uislamu na kumlea vema mtoto wao, Aishah رضي الله عنها. Khadijah رضي الله عنها alifariki dunia miaka mitatu kabla ya Mtume ﷺ kuhamia Madinah. Mtume ﷺ alikaa mwaka mzima bila kuoa. Kisha Mtume ﷺ alimuoa Aishah رضي الله عنها baada ya kupokea amri ya kufanya hivyo kutoka kwa Allah iliyoletwa na Malaiaka Jibril. Hivyo mama huyu, Ummu

Rooman رضي الله عنها akapata bahati ya kuwa mama mkwe wa Mtume ﷺ. Alionesha furaha ya wazi kabisa baada ya kujua kuwa mwanae anaingia katika wanawake wenye daraja kubwa, daraja la kuwa mama wa waumini. Unadhani angetaka heshima gani kubwa zaidi ya hii katika familia yao?. Mtume ﷺ alipopokea amri kutoka kwa Allah, amri iliyomtaka ahame na kuelekea Madinah, Mtume ﷺ alikwenda nyumbani kwa swahaba na rafiki yake, Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه. Alipomwambia kuhusu amri ile, Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه hakusita wala kutafakari mara mbili, bali alianza kujiandaa ili aongozane na Mtume wa Allah ﷺ katika safari ile. Alichukua vitu vichache na kuchukua pesa yote iliyokuwepo nyumbani. Pale nyumbani kwake, Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه alimuacha baba yake na watoto wake chini ya dhamana na uangalizi wa Allah na kuelekea safari ambayo ilitokana na amri kutoka kwa Allah.

Ulikuwa wakati mgumu sana kwa Ummu Rooman رضي الله عنها; kwa sababu alikuwa anatengana na mume wake, na walikuwa hawana pesa za matumizi kabisa. Kwa sababu Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه alikuwa amechukua pesa zote zilizokuwepo na kuondoka nazo. Hata hivyo, kilichotawala vinywa vyao ilikuwa ni dua, kuwaombea Mtume ﷺ na mume wake Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه wafike salama madinah. Baada tu ya kufika salama Madinah, Mtume ﷺ akamtuma Zayd Ibn Harithah na Abu Rafi' wailete familia yake; na Abu Bakr As-Siddiq رضي الله عنه akamtuma 'Abdullah Ibn Ariqat رضي الله عنه na kumuandikia ujumbe mwanae 'Abdullah kuileta familia yake (familia ya Abu Bakr Siddiq). Mama huyu, Ummu Rooman رضي الله عنها na mwanae Aishah رضي الله عنها wakapanda juu ya ngamia mmoja. Wakiwa njiani kuelekea Madinah, ghafla wakamuona ngamia akipoteza mwelekeo na kuanza kuruka huku na huko kiasi cha kuwarusha waliopanda. Ummu Rooman رضي الله عنها alikuwa na wasiwasi sana na binti yake Aishah رضي الله عنها na kuanza kupaza sauti akisema, "Ewe mwanangu, Ewe bi harusi wangu mdogo!" Ghafla mtu mmoja akawaambia kuwa amshike hatamu ngamia yule, na hii ikamfanya ngamia yule atulie na wakawa wamenusurika hatari iliyokuwa inawakabili.

Siku moja Abu Bakr Siddiq na mkewe, Ummu Rooman رضي الله عنها, walikwenda kumtembelea Mtume ﷺ, naye aliwauliza sababu ya safari yao. Wote kwa pamoja walimwambia Mtume ﷺ kuwa, wanaomba amuombee dua mtoto wao Aishah رضي الله عنها.

Kisha Mtume ﷺ alimuomba Mwenyezi Mungu Amsamehe Aishah bint Abu Bakr ndani na nje, msamaha ambao hautoacha dhambi yeyote. Wazazi wote wawili wakaonesha furaha kubwa kwa dua hii nzuri kutoka kwa Mtume wa Allah ﷺ.

Kisha Mtume ﷺ akasema, dua ile ilikuwa ni kwa ajili ya wote waliokubali Uislamu mara tu baada ya Mtume ﷺ kupewa Utume, wakadumu na kubakia katika msimamo wa imani yao. Mtume ﷺ alimuheshimu sana Ummu Rooman رضي الله عنها, na Ummu Rooman رضي الله عنها kwa upande wake, alijitahidi sana kuyapa kipaombele na kufanya mambo ambayo yalikuwa yakimfurahisha Mtume ﷺ. Hivyo maisha yalikuwa mazuri na ya furaha, na kila mmoja alikuwa akijitahidi kutekeleza wajibu wake kwa Muumba wake na watu wengine.

Siku moja Mtume ﷺ alimsifia mama wa Waumini, Bi Khadijah رضي الله عنها kwa kiwango cha juu kabisa huku akitaja sifa zake nyingi na nzuri nzuri. Aishah رضي الله عنها kama walivyo wanawake wengine, akajisikia wivu mkubwa; bila kutarajia, 'Aishah akasema, Mtume ﷺ alikuwa akimtaja na kumsifia Bi Khadijah رضي الله عنها kana kwamba kulikuwa hakuna mwanamke mwingine katika ardhi isipokuwa yeye Bi Khadijah. Mtume ﷺ hakuipenda kauli hii hata kidogo, na uso wake ukabadilika na kuonesha dalili ya wazi ya kutofurahishwa na maneno ya mama Aishah رضي الله عنها. Ummu Rooman رضي الله عنها alipopata habari hii, alikwenda nyumbani kwa Mtume ﷺ na kujaribu kumuomba radhi kwa niaba ya Aishah huku Ummu Rooman رضي الله عنها akimwambia Mtume ﷺ kuwa mwanae Aishah alikuwa bado mdogo, hivyo asiyape uzito mambo au maneno yake. Kwa upole na kwa utulivu, Mtume ﷺ akamuuliza Aishah رضي الله عنها kama hukusema kuwa hakuna mwanamke mwingine katika uso wa ardhi zaidi ya Khadijah. Mtume ﷺ akaapa kwa jina la Allah kuwa, hakika mwanamke huyu Mtukufu alimuamini Mtume ﷺ wakati watu wa kabila la Aishah رضي الله عنها wakikanusha kuwa yeye (Muhammad ﷺ) hakuwa Mtume wa Allah. Bi Khadijah رضي الله عنها amenipa zawadi ya watoto, kitu ambacho hakukipata kwa Aishah.

Ummu Rooman رضي الله عنها alisikiliza kwa makini na alikuwa amekaa kimya kwa utulivu, hii ni kwa sababu Ummu Rooman رضي الله عنها alifahamu kuwa kila alilokuwa akizungumza lilitokana na *Wahyi* na ilikuwa ni amri kutoka kwa Allah. Mtume ﷺ alikuwa hazungumzi kwa matamanio au kupenda kwake kuzungumza; siku zote maneno yake yalitokana na *Wahyi* kutoka kwa Allah.

Historia na kumbukumbu inaonesha kuwa, mama huyu, Ummu Rooman رضي الله عنها alifariki mwaka wa sita (6) baada ya kufanyika kwa Hijrah. Wakati wa maziko yake, Mtume ﷺ alimuomba Allah Amsamehe madhambi yake. Bila shaka hii ilikuwa ni bahati na jambo kubwa kwake, kuombewa msamaha na Mtume wa Allah, na dua yake ni yenye kukubaliwa. Ilikuwa ni wakati huu, Mtume ﷺ alisema: *"Yeyote mwenye kutaka kumuona mwanamke mrembo na bikira wa Peponi, basi na amuangalie Ummu Rooman."*

Maneno haya yanatoa dalili kuwa bila shaka Allah Akipenda, mama huyu Ummu Rooman رضي الله عنها, atakuwa mwanamke wa Peponi. Tunamuomba Allah Aijaze kaburi yake kwa Nuru itokayo Kwake. Hata hivyo kuna mapokezi mengine yanayosema, mama huyu, Umm Rooman alikufa baada ya kufariki Mtume ﷺ.

Hakika maneno ya Allah ni ya kweli,

إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ وَأَخۡبَتُوٓاْ إِلَىٰ رَبِّهِمۡ أُوْلَٰٓئِكَ أَصۡحَٰبُ ٱلۡجَنَّةِۖ هُمۡ فِيهَا خَٰلِدُونَ ٢٣

***"Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri na kunyenyekea kwa Mola wao; hao ndio watu wa Peponi; humo watakaa milele"* (11:23)**